Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Ishirini Na Mbili – Tarehe 12 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika, (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 183

**Mradi wa Ukusanyaji Taka Nchini**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. RIZIKI OMAR JUMA**) aliuliza:-

Mwaka 2010 Serikali ilikubaliana na Serikali ya Korea ya Kusini katika utekelezaji wa mradi wa Usimamizi wa Ukusanyaji Taka katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Arusha.

(a) Je, mradi huo umeshaanza?

(b) Kama haujaanza. Je, ni kitu gani kimesababisha usianze wakati upembuzi yakinifu umeshafanyika?

(c) Je, ni mafanikio gani yamepatikana kutokana na matangazo ya elimu ya suala hilo yaliyotolewa katika televisheni za *TBC, ITV na STAR TV* kwa vipindi visivyopungua sitini (60)?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mradi wa usimamizi na ukusanyaji wa taka ngumu unaohusu ufadhili wa Serikali ya Korea ya Kusini bado haujaanza.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya awali juu ya mpango huo yalikamilika mwezi Desemba 2010, katika

mkutano uliofanyika *Seoul,* nchini Korea Kusini. Mpango huo uliainisha miradi mbalimbali inayohusu shughuli mbalimbali ambazo zingegharimu Dola za Marekani bilioni 1.2.

Mpango unatarajiwa kuanza kutekelezwa baada ya Serikali kukamilisha mawasiliano na Jamuhuri ya Korea Kusini kuhusu upatikanaji wa fedha na mikopo nafuu kutoka Serikali hiyo.

Hata hivyo, Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kusimamia zoezi la usafi wa mazingira na ukusanyaji wa taka ngumu katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu, kutoa rai kwa Halmashauri zote hasa za Jiji la Dar es Salaam, kuendelea na kampeni ya usafi. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kuendelea kusimamia Halmashauri zetu ili kutekeleza zoezi hili la usafi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kutoa elimu kwa Umma ni kuwafahamisha na kuwahamasisha wananchi ili kushiriki katika utekelezaji wa mpango na mkakati wa ukusanyaji wa taka ngumu katika Miji yetu.

Kupitia programu ya elimu kwa Umma, Serikali imepata fursa ya kuufahamisha Umma juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira. Vipindi hivi vya elimu ya mazingira vimewezesha wananchi na wadau wengine kujenga uwezo wa uelewa juu ya athari za utupaji taka ovyo na umuhimu wa usafi na utunzaji wa mazingira.

Aidha, mafanikio yaliyopatikana na yatakayoendelea kupatikana ni kuongezeka kwa wigo wa uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ungerudi kidogo hapa, njoo kidogo na mtambo wako. Nilitaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika kwenda na kasi ya kisasa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anatumia teknolojia ya kisasa kujibu maswali hapa, tumpongeze kidogo. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu. Hakuna swali la nyongeza tunafuata swali linalofuata. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa hali kama hii, je Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha Miji yetu inakuwa misafi?

(b) Kutokana na kodi zinazokusanywa na Serikali kila mwezi. Je, kwa nini hizo pesa zisianzie kwenye huu mradi ya Korea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, sisi kama Wabunge na sisi sote tunakaa katika Halmashauri zetu na kwa kutumia Sheria yetu ya

mwaka 2004 kama nilivyosema wakati nikijibu maswali ya Wabunge mbalimbali wakati wa hotuba yetu ya Bajeti, tukiangalia kifungu cha 33 mpaka cha 41, kinatupa uwezo wa kusimamia Miji yetu iweze kuwa safi na inatupa mtiririko mzima wa kujipanga namna ya kutekeleza hilo.

Kwa hivyo niwaombe ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tutekeleze Sheria hiyo, tuweze kufanya mipango yetu ikawa safi.

(b) Vile vile suala la ukusanyaji pesa zinazotokana na ukusanyaji taka katika Halmashauri zetu, ni jukumu la Halmashauri zetu na niombe tena tuendelee kushirikiana tuweze kuweka Miji yetu katika hali ya usafi.

Lakini niseme tu kitu kimoja, ukiliangalia Bunge letu, ukaangalia makaratasi tuliyonayo, utaelewa ni miti kiasi gani imekatwa na huu ni uharibufu wa mazingira, niwaombe Kamisheni yetu waweze kuangalia namna gani tunaweza kutumia teknolojia tukapunguza hizi taka ngumu tulizonazo katika vitabu vyetu.

Vile vile niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo tunatumiwa taratibu za kila siku lakini kila mtu utamkuta asubuhi anaomba *Order Paper* pale mlangoni, lakini *Order Paper* ameshatumiwa *electronically* kwenye simu yake. Hayo ndiyo mabadiliko tunayohitaji Ndugu zangu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri ushauri wako tunauzingatia kwenye Tume. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Afya na Ustawi wa

Jamii naomba nimwite Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge Koani.

Na. 184

**Kuongeza Wodi ya Wagonjwa- Hospitali ya Muhimbili**

**MHE. AMINA A. CLEMENT** aliuliza:-

Hospitali ya Taifa Muhimbili ambayo ndiyo nchini imekuwa ikipokea wagonjwa wengi wa Rufaa kutoka Zanzibar na Mikoa yote ya Tanzania.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wodi za wagonjwa katika Hospitali hiyo ili kupunguza msongamano wa wagonjwa uliopo kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Hospitali ya Taifa ya Muhimbili inahudumia wagonjwa wengi kutoka sehemu mbalimbali nchini Tanzania. Kwa sasa Serikali haina mpango wa kuongeza Wodi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, badala yake Serikali inatekeleza mikakati ya kupunguza idadi ya wagonjwa wanaolazimika kwenda katika hospitali hiyo. Mikakati hiyo ni pamoja na upandishaji hadhi wa hospitali mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Gazeti la Serikali, toleo namba 46 la tarehe 12 Novemba, 2010, Serikali imezipandisha hospitali mbili (2) kuwa hospitali za Rufaa za Kanda ambazo ni Hospitali za *CCBRT* na Hospitali ya Jeshi ya Lugalo zote Dar es Salaam.

Vile vile, imepandisha hadhi hospitali tatu (30 za Manispaa ya Temeke, Mwananyamala na Amana kuwa Hospitali za Rufaa za Mkoa. Pia, hospitali 20 za Mikoa kuwa za rufaa na hospitali 10 za Mashirika ya Dini kuwa Hospitali za rufaa ngazi ya Mkoa.

Upandishaji hadhi huu, unakwenda sambamba na kuongeza idadi ya wataalam, dawa na vifaa na kuziwezesha kutoa huduma za kibingwa.

Lengo ni kusogeza huduma za rufaa karibu na wananchi ili kupunguza idadi ya wagonjwa ambao wangelazimika kupata huduma hizo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na kutoa fursa kwa hospitali hii iweze kutekeleza wajibu wake wa kutoa huduma za ubingwa wa juu. *(Makofi)*

**MHE. AMINA A. CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wagonjwa wengi wanaotoka Zanzibar ni wananchi wenye kipato cha chini. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia kuandaa mpango maalum wa kupeleka Zanzibar pamoja na Mikoa iliyokuwa haijapandishwa hadhi kuwa Hospitali za Rufaa kuwapatia Madaktari Bingwa angalau kwa mwezi siku tatu

ili kuwapunguzia usumbufu wale wagonjwa na pia gharama ya usafiri?

(b) Kwa kuwa ajali nyingi za barabarani zinatokea hapa kwetu Tanzania na Watanzania wengi tumepoteza viungo vyetu vya mwili, mifupa na kadhalika. Je, katika hospitali zilizopandishwa kuwa za Rufaa, wamefungua vitengo vya mifupa yaani (*Orthopaedic*) kwa ajili ya huduma ya mifupa vilivyokamilika, vyenye Madaktari na vifaa kamili? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Swali la kwanza linalozungumzia kuwepo na mpango wa kupeleka Madaktari Bingwa kwa ajili ya kutatua matatizo angalau kwa kupokezana ni wazo zuri nafikiri Wizara imelichukua, lakini vile vile nimfahamishe tu kwamba kitu hiki kilikuwepo kwenye miaka ya zamani. Kwa hiyo, inategemea tu na mpango, utaratibu wa kuweza kuyaandaa hayo na kuweza kufanyika kwa sababu ilishafanyika kwenye baadhi ya Mikoa hapa nchini. *(Makofi)*

(b) Kuwepo na huduma za *orthopaedic* katika baadhiye ya mahospitali hizi za Rufaa ndiyo kusudio la Serikali kusema kweli kwamba Hospitali hizi za Rufaa ziwe na huduma zote zile za kibingwa angalau kwa asilimia 25 au zaidi na kwa namna hiyo huduma hiyo ya *orthopaedic* imo katika kuboreshwa katika baadhi ya hospitali hizi za Mikoa.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa sababu moja ya namna inayoweza kupunguza msongamano kwenye hospitali yetu ya Taifa pale Muhimbili ni kutoa huduma kwenye Hospitali za Rufaa kwenye Kanda na kwa sababu kwenye Kanda ya Kusini kwa maana ya Mtwara na Lindi wananchi wake hawana mahali pengine wanapohitaji kwenda Rufaa ni kwenda Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa hivi karibuni kuhakikisha Hospitali ya Rufaa Mtwara inaanza kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njwayo, kama ifuatavyo:-

Hospitali ya Mkoa ya Mtwara imo katika kupandishwa kuwa hospitali ya Kanda na kwa namna hiyo utaratibu wa kuijenga na kukamilisha kufikia katika hadhi hiyo umo katika mkakati wa wakati huu kuweza kutekelezeka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Madiwani wa Newala mko hapa, mmesikia jamani? Hospitali ya Mtwara itakuwa Hospitali ya Rufaa. Tunahamia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini. Mheshimiwa Juma Nkamia.

Na. 185

**Ruzuku Inayotolewa na FIFA kwa TFF**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliliza:-

Shirikisho la Soka Duniani *(FIFA)* linatoa ruzuku kwa Vyama vya Mashirikisho ya Soka Duniani ili kujiendeleza.

Je, ni kiasi gani cha fedha kilichopokelewa na Shirikisho la Soka nchini *(TFF)* tangu mpango huo uanze?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Mpira wa Miguu Ulimenguni *(FIFA)* limekuwa likitoa Dola 250,000 za Kimarekani kwa kila nchi mwanachama tangu ilipozindua mpango wake kutoa ruzuku mwaka 1998. Fedha hizo hutolewa baada ya nchi mwanachama kuomba kwa kuwasilisha miradi hiyo katika maeneo yaliyotolewa na *FIFA*.

Baada ya maombi haya kuthibitishwa na kukubaliwa na *FIFA* hutuma fedha hizo kwa masharti kwamba zitumike kama inavyoelekezwa katika miradi iliyothibitishwa. Maeneo ambayo fedha hizi huelekezwa ni miradi ya vijana na watoto, maendeleo ya soka kwa wanawake, uamuzi, mpira wa ufukweni na ufundi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya utaratibu huo wa *FIFA* imeshatoa kwa Tanzania kiasi cha Dola 3.25 milioni tangu mpango wa kutoa ruzuku ulipozinduliwa miaka 14 iliyopita.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Nina maswali matatu madogo tu ya nyongeza:-

Katika siku za karibuni tumeshuhudia timu ya *Twiga Stars...*

**NAIBU SPIKA:** Maswali mawili ya nyongeza madogo.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, timu ya wanawake ikiomba kila mahali ili ipate fedha za kwenda Ethiopia kushiriki mchezo wake dhidi ya Ethiopia. Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba fedha hizi zinazotolewa na *FIFA* pia zinatumika kwa ajili ya kuendeleza soka la wanawake.

(a) Kwa nini timu hii ilikuwa inaombaomba wakati fedha ipo?

(b) Vyama vya Soka vya Mikoa ndiyo wadau wakubwa wa *TFF,* ukiacha *computer* moja moja waliopewa chini ya mradi huu vimefaidika nini na mradi huu wa *FIFA?*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana Utamaduni na Michezo napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Nkamia, kama ifuatavyo:-

(a)Kwanza, fedha hizi hutolea zikiwa na maelekezo kwamba zifanye kazi gani, ikiwepo mafunzo mbalimbali kwa vijana, waamuzi vijana kwa kukuza vipaji vya vijana,

walimu wa timu za vijana na utawala katika soka la wanawake.

Lakini pia, fedha hizi hutumika katika maandilizi ya awali hata ya timu ya *Twiga Star.* Tunapokea kwamba ni changamoto kwa timu yetu kuendelea kuombaomba. Nataka niwaahidi tu kwamba Serikali tumejipanga kwamba timu zetu za Taifa zisiwe ombaomba kuwe na mpango mkakati kabisa kuona kwamba zinakuwa na fedha.

(b)Mikoa inafaidikaje na mpango huu wa fedha za *FIFA.* Ni kwamba mafunzo yanayotolewa kwa walimu, waamuzi vijana, mipango ya *TFF* kwa vijana yametusaidia sana kupitia katika Mikoa kuwapata vijana mbalimbali kupitia mpango huu ambao vijana 8 leo wanacheza timu ya Taifa akiwemo Shomari Kapombe, Christopher Edward, Thomas Ulimwengu, Samata wametokana na mpango huu wa *FIFA* wa kuibua vipaji ambavyo vijana hawa wanatoka katika Mikoa yetu.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ziko taarifa ambazo sio rasmi kwamba, fedha hizi zinazoletwa huwa hazitumiki kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa na kusababisha miradi hiyo kutokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, Serikali, inasema nini kuhusu taarifa hizi? Na kama ni kweli, wanachukua hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu

swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka tu nimhakikishie kwamba, Serikali, inazifuatilia fedha hizi kwa umakini na kuona kwamba, zinatumika ilivyokusudiwa. Nataka nikuthibitishie tu kwamba, *TFF* ambao ndio wanapokea fedha hizi hawajawahi kuwa na Hati Chafu wala *querry* yoyote kutokana na fedha hizi. *(Makofi)*

Na. 186

**Serikali Kutumia Gharama Kuandaa Makocha Wazawa**

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR** aliuliza:-

Serikali inatumia fedha nyingi sana kuajiri Makocha wa Kigeni, wakati nchi yetu ina Makocha wazawa wengi sana, ambao wana uwezo na upendo kwa nchi yao:-

Je, kwa nini gharama hizo zisitumike kuandaa Makocha wetu, ili kuepuka gharama za kuajiri Makocha wageni?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mbunge wa Dimani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua michango na umuhimu wa makocha Wazalendo katika kuendeleza michezo nchini. Kwa kiwango kikubwa Makocha wazawa ndio wanaofundisha timu zetu katika ngazi za Vijiji, Wilaya, Mikoa na baadhi Timu za Taifa.

Aidha, tunao Makocha wa Kigeni ambao ni wachache na si katika michezo yote. Serikali, inaendelea na Mkakati wa kuandaa Makocha Wazawa, ili hatimaye Makocha hawa, waweze kutambulika na kutumika kama yalivyo matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu wa kawaida katika Sekta ya Michezo Duniani kote kuwa, Makocha wa Kigeni katika baadhi ya michezo, ambao kimsingi wanaonekana kukubalika na kuaminika zaidi kwa wachezaji.

Aidha, kwa kutumia makocha hawa wa kigeni, Makocha Wazawa, wamekuwa wakifaidika na mafunzo mbalimbali ambayo yamekuwa yakiendeshwa na Makocha hawa wa Kigeni. Makocha wa Kigeni, wengi wamekuwa wakifundisha kwa kusaidiwa na Makocha Wazawa, ambao hufaidika kwa kujifunza mbinu mbalimbali za ufundishaji kwa kuambatana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, mafunzo mbalimbali ya Ualimu na uamuzi kwa Makocha Wazalendo hutolewa, ili kuwaongezea ujuzi katika fani.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hivi sasa kuna Makocha wangapi Tanzania, ambao wana uwezo wa kufundisha Makocha Wazalendo, hapa Tanzania? Na lini mkakati wa kuanza kuwafundisha Makocha Wazalendo utaanza? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la nyongeza, la Mheshimiwa Abdallah Sharia Amir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa hapa Tanzania, tunao Makocha wenye sifa za kufundisha Timu za Taifa, wapatao 9. Kama nilivyosema katika Jibu langu la Msingi ni kwamba, mpira kama mpira unabadilika na kwamba, kuna maendeleo katika soka, ambayo tunahitaji kupata Walimu wa Kigeni, ili hawa wenzetu waliopo ambao ni Wazawa, waweze kupata ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba, Serikali, imejipanga na ndio maana mpaka sasa Chuo chetu cha Malya, kinatoa mafunzo. Lakini pia hawa hawa Makocha waliopo hapa, kwa mfano huyu aliyekuwepo Kim Poulsen, anatambulika na *UEFA* na anaendeleza mafunzo mbalimbali kwa Makocha Wazawa, ili hatimaye waweze kufundisha Timu zetu za Taifa. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nilitaka kumwuliza Waziri kwamba, msingi wa michezo unaanzia kuanzia Shule za Msingi, Sekondari mpaka kufikia kwenye Vyuo. Mpaka sasa,

Serikali, hatujaona jitihada zozote ambazo zimeelekeza kutoa mafunzo kwa Makocha, ambao wanafundisha kwenye Shule za Msingi, licha ya kuwa wameondoa Mtaala wa Michezo katika Shule hizi za Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajenga vipi Taifa la Michezo, bila kuwa na msingi kuanzia kwa Vijana na Watoto?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatambua kwamba, michezo inaanzia huko chini. Na kama nilivyoeleza awali, tunao mpango huo na *TFF* imekuwa ikifanya kazi kwa ushiriukiano mkubwa, kuanzia na katika Shule za Msingi, Sekondari, na ndio maana tumeweza kuibua vipaji na kupata vijana katika Timu za *Under 17,* na *Under 20.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nimhakikishie tu kwamba, Serikali bado inathamini hilo na ndio maana imerudisha michezo hiyo. Iko katika *UMISHUMTA,* ipo *UMISETA,* na walimu hawa wanaofundisha katika shule hizo, wamesoma katika vyuo. Kwa mfano Malya, wana taaluma hizo za michezo. Serikali, inatambua hilo na tutaendelea kulisisitiza kuona kwamba, tunaimarisha michezo yetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mkiangalia *Order Paper* yetu ya leo, mtaona ina maswali matano (5) badala ya maswali kumi (10), kitu ambacho na mimi

nimekigundua hivi sasa. Ni kutokana na kosa ambalo limefanywa na Meza yangu hapa kwa sababu, walidhani kwa sababu, leo ni siku ya Alhamisi, kama kawaida tungeweza kuwa na Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kitu ambacho tulikwishaambiwa tangu jana kwamba, hakitakuwepo kwa sababu ya udhuru unaotokana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba tuendelee na maswali haya yaliyopo, tutarekebisha wakati mwingine. Ila haya yanayofuata, nitaongeza kidogo nyongeza, kwa wale watakaotaka.

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Wizara ya Fedha. Swali linaulizwa na Mheshimiwa David Silinde, kwa niaba yake Mheshimiwa Mustapha Akunaay.

Na. 187

**Mfumuko wa Bei Nchini**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini Serikali, imeshindwa kuzuia mfumuko wa bei nchini, uliofikia zaidi ya 20% mpaka sasa?

(b) Je, ni kwa nini thamani ya shilingi yetu inashuka mara kwa mara ikilinganishwa na sarafu za nchi nyingine kama Kenya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujib u swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Disemba, 2010 mfumuko wa bei uliongezeka kutoka 5.6% hadi 19.8% mwezi wa Disemba, 2011 na baadaye kushuka hadi 19% mwezi Machi, 2012.

Sehemu kubwa ya mfumuko wa bei, inatokana na uzalishaji na upatikanaji mdogo wa chakula katika Ukanda wa Afrika Mashariki, bei ya mafuta katika Soko la Dunia, mfumo wetu wa kuagiza bidhaa na malighafi kutoka nje, mfumuko wa bei katika baadhi ya nchi tunazofanya nazo biashara na kupanda kwa thamani za fedha za baadhi ya nchi tunazonunua bidhaa na huduma kutoka kwao, pamoja na matatizo ya mgawo wa umeme ulioathiri uzalishaji katika viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka unaoishia Disemba 2011, chakula, usafiri na nishati, vilichangia 83% ya ongezeko la mfumuko wa bei.

Sehemu kubwa ya ongezeko hili ipo nje ya uwezo wa Sera ya Fedha. Sehemu ya ongezeko la bei lenye uhusiano na Sera ya Fedha ni 17% tu, na hii ndio ambayo Sera ya Fedha, inaweza kudhibiti.

Namna bora ya kupunguza mfumuko wa bei unaotokana na changamoto za uhaba na uzalishaji mdogo wa chakula katika baadhi ya maeneo, ni kukabiliana na tatizo la kutoa chakula kutoka sehemu zenye ziada na kupeleka sehemu zenye upungufu, kuongeza uzalishaji, kupunguza gharama za uzalishaji, hususan mazao ya chakula na kudhibiti mfumo mbovu wa madalali katika usambazaji na uuzaji wa chakula.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na jibu la swali (b) hili limetokana na kuchafuka kwa Masoko ya Fedha Duniani, hususan Soko la Ulaya, kumechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa thamani ya Sarafu ya Tanzania. Wawekezaji wengi walitegemea sarafu ya *Euro,* kama mshindani mkubwa wa Dola ya Kimarekani kibiashara. Kudorora kwa uchumi wa nchi za ulaya, kumedhoofisha Sarafu ya *Euro* na hivyo wawekezaji wengi kukimbilia Dola ya Kimarekani, kama Sarafu salama.

Kwa mantiki hii, wawekezaji wengi walianza kuhamishia akiba zao kwenye soko la Kimarekani na hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya dola ya Kimarekani. Hali hii, ndio iliyosababisha thamani ya Dola kuimarika zaidi dhidi ya Sarafu nyingine Duniani na hivyo kusababisha thamani ya Sarafu nyingi kushuka, ikiwa ni pamoja na Sarafu ya Tanzania na yamkini Sarafu nyingi za Aafrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ni matumizi makubwa ya Fedha za Kigeni, ukilinganisha na mapato yatokanayo na mauzo yetu nje, tofauti ya mfumuko wa bei kati yetu na nchi tunazofanyanazo biashara, kuchelewa kutolewa kwa fedha zilizoahidiwa na Wahisani, matumizi ya dharura ya kununua mitambo ya umeme, kuongezeka kwa

mahitaji ya mafuta ya kuendeshea mitambo ya umeme na kulipa malimbikizo ya madeni ya barabara, yaliongeza sana mahitaji ya fedha za kigeni na hivyo kuweka shinikizo la kushuka kwa thamani ya shilingi.

**NAIBU SPIKA:** Hili swali ni muhimu sana kwa hivyo, litakuwa na maswali ya nyongeza kadhaa. Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, kwa kuanzia.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza. Kwa kuwa, sehemu kubwa ya mfumuko, kwa majibu ya Waziri, imetokana na uingizaji wa bidhaa kutoka nje.

Je, Serikali, ina mpango gani wa kufufua viwanda vyetu au mpango wa kujenga vingine, ili tuwe tunazalisha bidhaa zetu wenyewe hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, nchi nyingi Duniani zina hifadhi pesa zao katika kununua dhahabu na kuweka katika Benki Kuu, ili kuzuia thamani ya fedha kushuka.

Je, lini Serikali ya Tanzania, itaweka thamani ya pesa zake katika dhahabu, ili kuzuia pesa zetu zisishuke thamani kama zinavyoshuka sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu maswali mawili. Nitajibu swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, na kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anisaidie kujibu swali la nyongeza la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kufufua viwanda. Hili ni wazo zuri na Serikali, tayari imeanza kulifanyia kazi. Ikumbukwe kuwa, niliwahi kujibu swali hapa kuhusiana na viwanda vilivyobinafsishwa na jinsi ambavyo vingine vimekuwa vikiendelea vizuri na vingine vimekuwa vikisuasua.

Lengo la Serikali, kutathmnini kwa undani zaidi jinsi gani ya kufufua vile viwanda ambavyo vina uwezekano wa kuvifufua na kuboresha uzalishaji kwa vile ambavyo vimekuwa vikiendelea na uzalishaji vizuri, ili kuhakikisha kuwa, bidhaa zetu nyingi zinaongezwa ubora na thamani, kabla ya kupelekwa nje. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nyongeza ya majibu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri katika masuala yake yote aliyoyajibu. Nina uhakika kabisa hata hili, angelijibu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Akunaay, anataka kujua ni kwa nini hatuichukui dhahabu, sisi kama nchi inayozalisha dhahabu kwa wingi, tukaitumia kama *International Reserve.* Ni kweli historia inaonesha dhahabu

kwa muda mrefu, imetumika kama *reserve* ya Kitaifa. Hata sasa hivi, nchi nyingine bado zinatumia dhahabu kama *International Reserve.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kwa nini *currency* fulani au mali fulani huwa inawekwa kama akiba? Kuna sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, pamoja na kwamba, dhahabu imekuwa ikitumika kwa muda mrefu kama akiba ya Kimataifa, lakini ilifika wakati kulikuwa na mtetereko au mtikisiko wa dhahabu kama bidhaa yoyote katika masuala ya bei na *exchange rate* katika uthaminishaji.

Pamoja na hilo, tunalichukua hili kama changamoto kutizama kama *stability* ya bei ya dhahabu kimataifa itaendelea kuwa inakuwa-*stable,* yaani kuhimilika katika hali ya mabadilishano ya bei katika biashara za Kimataifa. Ikiendelea kwa muda mrefu na ikathamniniwa na ikaaminika na soko la Duniani, hivyo ilivyo sasahivi bado inaonesha ina dalili nzuri ya kuwa, kuendelea na kuthaminika kuwa *International Reserve* ya kuaminika kuliko *currency* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa dakika hii, bado tuna imani kwama, tuna uwezo wa kuendelea kuweka katika *strong currencies.* Lakini *advise* ya Mheshimiwa Akunaay, tunaichukua kama changamoto. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na sababu ambazo amezitoa Mheshimiwa Naibu Waziri, kushuka kwa Shilingi yetu ya Tanzania, lakini mimi nahisi kwamba, Shilingi ya Tanzania

inashuka kutokana na sisi wenyewe, tunaidharau shilingi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inaona jinsi watu ama Makampuni na watu wengine ambao wanatumia dola kila sehemu. Ukienda mahotelini dola, ukienda kukata tiketi za ndege dola, ukienda vocha dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sisi wenyewe tunaishusha shilingi yetu ya Tanzania.

Je, Serikali, inalieleza nini Bunge hili, kuhusu kuishusha wenyewe shilingi ya Tanzania?

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuipandisha?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili vilevile ni swali la msingi. Ni swali ambalo wananchi wengi wangependa kuliweka sawa.

Mheshimiwa naibu Spika, kama Serikali, tunatizama vitu vikubwa viwili. Kwanza, je, Sheria tuliyonayo sasa hivi, inaruhusu Mtanzania kuweka fedha katika hela za kigeni? Yaani *Foreign Exchange Act.*

Tunatizama yale mapungufu, ili tuone ni namna gani Sheria yenyewe itatusaidia kudhibiti matumizi ambayo yana-*impact* kwenye kuangamiza shilingi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, tunatizama vilevile tumeshatizama nakuona kwamba, kuna maeneo ambayo wananchi wameshayalalamikia kwa muda mrefu. Tunakaa na vyombo husika, ili tutizame namna gani

tunaweza tukalikabili hili bila kuleta athari ya mbadala. Lakini ni suala ambalo, tunalifanyia kazi sasa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa jana tulilaumiwa kwamba, watu wa nyuma kabisa hatuwaoni. Kwa hiyo, nitatoa nafasi tatu za mwisho kwenye swali hili; atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Sakaya. Hao ndio watakuwa waulizaji wa mwisho. *(Kicheko)*

Haya Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, kwa kuwa uwepo wa fedha za kigeni katika Hazina ya nchi yoyote kuweza kuimarisha sarafu ya nchi ile. Kwa kuwa biashara ya maduka ya kununua dola katika nchi yetu hayadhibitiwi vya kutosha, matokeo yake yamekuwa ni mirija ya kupeleka nchi za nje fedha za kigeni. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha udhibiti wa maduka ya kununua dola katika nchi yetu kama nchi zingine zinavyofanya?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni masuala ambayo yanagusa sana Wizara ya Fedha na ndiyo yanayoleta changamoto katika Wizara hii. Niseme kwe ufupi tuna sheria, tuna taratibu ambazo zinaongoza namna gani bureau-*De-change* zifanye kazi na vyombo husika vinavyosimamia *bureau-De-change,* mpaka sasa dakika hii taarifa tulizonazo wanasimamia vizuri. Hoja iliyopo ni hoja ya kuthibitika kwamba *bureau de-exchange* nyingi zinatumiwa kufanya kazi au kufanya tofauti na kile ambacho wameagizwa kufanywa ndivyo hoja iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utupe nafasi sisi tulifanyie kazi kupitia wasimamizi wakuu wa bureau-*De–change* ili kiutaratibu wa usimamiaji waweze kuyafuatilia malalamiko hayo ili kazi zao za *bureau-de-change* zionekane zifanye kama sheria na taratibu zinazofanyika. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona kwa sababu tumeshuhudia mchezo ambao umekuwa ukifanywa na mabenki mengi kwa kufanya *speculation* ya *interest rate* kwa ku-*peg* kulinganisha na dola na hasa tumetizama *Barclays* wakifanya mchezo huo.

Je, Mheshimiwa Waziri hadhani kwamba hata mabenki yetu yamekuwa yakifanya mchezo huo na kusababisha *inflation* kwenye pesa yetu?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako Tukufu ni kweli katika siku mbili tatu zilizopita karibu wiki sasa tumesikia tokeo lililothibitika kutoka *Barclays Bank international* lililotokea kule si lazima kuwa limetokea hapa Tanzania tunaelewa utaratibu wa *pegging interest rate* kwa kutumia *LAIBBO* yaani *Lap in the Bank Borrowing Rate* katika kuhuisha riba za kimataifa wakati mtu anakopa au anaweka.

Kwa soko la fedha la Tanzania mpaka dakika hii hilo lilikuwa halijajitokeza kwamba lilikuwa limeingia hapa Tanzania mpaka dakika hii hakuna uthibitisho ambao umeonyesha kwamba kilichotokea kutoka *Barclays Bank International* kilitu-*affect* sisi katika soko la fedha la Tanzania. Lakini suala lake bado linaibakia la msingi pale. Je,

mabenki yetu nayo hayawezi kuwa yanafanya hivyo kama ilivyotokea kwa *Barclays Bank International.* Niwape uthibitisho kwamba namna gani *interest* zetu zinapatikana hapa Tanzania, tuna soko letu la ndani ambalo mabenki yetu yanakuwa yanalifuata kwa hivyo *interest rate* wiki moja na nusu iliyopita nieleza namna gani yaani riba inavyokuwa inatengenezwa na vyombo vya fedha. *(Makofi)*

Mpaka dakika hii utaratibu ule ambao unatumika bado unatumika vilevile na kwa sababu tuna chombo ambacho kinafuatilia yaani *regulator* wa vyombo vya fedha mpaka dakika hii hatuna taarifa ya kwamba kuna hitilafu yoyote inayofanana na kilichotokea kwa *Barclays Bank Internation. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nichukue nafasi hii kuwathibitishia Wabunge na Watanzania kwamba soko letu la fedha la ndani ya Tanzania *Market System* bado liko salama na hatuna taarifa zozote ambazo zinaweza kuwa zimetuathiri kwa namna yoyote kwa sababu tuna *regulator* wetu muhimu ambaye anaangalia vyombo vya fedha na mpaka dakika hii hatuna taarifa zingine tofauti na ninachoeleza hapa ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru niweze kuuliza swali dogo moja la nyongeza kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameainisha sababu nyingi zinazosababisha mfumko wa bei hapa nchini na kwa kuwa sasa wapo wananchi wanaopata mlo mmoja kwa siku kwa sababu wanashindwa kumudu gharama za vyakula.

Pamoja na kuainisha sababu hajatoa mikakati ya ndani ya nchi ya kukabiliana na changamoto kubwa la kupanda kwa bei ya vyakula. Je, Serikali sasa imejipangaje kwa yale masuala ambayo yako ndani ya nchi kwa mfano wanaoenda kununua vyakula bure wanaenda kuchukua bei ndogo vijijini wanakuja kuuuza bei kubwa mijini. Kuna mikakati gani ya kukabiliana na yale masuala ambayo yako ndani ya uwezo wa nchi ili wananchi waweze kuondokana na tatizo kubwa la mfumko wa bei?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimia Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Sakaya, swali lake anataka kujua sasa hivi kuna mikakati gani ya msingi ambayo itahakikisha kwamba *inflation rate* inashuka chini. Ni sahihi lakini niseme tu kwa ufupi majibu aliyoyatoa Naibu Waziri yalikuwa ni mazuri na yote yalikuwa yanakidhi sababu ambazo zimetufikisha mpaka hapa. Kwanza niyarudie yale, la kwanza sababu kubwa ya mfumko wa bei kinadharia inatoka na uzalishaji kuwa mdogo kuliko mahitaji. Inapotokea hilo katika yale mahitaji ya msingi katika uchumi na uzalishaji ukawa mdogo ni lazima mfumko wa bei utatokea.

Lakini la pili, kama gharama ya uzalishaji inakuwa kubwa kupita kiasi yaani *cost of doing business* hiyo italeta athari katika bei kwa ujumla. Lakini la tatu ambalo lilikuwa dhahiri katika nchi yetu ni upungufu wa chakula katika nchi jirani ambazo zinatuzunguka na hii ilisukuma pamoja na uzalishaji wetu mzuri kuwa tukaathirika na bei zilizokuwa kubwa kuvuka mipaka.

Lakini la nne, alibainisha kabisa akasema bado tulikuwa na udhaifu wa miundombinu ya soko la ndani la vyakula. Kwa nini alisema vyakula, alisema hivyo kwa sababu katika mfumko wa bei, sehemu kubwa sana iliyosababisha bei ikaenda juu ni vyakula ambavyo ilifika *24.7percent,* sasa hii na vyakula gani ni mchele, pamoja na unga lakini pamoja na sukari.

Sasa Mheshimiwa Mbunge anasema namna gani sasa tunajitayarisha kuzuia au kupunguza, maana yake ni lazima mkakati wetu ulenge kwa kile ambacho kinatokana na mapungufu ya ndani. Mapungufu ya ndani ni mapungufu ya uzalishaji wa chakula miundombinu pamoja na uimarishaji wa soko la ndani. Tumejipanga vipi, kwanza tumejipanga katika kuzalisha kwa uwingi katika maeneo ambayo tumeyaeleza katika Bajeti yetu na uwingi huo unalenga kuzalisha kile ambacho kinasababisha *inflation* kubwa katika *component* ya chakula ni mchele na tumelenga mabonde matano ambayo tutazalisha kwa wingi mchele na wawekezaji tayari wamesha-*line up* kwa ajili ya kwenda kuwekeza pale. *(Makofi)*

Sasa tutakapokuwa tumezalisha mchele ule kwa wingi kwa hivyo component ya *inflation* inayotokana na chakula itakuwa imekuwa-*addressed*. Sasa la pili, namna gani sasa kule tunakolima mahindi yanaweza yakanunuliwa yanapoanza kuvunwa ndipo Serikali kibajeti tumejipanga kwa ajili ya *NFRA* iwe na fedha mapema wakati tuna vuna.

Lakini la tatu, ni suala la miundombinu. Mahindi yale yanalimwa mbali kutoka mikoa ambayo pengine kwa bahati mbaya inapata ukame tunajiimarisha kuona kwamba usafirishaji kutoka yale maeneo yanalima uwe

dhahiri na wa haraka kuchukua yale mahindi na kufikisha katika maeneo yale ambayo yanakuwa na upungufu wa chakula. *(Makofi)*

Kwa hiyo katika mikakati hiyo mitatu utaona kwamba *inflation* au mfumko wa bei unaotokana na chakula tutakuwa tumeukubili. Lakini ya mwisho nimesema inatokana na *cost of doing business* katika kuwekeza katika mradi wa gesi ambalo ni bomba la gesi kuja mpaka Dar es Salaam, tuna uhakika kabisa tutakapofikisha *megawatt 2000* Dar es Salaam na ile gesi ikaingia katika viwanda vinavyozalisha na tukaingiza gesi ile katika majumba ya watu vitatokea mambo mawili makubwa;

La kwanza, viwanda vingi vitapata nafasi ya kutumia gesi badala ya umeme,

La pili, watu wanaotumia umeme majumbani kwa kutumia gesi basi *cost of living* itapungua kwa sababu tunatumia *energy resources* iliyo *cheaper*. Niwaambieni Waheshimiwa Wabunge gharama inayozalisha umeme wa gesi ni wastani wa senti kumi na tatu ukilinganisha na gharama ya kuzalisha umeme kwa kutumia *fuel* yaani heavy *diesel* ambayo *kilowatt hour* moja gharama yake kati ya senti 43 mpaka senti 44.

Kwa hiyo, kwa kutumia gesi tutakuwa tume-*shoot down* ile *cost of doing business* katika Tanzania kwa hivyo *in shortrun* tukimaliza tu hilo bomba na kuweka gesi katika mtandao mkubwa basi gharama ya kufanya biashara na gharama ya mfumko wa bei tutakuwa tumeiteremsha na uzalishaji utaanza kuonekana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha vyama vyote Bungeni vyote vimepata nafasi waliosimama kuomba katika swali hili isipokuwa *NCCR* ndiyo wamekosa nafasi sasa nampa Mheshimiwa Kafulila ndiyo awe wa mwisho kabisa kwa sababu bado tuna dakika mbili, tatu.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kukumbuka *NCCR Mageuzi,* sababu kubwa ya mfumko wa bei kama Naibu Waziri alivyojibu ni mambo mawili.

Moja uzalishaji ni mdogo hasa kwenye chakula na hii Mheshimiwa Waziri lazima akiri kwamba inaashiria kwamba Serikali inafikiria kidogo kidogo sana kwamba kwa mujibu wa taarifa ya hali za uchumi, Tanzania ina takribani hekta milioni 29 na laki nne zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Afrika ina *suffer* leo kwa njaa kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa kwamba mvua haipatikani.

Lakini sisi tulikuwa na mbadala kwamba tuna takribani hekta milioni 29,400,000 ambazo zinafaa kwa umwagiliaji. Kwa miaka 50 Serikali ya CCM imewekeza kwenye hekta 400,000 tu. Kwa mantiki hiyo mtachukua miaka 3,625 ku-*invest* kwenye ardhi hii ambayo mmepewa na Mwenyezi Mungu.

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali?

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Ningependa Mheshimiwa Waziri wa Fedha atupatie majibu ya msingi moja katika eneo la uzalishaji lakini pili tunataizo la ku-*import* mpaka vitu

ambavyo ni *unnecessary* kwa mfano leo Tanzania ina import mpaka *tooth picks ...*

**WABUNGE FULANI:** Swali swaliii!

**NAIBU SPIKA:** Swali ni moja tu Mheshimiwa Kafulila.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Naoma Serikali ieleze inawezaje kupunguza *importation* mpaka ya vitu ambavyo siyo vya lazima kama *tooth picks*? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa David Kafulila, ni kweli anachokisema. Kusema kweli ni vitu vya msingi. *(Makofi)*

Lakini hoja je, Serikali inawajibika kwa kiwango gani. Kwanza ni kweli hatuwezi tukawa na uzalishaji wa kudumu wa kilimo kinachotegemea mvua, ni kweli.

Katika Bajeti nilieleza katika mabonde hayo matano ambayo tumeshafanya mazungumzo na wawekezaji na tunaendelea kuwapata wawekezaji wakubwa tunakwenda kuzalisha kwa kutumia umwagiliaji siyo kilimo kinachotumia mvua. Tunalenga kuwapata wawekezaji wakubwa watakaoshiriki na *small holder* katika kuzalisha kwa kutumia *system* ya umwagiliaji ndipo nchi itakuwa *sustainable*. Kwa hiyo, hili tayari limeshajibika.

Lakini namna gani sasa nchi inaendelea kuagiza nchi za nje kwa kutumia fedha za nje ku-*import* hata vitu ambavyo anasema vya kipuuzi, yaani havina maana inawezekana.

Lakini ni jukumu letu sisi kama nilivyoeleza kuhakikisha kabisa kwamba uwekezaji wetu unalenga kuwezesha viwanda vyetu vya ndani vizalishe na mojawapo katika Bajeti na katika *strategic plan* ya kitaifa ambayo tumewaeleza ni kuhakikisha tunapata umeme wa kutosha kama nilivyoeleza.

Ukisha kuwa na umeme wa kutosha kama nilivyoeleza wawekezaji wengi lazima watawekeza na utakuwa na viwanda kuliko kuwa na *single schedule* ambayo unazima mchana au unazima usiku kwa sababu ya kukosa umeme. *(Makofi)*

Lakini tunakoelekea tutapata umeme wa kutosha na wewe hata Mheshimiwa Mbunge ukiwa na uwezo wa kuwekeza kwenye viwanda utavutika kuwekeza kwenye viwanda kwa sababu nguvu ya umeme itakuwepo.

Kwa hivyo wawekezaji wengi mpaka tunaozungumza nao wako tayari kuwekeza ikiwa watapata uhakika umeme huu utafika Dar es Salaam kwa kutumia gesi na sisi kama Serikali tumejipanga kuleta *energy* ya umeme huo *2000 Megawatt* kuingiza Dar es Salaam na kusambaza katika *system* zote za viwanda ambazo zina *produce* na hivyo viwanda vitafanya kazi na uagizaji wa vitu vidogo vidogo visivyo na maana sisi wenyewe tutachangamka hapa nchini kwa sababu tutakuwa na uwezo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nilitaka kumwambia Mheshimiwa Kafulila tumethubutu, tumeweza na tunasonga mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nashukuru sana muda wetu wa maswali umekamilika.

Waheshimiwa Wabunge tumeweza kupata kwa bahati tu bila kudhamiria, tumeweza ku-*test* kitu kimoja ambacho tunakifikiria mara kwa mara kwamba mfumo wetu wa maswali na majibu umekuwa ni ule wa swali moja au mawili kwa Wizara na tulikuwa tunafikiria huko mbele tunakoenda kama mtaridhia huko mbele huko kutegemeana na mijadala tutakayokuwa nao huko mbele kuwa na Wizara moja au Wizara mbili kwa kipindi cha Maswali.

Ili Waziri akisimama hapa basi Wabunge mmpate nafasi ya Wizara hiyo kuweza kupata muda wa kuuliza maswali ya kutosha maana yake inaweza ikawa labda katika kipindi fulani cha Bunge, labda kwa Wizara moja kama elimu maswali mengi mnayouliza ni yale yale.

Waheshimiwa Wabunge, utaona kwamba kinachotofautiana ni jina la Mbunge tu, lakini tungeamua siku ya Wizara fulani tungejikuta kwamba tunapata faida kubwa sana kama ambavyo leo tumeona kwa Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, nimambo ambayo tuendelee kuyafikiria na tuendelee kushauriana ili tuone mbele ya safari tunafanyaje kwa kushauriana na Serikali vilevile nao waone tufanye vipi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kipindi cha maswali kimeisha na sasa ni matangazo na matangazo hayo ni kama ifuatavyo:-

Nianze na wageni kama kawaida, wageni wetu waliopo Bungeni ni pamoja na wageni nane ambao ni wageni wangu viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu *SHIVYAWATA* wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Felician Mkude, wapo hapa Dodoma kufuatilia ujumuishaji wa masuala ya watu wenye ulemavu ndani ya mipango inayojadiliwa Bungeni. Ahsanteni sana na karibuni sana hapa Bungeni. Hawa wanajishughulisha zaidi na watu wenye ulemavu wa ngozi.

Wageni 43 wa Mheshimiwa George Mkuchika, ambao ni Baraza la Madiwani kutoka Newala wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala ambao ni Mheshimiwa Chitwanga Rashid Ndembo. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani kutoka Newala, niwahakikishie Wabunge wenu wote wawili Mheshimiwa Mkuchika na Mheshimiwa Njwayo wanafanya kazi kubwa sana hapa Bungeni. Tunawakaribisheni sana hapa Dodoma mjisikie mpo nyumbani.

Pia wapo wachungaji 20 ambao ni waangalizi wa Makanisa ya *Free Pentecostal Church of Tanzania* kutoka Arusha wakiongozwa na Mchungaji Samuel Nassari, ambaye ni Baba mzazi wa Mheshimiwa Joshua Nassari. Wachungaji karibuni sana na Bwana Asifiwe! Karibuni sana Bungeni Dodoma.

Pia wapo wanafunzi 103 na Walimu wao kutoka shule ya Msingi *St. Thome* ya Dodoma, mnapendeza kweli na karibuni sana wanafunzi mjifunze Bunge lenu linavyofanya

kazi maana ninyi ndio viongozi mtakaofuata hapo baadaye. Niwaambie shule nyingine zilizopo nchini kwamba kutafuta kila inavyowezekana kupata nafasi ya kufika Bungeni ili kuwapa fursa watoto wetu kuweza kuona Bunge lao linavyofanya kazi. Karibuni sana Walimu na Wanafunzi wa *St. Thome.* (*Makofi*)

Kuna wenyeviti 34 wa Serikali za Mitaa kutoka Manispaa ya Temeke wakiongozwa na Ndugu Othman Omar, ambaye ndiye Mwenyekiti wao. Karibuni sana wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Temeke Mheshimiwa Mtemvu ambaye ni mwakilishi wako humu ndani yupo, hajambo kabisa, karibuni sana.

Wanakwaya 30 kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mnadani Dodoma, wanaweza kuwa *basement*.

Viongozi sita Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Ardhi, na Chuo cha Takwimu wakiongozwa na Rais wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Bokombe Itembe na Rais wa Chuo cha Ardhi Ndugu Matiko Chacha. Ahsanteni sana na karibuni Bungeni viongozi wote wa wanafunzi, nawahakikishia kwamba tunawapenda sana. (*Makofi*)

Wapo pia wageni wawili ya Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, kutoka Jimboni kwake Iramba Magharibi. Karibuni sana, popote walipo!

Matangazo ya kazi za kawaida ni tangazo la kikao cha Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kutoka kwa Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa John P. Lwanji. Saa saba

Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ikutane katika ukumbi namba 231 jengo la Utawala.

Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba Mjumbe wetu kwenye Chuo Kikuu Huria anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwamba viongozi wa *Open University of Tanzania* watakuwepo siku ya Jumamosi tarehe 14/7/2012 kuanzia saa 3.30 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wote mnakaribishwa kuhudhuria mkutano na viongozi wa Baraza la Chuo Kikuu Tanzania, wana ujumbe maalum kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tangazo kutoka ofisi ya utawala ya Bunge inawaomba mfike kwenye ofisi ya *CRDB* ili mpate maelezo kuhusu huduma mpya ya Benki hiyo inayohusu Bima mbalimbali ili muweze kunufaika na Bima hizo endapo mtachagua kufanya hivyo.

Nimeambiwa Wenyeviti wa Mitaa waliokuja ni pamoja na wa Jimbo la Kigamboni, ambao ni wageni wa Mheshimiwa Ndugulile, wote tunawakaribisha Dodoma. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ndogo ya Nishati na Madini Mheshimiwa Charles Mwijage anaomba Wajumbe wa Kamati Ndogo ya Nishati na Madini wakutane saa 7 Mchana katika ukumbi wa Msekwa C.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwape taarifa ifuatavyo; mtakumbuka kwamba tarehe 29 Juni hadi 8 Julai 2012 sikuwa nanyi hapa Bungeni nilikwenda Ghauteng, Jimbo la Afrika Kusini ambapo Mheshimiwa Spika alikuwa ameniteua kwenda kuongoza msafara wa Bunge letu

katika mkutano wa 43 wa Chama cha Wabunge Jumuiya ya Madola yaani *CPA Africa Region.* Wajumbe wengine nilioambatana nao ni pamoja na Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Sarah Msafiri na Abdallah Hancha Katibu wa Msafara.

Mkutano huo umeiletea sifa kubwa nchi yetu ya Tanzania na Bunge letu kwa sababu kubwa mbili. Mosi, Bunge letu ndiyo Makao Makuu ya Sekretarieti ya *CPA* Barani Afrika hivyo mkutano huu wote uliratibiwa na watumishi wetu waliokwenda wakiongozwa na Katibu wa Bunge ambaye ndiye Katibu wa *CPA Africa* Dkt. Kashillilah. Walifanya kazi nzuri sana na ninachukua fursa hii kuwapongeza kwa niaba yenu.

Waheshimiwa Wajumbe ninafurahi kuwajulisha kwamba wakati tukiwa kule palitokea fursa ya uchaguzi na katika uchaguzi huo Mheshimiwa Anne S. Makinda, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama Jumuiya ya Madola Barani Afrika. Ni heshima kubwa kwa nchi yetu na Bunge letu na kwa Mheshimiwa Spika, na kampeni hiyo niliiongoza mimi mwenyewe. Najua kwa hakika tupo pamoja katika kumpongeza Mheshiwa Spika kwa nafasi hii muhimu na heshima aliyopita na kwa jinsi hiyo nchi yetu itakuwa mwenyeji wetu wa Mkutano wa *CPA* Africa utakaofanyika hapa Tanzania mwaka 2014. Hii ni fursa nyingine muhimu kwa nchi yetu katika kujitangaza kiutalii na kunufaika kiuchumi.

Kwa hiyo, nawaagiza Watumishi wa Bunge watakaokuwa wenyeji wa mkutano huo wajiandae kwa maandalizi kabambe ili tuendelee kuiletea heshima nchi yetu ya Tanzania. Mwisho wa taarifa yangu. (*Kicheko*)

Katibu tuendelee na hatua inayofuata!

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Kuna Mbunge amesimama, nafunga orodha, ni mmoja tu. Mheshimiwa Mwigulu Mchemba!

**MHE. MWIGULU L. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuomba mwongozo kupitia kanuni ya 68(7) inayosema;

"Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yanaweza yakatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala wa Ofisi ya Rais uliofanyika hapa Bungeni, Mbunge wa Jimbo la Ubungo Mheshimiwa John J. Mnyika alinituhumu kwa majina yangu na mimi *personally* kwamba nahusika kwenye tuhuma za *EPA* na hizo siku saba alizopewa zimekwisha wiki hii. Kwa kuwa, tuhuma hizo zimeishia Wiki hii naichukulia kwamba ni mapema na nilikuwa naomba mwongozo wako kwa kuwa jambo hili ukweli wake upo dhahidi Bunge lako Tukufu linajua na Watanzania wanajua kwamba wakati tuhuma za *EPA* zinatokea mimi nilikuwa Mwanafunzi wa Chuo Kikuu na nilikuwa bado sijaajiriwa *BOT.* Lakini pia na nilipoajiriwa nilikuwa nafanya kazi ambazo zinahusiana na uandishi wa *report* za kila mwezi pamoja na kila robo mwaka pamoja na mwaka.

Kwa hiyo, tuhuma hizi zilikuwa zimelenga kunivunjia heshima kwa makusudi, heshima kwa wananchi wangu wa Iramba, heshima kwa chama changu wanaoniamini sana na heshima kwa Watanzania.

Kwa hiyo, naomba mwongozo wako inapotokea jambo linafanywa kwa makusudi nijue kama linakubalika na kiti chako kitoe maelekezo kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Nilikuona Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kiti chako kimuelekeze Mheshimiwa Mbunge juu ya matumizi halali ya mwongozo wa Spika kwa mujibu wa kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 68(7) inahusu jambo ambalo limetokea mapema kwenye kikao kinachoendelea. Sasa hili jambo ambalo Mheshimiwa Mbunge analizungumzia lilitokea wiki iliyopita, hiyo ni moja.

Lakini pili, kuna maelekezo tayari yaliyotolewa na kiti chako kwamba Mheshimiwa Mnyika alete maelezo ya uthibitisho kwa kiti chako, maelekezo yalishatolewa kwa hiyo, ningefikiri ni jambo la busara tu kusubiri ofisi yako iseme kama imepata majibu au haijapata. Sasa anachotaka huyu anaomba mwongozo wa kitu gani wakati tayari mwongozo ulishatolewa kwamba Mheshimiwa Mnyika alete maelezo kwa Mheshimiwa Spika, kama siyo kuzungumza hili kuonekana umezungumza ni kitu gani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nianze na hili la Mnadhimu Mkuu wa Upinzani Mheshimiwa Tundu Lissu la kanuni na mimi nirudie maana wetu tunaitumia sana kanuni ya 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema.

Niliwahi kusimama wakati fulani nikasema kwamba katika baadhi ya maeneo ambayo mtu anaweza kufikiri kwama ina upungufu mojawapo ni hii, kwa sababu iliishia kusema mapema, ilitaka kufikiri kama anavyotaka kusema Mheshimiwa Tundu Lissu lakini sasa ile mapema huwezi kui-*qualify* mapema vipi, kwa wakati gani? Kwa hiyo, mpaka tutakaporekebisha kanuni zetu ndipo na ninyi mkikubali mkiridhia ndipo tutaifunga tuone iwe mapema kiasi gani. Lakini kwa kadri tuishivyo kwa sasa itabidi hiyo mapema iendelee kuwa mapema hiyo pana zaidi. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Lakini la pili kabla sijaenda kwa Mheshimiwa Mwigulu katika mwongozo wake, Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi sana kama viongozi wa Bunge hapa tumejitahidi sana kuwaomba kwamba unaposimama na kumtuhumu mtu na wakati mwingine kwa jina na kudai ushahidi unao kujiepusha sana na jambo hilo labda kama kweli una ushahidi dhahiri kuhusu jambo hilo.

Baadhi mmetusikia na baadhi wamekuwa bado hawasikii katika jambo hilo ambalo ni uvunjifu mkubwa sana wa kanuni na wa haki za binadamu na haki za watu wengine.

Niwahakikishie tu kwamba wale waliokwishasema tangu Bunge hili lianze na kutamba humu ndani kwamba wana ushahidi wa jambo fulani. Hakuna hata mmoja ambaye amekamilisha ushahidi hapa mezani, hayupo! Sasa hili jambo si jambo sawasawa na wengine wapo kwenye vyombo vya habari wakijitangaza kwamba wametoa ushahidi kitu ambacho si sawa, Mbunge huwezi kuwa ni mtu ambaye unatoa maneno huku na huku na maneno ambayo si sawasawa, si vizuri hata kidogo na niwahakikishie hata kwenye mitandao mnakokwenda huko tunasoma yote yale na wengine tunasononeka kuona Mbunge unasema uongo na unaandika uongo yaani unasambaza uongo, si mwenendo sahihi na huu ni mwenendo mpya katika Bunge letu. Mbunge ni mtu mwenye heshima katika jamii ni vizuri kila kauli yako iendane na uhakika wa jambo, tukikuomba kwamba toa neno, kama kweli umeteleza basi litoe kisha uendelee lakini uking’ang’ana kama ushahidi unao basi ushahidi ule uulete.

Sasa, kwa hili la Mheshimiwa Mchemba aliotaka mwongozo wangu ni kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba siku hiyo Mheshimiwa Mnyika alidai kwamba kuna kashfa inayoitwa *EPA* na Mheshimiwa Mwigulu Mchemba ni mmoja wa watuhumiwa, na kwa hiyo alitakiwa alete ushahidi.Kuna maandisi ameandika ya utangulizi lakini wala si ushahidi wa hilo, na kwa kuwa siku saba zimepita sasa mwongozo wangu ni huu ufuatao, kwamba sasa nalipeleka katika Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, ataandikiwa barua Mheshimiwa Mnyika ya kumfahamisha hilo na Kamati hiyo sasa ndiyo itakayoshughulikia ushahidi huo wa kuthibitisha kwamba Mheshimiwa Mwigulu anayesema kwamba alikuwa Chuo Kikuu wakati huo naye kumbe alikuwa anahusika na wizi wa fedha za *EPA.* Huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi)*

Tunaendelea na uchangiaji kama kawaida na mchangiaji wetu wa kwanza alitangaza tangu jana ambaye ni Mheshimiwa Esther Matiko na atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki S. Lulida.

Mheshimiwa Esther N. Matiko!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Katika hotuba ya Bajeti ya Ardhi, Nyumba na Makazi kadri muda utakavyoruhusu nahisi nitachangia maeneo manne. Nitachangia kwenye eneo la makazi, migogoro ya ardhi na fidia kwa wananchi, pango la za nyumba ada na matumizi ya fukwe zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kabisa na ninakubaliana na dhana nzima ya kuboresha makazi Tanzania kupitia *National Housing.* Lakini ninatatizwa na wanavyotueleza kwamba ujenzi wa nyumba za bei nafuu ningependa kupata ufafanuzi, huu ujenzi wa nyumba za bei nafuu unawa-*target* wananchi wa kada ipi? Kwa maana wanaopata kipato kipi? Isije ikawa kwamba wanajenga nyumba za bei nafuu ambazo wanaziita za bei nafuu lakini wanafaidika watu wenye fedha. Ninapenda katika majumuisho Waziri atueleze kwa takwimu nyumba zilizojengwa ni wananchiwa kada ya chini wangapi wameshafaidika na hizo nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nyumba zinazodaiwa ni za bei nafuu kiuhalisia siyo za bei nafuu. Ukiangalia nyumba ambayo inauzwa kwa shilingi milioni 47 nafikiri juzi walituonyesha katika *presentation* yao, wangapi wana uwezo wa kununua nyumba ile? Kwanza ni ndogo ina kama *square metre 56,* ukipata Mtanzania mwenye fedha za kujenga kiuhalisia anaweza akagharimia labda shilingi milioni 32 au 34. Nataka kujua, Wabunge wameeleza kwamba kigezo kimojawapo kinachochangia ukubwa wa bei zile ni ongezeko la thamani yaani *VAT.* Lakini kuna ongezeko la thamani na pia Serikali ina *charge capital gain tax* nayo pia nafikiri inaongeza gharama ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naelewa kwamba *National Housing* wanakopa fedha kwa maana wanadaiwa riba, nataka kujua *profit* wanayoiweka kwenye zile nyumba wanazojenga, isije ikawa ni *super profit* ambayo inawakandamiza wananchi wa kawaida.

Kwa hiyo, naomba dhana nzima kama kweli wanataka wawasaidie wananchi wa Tanzania wenye kipato cha chini wasio na uwezo wa kuweza kujenga nyumba kwa mkupuo au kwa wakati mmoja waweke kabisa dhamira kuu kwa kuondoa hiyo *VAT, Capital gains* na kuangalia gharama kwa ujumla wake kwa sababu pia ukiangalia nyumba inayouzwa kwa shilingi milioni mia moja kama Mtanzania wa Kawaida ana fedha kiuhalisia akiijenga nyumba ile itagharimu labda shilingi milioni 70 au 80. Kwa hiyo, naomba waangalie hili suala na wakifanyie kazi vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali ina dhamira kubwa ya kuboresha makazi ya Tanzania na makazi bora hu8wa ni kigezo kimojawapo cha uchumi, ambapo kwa kuangalia makazi katika nchi husika au jamii husika, kwa sababu wanasema wanapitia *National Housing,* ni kuendeleza makazimimi nahisi haitoshi, waangalie pia kwa Mtanzania mmoja mmoja kwa sababu *National Housing* haiwezi kwenda mpaka vijijini na hata huku mijini kwenyewe itachukua muda kuweza kujenga nyumba ambazo zitakidhi mahitaji kwenye miji yote. Ninashauri kwamba tuangalie pia ni kwa jinsi gani tutamsaidia Mtanzania mkulima, mfanyabiashara na mfanyakazi anayepata kipato cha chini kwa kuondoa kodi za kwenye vifaa vya ujenzi. Tuondoe kodi au tuangalie ni jinsi gani tunaweza tuka-*subsdise* tutoe ruzuku kama tunavyotoa kwenye kilimo na kadhalika. Hii itamsaidia Mtanzania mmoja mmoja kuweza kujipatia nyumba ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia mamlaka ya kudhibiti kodi za pango. Ni kweli hii ni kero kubwa na watu wengi ambao tunaathirika hapa ni wale

ambao wanaanza kazi, wafanyakazi ambao wamefanya kazi kwa siku nyingi lakini kipato chao ni kidogo na watu ambao hawana uwezo wa kujenga nyumba. Hii Mamlaka ya kudhibiti kodi ya pango ni muhimu sana katika nchi yetu na tuangalie sasa kwamba kuna umuhimu wa kukileta ili kiweze kuwasaidia Watanzania wa kada ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye matumizi ya fukwe zetu. Jana niliona Mheshimiwa Sakaya amegusia kwamba yeye amekwenda Brazil ameona fukwe za kule, wananchi wanakuwa wanapata *access* ya kwenda ku-*enjoy* na kuondoa *depression.* Lakini kule Brazil ni mbali mfano ni hapahapa nchi ya Afrika Mashariki, ukienda Mombasa na Mheshimiwa Waziri alikuwa Nairobi Kenya nafikiri ametembelea sana kule. Mahoteli ya kule hata kama yapo kwenye fukwe bado yanatoa *access* kwa *public* kwenda ku-*enjoy* fukwe zao, kubadilishana mawazo na kadhalika, ni tofauti na hapa kwetu ukienda kwenye hoteli za kule unachajiwa fedha shilingi 8,000/= au 10,000/= mimi nafikiri si vema kwa Tanzania tuiangalie na si kwa fukwe tu.

Kwenye Bajeti ya mwaka jana ya Waziri alijaribu kusema kwamba atajaribu kujenga bustani maeneo mbalimbali kwa Watanzania na watoto wao kuweza kwenda kupumzika, sijaona *implementation* yake na kwenye Bajeti ya mwaka huu pia sijaona kama ameiweka. Kwa hiyo, ningepata ufafanuzi kwa hiyo pia. Nirudi sasa kwenye migororo ya ardhi na fidia kwa wananchi. Kumekuwa na migogoro ya ardhi mingi, niliweka swali hapa mwaka 2011 kuhusu Susuni, Kijiji cha Nyabiongo, Kiongera na Ikoma kwa upande wa Rorya ambapo kuna wananchi raia wa Kenya wamekuja na kujimilikisha ardhi kwenye

eneo lile na Mheshimiwa Naibu Waziri alisema atafuatilia lakini mpaka leo hii hajafanya hivyo. Ninapenda kujua ni kwa nini haijafanyika kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna wananchi wa Kijiji cha Buhemba eneo la *FDC,* Kemoge na Biombwi Wilayani Tarime na wameshapeleka malalamiko yao kwa Waziri kwamba walitozwa fedha ya upimaji wa viwanja kuanzia mwaka 2003/2004 shilingi 40,000/= mpaka 70,000/= lakini mpaka leo hii hawajapimiwa viwanja na cha ajabu wamepewa watu wengine kwamba wanatakiwa walipie shilling 930,000/= mpaka shilingi milioni 3. Kwa sababu Waziri ana hiyo barua ninapenda kwenye majumuisho wananchi wajue ni hatua gani zinachukuliwa ili waweze kupata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumekuwa na mgogoro wa siku nyingi sana tangu mwaka 2007 kati ya wananchi wa *Consolti* na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Wale watu wamezuiliwa kufanya shughuli zao za maendeleo kwa miaka sita sasa. Hawakati mti, hawalimi hata choo kikibomoka hawaruhusiwi kujenga. Sasa tunataka tujue kwamba wanalipwa fidia au hawalipwi fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu Nyamongo fidia ni ndogo sana. Naibu Waziri wa Nishati alisema kwamba wanalipwa dola 22,000 lakini unakuta ni shilingi milioni nne (4) mpaka saba linalipwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther ni kengele ya pili!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kweli! Aisee!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, hapa mezani wananihakikishia kwamba ni kengele ya pili.

Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa na afya njema na niwatakie kheri Waislamu wote Tanzania na duniani kote duniani, kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ujao na Mwenyezi Mungu awajaalie kwa kuwapa nguvu na imani waendelee kufunga katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru na nimpongeze Waziri wa Ardhi Mama Tibaijuka na Naibu Waziri wake Bwana Ole Medeye kwa kazi nzito waliyokuwa nayo na juhudi kubwa wanazozifanya kwa kutaka kuisaidia Tanzania hii ifike katika mwelekeo ambao wananchi wanakuwa na imani naye na aweze kuwasaidia Watanzania.

Nitakosa shukrani kama sitamshukuru Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba Tanzania *(National Housing Corporation (NHC).* Katika miaka mitatu mimi nilikuwa mimi ni mpinzani wa *National Housing,* nilikuwa nahoji, hili ni shirika la taifa siyo shirika la watu binafsi? *(Makofi)*

Lakini sasa hivi ananionyesha dira ya kuonyesha *National Housing* ni Shirika la Taifa. Kwa kweli sifa kubwa zimetokea ndani ya Bunge hili kumpongeza Mkurugenzi huyu, yuko *committed* na ni *hard working.* Hivyo ninampongeza sana kwa dhati.

Lakini kwa idhini ya Waziri wa Ardhi ninaomba Mkurugenzi niende naye Lindi akaione Lindi halafu na sisi tupate majumba ya *National Housing* na wananchi wa Lindi waweze kufaidika. Tuna maeneo ya kutosha na tunahitaji na watu wa Lindi nao wafaidike kwa kupata nafasi za nyumba na wafanyakazi wanaokwenda Lindi na *morale* kufanya kazi Lindi.

Lakini kwenye sifa kama hizi changamoto hazikosekani, wakati wa enzi za Mwalimu kulikuwa na nyumba za Makabwela, na walijengewa Makabwela Magomeni, Temeke, Kinondoni na kadhalika na katika kila Mkoa kulikuwa na nyumba kwa ajili ya Makabwela.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii amwelekeze Mkurugenzi wa *National Housing* atenge maeneo kwa ajili ya Makabwela na mfano hai nimeuona Soweto Afrika Kusini. Soweto kuna majumba ya watu wenye uwezo wa *class* ya kati na watu wa *class* ya juu lakini na watu wa chini vilevile wamejengewa majumba ambayo na wao yanawasaidia. Akienda Soweto na akaona hali ya Soweto ana uwezo mkubwa wa kuwasaidia Makabwela wa Tanzania wakapata mahali pa kuweza kuishi lakini mfumo wa sasa hivi unawasaidia watu wa kiwango cha kati na kuendelea mbele.

Hii haikubaliki ni lazima na watu wa chini wapiganaji na walioiokoa nchi hii katika kupata uhuru na wao wapate kipaumbele katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la wageni kupata kipaumbele na kuwa na nafasi kubwa ya ardhi nchi hii kuliko wazawa. Hii ni sumu! Na sumu hii inakuja katika neno uwekezaji na wanakuja kwa kuhakikisha huko kwao wamekosa ardhi wanakuja kuchukua ardhi kubwa sana Tanzania na wanapata maelekezo baadhi ya wafanyakazi na watendaji ambao wana ubinafsi hawatakia kuisaidia hii nchi na wamechukua fukwe kuanzia Pangani mpaka Mtwara.

Katika kuchukua hizi fukwe wamekuwa madalali hawazitumii kikamilifu wameziweka kwa ajili ya udalali. Lakini changamoto zaidi ni kuuliza kwamba je usalama wa nchi uko wapi kama fukwe zinachukuliwa na wageni? Nchi inakuwa wapi wakiona wageni wanachukua nafasi za fukwe? Fukwe ni sehemu nyeti inabidi Tanzania yenyewe iangalie suala la fukwe, lakini fukwe zipo chini ya wageni. Ninamwomba Waziri aliangalie hilo suala na alipe changamoto kwa ajili ya kuweka usalama wa nchi uwe katika tahadhari ya hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la Makurunge, eneo ambalo wanataka kuweka kiwanda cha Sukari na mimi ni mdau wa Hifadhi ya Taifa ya *TANAPA.*

Mwaka 2005 Septemba Hifadhi ya Sadan ilipewa hati kuwa ndiyo mmiliki wa hifadhi ya Sadani na amepewa *GN* Namba 281, huyu mwekezaji amekuja juzi ameomba eneo la kulima Miwa, mimi sikatai uwekezaji lakini amechukua eneo mpaka ndani ya hifadhi, lakini ana *power* kuliko Serikali, mimi hapo napata kigugumizi. Nitatoa mfano.

Katika kuingia ndani ya hifadhi amechukua eneo ambalo ni mapito ya wanyama kwenda kunywa maji ndani ya mto Wami. Amechukua eneo ambalo ni *ecological system, eneo* ambapo Viboko na Wanyama wengine wanaishi humo ndani. Lakini yeye amechukua eneo juzi lakini ana hati ambayo imeingia mpaka ndani na hili suala Katibu Mkuu analifahamu na baada ya kwenda kusema anasema kwamba huyu Bwana amekataa, hivi jamani mwekezaji anakataaje mbele ya Sheria za Serikali?

Hili linakuwa ni changamoto na kigugumizi kwa Watanzania wengi, wawekezaji wanakuja kupata hati katika miezi mitatu au sita lakini Mtanzania wa kawaida akiomba ardhi itamchukua miaka 10 hajapata Hati. Baadhi ya watendaji wanaleta ubinafsi na kuondoa uzalendo na uzawa ndani ya nchi yetu.

Ninamwomba waziri mwenye dhamana aliangalie hili kwani wanyama nao wana haki, wanahitaji kunywa maji, wanahitaji kupata chakula na pale katika uwekezaji maji machafu yataingia katika ule mto, ina maana ua kizazi cha wanyama kwa kufaidisha mtu mmoja ambaye baadaye atakuwa halipi kodi, wawekezaji wa Tanzania wengi wao hawalipi kodi wamekaa hapa kwa ajili ya kutuhujumu. Hivyo, Waziri mwenye dhamana aliangalie hili na alipe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia mashamba ya Mkonge ambayo kwa muda wa miaka zaidi ya 30 haya mashamba yametelekezwa hata katika mkoa wa Lindi. Ninamwomba Waziri mwenye dhamana twende naye Lindi akayaone haya mashamba kwa muda wa miaka 30 yametupwa kuanzia Mkoa, Geza, Kikwetu na Mkwaya.

Haya mashamba yametupwa wanachi wameyasafisha wamejenga majumba mpaka wamewekewa maji na miundombinu na Serikali lakini sasa hivi wanasema haya mashamba ni yetu na wao walikuwa wanayatumia mashamba hayo kwa ajili ya kwenda kuchukua mikopo benki. Huu ni uhujumu uchumi.

Ardhi ya Mtanzania ambayo ilitunzwa kwa miaka yote wametumia pale ndiyo kijiwe chao cha kwenda kuchukulia mikopo benki, tunakwenda wapi? Ninaomba wananchi wale wasinyanyasike na mimi nikiona watanyanyasika nitashika bendera kwenda kukaa nao pamoja ili kuhakikisha hili ninasimama nalo pamoja. Naomba Mheshimiwa Waziri ulisimamie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la ada na bei za viwanja kuwa kubwa kwa watu wa chini. Leo hii nchi kuna tabaka la watu wenye uwezo na watu wasiokuwa na wezo, watu wasiokuwa na uwezo wakimbilie wapi? Leo unaambiwa bei ya kiwanja ni shilingi milioni tano au sita na alipe kwa muda wa mwezi mmoja au miezi miwili, anafanya kazi gani huyu Kabwela kuweza kuipata hiyo pesa ya kununua hicho kiwanja?

Ada ya kuangalia kiwanja chake anaambiwa ni shilingi 80,000/= hapa Mbunge anashindwa kwenda ku-*such* kwa shilingi 80,000/=.

Je, huyu Kabwela atakuwa hana nafasi. Watu wanadhulumiwa ardhi zao tayari wanatengenezwa Hati lakini kwenda kuangalia katika Wizara anaambiwa alipe shilingi 80,000/= anaipata wapi?

Ninamwomba Waziri atengeneze madeski matatu moja la watu wa chini ilikwenda kukagua viwanja vyao ili wasidhulumiwe na wajanja ambao wamefikia mahali ambapo wanawanyanyasa hawa watu ili na wao haki zao za msingi wazipate katika nchi yao ambayo wameitolea jasho na kuifikisha hapa.

Leo wageni wanakuja kuvuna ardhi kirahisi tu, ardhi ambayo ilitengenezwa miaka nenda kwa ajili yao lakini wao ndiyo wamekuwa ni *beneficiary* lakini Mtanzania wa hali ya chini ni wa kudhulumiwa kwa kwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi namwunga mkono Mama Kilango kwa Mama Chaduma ambaye alikuwa na shamba lake Kipunguni, lile shamba ni la mirathi na mume wake na kaka yake wamekaa nalo toka miaka ya 60 lakini leo wamekuja watu kumnyang'anya yule Bibi kikongwe na kumwambia wanakuja na mapanga na silaha tukae pale ili shamba na wanataja majina ya viongozi wakubwa ili kumdhulimu yule Bibi. Ni dhambi ya aina yake watu sasa hivi wamekuwa na uroho wa ardhi kuhakikisha kwamba watu ambao walikuwa na ardhi zao za asili wasizipate na wasizitumie.

Leo mji wa Dar es Salaam mpaka Kisarawe yote ni mji wa Wazaramo, yale mashamba ni yao ya asilia na wakati huo wanayapata hayo mashamba wakulikuwa hawana hati lakini leo Mama Chaduma anatolewa anaambiwa hapa siyo kwako hili shamba wanamtaja kiongozi mkubwa, naomba ninukuu na tangazo ambalo wameliandika.

Wananchi wote wa Kipunguni mchukue silaha, mapanga, visu mkalilinde shamba lile kwani lile shamba limeandikwa jina la Bwana Kikwete haiujulikani vizuri maana yake Kikwete wapo wengi, inawezekana ni Mheshimiwa au nani lakini hii wanatumia mbinu za uongo za kuwahadaa wananchi ili Bibi yule ajikute ananyanyasika katika eneo lake. *(Makofi)*

Je, Bibi kama yule mtu mzima nani atamtetea? Hivyo ni sisi tuwatetee watu kama hawa ambao wananyanyasika katika nchi hii wakinyimwa haki zao kwa kutumia wajanja, kwa kutumia wakubwa katika Halmashauri na kwa kutumia Madiwani wanakosa uzalendo kwa kuwasaidia wananchi wao. Naomba hii *document* nikukabidhi kama uthibitisho wa hili ninalolizungumza na huyu Mama Chaduma aweze kusaidiwa kama mwanamke nay eye apate haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru na ninaunga mkono asilimia mia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Ezekia Wenje atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Turky.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara ya Ardhi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyamagana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 tulipokuwa tunachangia Bajeti ya Wizara hii mimi nilitoa matatizo ya watu wa Jiji la Mwanza maeneo mengi ambayo kuna migogoro ya ardhi nikasema maeneo kama Luchelele, Bugarika, Kata ya Mkolani na Ilemela kuna mgogoro mkubwa kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wanagombania ardhi na tuliongea kwa machungu kweli kweli.

Mheshimiwa Waziri aliahidi wakati alipokuwa ana *wind up* kwamba atakuja Mwanza ili pia apate fursa ya kusikia kutoka kwa wananchi malalamiko yao ni yapi. Professor aliahidi lakini ninasikitika kusema kwamba Professor alipotoa ahadi mpaka leo Professor hajawahi kuonekana Mwanza kuja kusikiliza wananchi wale na kero zao.

Sasa kama Professor mimi nilifikiri kwamba *at least the difference between a Professor and an ordinary person* ni kwamba Professor akitoa ahadi ni lazima atekeleze. Sasa kama Professor naye anatoa ahadi halafu hatekelezi, hii kwa kweli inatuvunja moyo.

Mheshimiwa Professor sitaunga mkono Bajeti yako kwa sababu ulinidanganya kwamba utakuja Mwanza kusikiliza wananchi wangu.

Mheshimiwa Profesa narudia kwamba sitaunga mkono Bajeti yako kwa sababu ulinidanganya kwamba utakuja Mwanza kusikiliza wananchi wangu ambao wana matatizo na migogoro kwenye ardhi upate kusikiliza kutoka kwao. Profesa hukuja inanisikitisha sana, sijui kipindi hiki utanipa ahadi gani tena Profesa. Lakini Profesa nitakuunga

mkono kwenye Bajeti hii kama utaniambia *specifically* utakuja Mwanza lini ili twende na wewe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje ongea na mimi Mheshimiwa.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishauri vile vile kwenye Majiji ukienda Dar es Salaam, Arusha uende Mbeya na Mwanza kuna matatizo kweli kwenye Idara ya Ardhi na tulishauri kwamba Afisa Ardhi ambao wako kwenye Halmashauri zile ikiwezekana waripoti moja kwa moja Wizarani ili Wizara iweze ku-*oversee directly* matatizo na kusimamia Maafisa Ardhi kwa sababu wao kwa kiasi kikubwa ni chanzo cha migogoro ya ardhi kwenye hizi Halmashauri. Lalini mpaka sasas hatujaona utekelezaji wa hili mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi kwa mfano Mwanza ninakotoka au Jiji wanapima ardhi wakishapima ardhi ya watu wanauziwa watu wengine yule mwenye ardhi ambayo alikuwa anamiliki lile eneo bado yuko kwenye kiwanja kile kile anaweza akakaa hata miaka mitano (5) hajapewa fidia haruhusiwi kupaendeleza, haruhusiwi kutengeneza pale kama nyumba inavuja, haruhusiwi kufanya kitu chochote. Kwa hiyo, tunawahimiza wananchi kwa stahili kama hizi.

Kwa hiyo, tunaomba kuanzia sasa Wizara itoe maelekezo kama Halmashauri au kama Wizara yenyewe haijaandaa fedha kwa nini muende kupima ardhi za watu

halafu mnachukua miaka 5 pasipo kuwapa fidia, hii inahumiza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine Mwanza ni mji wa kwanza Tanzania unaokuwa kwa kasi kubwa na hii hatuhitaji *research* hata wewe unaelewa. Sasa nilitegemea kwa mji kama Mwanza unaokua kwa kasi kubwa mtatusaidia kupata fedha kwa ajili ya kurasimisha makazi na kwa ajili ya kupima viwanja vingi zaidi ili mji wetu uwe na mpangilio uwe *organised,* uwe mji wa kisasa ambao unaendana na ukuaji huo jinsi Mwanza inavyokua leo.

Sasa Halmashauri yetu haina *capacity* ya kutosha kwa maana fedha ya kurasimisha makazi na kupanga ule mji kwa maana ya kupima kwa kasi hiyo inavyotakiwa. Sasa tunaomba kama Serikali itasaidia kwenye Halmashauri yetu fedha nyingi zaidi kufanya hili zoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi nchi hii ni pale ambapo ardhi ya watu inapimwa bila ya wao kushirikishwa. Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamezungumzia hilo naomba kama inawezekana iwekwe sheria pale ambapo hata kama kuna ardhi wanakijiji inaenda kuchukuliwa inaenda kupimwa wawe kwanza washirikishwe kikao kikae wajadiliane ridhaa yao ipatikane ndiyo upimaji au mradi wowote unaotaka kufanyiwa kwenye ardhi yao ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo mengi ya ardhi jimboni kwangu, kwa mfano kuna sehemu kwenye Kata ya Buhongwa wananchi wameishi pale toka miaka yote wanaishi hapo, leo *all over sudden* wanaambiwa eti wahame eti ni eneo la *NDC.* Wameishi hapo toka

wamezaliwa wako hapo leo wanataka wahamishwe kwamba ni eneo la *NDC* na *NDC* ilikuwa wapi na kwamba wananchi wameishi mpaka wamejenga na *NDC* ilikuwa wapi? Haya ndiyo mambo yanayoleta migogoro na naomba Waziri achukue hata kama ni siku moja tu aje Mwanza shida iliyokuwa hapa ni kwamba Waziri anakaa Dar es Salaam anaomba taarifa kutoka Halmashauri anapewa taarifa ya Halmashauri tu ndio anaifanyia kazi bila kusikiliza upande wa pili wa watu wanaolalamika ambao ni wananchi.

Hili tatizo ni lazima muwasikilize wananchi ili mpate pande zote mbili ili hata kama ni maamuzi mnafanya yawe ni maamuzi ya haki zaidi, hakuna Mahakama inayohukumu watu bila kusikiliza pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri ardhi ndio rasilimali kwa Watanzania walio wengi. Uwe vijijini hata unapoishi mjini. Lakini ardhi ya nyumbani kwenu ni rasilimali kubwa mlionayo. Naomba nitoe ushauri kwamba hawa wawekezaji wanaokuja mara wengine wanaitwa *Agreco* na mara nyingine wanaitwa akina nani kama wanakuja kuchukua ardhi kwa nini sheria isitekelezwe.

Sasa badala ya kuuziwa kwa wananchi au Serikali iliingia nao *share* kwa hiyo sisi tunaingia na ardhi ndiyo inakuwa *part of the capital* yetu tunayoingia nayo kwenye *share only* ili kama wanafanya *production* basi faida itakayopatikana hata kama itakuwa tunagawana asilimia 20 tu ndiyo inabaki kwenye hivyo vijiji ili kuendeleza vijiji, kuliko leo tunachukua ardhi jumla jumla halafu tunamwuzia unampa *lease* ya miaka 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme juzi hapa tumeona hapa kwenye vyombo vya habari majengo yanabomolewa Dar es Salaam halafu watu wanapiga makofi eti kisa watu wamejenga ufukweni. Nauliza hivi kipindi watu hawa walikuwa wanajenga mpaka maghorofa Dar es Salaam Serikali ilikuwa wapi, hawa watu walijenga wana Hati mpaka wana leseni kutoka Halmashauri za kujenga yale majengo Serikali ilikuwa wapi, kwa vile mna-*apply* sheria *selectively*.

Kama hawa watu walipewa Hati na Halmashauri hawa watu mpaka majengo yao yameenda yakawa-*approved* na Halmashauri kwamba wajenge maghorofa wakajenga tunasema wamejenga ufukweni hawa watu waliotoa hivyo vibali mnawachukuliwa hatua gani? Hawa wafanyakazi waliotoa vibali kwa hawa watu kujenga mmewachukulia hatua gani?

Leo mnaenda mnabomoa maghorofa ya watu bado mnasheherekea hapa mnapiga makofi hii nini hii dhambi. Watu wanajenga Serikali mnajificha, mtu anajenga miaka kumi mpaka anaishi miaka kumi halafu unaenda unabomoa ghorofa yake mnawavizia ni nchi gani hii ya kuvizianaviziana, hao waliotoa vibali vya watu kujenga wako wapi wenyewe mmewachukulia hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa Bungeni nasikia Waziri mmoja amejenga hoja hapa eti lile jengo la *TANESCO* Makao Makuu lazima libomolewe. Hii nchi yaani mnasubiri jengo linajengwa kwa fedha za walipa kodi, jengo kubwa kama lile Serikali ilikuwa wapi wakati wa kipindi hicho yawezekana huyu Waziri yeye hakuwemo lakini Serikali *is an instutituon* ilikuwepo *The Government was*

*there, you guys you were sleeping* watu wanajenga mpaka ghorofa wanamaliza halafu leo ndio unasema mnakwenda kubomoa na mnapiga makofi. Mnaendeshaje nchi kwa kuvizianaviziana kulipizana kisasi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, jukumu la Serikali ni kusaidia wananchi wasifanye makosa sio kujificha wafanye makosa halafu aende kubomoa halafu unasheherekea. Mnakuja hapa mnapiga makofi eti mnabomoa maghorofa ya watu mnafikiri ni sifa. Hizi ni dalili za Serikali sasa inayodidimia inayotafuta *cheap popularity* za kuvunja vunja majengo ya watu mnajificha wanajenga ni dalili kwamba mmeshindwa kazi ni dalili kwamba kuna rushwa ile iliyokithiri kwenye *system* yenu ya ardhi na ndiyo maana wengine wanatoa vibali kwa watu wanajenga maghorofa nyie mnajificha hamchukuwi hatua mwishowe mnaenda kubomoa, hii sio haki. Mlikuwa wapi kipindi wanajenga halafu leo mnakuja hapa mnasheherekea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wenje tunakushukuru sana na hii saa huwa inajua kweli maana yake alikokuwa anaelekea Mheshimiwa Wenje. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Salim Hassan Abdulla Turky atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Rashid Nundu.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLA TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Watawallah* kutujalia kuamka salama kuweza kuhudhuria kikao cha leo. Pia nichukue fursa hii kuwapongeza waumini wote kwa

Mfungo unaotukaribia *inshallah* Mwenyezi Mungu ajalie Ramadhani iwe ya kheri na ibada njema.

Baada ya hayo naomba sana pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba zao nzuri walizozileta hapa ambazo kwa kweli zinatufanya tuhamasike na kupongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Yale matarajio ambayo watu wengi tulikuwa nayo kwamba mama huyu alikotokea na alikopewa Wizara hii ile imani inaanza kuonekana, kwa hivyo nampongeza sana kwa fursa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nataka nitoe usemi unaosema: "Usiache Mbachao kwa Msala upitao". *National Housing Corporation* bahati nzuri wanafanya kazi nzuri sana ya kuendeleza Shirika na kwa kweli huko tunakoelekea mwanga unaonekana kwamba tutafanikiwa. Lakini usemi wangu unarudi kwamba usiache mbachao kwa msala upitao na mali ya kurithi mara nyingi hupotea bila ya kuwa na ile heshima ya kuilinda.

Nikisema hivyo nina maana kwamba tuna mipango mizuri ya kuelekea mbele, lakini haya majengo ambayo tumeyarithi ebu tuyatazame yalivyo, tuyatazame mazingira yake na *National Housing* jinsi inavyojipanga kwenda mbele bila ya kugeuka nyuma ikatazama hawa wapangaji ambao wamewapa nguvu hizo kwa sababu mimi naamini sasa hivi kama wanaheshimika katika mabenki ni kwa sababu ya majengo waliorithi.

Sasa ikiwa yule ambaye amekuwezesha unamdharau jamani tutaweza kufika safari yetu, nikiwa na maana kwamba pale Upanga ilikuwa ni eneo moja ambalo

Watanzania tunajionea ufahari sana kwamba majumba kwa wakati ule yalikuwa yamejengwa pale yalikuwa mazuri, bustani nzuri, barabara nzuri, lakini leo ukifika Upanga ukatembelea sehemu ile kwa kweli utaanza kuona kwamba sehemu hiyo imetupwa vibaya sana na ndio hapo ninapoanza kuwa na wasiwasi kwamba kwa nini hatuvienzi vyetu au vile kwa sababu tumevirithi tunaona hatuna haja navyo. Kwa sababu leo ukipita Upanga utashangaa mashimo na maji na uchafu wote unaoujua wewe huko pale mji ambao leo miaka 15 au 20 ulikuwa ni mji wa historia, mji unapendeza. Huo ni mfano mmoja tu lakini kuna mifano mingi kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumesikia kwamba *NHC* mnapojenga mnaangalia mazingira yote ya barabara, maji, umeme sasa hizi pia nyumba zenu mnawajibika pia kuangalia sehemu hizo ziboreshwe namna gani na ili Dar es Salaam ipendeze namna gani au miji ambayo iko kama hiyo ipendeze. Wazo langu kwenu ni kwamba mbali na nyie kwamba mnajenga majumba mapya mna barabara zenu na hizi pia mnatakiwa mchangie katika Mfuko wa Barabara labda kwa kupitia Serikali za Mitaa.

Lakini sio nyie peke yenu tu pia na wale watu ambao wanajenga maghorofa sasa hivi, utakuta mtu anajenga ghorofa la shilingi bilioni 10 au 15 lakini likiisha lile ghorofa ukitazama hiyo barabara ya kuelekea hapo nyumbani utashangaa.

Sasa jamani hawa watu sisi pia tunayo haki ya kukaa nao tukazungumza kwamba kuwe na mchango wa kuchangia barabara hizo kwa sababu hao wapangaji pia

watatumia barabara hizo. Kwa maana hiyo ninatoa wito kabisa tushirikiane kuboresha mji wetu na hili Shirika la *NHC* mjipange vizuri sana mtakapokuja mtupe majibu mazuri tuone kwamba tunaweza kuboresha vipi miji yetu hapa nchini Tanzania.

Mfano mdogo sasa hivi kwamba kuna barabara mbili tatu za Upanga zimetiwa lami tayari *traffic* imepungua vizuri sana watu wanazitumia barabara zile fikiria kama pale pote pakitiwa lami patakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoka hapo Kariakoo. Kariakoo sasa hivi ndio mji mpya unajengwa unapendeza. Lakini naona kuna *NHC role* yake kubwa sana wanaweza kufanya Kariakoo pamoja na kuwa mjin pakavutia zaidi. Kwa sababu majengo mengi sana yapo *NHC* la kushangaza kwamba hawana *plan* hata moja ambayo tumeiona kwamba wako tayari katika nyumba zao mbili tatu ambazo ziko Kariakoo.

Kama hawana nyumba Kariakoo basi wanunue lakini wahakikishe wanawekeza katika kujenga maegesho (*parking).* Nyumba za kuegesha magari, hilo ni jambo muhimu sana na litaondosha msongamano wote na kwa sababu wao wana uwezo mkubwa. Majumba mengi wanayo basi hili jambo walibebe kwa nguvu zote kuhakikisha Kariakoo mjini tunapata maegesho. Aidha tuone uwezekano wa sehemu zote hizo ambazo tuna matatizo ya maegesho ya magari tuwe na maegesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya *parking* basi sasa hivi *parking* za kuweka barabarani jamani zimepitwa

na wakati tuanze kujenga maghorofa ambayo yanachukua *parking*.

Kwa hivyo napendekeza *NHC* wakija hapa watupe majibu kwamba wamejipanga vipi katika kuondosha shida hiyo ya wananchi. Kwa mfano pale Kariakoo tukijenga majengo manne, matano kwa kila *angle* tukahakikisha magari hayakai barabarani basi hii adha iliyopo sasa hivi ya kupita Kariakoo itaondoka mara moja. Kwa hivyo wakati mnakuja kutujibu naomba hili lipatiwe majibu mazuri sana ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo naomba kuchangia ni uwekezaji katika nchi yetu na ardhi. Wawekezaji wanapokuja nchini wanaangalia maeneo ambayo wanataka kuwekeza, wananchi wa eneo lile wakishasikia kwamba pale pana uwekezaji basi kuna wajanja wanatoka mjini wanaelekea maeneo hayo wanayanunua baada ya ile *project* kupitishwa.

Sasa ukienda kulipa fidia wewe unakutana na mtu ambaye sio kabisa amekuja mtu mpya amenunua *site* ile katika muda wa miezi minne mitano iliyopita wakati wewe *project* yako tayari pengine ina miezi minane. Sasa la kushangaza hawa watu wanaenda kununua maeneo yale sio kwa sababu ya kusaidia bali ni kudumaza maendeleo yetu. Kwa sababu fidia ambayo Serikali imeweka ya kulipwa utakapoenda kwake masharti anayokwambia na anakwambia mimi nimenunua eneo hili kwa sababu hii hii wakati Halmashauri inajua kwamba *plan* iliyokuwepo pale ni ipi na inaeleweka lakini wanashirikiana na wajanja fulani katika Halmashauri hizo kuwapa maeneo yale kwa sababu na wao wanakatiwa vitu vidogo. Naomba sana hili

litazamwe na kama kuna mradi ulipitishwa tayari katika eneo husika na Halmashauri ilikubali halafu mtu akaenda akanunua eneo katika eneo husika naomba ile fidia aliyolipa yeye kwa yule aliyemhamisha ndiyo ichukuliwe na yeye alipwe, hii itakomesha ujanja huu na uwekezaji nchini utakua kwa nguvu. Naomba sana hili litazamwe vizuri sana, nafikiri nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo naomba nizungumze ni kwamba katika utoaji wa Hati za ardhi. Kwa kweli sehemu hiyo moja inaumiza sana. Unapokwenda ukapimiwa mahali ukaanza *documentation* ukifika Wizarani kwa Mkurugenzi wa kutoa Hati hizo unaweza ukakuta miaka miwili Hati yako haijatoka. Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa naomba utupe utaratibu mzima wa Hati hizo na haki zetu tuzifahamu kwa kupitia Bunge hili kwa wananchi wote tuzifahamu kwa sababu inaonekana ni sehemu moja ambayo labda kuna rushwa kubwa sana katika utoaji wa Hati hizo ndiyo maana wananchi wanahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba sana kuna kitu kinaitwa kama alivyoeleza wenzangu katika fidia hizi za ardhi kwamba wananchi wanachukua miaka mitano Halmashauri kuwalipa kwa kweli hilo ni jambo la kumtesa mwananchi na linatakiwa likomeshwe mara moja. Kama una uwezo chukua haki ardhi ya mkulima au mwananchi lakini mlipe fedha zake mara moja. Lakini kama utakaa miaka mitano kwa kupiga hesabu za *six percent* kwa kweli hapo naona tunakosea kwa sababu ardhi sasa hivi ni mali inapanda bei kila siku, kwa hivyo hili tulitazame kwa macho mawili na akili timamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru sana kwa muda wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Turky, Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, atafuatiwa na Mheshimiwa Phillipa Mturano na Mheshimiwa Said Arfi ajiandae.

**MHE. OMARI RASHID NUNDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo kadha wa kadha majirani zetu.

Kwanza kwa kunipa kauli ya kuweza kuongea leo, pili kwa sisi Watanzania kutubariki kutupa ardhi kubwa na tatu kutupa viongozi wa awali wa *TANU* ambao waliona na wakaamua tangu mwanzo kuwa ardhi hii ya Tanzania ni ardhi ya Watanzania wote kinyume cha nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napongeza Wizara, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa ushirikiano mkubwa sana ambao wametupa kutatua matatizo ya ardhi kule Tanga.

Mwezi Januari 2012 nilienda na Naibu Waziri akashughulikia masuala ya kijiji cha Pande B na akashughulikia suala la mama ambaye alidhulumiwa kiwanja chake na mfanyakazi wa ardhi. Nataka nikupe shukrani zao wananchi wa Pande B wanakushukuru sana kwa kile tulichokifanya siku ile na yule mama anakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Pande sasa hivi sementi imeshalipa shilingi milioni 400 kwa kijiji kile na wakazi wamelipwa kiasi chao. Sasa kinaendelea kushughulikia mambo mengine ambayo hayahusiani na Wizara yanahusiana na Halmashauri na kwenye Halmashauri ya Tanga tunashughulikia masuala hayo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa kijiji cha Pande B umesimamishwa, watendaji kwenye Halmashauri ambao walihusika na tuhuma hizi nao wamesimamishwa na sasa tunaangalia ziada ya kijiji kile italipwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Tanga kuna matatizo mengi na ninaona Wizara kama itakwenda tena kama tulivyofanya Januari; na Waziri au Naibu Waziri ataweza kupata kunywa mlolongo wa matatizo ambayo yako katika kila sehemu nchini. Nitataja baadhi ya vitu ambavyo bado vinahitaji kushughulikiwa. Pamoja na kuangalia mbele kuona ardhi yetu itatumikaje na mipango ambayo Wizara imeweka. Kuna wajibu pia wakuangalia nyuma, kuangalia makosa yaliyofanywa na kuona makosa hayo sasa hivi yanarekebishwaje. Kwa sababu yakirundikana huko mbele ya safari kupanga matumizi ya ardhi yetu itakuwa ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika. makosa yaliyofanywa ni pamoja na ufukwe wa mwambao ambao msemaji wa pili aliyepita hapa aliliongelea hilo. Tanga tatizo hilo lipo, ardhi ya ufukwe mzima wa Tanga umechukuliwa na watu wanaojiita wawekezaji kwa bei duni na kwa ulaghai kwa watu ambao walikaa kule. Mpaka sasa sehemu hizo hazijafanywa chochote. Tungeomba kabisa Sheria hususan zinazotumika kuhakikisha kuwa watu ambao wanahodhi

sehemu bila kuzitumia kama ambavyo wameahidi na wakati mwingine kutokuzitumia kwa njia yoyote nyingine sehemu hizo kama hazirudishiwi vijijini basi Serikali izichukue ili ziweze kutumika kwa matumizi yanayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashamba ya mkonge ambayo yameongelewa na nadhani hili la mashamba ya mkonge tumeshalichukulia hatua na nadhani sio kubwa sana. Sio kubwa zaidi ya mashamba ambayo yana vijiji vilikuwemo ndani tangu zamani. Sio kubwa zaidi ya sehemu ambazo zina vijiji ambavyo vilikuwemo ndani tangu zamani. Sehemu ya Kichangani kwa mfano katika Kata ya Maweni. Kijiji kikubwa ambacho ni kama Mji mdogo kina wakazi na mpaka maofisi ya Serikali lakini kijiji chote kile kinamilikiwa na mtu mmoja hapa Tanzania. Mimi nilitegemea kuliona jambo kama hilo Afrika Kusin, siyo Tanzania. Mtu huyo anadiriki kusema kuwa anawaruhusu wajenge, anawaruhusu wakae. Hii ni ardhi ya Tanzania sio ardhi ya mtu mmoja. Suala hilo liko hapo Kichangani. Suala hilo lipo pia Mkembe. Naomba sana Mheshimiwa Spika, Waziri au Naibu Waziri tukiweza kwenda pamoja tuliangalie hilo na tuone suluhisho lake linakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa viwanja umekuwa ni kero kubwa. Ni kero kwa sababu watu ambao mashamba yao yalikuwa yanachukuliwa ili jiji la Tanga liongezwe wanagawiwa viwanja, mtu anaweza kupewa vitatu na kuambiwa kumi vinakwenda Serikalini.

Lakini Serikalini ni Maafisa Ardhi. Wanahodhi viwanja chungu nzima na mfano mmoja aliona mwenyewe Naibu Waziri tulipokwenda pale hakuridhika yule Afisa na viwanja alivyochukua lakini alikwenda mpaka alivyomwachia

mwenye shamba. Pia akakichukua na hakutaka kukirudisha mpaka Naibu Waziri wa Ardhi alipokwenda. Hakusikiliza la mnadi swala wala la mwadhin, la Halmashauri wala la Mbunge. Sasa itabidi muende nyie mkatatue matatizo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wadhalilishaji hawa wachukuliwe hatua za kisheria, maana wameshafanya makosa na mnawajua na wamejitokeza. Kwanini hawachukuliwi hatua ili liwe ni somo kwa wengine wasije wakarudia makosa kama hayo. Matatito wanayoyafanya ni mengi na mimi ninaushahidi wa mengi, mkija kule tutaweza kuyaongea kwa pamoja. Haiyumkini mtu anapotaka kubadilisha nyumba yake katikati ya Jiji la Tanga aambiwe mahali hapo hapajapimwa halafu wampimie kwa gharama zao wakishampimia hakuna hati iliyopatikana. Halafu inabainika kuwa Hati ya kiwanja hicho aliyoomba huko nyuma miaka kumi iliyopita inakuja kuibuka inatoka tu. Afisa Ardhi anakuwa amefuata yeye akaichukua na amekaa nayo nyumba Afisa wa Ardhi. Hawa watu hawezi kuachiwa kuendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanga ni Jiji na ni Jiji ambalo nilitegemea sasa hivi liwe linashindana na Dar es Salaam lakini haiko hivyo. Pamoja na hivyo mandhari ya Jiji la Tanga na kutokuendelea bado yanaharibiwa.

Kulikuwa na zoezi la kuuza viwanda kikauzwa kiwanda cha mbolea, Kiwanda kile kina sehemu ambayo ni zaidi ya hekta 63 katikati ya sehemu ambayo ni *prime area* ya Tanga. Raskazoni ni sawasawa na *Oyster Bay* ya Jiji la Dar es Salaam. Ufikirie pale mtu aende akazungushe ukuta mkubwa hekta 63 halafu ndani kumeota miti tu hakuna

kinachoendelea. Amechukua kiwanda cha mbolea, hata mbolea hatengenezi mbolea na wala sitegemei afanye hivyo kwa sababu hilo lilikuwa ni kosa kuweka kiwanda cha mbolea katikati ya sehemu ile. Lakini amezungusha ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Novemba, 2011 nilipokwenda na Waziri wa Uchukuzi wa Uganda tulipokuwa tunaangalia tutajenga reli wapi, alishangaa akasema hii ni jela au nini? Tanga haina sehemu za watoto kucheza lakini mtu hekta 63 amezungusha ukuta na anaangaliwa tu. Kwenye Halmashauri tunataka tuliangalie hilo tuone tunafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka ya nchi yetu. Mpaka wa sisi na Malawi inabidi litafutiwe suluhisho na naomba tusiongelee mipaka ya nchi na nchi tu.

Pia naomba niongelee mipaka ndani ya nchi. Haiingii akilini leo Wilaya na Wilaya zinagombana kugombania mipaka. Kata na Kata zinagombania mipaka, n asema kugombania mipaka. Pale ambapo Halmashauri zinashindwa tungewaomba wizara mwingilie kwa sababu ninyi mna kauli kubwa na mnasikilizwa zaidi nas mna utaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaunga mkono mipango ya Wizara. Mipango ya kuboresha makazi hapo zamani kwenye miaka ya 1960 zilijengwa nyumba za *National Housing* na pia zikajengwa zile za shilingi 9,600/-.

Kwa wakati ule shilingil elfu tisa na mia sita (9,600/-) zilikuwa ni pesa nyingi sana lakini ilikuwa ni mipango ya watu kuweza kulipa. Hizi nyumba mfikirie njia ambazo watu wataweza kulipa. Msifikirie kuwa mkishajenga basi baadaye watashindwa, watakuja kunyang'anywa. Kuna mambo mengi ambayo mnaweza kuyafanya hamna muda wa kuweza kuyaongelea yote hapa. Tutakapopata muda pamoja tunaweza tukayaongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naafiki ujenzi wa bustani za Jiji. Wizara naiangalia Dar es Salaam tu, naomba ije iangalie na Tanga. Ndiyo maana nataka twende nao tuonyeshe sehemu ambazo kweli zinaweza kuwekwa bustani ikafanya mji ukaonekana kama ni mji. Twende tukaangalie tuweze kupanga pamoja. Mambo ya ujenzi wa nyumba za *National Housing* naona mmejikita sehemu nyingine. Naomba mje Tanga. Maana mnapokwenda mkasema tusijenge ufukweni na hiyo ni sababu mojawapo ambayo ilifanya mimi niingie kwenye siasa kuona watu zile mita 60 kule walikokuwa wanajaribu kutaka kujenga.

Lakini kuna vijiji ambavyo viko ufukweni. Nini hatima ya vijiji hivi, nini hatma ya mandhari ya ufukwe wa bahari ambavyo vijiji hivi viko. Basi muwe na mkakati wa kuweza kuona mtawasaidiaje wananchi hawa kujengewa nyumba sehemu ambazo watakuwa mbali na ufukwe ili kwa muda mrefu baadaye tuweze kuona kweli fukwe zetu kweli zinalindwa ipasavyo, hazitumiki kiholela. Shirika la nyumba l isaidie kuwajengea wananchi hawa sehemu stahiki.

Mheshimwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuomba Wizara ifikirie kuja tena Tanga kumaliza ile kazi ambayo tuliianza na nina hakika kabisa unaweza kuitumia Tanga kama mfano

wa kutatua matatizo, kama mfano wa kuboresha sio tu mandhari na sehemu ya Jiji lakini pia vijiji. Tanga tumeanza kwa kuona mambo ambayo waasisi wetu wa Chama cha *TANU* walifanya kuhakikisha ardhi inabaki kuwa mali ya Watanzania wote. Tumeanza kubadilisha hata baadhi ya majina ya mitaa ya miji ili tuwataje watu hao na nashukuru kuwa umeliongelea hilo. Haingii akilini kuwa Tanga hakuna mtaa unaoitwa Mwalimu Julius Nyerere, haingii akilini. Lakini watu wachache wajuzi na jana tayari barabara zimepewa majina yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Omar Nundu kama nilivyosema Mheshimiwa Philipa Mturano atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Rukia Kassim Mohamed ajiandae na Mheshimiwa Tundu Lissu atafuata. Mheshimwa Philipa Mturano hayupo. Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. SAID AMOUR ARFI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na fadhila zake nyingi na nikushukuru nawe kwa kunipa nafasi hii ya dakika kumi ambazo hazinitoshi kwa kuwa nina hoja yangu ardhi ambayo inapigwa danadana kwa takribani mwaka mzima sasa bado dhamira yangu ni kuiwasilisha tena katika Mkutano wa mwezi Oktoba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia machache nianze kwa nukuu ya Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius

Kambarage Nyerere ambayo aliitoa miaka minne kabla ya uhuru aliitoa mwaka 1958, na alisema:-

"Katika nchi kama yetu ambamo Waafrika ni maskini na wageni ni matajiri kuna uwezekano mkubwa kwamba Mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi katika miaka 80 ijayo ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasingekuwa matajiri litaibuka tabaka la Watanganyika matajiri na wajanja tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu. Katika muda mchache kutakuwa na kundi dogo la Waafrika wakiwa na ardhi na waliowengi watakuwa watwana." Mwisho wa kununukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya aliyasema Hayati Baba wa Taifa miaka 54 iliyopita miaka minne kabla ya uhuru. Alikuwa anaizungumzia Tanganyika wakati huo. Matokeo yake tunayaona leo. Pamoja na yeye alibashiri miaka 80 haijafika miaka 80 hayo aliyoyasema Mwalimu Nyerere tunayaona. Kwamba kundi la Watanzania wachache wajanja wameibuka kuhodhi ardhi kubwa na Watanzania wengi maskini wamekuwa watwana wa Watanzania wenzetu wajanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee tu mfano kule Mpanda kuna shamba maarufu linaloitwa shamba la Benki. Shamba hili nimelisemea mara kadhaa, nimeiomba Serikali kama Mheshimiwa Rais kwa mamlaka tuliyompa na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayo mamlaka ya kufuta Hati na amefanya hivyo hasa mijini kwenye makazi ya watu amewanyang'anya, amefuta Hati za miliki, inakuaje wananchi wengi ambao hawana

ardhi na wanapoomba Hati ifutwe ili waweze kupewa ardhi inakuwa kizungumkuti?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa katika hilo shamba la Benki katika Kata ya Kakese kule Mpanda kwa miaka nenda miaka rudi wamekuwa ni watwana kwa Watanzania wenzao wajanja wachache.

Wanawakodisha ardhi kwa heka moja wanalipa shilingi laki moja au gunia moja au nne za mpunga ambazo leo bei yake ni shilingi 50,000/- kwa maana kwamba anakodisha kati ya shilingi laki moja mpaka laki mbili.

Ni kuwadhulumu Watanzania ambao hawana ardhi kwa sababu tu ya wajanja wanojua mahali gani pa kupita wanahodhi ardhi kubwa ambayo hawaitumii kwa kuiendeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa na ni kero na limeendelea kupanuka na hatimaye maeneo mengine vifo vimetokea. Kule Kabage hali kadhalika, Mpanda tatizo ni la muda mrefu, watu wamehodhi ardhi matokeo yake watu wamepoteza maisha yao. Nilibahatika kumpa Mheshimiwa Spika, *CD* ya matukio ya kule Kabage na kwa sababu jambo hili bado liko chini ya uchunguzi wa Polisi sitapenda kulizungumzia sana. Lakini haya ni miongoni mwa migogoro mingi ambayo tunayo katika nchi yetu. Ni lazima hatua madhubuti zichukuliwe sasa ili kuweza kuondosha hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda nilizungumzie ni mfumo wa Serikali. Nadhani ipo haja ya Serikali ikajitathimini, ikajipima ikaona kama iko sawasawa au turudi katika mfumo ambao tulikuwa tumeuzoea.

Mamlaka mengi yamepelekwa kwenye dude moja linaloitwa TAMISEMI, limekuwa kubwa sana, linahodhi kila kitu matokeo yake linashindwa kusimamia shughuli nyingi. Leo Waziri unakuja kuomba fedha mabilioni hapa tutakupitishia Bajeti yako lakini unasimamia Sera tu. Huna mamlaka yoyote ya kisheria juu ya watumishi ambao wapo katika idara ya ardhi. Hawa watu wanawajibika kwa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri Serikali ikaangalia kwamba tuendelee na utaratibu huu ambapo Wizara haina mamlaka juu ya watumishi, huwezi kuwawajibisha, huwezi kuwahamisha. Mtu akipelekwa mahala basi ndiyo hapo hapo aende akafie hapo. Matokeo yake hawa watu ambao mmewapeleka wameshakuwa katika maeneo yale kwa takribani miaka 20 au zaidi na sasa si watumishi tena isipokuwa wana mamlaka juu ya ardhi yote, wanafanya biashara juu ya ardhi kwa kadri inavyowapendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni vizuri sasa Serikali ikaangalia ni namna gani inaweza kuangalia hii mifumo ili tuwe na mifumo ya uwajibikaji na Serikali inayowajibika. Tunapokusulubu Mheshimiwa Waziri, basi tukusulubu kwa haki. Ni makosa yanayofanywa na watendaji ambao wewe huna mamlaka nao mwenye mamlaka ni mtu mwingine.

Lakini wewe unaomba fedha hapa, tunakupa fedha, unatuma fedha, unawasilisha taarifa hapa Bungeni lakini huwezi kuzifuatilia fedha ulizoziteremsha huko chini.

Nimeona hapa katika taarifa yako uliyotugawia katika jedwali namba 9(a) linazungumzia fedha ambazo mmegawa kwa ajili ya kuendeleza kupima viwanja. Kuna zaidi ya shilingi milioni 14 mmepeleka kwenye Halmashauri ya Mji wa Mpanda fedha ambazo mnadai.

Lakini leo viwanja Mpanda ni tatizo fedha zipo matokeo yake yamekuja makampuni yanaingia ubia na idara ya Serikali kupima viwanja na kuwauzia wananchi kwa bei kubwa jambo hili kwa kweli hamwatendei haki wananchi mnawadhulumu wananchi, mnawaonea wananchi. Ni lazima muangalie sasa jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba linapima viwanja na wanawauzia wananchi kwa bei nafuu linaendelezwa. Hatuwezi kukubali kuendelea kuvumilia hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia pia utendaji kwa mfano katika jedwali namba 9 Kigoma wamepima viwanja saba tu, kwa mwaka mzima. Hivi ni kweli inawezekana mkawa na idara ya ardhi katika mji wenye changamoto nyingi kama Kigoma mkawa mmepima viwanja saba kwa mwaka? Inasikitisha sana. Lakini kwa sababu huwezi kufuatilia, huna mamlaka juu ya hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la ardhi. Mpaka sasa hivi baada ya miaka 50 hatujaweza kujua tuna ardhi akiba kiasi gani. Tunaendelea tu kukaribisha wawekezaji na kuwapa ardhi ambayo tunanyang'anyana na watu wetu. Nitolee mfano Wilaya ya Mpanda ambayo asilimia 18 ya ardhi ya Wilaya ya Mpanda ni hifadhi ya wanyama, asilimia 58 ni hifadhi ya misitu, asilimia nne (4) ni maji. Imebakia asilimia 18 idadi ya watu inaongezeka kwa

asilimia 2.9. Katika asilimia 18 iliyobaki ya ardhi nzuri inagombaniwa sasa na Serikali kupitia mlango wa wawekezaji na wananchi. Hamwatendei haki hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima kabla ya kuwakaribisha wawekezaji muangalie hiyo ardhi mtakayotaka kuwapa. Leo kuna mpango wa G8. Mbunge mmoja alisimama akasema tujipongeze sana kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi chache katika Afrika ambazo G8 imekubali kuisaidia. Si jambo la kufurahia wala si jambo la kujipongeza hili.

Hatuwezi kukubali kuuza uhuru wetu na utu wetu kwa sababu tu kwamba wakubwa wanataka ardhi yetu. Tumepata uhuru ni kwa sababu ya ardhi. Rasilimali pekee ambayo imebakia Tanzania ambayo haijauzwa kiholela ni ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusikubali ardhi yetu ikauzwa kiholela. Leo G8 wanatoa msaada lakini kupitia kwenye sekta binafsi. Hatuwezi kukubali misharti na misaada mikubwa ya wazungu hawa ambayo inaambatana na masharti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hawajaanza hata kulima kule Rufiji lakini Wamarekani haohao ambao wanataka kutupa misaada wameshamwandikia Mheshimiwa Membe barua ya kueleza kwanini meli zimeandikishwa Tanzania.

Mmarekani anataka kutuchagulia sisi marafiki katika nchi hii. Anatupa msaada kwa masharti. Kwa maana hiyo kukubali masharti ya Mmarekani ni kuuza uhuru wa nchi hii. (*Makofi*)

Ni afadhali tukabakia masikini tukatafuta njia zingine za kuwaendeleza watu wetu kuliko misaada ambayo inayofungana na masharti watu wanataka tushangilie na tusifie. Hatuwezi ni nchi tatu katika Afrika ambazo zimekubali kuuza uhuru wao kwa ajili ya misaada kutoka Marekani ninashukuru mengine nitawasilisha katika hoja yangu. (*Makofi*)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuzungumzia hii hoja ya ardhi. Sasa hivi katika nchi yetu, mfumo wetu wa Kimahakam, kwa mfano, ukienda kwenye Mahakama Kuu na Mahakama za chini kwenye Mabaraza ya Ardhi na kwingineko, hata katika Mahakama za Jinai, migogoro inayoongoza kwa kesi nyingi ni ya ardhi. Jana nilikuwa ninaongea na Waheshimiwa Majaji wanasema kwamba, kuna kesi 6,000 katika Mahakama Kuu za ardhi peke yake. Sasa hiyo ni ile ambayo imepelekwa katika mfumo wetu wa Kimahakama, imepelekwa kistaarabu, kuna migogoro mingine ambayo haiendi Mahakamani tena kwa sababu Mahakama limekuwa gulio ambalo haki inauzwa na kununuliwa na wenye uwezo wa kuinunua sasa hivi wananchi wanachukua njia ambayo imechukuliwa na wananchi waliochoka zama zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya kuchukua hatua wao wenyewe kilichoonekana Rufiji, Kilichoonekana Babati na maeneo mengine, ambako wananchi wanachukua silaha,

wanakata mapanga ni dalili ya kuonesha kwamba, migogoro inayohusiana na ardhi inazidi kuwa mikubwa, inazidi kuwa *complex* na wananchi wanakosa imani na mfumo rasmi wa kutatua hii migogoro. La pili, ni kwamba, katika zama zote, mapinduzi huwa siyo *tea party* (siyo karamu ya chai), mapinduzi huwa ni vita, mauaji na umwagaji damu. Mapinduzi kila mahali, ukiangalia kwa umakini unajua mgogoro unaosababisha mapinduzi ni ardhi siyo Mapinduzi ya Zanzibar, siyo Maumau ya Kenya, wala siyo mgogoro wa juzi wa Kenya baada ya uchaguzi wa 2007. Mapinduzi *everywhere,* vita vya ukombozi *everywhere;* Zimbabwe, China, Cuba, ukiangalia chini yake *the basis is always the land question. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafuata mfumo wa Kibepari, katika nchi hii tumeingia kwenye mfumo wa Kibepari na kwa sababu mabepari wetu ni mabepari uchwara, siyo mabepari wa viwanda, kitu ambacho mabepari uchwara na Serikali yetu vinafanya ni kufanya ukuwadi na ukuwadi maana yake siyo ule ukuwadi unaojulikana; ni kufanya kazi ya uwakala kwa wenye fedha ambao wengi ni wa Mataifa makubwa, Mataifa ya Magharibi na wanafanya uwakala kwa kuuza ardhi na rasilimali zake siyo Rukwa, siyo Umasaini kwenye Hifadhi za Taifa, *everywhere.* Serikali, Watumishi wake na mabepari uchwara wetu, kazi yao ni kufanya ukuwadi wa kuuza ardhi kwa wageni na kwa kufanya hivyo, tunaundiwa misingi ya vita ya muda mfupi ujao kwa sababu watu wetu wamechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Sekta ya Madini, mahali popote ambapo kuna mgodi wa dhahabu leo kila mahali wananchi wamenyag'anywa kwa nguvu za

silaha na Serikali ili wakabidhiwe wageni. Siyo Bulyagh'ulu, siyo *North Mara,* siyo Geita na siyo Mang'onyi Singida Mashariki ni nguvu za kijeshi zinatumika na vibepari uchwara vyetu na Serikali ambayo inajiona kwamba ni Serikali ya kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na kwa wawekezaji maana yake ni makampuni ya Magharibi ili yatengeneze fedha, wananchi wawe wakata kuni na wateka maji. *(Makofi)*

Tunatengeneza mazingira ya mapinduzi ya umwagaji wa damu siyo muda mrefu ujao na hii tusipoizungumza leo tutaizungumza lini? Mimi sitaki dhambi ya kutotimiza wajibu, ninataka wajukuu zangu wakiniuliza niwaambie tulizidiwa nguvu, lakini tulizungumza. Kwa hiyo, ni lazima tuzungumze haya masuala. Ninaomba nitoe mifano michache kwa haraka haraka; Jimboni kwangu Singida Mashariki, tunaletewa balaa, inaitwa *Shanta Mining* na hii balaa imekuwepo kabla sijawa Mbunge tangu mwaka 2005, wameingia kwa nguvu, wamechukua mashamba ya wananchi kwa nguvu, wamejenga kiwanja cha ndege kwa nguvu, wamejenga kambi kwa nguvu kwenye mashamba ya watu, wanafanya *drilling* na kufanya *exploration* kwa nguvu na kila mtu anajua siyo Waziri, siyo Mkuu wa Mkoa, siyo Mkuu wa Wilaya, siyo Polisi, kwa sababu sote tumekuwa makuwadi wa mabepari wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya *Comprador,* Wachina wanaita *Comprador* (ukuwadi) kwa Kiswahili, Marehemu Chachage alisema, makuwadi wa soko huria. Kwa hiyo, tuna mwaka wa saba wananchi hawalimi, hawajalipwa fidia, hakuna tathmini, hakuna chochote kinachofanyika, wanashindwa kulima kwa sababu sisi na Serikali yetu tumekuwa makuwadi wa soko huria, makuwadi

wa wawekezaji. Tunatengeneza mazingira ambayo wananchi sasa watasema kama Serikali ndiyo inatufanya hivi, basi tutafute namna ya kujibu na namna ambayo zama zote imefanyika ni wananchi kuchukua silaha na kudai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuna mapembe, hatuko tofauti na Wakenya, hatuko tofauti na Wazimbabwe, hatuko tofauti na Dunia nzima ambao baada ya kuchoshwa wameamua sasa liwalo na liwe kama tulivyoambiwa siku moja hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya majumuisho, mimi watu walionituma, walionichagua wanasema, ama zao, ama za *Shanta Minning* na hatutakubali tena kutishwa, hatutakubali tena kuambiwa fuateni njia hizi ambazo tunajua hazifanyi kazi kwa sababu mfumo mzima uko *rigged against* wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu vingine vinatia aibu; kampuni ya uwindaji, hati ya uwindaji kwa mujibu wa Sheria za Tanzania ni haki ya kuwinda wanyama lakini kwa sababu sisi tumekuwa makuwadi wa wawekezaji, kampuni ya kuchimba madini ya *uranium* inachimba eneo ambalo kuna mtu anawinda wanyama. Yeye ni muwekezaji halafu anaingia mkataba unaosema ...

**MWONGOZO**

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, lugha chafu katika Bunge haziruhusiwi na Kiswahili.

**NAIBU SPIKA:** Soma Kanuni kwanza.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Kanuni ya 64 kama sikosei.

**NAIBU SPIKA:** Isome.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Sina hapa lakini hiyo lugha.

**NAIBU SPIKA:** Basi Mheshimiwa Tundu Lissu endelea. *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninazungumzia Mbarag'andu huko Selous, kampuni ya madini inaingia mkataba na kampuni ya uwindaji, wote ni Wazungu, wote ni wawekezaji wanaitwa wawekezaji. Mkataba unasema vijiji vyenye ardhi vitalipwa Dola 10,000 halafu hawa wawekezaji wawindaji ambao leseni yao ni ya kuwinda wanyama watalipwa dola 6,000,000 na wataendelea kulipwa Dola 250,000 kwa muda wote ambao wachimba *uranium* hawa watakuwa kwenye hilo eneo. Sasa wenye ardhi Dola 10,000, wasiokuwa na haki yoyote juu ya ile ardhi, wana haki tu ya kuwinda swala, wana Dola milioni ngapi; kama siyo ukuwadi ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuwadi kwa wageni hawa ambao leo tunawatukuza kwa lugha ya uwekezaji; hii ni hatari, tunatengeneza mazingira ya *civil war.* Tunatengeneza mazingira ambayo wananchi wetu watasema kama hatuwezi kupata haki zetu kwa amani, kama Serikali yetu haitusikilizi, basi tutumie namna ile ile ambayo zama zote wameitumia wanaonyimwa haki na hawatakuwa wanakosea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri

atakapokuwa anafanya majumuisho, naomba vilevile ... Ooh, ahsante.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Turky.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru baada ya kuipata Kanuni. Kanuni ya 64(1)(f).

**NAIBU SPIKA:** 64 (1)(f) isome.

**MHE. SALIM H. A. TURKY:** Inasema; mchangiaji hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au kwa mtu mwingine yeyote. Lugha hapa zinazotumika za ubepari, lugha inayotumika ya ukuwadi, ukuwadi ninaoujua mimi ni mtu kumkuwadia mwanamke, mtu ambaye anafanya vitu vingine ni dalali, kwa hiyo, ninaomba lugha irekebishwe.

## T A A R I F A

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari, unatoa taarifa unampa nani na hakuna anayeongea; kaa chini. Mwongozo wangu nitautoa baadae, anaendelea Mheshimiwa Moses Machali. *(Kicheko)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Kimsingi, nitakuwa na mambo kadhaa ya kuchangia na pengine kuomba kauli ya Serikali juu mambo hayo ambayo yamekuwa yakisababisha matatizo katika maeneo mbalimbali ndani ya mipaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, ambao wamechangia tangu jana mpaka leo wanalalamikia mfumo wa upatikanaji wa ardhi na matumizi yake. Moja, ningeiomba Serikari ijaribu kufanya mabadiliko katika Wizara ya Ardhi, kwa sababu mlolongo ni mrefu sana, leo unakuta mtu ametafuta ardhi, kwa mfano, ametafuta kiwanja Kasulu Mjini, ipo shida moja Maafisa wa Ardhi wamekuwa wanawachonganisha wananchi wetu. Leo unakuta Juma amepewa kiwanja X halafu kesho Kelvin anapewa kiwanja hicho hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kuwa, huu ni uhuni ambao unafanywa na baadhi ya Maafisa Ardhi ambao siyo waadilifu. Haya yanafanyika Jimbo langu la Kasulu Mjini na Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikupigia simu nikikuuliza huyu Afisa Ardhi analindwa kwa misingi gani? Leo ukija Kasulu Mjini, utakuta kuna maeneo ambayo ni ya barabara wamegawa viwanja watu wanajenga; tunawaacha kwa misingi gani watu hawa? Nenda kwenye *open spaces,* Idara ya Ardhi katika Jimbo la Kasulu Mjini wamegawa viwanja watu wanajenga kwenye *open spaces.* Mheshimiwa Waziri nimekupigia simu nimekueleza, hakuna hatua ambayo mnachukua mnataka tufanye nini? Tutakwenda kuchukua Sheria mkononi wakati mwingine kwa sababu Serikali mnachochea migogoro miongoni mwa Wananchi wa Kasulu Mjini na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haingii akilini, mtu mmoja anajitutumua kwamba yeye ni Afisa wa Ardhi hata Viongozi ambao tumepewa dhamana na wananchi wetu tunawataarifu kwamba mtu wenu anaharibu hapa na hamumchukulii hatua; kuna nini? Kulindana huku kumetoka wapi? Watu wamekuwa wajeuri, wanathamini watu wenye fedha, watu maskini ambao wamepigika, maisha ni magumu, wananyanyasika. Hatuwezi kukubali, matokeo yake mtakuja kusikia kuwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanatangaza sasa hatutaki kuisikia Serikali kwa sababu tunawataarifu na hamchukui hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba nipate mustakabali wa Afisa wa Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na vitendo vya kugawa *open spaces* na tabia za kugawa kiwanja kimoja kwa watu wawili tofauti; kama siyo kuwachonganisha wananchi ni kitu gani. Naomba wasiogope sauti yangu kwa sababu inakera sana na ninaongea kwa hisia kwa sababu ni matatizo ya muda mrefu sana. Nimekwenda *field* mwenyewe, nimewachukua siku moja tumekwenda kushuhudia matatizo haya, majibu wanayotoa hayaeleweki, ndiyo maana nimekuletea Mheshimiwa Waziri, nitaomba nipate mustakabali wa Afisa Ardhi wa Wilaya ya Kasulu na Watumishi wengine; ni hatua gani ambazo utakwenda kuwachukulia *immediately* na kama hamtachukua tutajichukulia hatua wenyewe mimi na wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo ambalo linazungumzia suala la mfumo, watu wameiharibu Kasulu lakini wakati mwingine unajikuta wakati wa kutafuta haki unakwenda mpaka huko juu. Ningeomba kuishauri Serikali

ijaribu kufanya vitu vingine tuweze kumaliza huko huko, siyo kila kitu mpaka twende juu. Nchi hii ni kubwa sana, Waziri wewe ni mmoja, leo tukikutaka kwamba mimi Machali ninakuhitaji njoo ufanye ziara Kasulu Mjini, Mheshimiwa Tundu Lissu atakuhitaji uende Singida, Mheshimiwa Lukuvi naye atakutaka uende Iringa huko; utajigawa mara ngapi na Wabunge tupo zaidi ya 350. Haiwezekani, kuna vitu vingine jaribuni kukasimu madaraka Mikoani ili tuweze kumalizana huko huko kwa sababu matatizo mengine yamesababishwa na mfumo uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii dhana ambayo inahusiana na masuala ya wawekezaji na matumizi ya Ardhi ya Tanzania. Kila kitu kimekuwa kinazungumzwa kwamba, hii ardhi atapewa mwekezaji, kuwa kuna mwekezaji anakuja atawekeza pale na wawekezaji ambao tunawazungumza ni wa kutoka nje siyo wawekezaji wakubwa kutoka ndani. Tunaweka rehani na kuuza ardhi yetu ambapo baadaye tutakuja kuitafuta na tutaikosa. Serikali katika hili naomba niseme kwamba, mmedhihirisha kuwa mnaonekana mna matatizo makubwa katika suala zima la kufanya maamuzi, inaonesha kwamba mmefika mahali uwezo wa kufikiri sasa umegota mahali, hamuwezi kusema kwamba sasa tutafute suluhisho lingine kwamba sasa tufanyeje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa ya wenzetu yameamua kuanzisha makapuni ambayo yanashughulika na shughuli mbalimbali, Tanzania tunashindwa nini kuhakikisha kwamba tunaweza kuanzisha makampuni ambayo yanaweza kumilikiwa na Serikali na Wananchi wa Tanzania na Serikali inaweza ikatoa *guarantee* kwa makapuni haya ambayo yatakuwa yakimilikiwa na Serikali

yaende yaka-*invest* katika kilimo kwa sababu ardhi tunayo ya kutosha. Kuna tatizo gani mpaka kila kitu imekuwa muwekezaji anakuja, tunataka kulima labda ku-*improve* kilimo cha miwa na tuzalishe sukari mwekezaji anakuja! Kigoma kule, wamezungumza jana katika Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwamba, mmegawa hekta zipatazo 10,000 eneo la Lugufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kasulu Mjini mwaka jana mmeshuhudia aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, amekwenda kuwaondoa wananchi waliokuwa wanalima katika Mapori ya Kagerankanda ambao wamekuwa wakilima kwenye maeneo yale zaidi ya miaka 20. Kwamba, kwa sababu kuna kampuni moja inataka kuja ku-*invest* kwenye masuala ya utalii, wazawa wanapuuzwa wageni ndiyo ambao wameoneka kuwa *deal* kubwa sana, huu ni ugandamizaji na matokeo yake kesho na kesho kutwa tutawa-*term* Serikali mnachochea vurugu ndani ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachochea vurugu ndani ya Taifa hili, kwa sababu haiingii akilini katika mazingira ya kawaida wageni wanawathamini, wazawa wanawapuuza. Mbaya zaidi, siku ile nimeuliza swali hapa kwamba, Serikali iliahidi akiwepo Waziri wa Maliasili na Utalii wakati huo Mheshimiwa Ezekiel Maige kwamba, wale watu mnawaondoa halafu mtawatafutia ardhi mbadala kwa ajili ya kuendelea kuendesha shughuli za kilimo ambapo uchumi wao wanategemea kilimo. Tangu mwaka jana mpaka leo tunapozungumza ni zaidi ya miezi ya saba hakuna kitu chochote ambacho kimefanyika wala mpango hakuna. Nimemwuliza Waziri wa Kilimo amesema kwamba atalishughulikia. Mkazi mwenzangu kutoka Kigoma, hakuna

kilichofanyika, sioni mkakati wowote, tunadanganyana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu ya nini mbadala na nini hatma ya Wakulima waliokuwa wanalima katika Pori la Kagera Nkanda ambapo Halmashauri juzi imeingia mkataba ambao Mheshimiwa Buyogera aliuzungumzia vizuri sana hapa; hatujaona mnataka kufanya nini. Nini hatma ya wakulima ambao walikuwa wanalima kule ambao Serikali imewaondoa? Nini hatma ya ardhi yao ya kulima ambayo Serikali iliwaahidi na Uongozi wa Mkoa na Halmashauri ya Kasulu waliagizwa waweze kushughulikia hilo chini ya Ofisi ya DC wamefanya nini? Nitaomba nipate majibu kwa sababu wananchi wanaihitaji ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi inafanya vitu ambavyo sivyo, nitaomba majibu ya barua iliyoandikwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kuhusiana na ujenzi wa Masjala ya Ardhi Wilaya ya Kasulu. Barua yenye Kumbukumbu *No. KAS/AR/VOLUME. V/141* ya tarehe 14 mwezi wa pili mwaka 2011, iliyokuwa inamwuliza Katibu Mkuu aeleze juu ya kumalizika kwa Jengo la Masjala ya Ardhi Kasulu ambalo limesimama mpaka leo na haieleweki wanajenga. Mfumo uliotumika katika kusimamia Jengo hili ulikuwa ni wa Wizara moja kwa moja; tujiulize kazi inafanyika Kasulu wewe Katibu Mkuu unasimamia ujenzi wa jengo hili unaona kinachofanyika? Hivi kama haya yanafanyika Kasulu, yanafanyika Muleba, yanafanyika Mwanza, Katibu Mkuu utajigawa mara ngapi? Nataka nipate hatma ya Jengo hili la Masjala ya Ardhi ambayo ingeweza kusaidia watu kupata hati miliki za kimila waweze kutumia hati zao katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo inaonekana kitu kilichofanyika hapa hatujui kwanza hata lile jengo limejengwa kwa shilingi ngapi, hata Afisa wa Ardhi wa Halmashauri ya Kasulu hajui jengo lilikuwa linajengwa kwa kiasi gani. Katibu Mkuu ndiye anayesimamia yupo Dar es Salaam, kazi inafanyika Kasulu; mambo gani haya kama si kuchezeana akili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo moja la Ofisi ya Ardhi Wilaya ya Kasulu, leo kuna watu wanamiliki ardhi zao wana mashamba, ili wakupimie ardhi, Afisa Ardhi anakwambia utanipa viwanja sita ndiyo nitakupimia, ukikataa hawakupimii. Matatizo haya yapo, ndiyo maana naomba Waziri ufanye ziara katika Jimbo la Kasulu Mjini na nijue suala la kuanzishwa kwa Baraza la Wilaya la Ardhi katika Jimbo la Kasulu Mjini. Mkoa mzima wa Kigoma tuna Baraza moja tu pale Mkoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mkoa wenye wakazi zaidi ya milioni mbili unategemea nini; ukisema watu wa kutoka Kibondo waende Kigoma Mjini inawezekana vipi wengine hawana uwezo. Watu watoke Kasulu, Uvinza, Kakonko, Buhigwe, Wilaya zote hizi kwenda kutegemea Baraza moja tena hata watu ambao wanashughulikia mashauri haya ya ardhi ni wachache sana; haki itatendeka saa ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atueleze ni lini Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kasulu litaanzishwa au hata katika Wilaya nyingine, kwa sababu mrundikano wa matatizo ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze moja kwa moja kutamka hadharani kwamba, katika nchi yetu ya Tanzania, wakulima na watu wa kawaida, kitu ambacho wanaweza wakajivunia katika nchi yetu ni kuwa na ardhi. Hii ardhi naomba Serikali isiichezee, iilinde ardhi ya Watanzania kwa kiasi kikubwa.

Jambo la pili, naomba kuongelea suala la Mipaka ya Kimataifa hususan katika Jimbo langu la Tarime na Wilaya ya Rorya. Utakuta kwamba, alama za mipaka hazijulikani ziliwekwa mwaka gani na mpaka sasa hivi hazionekani na hali hii inachangia watu kutoka Kenya na wengine kutoka Tanzania wanaingiliana. Unaweza kukuta mtu amejenga choo Kenya, Tanzania amejenga nyumba ya familia yake anaishi huku. Hii inaleta matatizo, akifanya uhalifu Tanzania anakimbilia Kenya, akifanya uhalifu Kenya anakimbilia Tanzania. Suala hili linatusumbua, naomba mliangalie kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mipaka ya ardhi kati ya Wilaya ya Rorya na Tarime, Mheshimiwa Esther Matiko ameliongelea sana sitaki kuliongelea. Kila siku watu wanapigana pale kwa sababu hiyo mipaka. Naomba hilo pia tulitafakari mno. Vilevile ifahamike wazi na dhahiri kwamba, kuna suala la rushwa katika mchakato mzima wa kumilikishwa ardhi kutoka Mabaraza ya Ardhi, Halmashauri

zetu, Manispaa na mpaka kwenye Wizara yenyewe. Nafahamu kabisa kwamba, Waziri wewe ni mchapakazi, angalia ni namna gani utadhibiti suala la rushwa katika Miji yetu, Manispaa zetu na katika Wizara yenyewe hasa Manispaa ya Kinondoni. Nafikiri Waziri unalifahamu sitaki kulieleza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mwalimu Nyerere alishawahi kusema kwamba, kuongoza ni kuonesha njia, naomba kumwuliza Waziri, mpaka sasa hivi tangu uingie katika Wizara hii na tunawaangalia watu wanajenga kiholela na watu wengine wanajitwalia ardhi pasipo kupimwa; ni mbinu gani umetumia au njia zipi kuhakikisha kabisa kwamba maeneo ya miji kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, viwanja vinapimwa kabla watu hawajajenga? Hilo ni swali ambalo inabidi tukae na tulitafakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzangu wameongea sana na sasa hivi suala la umilikaji wa ardhi linatupeleka katika matabaka, hata ukienda huko vijijini, watu unaokuta wanamiliki ardhi ni wale ambao labda walikuwa Watumishi wa Serikali wamestaafu, mfano, wanajeshi na watu wengine. Watu ambao hawajapata elimu hata kidogo bado wananyang'anywa ardhi, mwisho wake wanageuka kuwa watwana wa wale watu ambao wamenunua ardhi kwao. Hilo Watanzania wenzangu popote pale walipo, Waziri kupitia Wizara yako, utoe elimu kuhusu matumizi ya ardhi katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Madini na Ardhi, wale wawekezaji wanaokuja wakishaingia ile mikataba, kwa hali ya kusikitisha sana katika Wilaya yangu

ya Tarime, kuanzia mwaka 1992 nasikia watu walikuwa wanalipwa hekta moja kwa shilingi mia moja; ni jambo la kusikitisha na mwaka jana nilipiga kelele kwamba ikiwezekana mikataba ile tuipitie tuiangalie na tukishaiangalia naomba Wizara ya Ardhi isimamie kihalali, wale ambao wanatolewa katika maeneo ambayo Mwekezaji anaendelea kuyatumia, walipwe fidia halali iwasaidie Watanzania wenzetu ambao wanataabika kutokana na lindi la umaskini unaowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napendekeza kwamba, kuna shule zetu za msingi katika Halmashauri zetu na shule zetu za sekondari za Kata, bado hazijapata hati miliki. Naomba Wizara ikishirikiana na Wizara ya Elimu, wazipatie hizo shule zetu hati miliki ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima katika jamii zetu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nataka kulizungumzia na ambalo Mheshimiwa Esther Matiko ameliongelea ni suala la mgogoro wa ardhi Wilayani Tarime. Hili Waziri naomba unisikilize kwa makini. Tumelishughulikia suala hili na aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Hussein Mwinyi, lakini tumeishia njiani. Vile vile nilikuandikia barua ambayo mpaka sasa hujaijibu na sijui utaijibu lini, kuhusiana na tatizo lililopo kule Tarime. Kwa kweli inashangaza sana; Wananchi wa Tarime wamenituma na ninavyo vielelezo kuhusu mgogoro uliopo baina ya Wanajeshi wa Nyandoto na Wananchi wa Ronsoti. Wananchi wa Tarime wamesema wamechoka, kila siku imekuwa ni mjadala tu. Mwaka jana nakumbuka swali la kwanza kabisa kuuliza Bungeni lilikuwa ni suala la migogoro ya ardhi Tarime na niliahidiwa kwamba, tutajitahidi kushirikiana na Wizara, kushirikiana na

Halmashauri, kuhakikisha tunatatua tatizo la migogoro lakini mpaka sasa ninavyoongea, hakuna hatua yoyote ile iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarime katika Mtaa wa Ronsoti, mwaka 1974 Wanajeshi wa Jeshi la Tanzania walijenga Kambi yao katika Kata moja inayoitwa Nyandoto. Mto Mori unapita katikati ya Nyandoto na Ronsoti, hapakuwepo na daraja kwenye ule mto. Kwa hiyo, mto ukafurika wananchi wakatoa hifadhi tu kwamba ninyi ni Watanzania wenzetu hifadhini mizigo yenu huku Ronsoti, baada ya hapo wakaendelea kukaa. Tumejitahidi tumejenga daraja tukawaambia jamani kwa sababu daraja lipo mnapita mnaenda kwenye Kambi yenu hameni hawataki kuhama. Wamezuia pale hakuna chochote kinachoendelea, inatia huruma sana na Wananchi wa Tarime wameniambia kabisa kwamba, tutajichukulia hatua mikononi hata kama ni wanajeshi wataua, lakini watakuwa wanadai haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombeni na natamka hadharani kwamba, wale Wanajeshi waondoke kule Ronsoti na hata ikiwezekana kuanzia leo. Ni jambo la kusikitisha. Vilevile nitumie nafasi hii kuwaonya wale wote wanaomiliki ardhi ya Tarime, ambao wamewalaghai watu wakaichukua na wakapata hati miliki ambazo si za halali, hasa Wananchi wa kule Nyandoto kuna watu wanaojiita Vigogo wanaomiliki ardhi Tarime. Mimi nawaomba kupitia Bunge hili, waachie hiyo ardhi ibaki mikononi mwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji cha Gibaso, kuna mtu amechukua ardhi kubwa karibu ekari mia tatu na kitu, utakuta amezungushia uzio hakuna chochote kinachofanyika, watu wanakosa sehemu ya kuchunga. Hii sitakubaliana nayo na huyo mwekezaji kama ni mwekezaji halali au si halali, ninachokitaka ni kwamba, kama ana mkataba, ana hati miliki au hana hati miliki, naomba hilo eneo la Gibaso arudishe kwa Wananchi wa Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, kitu ambacho napenda kusisitiza ni kwamba, migogoro mingi ya Tarime ukiachilia wizi wa mifugo ambao upo kila sehemu, lakini ardhi inachangia sana mapigano ya koo kwa koo. Ndiyo maana katika kipindi kilichopita kulikuwepo na mapigano kati ya Waanchari na Warenchoka, mlishuhudia ni kwa sababu ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtusaidie tupime ardhi Tarime, hali hii itasaidia kuepukana na migogoro ambayo siyo ya lazima. Kwa nini Miji kama Nyamwaga, Nyamongo, Komaswa na Sirari isipimwe? Kuna tatizo gani na kule tunazalisha kila siku, tunalipa kila siku kodi za Taifa, madini mengi; uwezo wa kufikiri ndiyo hatuna. Naomba Waziri hilo uliangalie na ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Waziri kwa juhudi za kuongeza eneo la bahari katika nchi ya Tanzania, hili nitakuwa sina fadhila kama sitalisema. Hali ya kumiliki ardhi kama hiyo tunaita ukabaila au ubepari itakuwa ni nzuri sana kama Tanzania tutajivutia eneo kubwa la bahari ili hata baadaye vizazi vinavyokuja vimiliki. Kwa hilo, Waziri nakupongeza kwa juhudi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naamini kabisa kwamba, kuna tatizo kubwa sana katika suala la umilikishaji wa ardhi katika sehemu zetu za Tanzania. Tunahitaji utafiti ufanyike, tuna wataalam kutoka Wizara ya Ardhi hata kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, tuangalie wale Maafisa wote wa Halmashauri ambao kwa kiasi kikubwa wanapokea rushwa kila siku, tuwachukulie hatua. Tukishafanya hayo mambo yote hapa Tanzania, naamini Watanzania wengi watakuwa na haki ya kujivunia kumiliki ardhi. Ardhi ndiyo mkombozi, imetuwezesha hata sisi kusimama katika Bunge kama hili, tumesomeshwa kupitia ardhi, wazazi wetu wamelima, wameuza mazao na tumesoma mpaka tumefikia hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi hii, kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu na Wananchi wote wa Babati Vijijini, walionipa fursa hii kuja kuzungumza na kuwatetea hapa Bungeni.

Kwanza, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Watalaam wote katika Wizara, kwa kazi nzuri na mabadiliko makubwa ya *reform* waliyoyaleta katika Wizara hii ya Ardhi; tunawapongeza sana. Tumeweza kuona mabadiliko makubwa na tunaamini kwamba, huwezi kumaliza matatizo yote kwa siku moja. Tunaomba mwendelee na juhudi hizo ili matatizo ya ardhi ndani ya nchi yetu yaishe na tuweze kuishi kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa kuanzisha na kuleta *system* ya kuweka *satellite* tuweze kupima ardhi zetu kwa kutumia *satellite imaging.* Ni mfumo ambao utaweza kuisaidia Serikali na wananchi kupata hati miliki za kimila, lakini pia kurahisisha mambo ya upimaji wa ardhi ndani ya nchi yetu. Tutakuwa tunaenda na wakati na pia mnaweza kuangalia maeneo mbalimbali mkiwa pale Dar es Salaam au hata katika Mikoa kama itakuwa imeunganishwa kuona maeneo mbalimbali ya nchi hii kwa kutumia hizo *satellite image*. Pia tunawashukuru kwa kujitahidi kutatua matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuiomba Wizara iiangalie Wilaya ya Babati Vijijini kwa umakini, kwa sababu ni Wilaya ambayo sasa hivi kuna tatizo kubwa la migogoro ya ardhi. Tuna matatizo kule ya muda mrefu ya miaka zaidi ya 25 hasa katika Bonde la Kiru na niliuliza pia wakati nachangia katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mara ya mwisho kuna tuhuma ilikuja na Mawaziri watano bado hatujapata majibu, wale wananchi na wawekezaji wanaendelea kuishi kwa hofu hawajui hatima yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapendekezo mbalimbali tumeshatoa, tunaomba yaendelee kufanyiwa kazi na kabla ya msimu kufika, watu wapatiwe majibu ili wajue wanachokifanya. Pia tatizo la mgogoro Tarangire na Vijiji vya Ayamango, Gedamari, Gedejaboni, tayari wananchi walishakubali kuanza kulipwa fidia lakini bado eneo mbadala hawajapatiwa. Tunaomba Serikali iangalie namna ya kuwapatia eneo mbadala ili na wao waweze kuhama na waweze kupatiwa ufumbuzi kwa suala la siku nyingi. Tulikuwa tunamwomba Waziri wa Maliasili, kama

anaweza kuja pale, aangalie wale wananchi waliowekwa pale kihalali wakati wa Operesheni Kijiji kama wanaweza kuangalia namna ya mipaka ikabadilishwa angalau basi waendelee kuishi katika mazingira ambayo walishayazoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tunaomba Serikali iangalie kuna mashamba mengi huko ambayo hayatumiki, kutumia kwao ni kukodishia watu wengine; kwa mfano, Mashamba ya *Breweries* kule Dareda, Shamba la *RIVACU* ambao wana mashamba mengi ndani ya Mkoa wa Arusha na Manyara na kazi yao kubwa ni kukodisha tu kinyume na sheria. Tunaomba hiyo ardhi ichukuliwe wapewe wananchi ambao wapo jirani na hapo na wana shida kubwa ya ardhi. Maeneo ya kwetu tatizo la ardhi ni kubwa sana. Tunaomba, kwa mfano, Shamba la *RIVACU* kuna vijiji ambavyo vinazungukwa na *Breweries* kama vile Vijiji vya Sigino, Kijiji cha Endasagu, Kijiji cha Dohomu, Kijiji cha Singu, vyote vile vina matatizo. Leo hii Shamba la *Breweries,* Wizara iliahidi kwamba sheria itafuatwa, lilikuwa ni Shamba la Kampuni ya *Breweries* leo limeshageuzwa limekuwa la mtu binafsi na hatujui kama sheria ilifuatwa na ni nani ambao walipitisha hiyo kwa sababu wana mgogoro? Tayari yule mtu ameshaanza kwenda mahakamani kuwafungulia mashtaka sawa na *RIVACU* walivyoanza kwenda kuwafungulia mashtaka wale watu ambao wao kutokutumia ile ardhi watu wameingilia leo wanadai kwamba ni ya kwao.

Pia wanawanyima fursa, leo hii Wabunge wote hapa tunapiga kelele kwamba, ardhi tunalipia shilingi 200 wao wanakodisha kwa shilingi 50,000 mpaka 100,000, lakini inamnyima mkulima wa kawaida ambaye anahangaika kulima. Tunataka kumpandishia kodi yeye kwa ajili ya hawa

watu ambao wanahodhi ardhi. Wale ambao wanahodhi ardhi, ardhi zao zichukuliwe lakini mkulima ambaye analima vizuri asipandishiwe kodi ili gharama za kilimo zipungue. Kuna maeneo mengine kama Mwada, wananchi wana mgogoro na Shamba la *RIVACO,* ambalo lilikuwa ni mali ya kijijil leo hii limegeuzwa tayari limeshakuwa mali ya *RIVACO*, tunaomba Serikali iingilie kati itusaidie kutatua haya matatizo. Wakati wa kubadilisha matumizi ya ardhi katika *WMA*, tunaomba elimu zaidi iendelee kutolewa ili migogoro isiendelee kukua. Tunaendelea kuipongeza Serikali, kwa Shirika la Nyumba, kwa kuwa na mtazamo mpya na uongozi mpya ambao imeonesha kwamba wapo *young* na *dynamic* na wanaongozwa na Waziri ambaye ameweza kuleta mabadiliko makubwa.

Tulikuwa tunaomba mwangalie maeneo ya wafugaji kwa sababu leo hii hakuna mahali popote walipozungumziwa. Itafika mahali itakuwa hawana pa kwenda. Maeneo ya wafugaji tusibadilishe matumizi ya ardhi zao ili wapate haki, waweze kupata haki sawa na Serikali iangalie namna ya kuwaboreshea miundombinu mbalimbali; majosho, malambo na dawa za kuogeshea. Tulikuwa tunaiomba Serikali iangalie namna ya kuboresha upatikanaji wa hati miliki za kimila. Leo hii mkisema Halmashauri zetu ndiyo ziendelee kutoa hizo hati miliki, hawana uwezo. Tunaomba Serikali iangalie mkakati, ibuni, ambapo kila ardhi ndani ya nchi yetu iweze kupimwa na tuweze kupata hati miliki ili mwananchi aweze kujiendeleza. Tunaiomba Serikali na Wizara ije na mabadiliko ya Sheria ya Fidia. Hii Sheria ya Fidia imepitwa na wakati, ni Sheria ambayo ni kandamizi. Naomba niwape mfano, eneo la Komoto pale Babati, wananchi ardhi yao ilichukuliwa kwa shilingi 300,000, sheria inasema kwamba utanilipa fidia

asilimia sita kwa kila miezi sita. Kipindi walipochukuliwa hata kama atalipwa baada ya miaka mitano, atalipwa asilimia sita, utakuta analipwa shilingi 450,000 au 500,000, lakini bei ya ardhi leo pale badala ya shilingi 300,000 ni shilingi milioni tano hadi milioni sita kwa heka. Hiyo hiyo, Halmashauri ikichukua hiyo ardhi ikigawa *plots* inapata zaidi ya shilingi milioni 11. Kwa nini huyo mwananchi asingelipwa ile fedha yote ya fidia ambayo Halmashauri inapata yeye akabaki kulipa *capital gains tax?*

Leo hii wananchi wengi wanaona ni laana kwao, kwa mfano, sehemu ikigeuzwa kuwa mji, maeneo ambayo ni kwa manufaa ya umma ikianza kupita kwao, kwa mfano shule, barabara, inakuwa ni laana kwao. Kwa nini ifikie huko; mwananchi anatakiwa kulipwa fidia halali? Pia apate na fidia ya usumbufu pamoja na kuwa yuko tayari kwa sababu hana namna ya kukataa, lakini alipwe ile haki anayostahili kulipwa. Serikali ije na sheria ya kubadilisha matumizi ya ardhi; kwa mfano makazi, leo hii maeneo yote ya kilimo muhimu yamegeuka kuwa makazi, itafika mahali hatutakuwa na maeneo ya kilimo. Pawe na Sheria Maalum, maeneo ya makazi yawe katika maeneo ambayo hayafai kwa kilimo ambapo tunaweza kupeleka miundombinu ya maji, barabara na umeme. Huko unaweza kujenga hata kama ni maeneo ya milimani au maeneo ambapo hapafai kwa kilimo. Itafika mahali tutakosa eneo la kulima.

Tuwe na Sheria ya kutokuuza ardhi kiholela ili hawa watu ambao wanatoka mijini, watu wenye uwezo, isije ikafika mahali ambapo ardhi yote ya Tanzania inamilikiwa na watu wachache na hawa waliobaki wengi ikawa ni migogoro. Tutaingia katika mgogoro ambao hatutaweza

kuuzuia. Tuwe na sheria ambayo itazuia mtu kuuza ardhi yake na tuwe na *register*, mtu akishauza ardhi yake akiwa kwenye *register* baadaye hatakuwa na haki ya kuja kukudai kwamba hajawahi kuwa na haki. Ardhi ni njia pekee ambayo unaweza kuwaachia urithi Watanzania walio wengi na hasa wale wa vijijini. Tuwape haki yao, lakini pia tuangalie sheria mbalimbali. Tunapotaka kuchimba madini au kufanya uwindaji, usimwondoe yule ambaye alikuwa juu ya ardhi, kwa sababu sheria inasema kilichopo juu ya ardhi ndiyo una haki nacho, kilichopo chini wewe huna haki nacho. Je, wakati alipokuwa hana uwezo wa kufanya utafiti huko chini au labda katika sehemu ambayo ina wanyamapori na katika maeneo ambayo yanageuzwa kuwa *WMAs* hali ilikuwaje? Iangaliwe namna ya kutoa elimu. Muhimu kuliko yote, ili migogoro yote iondoke ni kujitahidi kutoa elimu zaidi na sheria hizi zote ziwafikie wananchi.

Tunaomba Mabaraza ya Ardhi yote yawe chini ya Wizara moja; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi. Baraza za Wilaya, Kata na Vijiji ili wawajibike lakini Maafisa Ardhi wawe chini ya Wizara ya Ardhi. Leo hii Wabunge wengi wanalalamika huko chini kwamba, hao Maafisa Ardhi ndiyo wanaowauzia watu viwanja mara mbili au mara tatu. Hawawajibiki kwa Wizara, yule Afisa Ardhi anawajibika huko kwetu katika Halmashauri ambapo sisi pia ni Madiwani ambao ni Wabunge wapo chini yetu.

Ukienda kule anakwepa anasema yeye yuko Wizarani, iwekwe bayana wawajibike moja kwa moja Wizarani, kwa sababu hati zote zinatolewa moja kwa moja kutoka Wizarani. Tukifanya hivyo, sawa na wale waliofanikiwa, kwa mfano, kwenye *TANROAD* mimi naamini kwamba, matatizo

haya yatapungua. Tunaomba wakati *National Housing* inapanga mikakati, tunawakaribisha karibuni Babati, karibuni katika Miji ya Magugu, Galapo, Dareda, ni miji ambayo inaendelea kukua, muwekeze pia zaidi vijijini ili sote tunufaike na rasilimali hii. Muhimu kuliko yote, tunaendelea kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Makamishina wote, kwa kazi nzuri wanayofanya, endeleeni na msirudi nyuma.

Tunaomba Wizara hii ishirikiane na Wizara zingine zote; ya Maliasili, Kilimo, Maji na Mifugo, kuhakikisha kwamba, wanaendelea kutunza na kufuatilia vizuri zile sheria ili tuweze kutunza ardhi na matumzi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninawashukuru, tunaomba mtutatulie matatizo ya migogoro kule Babati. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI SAIDI JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, kama ilivyo ada, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye kwa mara nyingine amenipa fursa ya kuweza kuzungumza mchana huu wa leo. Kubwa zaidi, nikiwa nimepata fursa katika Wizara ambayo ni muhimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina mambo machache kweli kweli, lakini katika haya machache naomba Waziri mwenye dhamana anisikilize kwa umakini. Jambo la kwanza, napenda kuwazungumzia wazee wangu wa Kisarawe, kuna wazee ambao toka mwaka 1982 walivunjiwa majumba yao kwa ajili ya taratibu za Mipango Miji ya Mji wa Kisarawe. Bahati mbaya, toka mwaka 1982 mpaka leo hii, wale wazee hawajalipwa. Wengi wao wameshafariki, namwomba Waziri ulichukue hilo na

naomba majibu katika kuhitimisha kwako utueleze ni nini mustakabali wa wazee wangu, akina Mzee Kidevu wapo pale, akina Mzee Kizuki wapo, wanapata shida na kila siku wanahangaika. Mimi kama Mbunge wao, sijaridhika katika hilo, naomba majibu mwafaka ni lini wale wazee watalipwa. Kama utapeli umefanyika, naomba hao watu waliofanya utapeli huo wachukuliwe hatua, lakini naomba wazee haki zao zipatikane; hilo ni jambo la kwanza.

Jambo la pili, naomba kuzungumzia suala zima la mipaka. Mheshimiwa Waziri, naomba nikujulishe, Kisarawe yetu leo hii ukiiangalia kihistoria, haikuishia pale ilipo hivi sasa. Maeneo ya Kisarawe na maeneo ya kaka yangu kule Adam Malima, Mkuranga, Dar es Salaam sasa hivi inaingia katika Mkoa wa Pwani. Juzi juzi tumeshuhudia maeneo ya Ilala huko yakichukua maeneo katika Msitu wa Kazimzumbwi, nilimwuliza Mkuu wangu wa Mkoa kama taarifa anayo. Inaonekana Watendaji wa Wizara ya Ardhi, walikuja kupima maeneo yale hata bila kuwashirikisha Viongozi wenye dhamana katika Mikoa husika. Hili jambo halikubaliki, ndugu zangu majengo yale yote yanapojengwa, maana hata ushuru au gharama zote zinalipwa katika Jiji la Dar es Salaam, inauacha Mkoa wa Pwani ukiwa maskini, hatukubali katika hili. (*Makofi*)

Hii tabia ya Watendaji wanaotoka huko Wizarani wanavamia katika Mikoa ya watu bila kutoa taarifa katika ngazi husika, hatuitaki na hatuipendi. Leo hii kwa kaka yangu Adam Malima kule Mkuranga inafyonzwa, sasa hivi ukitoka Kongowe mpaka Mwandege inaonekana yote ni Dar es Salaam kumbe ukiangalia mipaka halisia haikuwa hivyo. Hali kadhalika, ukija Kibaha haikuwa hivyo. Mkoa wa Pwani, naomba muuthamini kwa hali zote. Tunaomba

heshima, msione majumba yanajengwa basi mkaona kila jumba zuri la Dar es Salaam hapana. Kama ardhi ni ya Mkoa wa Pwani, ardhi ya Kisarawe, jengo hilo lazima liende Kisarawe, liende Mkoa wa Pwani. Tunakuomba Waziri hili ulisimamie kwa kina. Hili huhitaji masihara, kwa kweli tumechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nililopenda kulizungumzia ni suala zima la mashamba pori. Naomba mnisikilize ambao mko nje ya Bunge hili, kuna watu wengi wamekuja kuvamia Kisarawe, wamekuja kuvamia Kibaha Vijijini; ndugu yangu Mheshimiwa Hamoud Jumaa amezungumza hapa kwa kina; wamekuja kuvamia maeneo yetu wameweka mashamba pori, tena wengine wamekuja kwa utapeli bila kufanya utaratibu mwingine wa kisheria, kwa sababu sheria inaeleza kwamba, mtu akichukua ekari 100, ekari 200, sheria inasema vipi, wamekuja kuvamia mashamba pori. Jana Mheshimiwa Hamoud Jum alizungumzia Kibaha Vijijini na hali hii ipo Kisarawe, ipo Mkuranga na ipo Kibaha kwa ndugu yangu Mheshimiwa Koka, maeneo yote. Jambo hili kwa Mkoa wa Pwani hatulikubali. *(Makofi)*

Wale wote ambao wana mashamba pori kule Kisarawe na ambao wameshindwa kufuata sheria, Mheshimiwa Waziri tunasema kwamba, mashamba yale tutayanyang’anya na wewe tunaomba utusaidie katika hilo. (*Makofi*)

Kubwa zaidi, napenda kuzungumzia suala zima la jatropha. Nililizungumza hili katika swali la papo kwa papo kwa Waziri Mkuu Siku ya Alhamisi, tena nilizungumza kwa uchungu sana. Nilipata masikitiko siku moja, mara baada

ya kuzungumza Mheshimiwa Waziri siku moja ulikuwa kikaoni, nilikuona katika televisheni ukiongea na wadau Wakazi wa Kisarawe wakizungumzia hili lakini ulisema huna habari. Mimi nimejua kama suala limeshafika kwa Waziri Mkuu maana yake na Waziri umeshakuwa na habari. Kisarawe tuna tatizo kubwa, kuna watu wa *Sun Biofuels* wamekuja kuchukua ardhi kwa utapeli wa maneno mazuri; wananchi watapata ajira, barabara zitatengenezwa, vituo vya afya vitajengwa, miundombinu itatengenezwa, hakuna lolote lililofanyika mpaka sasa. (*Makofi*)

Bahati mbaya, naomba niwaambie sheria ilikiukwa, kuna mtu amepewa hati miliki hata fidia hajamaliza kulipa. Kwa nini mtu apewe hati miliki bila kumaliza fidia? Nini maana yake? Maana yake amevunja sheria. Kwa hiyo, Waziri hili hatuhitaji mjadala wa aina yoyote, tunataka ardhi ya Kisarawe irudi, ifutwe hati miliki ile aliyopewa mtu wa *Sun Biofuels.* Katika hili hatutaridhika bila kuona hati miliki ile ya *Sun Biofuels* imefutwa na mitambo yote ameshaondoa. Sasa hivi anatafuta wawekezaji kitapeli, kuna mtu mmoja *Thirty Degree East,* nilizungumza hapa siku ile anatafuta watu wa kuwauzia *share* eneo limebaki Wanakisarawe hawana ardhi; nini hatima ya kizazi cha Kisarawe, miaka kumi au ishirini ijayo? Ina maana kwamba, Vijana wa Kisarawe ambao sasa hivi wapo Shule ya Msingi na walioko Sekondari, baada ya miaka kumi, ishirini, maana yake watakuwa dhalili hawana hata sehemu ya kujenga. Kwa hiyo, jambo hili haturidhiki, vijiji 11 vipo katika mazingira magumu kweli kweli. Tunaomba ardhi yetu kama mtu amepewa hati miliki bila kulipa fidia iliyokamilika, ina maana amevunja sheria na tunaomba Serikali iturudishie sisi wenyewe, tutapanga jinsi gani ardhi ile itumike kwa mustakabali wa Wananchi wa Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ninayazungumza kwa uchungu sana, nikimaanisha kwamba, Kisarawe siyo shamba la bibi; Kisarawe ina wenyewe na wenyewe ndiyo sisi na tupo hapa nia yetu ni kuwatetea Wanakisarawe na Kisarawe kwa ujumla. Bahati mbaya, ninazungumza haya kwa uchungu leo nikijua wazi kwa mfano maeneo ya Muhaga kuna wengine walikuwa madarakani humu Bungeni na wengine walikuwa na nafasi mbalimbali, wakaamua kuvamia Kisarawe na wana karibu ekari 500 mpaka ekari 1,000 kwa kuwa walitumia nafasi zao. Kwa wale waliopata ardhi ya Kisarawe kwa kutumia nafasi zao, tunasema kwamba, nafasi haijalishi kuchukua ardhi ya Kisarawe. Tunayasema haya kwa uchungu; ni kwamba kuna watu wengine wana ekari 1,000, wengine wana ekari 2,000 maeneo ya *Muhaga Reference;* hiyo ipo. Tunasema kwamba, ardhi ile ni ya Wanamuhaga, ni ya Wanakisarawe na maeneo yote kuzunguka Wilaya ya Kisarawe na hili hatuhitaji masihara hata kidogo, kwa sababu ardhi ndiyo uchumi wa Wananchi wa Wilaya ya Kisarawe. Ningeruhusiwa hapa kuna neno ningelisema lakini sitaki kulisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimezungumza hili kwa *mood* tofauti sana, nikijua kwamba Tanzania tusipokuwa makini tutawaacha wananchi wa kawaida wakiwa dhalili katika nchi yao. Nina imani udhalili huu utaletwa na baadhi ya watendaji wachache ambao ni waroho. Serikali ya Chama cha Mapinduzi imelenga kuhakisha inapambana, lakini kuna baadhi ya Watendaji wanaweza kuzitumia hizo nafasi vibaya kwa ajili ya kuiharibu Serikali yote. Naomba tuwe makini sana katika hili. Naishukuru sana Ofisi yako, pale tulikuwa na Afisa Ardhi ambaye ametusumbua kweli kweli, bahati nzuri umetupa Afisa Ardhi, kijana mmoja

anaitwa Kijiji, tunafanya naye kazi vizuri; nakupongeza katika hilo. Naye namwagiza kwamba, ahakikishe anasimamia kwa mujibu wa utaratibu wa sheria jinsi gani inataka kwa Wilaya yetu ya Kisarawe. Nashukuru san, kijana uliyetupa ni makini, tunakwenda naye kwa umakini sana katika Wilaya yetu ya Kisarawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa na hayo machache, lakini yenye uzito wa aina ya pekee. Tunasema kwamba, Kisarawe na Mkoa wa Pwani kama nilivyozungumzia, lazima tuilinde. Juzi juzi Mkuu wa Mkoa wangu alinipa ramani ya mipaka, watu wameingia mpaka kwenye Msitu wa Kazimzumbwi, tumemwuliza hata Mkuu wa Mkoa hana taarifa hiyo. Watendaji wanapima tu na majengo yakiwa mazuri wanasema haya majengo ni ya Dar es Salaam, kodi zinakwenda Dar es Salaam. Jambo hili hatuwezi kulikubali hata kidogo. Kaka yangu Mheshimiwa Malima, kwa sababu hana nafasi ya kuzungumza hapa, angekuwa na nafasi ya kuzungumza angeharabwanya kweli kweli kwa sababu linamuuma sana. Pale Kongowe sasa hivi wanaona kana kwamba yote imekuwa Dar es Salaam mpaka wanaondoka Mwandege; haiwezekani hata kidogo. Kama angekuwa anazungumza mngemsikia kabisa kishindo chake, maana Watu wa Mkoa wa Pwani sisi tumechoka kunyanyaswa katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. Siwezi kuunga mkono hoja mpaka nipate majibu halisia, ndiyo maana nimemwomba Waziri anisikilize nipate majibu ya moja kwa moja nini mustakabali wa hati miliki ya *Sun Biofuels.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na Naibu Waziri wake, jirani yangu Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kwa kazi ngumu ambayo wanaifanya. Niseme tu kwamba, miongoni mwa Wizara ambazo zina changamoto kubwa nchi hii kwa sababu matatizo yake yako katika kila kona ya Taifa letu, ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na watu hawa wawili wamekuwa wakijitahidi sana; niseme tu kama wengine walivyosema kwamba mnyonge mnyongeni lakini mpeni haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, katika mabadiliko yake ya Wakuu wa Wilaya nchi hii, Wilaya yangu ya Arumeru pia ilipata mabadiliko; na kwa kuzingatia changamoto kubwa ya ardhi ambayo ipo kwenye Jimbo langu la Arumeru Mashariki na Wilaya yetu ya Arumeru, ametuletea Mkuu wa Wilaya mpya, kijana ambaye tutakimbia pamoja, lakini vile vile ni mtaalam mzuri wa masuala ya ardhi. Kwa hiyo, kwangu hiyo ni *credit* kwa sababu Naibu Waziri wa Ardhi naye tunatokea kwenye Wilaya moja, naamini tutashirikiana kuhakikisha kwamba hizi changamoto ambazo zimekuwepo kwa miaka mingi pengine huu ndiyo wakati wa kufika mwisho sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kwa masikitiko makubwa, jana nimepigiwa simu na wananchi walikuwa wapo kwenye mazishi kwenye Kata ya Usa River na watu hawa wakaniambia wanasikitika kwa sababu walikuwa hawana sehemu ya kuzika. Walipokwenda kuzika

jana walilalamika kufukua kaburi ambalo alishazikwa mtu siku za nyuma, kwa hiyo, wakafukua wakamzika marehemu mwingine juu yake. Hii ni aibu kubwa sana kwa nchi yetu na siongei kwa maana ya ushabiki, naongea kwa sababu ni kitu kimetokea jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu ya mwaka 2011/2012, nilisema kuwa, kwenye suala la ardhi walisema kwamba, Serikali ingetayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuondoa migogoro ambayo ingekuwa chanzo cha maafa katika jamii yetu. Cha ajabu, mwaka huu tulipokuwa tunasoma hotuba yake ilionesha kwamba, kikubwa kilichofanyika, vijiji 11,000 katika nchi hii mipaka yake imekuwa *defined*. Yale matatizo makubwa maana migogoro mikubwa ya ardhi ambayo imekuwepo kwenye nchi yetu hatujaona ni hatua gani Serikali imechukua na kwa kiasi gani matatizo haya yalitatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Halima Mdee, ukurasa 28 ameonesha pale mashamba 11 kwa barua ambayo imeandikwa mwaka 1999 ambayo inaainisha mashamba 11 ambayo yako kwenye Wilaya ya Arumeru ambayo yalipata kibali cha Mheshimiwa Rais kufuta hati miliki na ili yaweze kurudi kwa wananchi. Katika mashamba haya, baadhi yake yako kwenye Jimbo langu na baadhi ya haya mashamba wananchi walichangishwa fedha ili watu waweze kurudishiwa fidia zao na yarudi kwa wananchi, lakini leo tunazungumza mwaka 2012 ikiwa ni miaka 13 baadaye bado kuna sintofahamu kubwa juu ya haya mashamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukitaka kuelewa vizuri, kwenye hotuba hii ya Msemaji Rasmi ya Kambi ya Upinzani Bungeni, mwisho kabisa kule ameweka kiambatanisho cha hiyo barua ipo na nafikiri Mheshimiwa Waziri ameiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu kitu kimoja. Wakati wa majumuisho ya Wizara hii, napenda Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri watuambie, watupe *clarification* ya kutosha kwenye mashamba yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wa-*note down* Shamba la Madira, Shamba la Mito Miwili, Shamba la Aga Khan, Shamba la Karamu, Shamba la Valeska, Shamba la Karangai *Sugar Estate,* Shamba la Dolly ambalo limesababisha maafa juzi; Shamba la Maweni lililopo Kata ya Kikwe; Shamba la Machumba na Shamba la Magadirisho, Shamba la Naic, Usa River na Shamba la Duluti *Coffee Estate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni miongoni mwa mashamba makubwa kwenye Jimbo langu ambayo mpaka leo tunapozungumza yameshikiliwa na walowezi na mengi yake hayajaendelezwa, yamekuwa ni vichaka. Halafu inasikitisha kwamba hapa yuko mtu anamiliki ekari 4,000 za ardhi, hajaziendeleza, hazilimwi, hazifanyiwi chochote, halafu nje kuna mwananchi ambaye hana sehemu ya kulima mchicha, halafu leo tunasema eti kwa sababu hawa watu wanamiliki mashamba hayo kihalali tuwaache waendelee kumiliki kihalali. Ni aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Shamba la Machumba kwamba Kijiji ambacho kinatokana na shamba

hili hakina shule na hakina sehemu ya kujenga Shule ya Msingi, lakini kuna mtu ana ekari nyingi ziko hapo, wamebadilisha na matumizi na zingine hazitumiki, tunasema anamiliki kihalali Kisheria tumuache. Hivi hizi Sheria si tumetunga sisi? Haya mashamba si tumewapa sisi? Ardhi ya Tanzania si ni mali ya Serikali sio mali ya mtu binafsi. Inakuwaje sasa watu wanamiliki mashamba makubwa wanayaacha wameyatelekeza, wengine wamekwenda nje ya nchi, halafu leo wananchi wakitaka ardhi tunasema wanafanya vurugu?

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea hapa juzi, nikasema tangu mwaka 1952, Arumeru walimtuma Mtanganyika wa kwanza kwenda Umoja wa Mataifa *UN* alikuwa ni Japhet Kiriko, lakini ilikuwa ni kwa sababu ya Meru *Land Case Disputes* ya miaka ya hamsini. Leo ni mwaka 2012 bado migogoro iko pale pale haijapata utatuzi. Madiwani wetu wamefanya kazi, niliongea juzi hapa, Madiwani mwaka jana wakaunda Kamati, ikiwa na wataalam ndani yake, wakatembelea mashamba yote na wakaandika mapendekezo. Yamepelekwa kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili yafike Wizarani, mpaka leo hii hatujapata majibu. Sasa wakati mwingine mpaka tunawachosha watu, tunawachosha Madiwani na Wataalam pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niondoke hapa, niende kwenye suala la matumzi ya ardhi. Kuna Shamba linaitwa *Dolly* na hili nitalizungumzia sana, kwa sababu pia nimeshaongea na Waziri na Naibu Waziri kuhusu hili shamba. Hili shamba lilikuwa ni kwa ajili ya kilimo. Wamekuja wazungu wamelichukua, wamebadilisha matumizi yake, leo umekuwa ni uwanja wa *golf* wakati wananchi hawana sehemu ya kulima. Leo wameanzisha *zoo* ya wanyama,

wanafuga swala ndani, wakati swala wako *Arusha National Park*, wananchi hawana sehemu ya kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni miongoni mwa mambo tungepashwa tupatiwe maelezo ya kina na nafahamu kwamba shamba hili limebadilishwa matumizi kinyume na utaratibu, kinyume na Sheria, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako hapo wanajua na watatupatia maelezo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye masuala la Maafisa Ardhi. Kilio cha Wabunge wengi hapa wamekuwa wakilalamika kuhusu Maafisa Ardhi. Hawa watu wamejiona ni Miungu watu katika Halmashauri zao na nimeona juzi kwa mfano, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi alikwenda Babati na akakuta kulikuwa na uozo mkubwa pale kwenye Ofisi ya Ardhi, wakati anasubiri timu yake impatie majibu, akasikia wale watu wahusika wamehamishwa, wamehamishiwa kwenye Halmashauri nyingine. Sasa Wizara ya TAMISEMI inahusika kwenye kulea hawa watu na lazima tuseme ukweli wakati mwingine tunawabebesha watu mizigo ambayo sio ya kwao wakati uozo uko sehemu nyingine. Yaani mtu ana tatizo Babati kwa sababu ameshaharibu unamhamisha unampeleka Meru, ina maana wao ndiyo wanataka wezi? Watu wana tatizo Meru unawaamisha unawapeleka Newale, Newale ndiyo wanataka watu wenye tabia mbaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwe *serious* katika suala hili. Maana juzi nimesema tuna migogoro mikubwa kwenye madini leo hii, lakini madini ni sehemu chache tu ambazo zina madini kwenye nchi yetu. Matatizo haya ya ardhi yako kwenye kila kona kwenye nchi yetu na

itafika siku miaka inayokuja, haki ya Mungu tutakuja kulaumiana kwa sababu wananchi hawatakubali tena na tunaweza tukashangaa *dispute* kubwa ambayo hatujawahi kuitarajia kwenye nchi yetu kwa sababu ya tatizo la ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la *EPZ*. Kuna ardhi ya *EPZ* ambayo ipo kwenye Kata ya Kilori eneo la Malula kwenye Jimbo langu, imechukuliwa kwa wananchi, ni muda mrefu, ni miaka kadhaa sasa kwa maana kwamba watalipwa fidia, mpaka leo hakuna hata mmoja aliyelipwa fidia na hawajui watalipwa lini na watalipwa kwa *rate* gani. Kama Serikali ilikuwa bado haijakuwa tayari iwaachie wananchi ardhi yao waendelee kulima, itakapokuwa tayari ndiyo ije ifanye nini? Ichukue ardhi na haya ndiyo mambo ambayo hata Ndugulile alikuwa analia nayo juzi hapa. Yaani kila Mbunge analalamika, kama Serikali haiko tayari ku-*run* mradi iache wakati utakapofika ndiyo ije kuu-*run*, wananchi waendelee kumiliki ardhi yao, siku Serikali ikiwa tayari ije. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwangu ni hayo, naomba nipate majibu stahiki kwenye mashamba ambayo nimeyataja na nirudie tena kwamba nawapongeza Mawaziri hawa wawili kwa kazi kubwa wanayoifanya na naomba Mheshimiwa Waziri Profesa wakati anahitimisha, aniambie ni lini tutakwenda Arumeru, najua mwezi wa nne ilikuwa twende Arumeru, kukawa na rabsha kidogo, Baraza la Mawaziri likabadilika, wakashindwa kuja. Kwa hiyo, naomba wakati wa kuhitimisha aniambie ni lini anakuja twende mimi na yeye, mguu kwa mguu ili akaone vituko, watu wamemiliki ardhi na wananchi hawana sehemu ya kulima mchicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Leo nitajikita zaidi kwenye Jimbo kwa sababu jana nilizungumza Kitaifa zaidi. La kwanza ambalo sio la Jimboni kwangu linahusiana na msitu wa Kazimzumbwi ambao Mbunge mhusika pia amezungumza ambapo kwa kufuatia hotuba ya Kambi ya Upinzani mwaka jana, inaonekana kuna *survey* ambayo Wizara ilikwenda kufanya. Katika *survey* ambayo ilifanyika, waligundua kwamba uhakiki ambao ulifanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii ulikuwa na kasoro na kwamba kuna maeneo ya Vijiji ambayo yalikuwa yameingiliwa kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa licha ya kutoa hili tangazo na kuonesha kwamba kuna maeneo kweli yaliingiliwa ambayo ni ya wananchi, hakuna chochote ambacho kimefanyika mpaka sasa kwa mantiki ya kwamba wananchi bado wanasumbuliwa sana na Maafisa wa Maliasili na Utalii na hawajaweza kukaa kwenye maeneo yao vizuri. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha alitolee maelezo kwa sababu walishakwenda, walishalifanyia kazi, lakini bado kuna utata mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nirudi Jimboni kwangu. Hivi majuzi katika eneo la Tegeta, pale Namanga ambapo kutokana na kero za ardhi kuzidi na kutokana na wananchi wanyonge kunyanyaswa, ilibidi Mheshimiwa Rais wakati anakwenda Bagamoyo, walimshtua kidogo kwa kumpopoa kwa mawe ili ajue kwamba mabeberu ama mapebari wameikamata hii nchi na ili aweze kusimama na kuwasikiliza wanyonge ambao kwa sasa maeneo yao ambayo matajiri wakiona yako *prime areas*, wako tayari

kwa kushirikiana na Maafisa Ardhi wasiokuwa waaminifu, kutengeneza hati juu kwa juu, wananchi kuuzwa wakiwa ndani ya ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, hili suala la Tegeta ambayo sasa hivi, zamani ilikuwa kwenye Kata ya Kunduchi kiujumla, sasa hivi iko Kata ya Wazo kwa mantiki ya Tegeta-Namanga kuna hati ambayo imetolewa kwa hii Tegeta *Petrol Station* na naomba kuisoma hii hati: Hati namba 52, *Title* namba 52130 na ilitolewa na Kamishna wa Ardhi mwaka 2001 baada ya ramani za kimagumashi kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake wananchi wangu waliokuwa pale toka mwaka 1958, juzi wanavunjiwa nyumba na Mwarabu wa *Big Bon* ambaye Mwarabu wa *Big Bon* anasema yeye ana kifua Ikulu na kwamba ana uwezo wa kuhonga Mahakama na kwamba wananchi watoke kwa sababu yeye ana fedha. Sasa niseme hivi, wananchi wangu nimeshawaambia kwamba kama mnaona vyombo vya dola haviwasaidii, kama mnaona Serikali yenu haiwasaidii, tumieni Sheria mkononi mwenu na Mbunge nitawalinda. Sasa kama kikitokea cha kutokea, kwa sababu Polisi hajatekeleza wajibu wake, naomba wa kwanza mje kunikamata Mbunge, wananchi wangu muwaache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tu naingia baada ya kuwa Mbunge wa Kawe, nilimtaarifu Mheshimiwa Waziri juu ya uvamizi ambao ulianza kidogo, lakini kwa sasa kasi imekuwa kubwa sana. Wizara inajua, jana nimemsikia Mheshimiwa Waziri anasema suala la uvamizi ni suala la

ujambazi, nenda ukatoe taarifa kwenye vyombo vya usalama vikakamate mwizi wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwambie Mheshimiwa Waziri, akiona watu wanakuja mpaka Wizarani, ajue huku kote wameshajaribu wamekata tamaa. Sasa hivi ni jambo la kawaida sana kwenye maeneo ya Mabwepande, Mbopo, Kinondoni, Mawazo, watu wana maeneo yao, wameyasafisha, wameweka vibanda vyao, wanakuja watu na machepe na silaha za jadi wanavunja nyumba, wanatishia watu maisha, watu wanageuka wakimbizi katika maeneo yao. Mkuu wa Wilaya anajua ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mkuu wa Mkoa anajua, Polisi kuanzia *RPC, OCD* wanajua, hakuna hatua wanayochukua. Sasa nirudie kusema kwamba, mtekeleze wajibu wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefikia mahali kuna tuhuma kwamba wale watu wanaovamia maeneo ya watu na kuvunja na kuuza kwa bei chee, kuna mgao ambao wanapeleka Polisi Kawe ndiyo maana Polisi Kawe wanapoitwa kwenda kuingilia, kuondoa majangili wanakuja siku mbili, tatu, wanazuga, wanaondoka na wengine wanasema wao sijui wa upande wa pili, wanasema kwamba Mheshimiwa Mbunge anatuma watu wavamie. Labda niseme mbele ya hili Bunge lenu Tukufu ama Bunge letu Tukufu, si-*support* mtu yeyote anayevamia mali ya mtu. Kwa hiyo, kama kuna watu wanapita pembezoni kusema Mbunge wa Kawe anawatumia vijana wakavamie, ni kitu ambacho hakipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, damu ilishamwagika kule Wazo, damu imemwagika juzi

Tegeta–Namanga watu wameuawa, wale mabaunsa waliokuja kuvunja maeneo, damu itaendelea kumwagika Kawe na damu itamwagika nchi nzima. Sasa hivi tuko hapa, mtu amenitumia *message* kutoka Songea. Anasema; kuna Mzungu amepewa eneo katika Kijiji cha Lukutila, *message* zinamiminika. Mzungu amepewa ekari 50, ameshapewa *title* namba 418, shamba limeingilia Kijiji cha Madaba, wananchi hawana ardhi, mnawapa mabeberu ardhi ya kwetu ambayo ndiyo urithi wa pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe, mnasema Tanzania nchi ya amani, kuna mtu alisema kweli hatuna mapembe. Mmeiba dhahabu huko, zimekwenda. Sasa ardhi? Dunia ya kwanza imeona sasa hivi, dunia nzima ina uhitaji wa chakula, wanakuja huku kwa hela kiduchu, wanavamia maeneo yetu wazalishe vyakula waende wakalishe dunia ya kwanza. Kwa nini sisi tusizalishe? Kwa nini tusiwawezeshe Watanzania wenzetu wamiliki Tanzania…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, sina nia ya kuingilia katika mazungumzo yako, nia yangu uendelee tu vizuri. Nataka tu Bunge letu lisije likatoa picha kwa wananchi kwamba kila Mzungu nchini ni beberu, tutakuwa tunapanda ubaguzi ule ule ambao tulipigana nao sana wakati wapigania uhuru wakiwa Kongwa na maeneo mengine tukitaka kupambana na ubaguzi huu dhidi ya watu weupe. Endelea Mheshimiwa. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mweupe ni mweupe tu na mweusi ni mweusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuiomba Serikali kwa kweli; naomba mfanye *operation* maalum kuokoa

wananchi wa Jimbo la Kawe, naomba muunde kikosi maalum msitegemee wale askari waliokuwepo, wanalijua hili suala na inaonekana kuna *syndicate* inayofanyika. Lakini lingine Mheshimiwa Waziri, naomba pia, kuna haja kama Serikali kuangalia kwa utaratibu gani tutagawa maeneo kwa watu maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni ngumu sana kwa Mtanzania wa kawaida kununua viwanja ambavyo vinatengenezwa na Halmashauri zetu, zinatengenezwa na Wizara yetu. Miradi ya Wizara ya viwanja 20,000, miradi ya Halmashauri, wananchi hawawezi ku-*afford*. Kwa hiyo, kama ardhi tunayo ya kutosha, tuandae utaratibu ambao mwananchi wa kawaida anaweza akanunua. Tafadhali naomba hilo tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ni suala la *National Housing*. Jana Mbunge kaka yangu Mheshimiwa Mtemvu amelizungumza kwa kina kuhusiana na Serikali kuridhia kuuza nyumba zile za *size* ya chini na zile za *size* ya kati na zile ambazo sio za *size* ya juu, zilisemekana kwamba hazitauzwa. Inasikitisha kwamba kila Waziri anayekuja, anakuja na utaratibu wake. Kuna nyaraka hapa zinaonesha kwamba maamuzi ya kuuza zile nyumba za gharama ndogo na gharama ya kati, zilitoka tokea miaka ya tisini. Wakati huo Mheshimiwa Cheyo alipokuwa Waziri. Zikaja, zikahalalishwa kipindi cha Mheshimiwa Chiligati na yeye akaja akalizungumza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Chenge?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nilimaanisha Mheshimiwa Gideon Cheyo, sijasema Chenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile mwaka 2003 aliandikiwa barua kwa Naibu Waziri, akasema kwamba anasubiri tupitishe Sheria mbalimbali ambazo tulizipitisha ili kuwezesha wale wananchi ambao walikuwa kwenye zile nyumba za thamani ya chini na thamani ya kati kuweza kununua zile nyumba, Sheria zikapita. Mwaka 2008 akiwa ziarani, Manispaa ya Iringa kufungua majengo na maduka 74 yaliyojengwa na *National Housing,* Rais akasema Sheria zikishawasilishwa Bungeni wananchi watapata ile haki ambayo tumewaahidi miaka mingi iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kauli za namna hii ambazo zinatoka mpaka kwa Kiongozi mkubwa wa nchi, mnawaaminisha Watanzania kwamba hizi nyumba za kiwango hiki na kiwango hiki mtauziwa kama ambavyo na nyie mlijiuzia nyumba kipindi kile, kwa nini msiwape hii haki? Kitu gani ambacho kinafanya hizi nyumba tena zile za thamani ya chini, hawa watu hawataki yale majumba yaliyokuwa kwenye *prime areas* kule, hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Tibaijuka, tunamheshimu sana, tunamwamini sana kwa kazi ambayo ameionesha na nashukuru kwa yale ambayo ameanza kuyafanya Dar es Salaam kwa watu wa mazingira, lakini bado nina deni na yeye. Haimaanishi kuvunjia wanyonge akawaacha matajiri. Nitamwona amefanya jambo la maana kama yale mabangaloo ambayo tuliongozana siku ile tukafungiwa geti mimi na Waziri, tunafukuzwa na kamlinzi, akashiba lakini anamwambia Waziri wa Ardhi huwezi kuingia. Yale yakivunjwa ndiyo nitajua kweli ana maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakivunja zile za wanyonge, atakuwa hajafanya kazi yoyote. Watu wanadharau wakati wanaanza kujenga kwenye msingi mnakwenda mnawazuia, mtu ambaye ameonesha dharau toka anajenga kwenye msingi, leo hata kama amejenga hekalu mpaka juu, muache avunjiwe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi kama Mbunge wa Kawe, nataka haki itendeke na masuala ya watu kutumia Mahakama kama uchochoro, kwa sababu wale Mabwana wanajua wamevunja Sheria wanakwenda kwenye Mahakama, wanajua kabisa kwenye Mahakama tutakuta Mahakimu sio waaminifu, Majaji sio waaminifu, watahonga, halafu maskini atakosa haki yake. Tusiwe na *double standard* wakati wa kufanya maamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe suala la uvamizi Kawe mlishughulikie. Makongo naomba mje tuzungumze, mbali ya kwamba yeye ni Waziri, mimi ni Mbunge wake, si anakaa Makongo. Aje tuzungumze na wananchi, wananchi wana nia njema sana, wanataka maendeleo, lakini sasa kule Makongo ni maendeleo ya kibabebabe na vizuri mimi nakaa kule, tutazuia tu. Akija vizuri tutakaa vizuri, tutazungumza, tutafanya kazi. Lakini akija kwa dhamira ya kuwaondoa wale maskini ambao hawatakuwa na uwezo wa kufidia zile gharama za kale kamkopo ambako wanakachukua, hiyo hatutakwenda pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini nimeeleweka. Siungi mkono hoja, mpaka nipate maelezo. Naomba nipate maelezo ya kina kuhusu *National Housing,* naomba nipate maelezo ya kina kuhusu Makongo, naomba nipate

maelezo ya kina kwa wavamizi, naomba nipate maelezo ya kina *Tegeta Petrol Station* na huyu mtu wa *Big Bon* anayesema kwamba, anaijua Ikulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Looh! Mheshimiwa Assumpter Mshama, kwa kifupi sana.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kulingana na Kanuni Namba 68(7): "Halikadhalika Mbunge, anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika, atoe ufafanuzi kama jambo hilo…"

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, endelea.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anaongea, ameunganisha tatizo lililotokea kule Tegeta na kuhusisha Ikulu. Kwamba, yule mtu wa *Big Bon,* ana sauti kule Ikulu, ndio maana watu wanapata matatizo na anaweza kufanya lolote. Hivyo, anaweza kuthibitisha kwamba, kweli, Ikulu inaweza kusababisha wananchi wake wapate matatizo na…

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari, uwe na uvumilivu angalau kumsikia mtu mpaka mwisho, halafu ukisimama nakupa nafasi.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hairuhusu Taarifa baada ya yeye kuzungumza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari, Taarifa. Mpe Taarifa Msemaji.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Assumpter Mshama, kwamba, alichokisema Mheshimiwa Halima Mdee, ni kwamba, huyu tajiri wa *Big Bon,* anachokisema au kinachosemekana ni kwamba, yeye ana sauti anaweza akazungumza na Ikulu, anaweza kuzungumza na watu wakubwa kwenye Serikali hii na ndio sababu anawanyanyasa wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Mdee, hakusema kwamba, ana *documents* ambazo zinaonesha kwamba, huyu mtu ana mkono Ikulu. Alichosema ni kwamba, inasemekana kwamba, huyu mtu anasema yeye anaweza kufika mpaka Ikulu. Kwa hiyo, hawezi kufanywa chochote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, ni mambo ya kufikirika? Mheshimiwa Koka, endelea kuchangia.

**MHE. SYLVESTER F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Wizara, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya. Lakini vile vile, nipongeze Mji wangu Mdogo wa Kibaha, nimpongeze Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Mkurugenzi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kuupanga Mji Mdogo, ambao unakua kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunazo changamoto kubwa sana katika hii sekta ya ardhi. Nikirudi Jimboni kwangu, bado tunayo matatizo makubwa na wananchi kila mara wamekuwa wakilalamika. Hivi sasa ninavyozungumza hapa, eneo la Mji Mdogo wa Maili Moja, ambalo hata liko nje ya barabara, tayari limewekewa *X*. Hata wananchi hawajapata taarifa inayoelezea kiundani kuna utaratibu gani unaotokana na *X* hizi na kuna mpango gani wa baadaye wa kuwafanya wapate maeneo mengine endapo uvunjaji unakuja. Halikadhalika, tatizo hili liko Mji Mdogo wa Picha ya Ndege. Namwmba Mheshimiwa Waziri, wakati atakapokuwa ana-*wind up,* aweze kulitolea maelezo, ili wananchi hawa waweze kukaa kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi ni Wizara ambayo ni mtambuka, kwa maana ina mwingiliano na sekta na Wizara zote. Kwa sababu, ndio inayosimamia Sera za Ardhi, ambapo shughuli zote zinafanyika. Kama tulivyosikia, kila anayesimama Mheshimiwa Mbunge, analalamika kuhusu matatizo ya ardhi na migogoro. Hatuwezi kuendelea hivi tukafanikiwa. Ni lazima sasa Wizara, ijikite kufanya mambo kisasa na kutatua matatizo haya, ili tukisimama hapa, tuzungumze mambo mengine ya maendeleo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia pekee ya kuondokana na tatizo hili ni kuwa na mpango kabambe au *Master Plan* ya matumizi bora ya ardhi kwa nchi nzima. Mpango huu upewe msukumo na upewe pesa za kutosha, sio maneno na maandishi peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri wakati anamalizia, atueleze mpaka hivi sasa ni Vijiji vingapi ambavyo tayari viko katika mpango wa matumizi bora ya ardhi? Ni Miji mingapi Midogo? Ni Miji mingapi ya Wilaya? Ni Miji mingapi ya Mkoa na Majiji, ambayo tayari yanayo *Master Plan* na kwamba, mipango ya matumizi bora ya ardhi, inafanyika? Tukifanya hivi, tutaondokana na matatizo na migogoro na mambo yote ambayo tunayazungumza, ambayo yanawakera wananchi; yanaendelea kutupa sifa mbaya kwa wananchi wetu na kuilaumu Serikali, yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Miji yetu hivi leo, hata maeneo ya viwanja vya michezo kwa vijana hakuna. Maeneo ya kujenga shule, hakuna. Ni mpaka Serikali, ianze upya kusigana na wananchi na kusigana kwenyewe ni pamoja na kuchelewesha fidia. Hii yote inasababisha sasa mchakato mzima wananchi wanaona kama Serikali yao inawaonea, kumbe ina nia njema ya maendeleo. Sasa ifike wakati kupitia mpango huu kwani ardhi yote ina mpangilio, inaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia vijana wetu, wote wamekimbia vijijini wanakimbilia mjini. Wanakimbilia mjini kwa sababu, kule wanakotoka hakuna mpango mzuri wa matumizi ya ardhi. Wote tunafahamu hata ile *Industrial Revolution* iliyotokea ndio inayosababisha watu wanakuja

mjini, lakini sisi ni kinyume, watu wanakuja mjini wakati hakuna shughuli muafaka za kufanya. Kwa hiyo, matokeo yake vijana wetu wote wameishia kwenye bodaboda na mambo mengine madogo madogo, ambayo kihakika hawapati tija ya kutosha katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufike mahali tuwe na mipango ambayo ni muafaka. Maeneo ya viwanda yanajulikana, maeneo ya huduma za jamii yanajulikana na maeneo ya biashara mbalimbali yanajulikana. Vijana wetu waende huko wafanye biashara, wote wasisongamane Mjini, ili tuweze kupata maendeleo kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli uhamiaji wa Mjini unakua kwa kasi. Kwa takwimu kidogo ambazo ninazo, tukiangalia mwaka 1957 wakati Tanzania Bara, tukiwa takribani 9,000,000 tayari miji yetu tulikuwa na wakazi wapatao 436,000 ambayo ilikuwa ni kama 4.8%. Lakini mwaka 2002 ambapo inakadiriwa kwamba, tulikuwa zaidi ya 35,000,000 tayari mijini tulikuwa na wakazi *almost* 8,000,000 ambayo ni 23%. Lakini bado inakadiriwa itakapofika 2025, karibu 50% ya wananchi watakuwa wanaishi Mijini. Sasa Wizara ya Ardhi, ina mipango gani ambayo itaweza kubeba mabadiliko haya yanayotegemewa katika nchi yetu? Kama hautakuwapo mpango, tutaishia kuwa na Miji mikubwa, ambayo ni *squatter* na hatutaweza kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kama mipango mizuri hii itafanyika na itasukumwa kwenye Miji yetu hadi katika Mitaa na Vijiji, tatizo hili tutaondokana nalo. Tutakuwa na Miji iliyopangika na shughuli za kiuchumi zitakuwa *evenly distributed* kwa nchi nzima. Hapo kutakuwa hakuna watu ambao watakimbilia Dar-es-Salaam tu au katika Miji mikubwa tu, nchi nzima itakuwa imechangamka kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo suala la Mji Mpya wa Kigamboni. Ni kweli, hata Mheshimiwa Mbunge, aliongea kwa jazba kulingana na hali inavyoendelea, lakini ni lazima tukubali kwamba, hakuna maendeleo ambayo hayana matatizo na athari. Unapoona unapata mtikisiko katika jambo fulani unalotaka kulifanya, maana yake ndio unafika kwenye mafanikio. Nasema hivi, tusikubali kurudi nyuma katika suala la Mji Mpya wa Kigamboni, kwa maana ndio mahali pekee ambapo Dar-es-Salaam sasa itakuwa mahiri katika Mji ulipangika na tukaondokana na kuendelea kuupanga Mji wa zamani, ambao unatupa matatizo kwa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wakazi wa Kigamboni kwamba, sasa ifike muda wakae na Serikali. Mheshimiwa Waziri, akae na Mheshimiwa Mbunge, waendelee kuwasihi wananchi, ili wafikie muafaka na mradi huu uweze kuendelea. Si kweli kwamba, mradi kama huu unaweza kuufanya mahali popote; unaweza ukafanyika Kigamboni kwa sababu, ni eneo ambalo liko kwa namna ya pekee na lenye mvuto wa pekee na litakaloleta thamani kubwa kwa Dar-es-Salaam na nchi nzima kwa ujumla. Si rahisi utoke hapa uende kabisa katikati porini huko, useme unaanzisha

mji na ulete tija. Kwa hiyo, ni bora lile eneo lilivyokaa na ambapo lina uwezo mkubwa wa kuleta tija, tuendelee kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali, kama wenzangu walivyosema kwamba, tunapokwenda katika miradi, tuheshimu ule muda. Lakini vile vile turudi nalo, hata sisi wananchi mara nyingi tumekuwa tukipewa ardhi na Sheria za Ardhi ziko wazi, lakini ni mara chache tunaweza tukatimiza masharti yale ya ardhi kwa muda ule. Kwa hiyo, mimi ningeshauri Mheshimiwa Waziri, aendelee kuwasiliana na viongozi pamoja na wananchi, kuhakikisha mradi huu unasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa sana jambo la Sheria ya Kulinda Wapangaji na Nyumba. Naunga mkono sana suala hili na kama likija kwa wakati muafaka, litatusaidia sana. Lakini natofautiana kidogo kwa kuona hii bado ni *pre-mature,* kwa sababu, kama tutaileta Sheria, wakati hatujawa na nyumba za kutosha, bado Sheria hii itakuwa ni ngumu kutekelezeka. Lakini vilevile tutawakatisha tamaa wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika ujenzi wa nyumba, matokeo yake tutashindwa.

Mheshimiwa Spika, tuweke mipango mizuri kama tulivyoanza na ile ya *Refinancing Mortgage,* ambayo ikiwa kubwa ya kutosha, kutapatikana mikopo ya bei rahisi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na hapo sasa nyumba zinaweza zikawa kwa bei nzuri na tunaweza tukaiweka Sheria hii ikawa na tija na ikatusaidia. Maana leo hii watu wanaojenga nyumba zao binafsi, wanakopa katika *commercial rate,* kama vile unachukua *overdraft* ya kufanya biashara. Unajenga nyumba, unawezaje

ukampangia mtu bei ya kurudisha pesa zake na kurudisha mkopo aliokopa benki kwa sasa hivi? Kwa hiyo, niiombe sana Wizara ya Ardhi, ikazanie sana kukuza mtaji ule wa kukopesha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ili nyumba ziweze kujengwa kwa bei nafuu na kuweza sasa kuweka Sheria hii ambayo itaendelea kuwalinda wapangaji na wale ambao wanatumia nyumba za kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niliyozungumza, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wakati aki-*wind up* aweze kunipa majibu, ili tuweze kuunga mkono na kusonga mbele katika bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7). Hii inampa fursa Mbunge yeyote kusimama tu na kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba, Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ina hisia kali na nafahamu kabisa kwamba, matatizo ya ardhi ni makubwa sana. Pia nafahamu na ukweli ni kwamba, baadhi ya Maafisa Ardhi wasio waaminifu, wametufikisha hapa tulipo na hasa katika Mikoa ambayo mimi naijua, kama Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu Mheshimiwa Halima Mdee, anachozungumza kwa uchungu kabisa na

ushahidi anao, hata mimi baadhi ya ushahidi ninao. Najua Dar-es-Salaam kuna wababe, wanaonyang'anya ardhi kila mahali. Najua habari ya uvamizi na mimi nimewahi kushiriki katika kufanya kazi hiyo, ni ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesimama kuomba Mwongozo wako kwamba, ni kweli, pamoja na matatizo yote tuliyonayo kila kona ya ardhi, lakini nataka kulishauri tu Bunge lako Tukufu na kuomba Mwongozo kwamba, sisi kama Wabunge, kwa kauli tunazotoa humu za kuhamasisha tunasema, sasa tutumie Sheria mkononi, kuhamasisha umwagaji wa damu. Kauli zetu hizi, nafikiri zimevuka mipaka kidogo kwa sababu, sisi tuna nguvu hapa hata ya kubadilisha Sheria, tuna nguvu ya kutumia Kanuni zetu na uwezo tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwamba, pengine pamoja na kwamba, mambo ni mabaya kiasi hicho, lakini pengine lugha hizi ambazo tumetumia ni kama vile tunahamasisha vurugu, watu kutumia...

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mwongozo wako, ili lugha kama hizi kwa viongozi kama sisi wenye madaraka makubwa kwamba, pengine tusikate tamaa kwa sababu, sisi ndio wenye uwezo. Tukikata tamaa sisi, wananchi wengine watafanyaje? Pamoja na kukiri mimi binafsi kwamba, kweli tatizo hili ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako juu ya hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Nianze na kusema kwamba, muda si mrefu tutasitisha shughuli zetu hadi baadaye saa 11.00. Kwa hiyo, mchangiaji atakayechangia jioni atakuwa mmoja tu, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, halafu baada ya hapo Waheshimiwa Mawaziri, wataendelea na utaratibu tutakaokuwa tumeshaelezana. *(Makofi)*

Nikirudi kwenye Miongozo, nikubaliane na Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwamba, Waheshimiwa Wabunge, sisi ni viongozi tuliochaguliwa na wananchi au kuaminiwa kwa taratibu mbalimbali zilizotufikisha hapa. Si vizuri kabisa tukakata tamaa na kwa hiyo, tukawaachia wananchi wetu sasa wachukue Sheria mkononi na kuanza kufanya wanavyotaka kufanya kwa njia za mkato.

Kwa hiyo, nawaombeni sana tujitahidi sana. Najua mambo haya yanauma, ni mambo yenye dhuluma kubwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nchi, yapo, sisi ni Wabunge, wawakilishi wa wananchi, tunayafahamu. Mengine yanafanywa na baadhi ya Maafisa wetu, baadhi ya watendaji wetu mahali mbalimbali, lakini tuwe na uvumilivu, wakati wote tuhimize taratibu za Kisheria, zichukue nafasi yake. Hilo ningewaombeni sana Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, nakubaliana na wewe Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwamba, Waheshimiwa, pamoja na munkari kidogo, lakini tuwe makini katika kauli zetu, ili tusije kufika mahali hata sisi wenyewe tutakapowaambia wananchi hebu tusikilizane, itakuwa tena hakuna nafasi hiyo ya kusikiliza.

Mwongozo mwingine, ulitolewa na Mheshimiwa Turky. Mheshimiwa, naona unasimama, Mheshimiwa Mangungu. Nikishasimama, huwezi kusimama, mpaka nikae kidogo.

Mwongozo wa Mheshimiwa Turky, mwanzoni pale. Wakati Mheshimiwa Tundu Lissu anaongea, yeye alilalamikia matumizi ya neno kuwadi. Akashauri, neno udalali, ndilo ambalo hasa lingetumika. Sasa, mimi si mtaalam wa Kiswahili. Tuna Wataalam wawili wa Kiswahili hapa na wote wawili hawapo; Dokta Mohamed Khatib, upande wa Chama Tawala na Profesa Kulikoyela Kahigi, kwa upande wa Upinzani. Hawa ni Wataalam wa Kiswahili, waliobobea. Lakini, nataka kusema tu kwamba, udalali ni kazi rasmi ambayo, inatambulika. Madalali hawa wapo, hata katika Soko langu la Kimataifa la Kibaigwa, kuna madalali pale, wanafanya kazi halali. Lakini hii ya ukuwadi, hii si rasmi. Lakini nao wapo inasemekana. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Tundu Lissu, alichotaka kusema wale kwenye Sayansi ya Siasa wanaita ma-*Comprador* na nini. Basi naomba tuvumiliane tu kwamba, alitaka kumaanisha hao watu wenye sifa hizo mbaya, ambazo sijui yeye anamaanisha wako wapi. Lakini tuliachie hapo, Mheshimiwa Turki, tunarudi kule kule kwenye kutumia tu lugha nzuri, ili tuweze kuelewana.

Nikae chini kidogo, nimemuona Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nitumie Kanuni ya 68(7), ambapo kama utaniruhusu naweza kuisoma, lakini

Mwongozo ambao nauomba hapa ni kwamba, kumekuwa na mjadala mkali sana unaohusiana na masuala mbalimbali ya ardhi. Lakini katika huu mgogoro ambao ni wa Tegeta. Hili suala kwa ufahamu nilionao na nina uhakika kabisa, suala hili liko Mahakamani na tumekuwa tunazungumzia jinsi gani ambavyo mihimili hii isiingiliane. Sasa tukiwa tunaingia sana kwenye mijadala ambayo inahusu mihimili mingine kuifanyia kazi, naona kama tunakiuka Kanuni ambazo tumejiwekea na Sheria ambazo zinatuongoza katika Mabunge yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate Mwongozo wako kwa sababu, naona kidogo hapa, tunaweza tukaingia katika tafsiri ya mambo ambayo tutakwenda kinyume na taratibu tulizojiwekea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, atapitia Hotuba za Waheshimiwa Wabunge, jioni ya leo, atakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutuweka vizuri zaidi katika jambo hilo. Kama kweli, liko Mahakamani, utaratibu wetu ni ule ule ambao tumeambiana siku zote kwamba, tusiingilie masuala yaliyoko katika mhimili mwingine.

Mwisho, kwa sababu, muda wetu umekwisha kabisa, Waheshimiwa Wabunge, nimepokea malalamiko yako hapa Mezani, ninayo mkononi, kutoka kwa Waheshimiwa Madiwani wanne; Mheshimiwa Dotto Msawa, Diwani wa Kata ya Kigamboni; Mheshimiwa Albert Luambano, Diwani wa Kata ya Tungi; Mheshimiwa Suleiman Mathew, Diwani wa Kata ya Vijibweni na Mheshimiwa Juma Nkumbi, Diwani wa Kata ya Kibada.

Madiwani hawa, wanasema ifuatavyo, kwamba, wakati Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni Dokta Faustine Ndugulile, akizungumza jana humu Bungeni, alitoa shutuma nzito ndani ya Bunge dhidi yao kuwa, Wizara ya Ardhi, imewahonga Madiwani waliokuja kusikiliza Bajeti hiyo kwa misingi ambayo sisi Madiwani, imetushangaza na kutusononesha kwa kuwa, ujio wetu umetokana na matakwa yetu wenyewe na wala si kwa shinikizo kutoka mahali popote, ikiwemo Wizara ya Ardhi.

Hivyo basi, tuhuma hizo ni za uwongo na uzushi mkubwa na zina lengo la kutuchafua mbele ya jamii na wananchi wetu katika Kata tunazoziongoza, hivyo kuwajengea hisia za kutokuwa na imani na sisi. Kwa misingi hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, athibitishe tuhuma hizo mbele ya Bunge lako Tukufu na kutuomba radhi sisi Madiwani, mbele ya Bunge lako Tukufu, kama alivyotamka katika Bunge lako. Tunaituma barua hii kwako, iwe ni tamko letu na lalamiko letu, dhidi ya Mbunge huyo. Tunaomba kuwasilisha.

Sasa baada ya kupata malalamiko haya, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge, nimekuwa nikizungumza na nilisema hata leo mapema kwamba, katika uchangiaji wetu tujiepushe sana na kuwalenga watu na kuwatolea tuhuma ambazo ni nzito nzito. Kwa hiyo, katika kufuatilia jambo hili, imebidi niitishe *Hansard,* nione hasa Mheshimiwa Ndugulile, alisema nini.

Mheshimiwa Ndugulile, alisema ifuatavyo, sasa namnukuu yeye: “Huu utaratibu ambao Wizara na Waziri ameanzisha wa kuwahonga Waheshimiwa Madiwani kwa gharama ya Serikali kuwaleta Dodoma, nikwambie kabisa

pasipo ushirikiano wa Mbunge, hutaweza.” Mwisho wa kunukuu.

Kwa hiyo, nimepitia Kanuni ya 71, inayotawala mambo yanayofanana na haya, kwa sababu, hawa Madiwani waliolalamika, sio Wabunge wenzetu. Malalamiko ya namna hiyo yanatajwa na Kanuni ya 71 inayosema: “Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 na 101 ya Katiba, mtu yeyote asiye Mbunge, ambaye atajisikia kuwa amepata athari hasi, kutokana na kauli au maneno au shutuma zitolewazo Bungeni, kumhusu yeye binafsi, anaweza kupeleka malalamiko pamoja na maelezo yake ya kujitetea kwa Spika.” Sasa mimi nimepokea malalamiko haya na nimeyatazama, nimejiridhisha kwamba, mambo haya yalizungumzwa humu Bungeni. Waheshimiwa hawa, wametaka Mheshimiwa, apewe nafasi ya ama kuwaomba radhi humu Bungeni au vinginevyo.

Kwa hiyo, tutakaporudi jioni, baada ya Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, nitampa nafasi Mheshimiwa Ndugulile, ama afafanue kauli yake ama afute maneno yake. Vinginevyo jioni hiyo hiyo, Kiti kitachukua hatua zipasazo kuhusiana na jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda wetu hauturuhusu kuendelea, naomba sasa kusitisha shughuli za Bunge, hadi saa kumi na moja leo jioni.

*(Saa 7.04 mchana, Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Niliahidi kumwita Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed kuwa mchangiaji wa mwisho. Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uzima nikafika katika ukumbi huu kwa miguu bila kushikwa mkono, hiyo pia ni neema ya Mwenyezi Mungu sina budi kumshukuru. Pia napenda nimpongeze Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Naibu wake kwa kazi yao nzuri wanayoifanya mpaka kufikia sasa hivi tumeanza kuuona mwanga wa mafanikio katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nichangie kwa kusema kwamba, tatizo la ardhi ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Kesi za ardhi zimeenea kila upande, kila Halmashauri unayokwenda matatizo hayo hayo tu, kesi za ardhi zinaendelea. Kwa kweli tatizo kubwa ninalolilona ni mkizano wa sheria hii baina ya Maafisa Ardhi wa Halmashauri na Maafisa Ardhi wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa na kwa kweli tatizo hili likiwa halikupatiwa ufumbuzi yaani Maafisa Ardhi hawa wa Halmashauri wakiwa wako chini ya TAMISEMI na hii Wizara ya Ardhi, pakiundwa chombo kimoja ambacho kitawashirikisha wote, hapa ndiyo tutapata ufumbuzi wa matatizo haya, lakini bila hivyo kila siku kesi zitaendelea na inavyoonekana hasa kwa dhahiri, hawa Wakurungezi wa Halmashauri ndiyo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, maeneo yale ya wazi yaliyoachwa kwa ajili ya michezo na shughuli nyingine za kijamii, mara nyingi inatokea hawa Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwa kushirikiana na maafisa wao wa Halmashauri ndiyo wanaouza haya maeneo. Sasa badala yake watu wa Wizara hawa wa ardhi wanapokwenda wakakakuta maeneo yale yameuzwa na wao hawakubaliani na hili, kunakuwa na mvutano. Kwa hiyo, mie naishauri Serikali iunde chombo kimoja kitakachowashirikisha hawa wote hapo tutapata ufumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza sana Serikali kwa kuunda Mahakama ya Ardhi, lakini pia najiuliza katika Mahakama hii ya Ardhi nani atasimamia hizi kesi. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atakapo-*wind up* atuambie nani atasimamia kesi ni hawa Halmashauri au ni Wizara yenyewe ili tuweze kujua, matatizo haya ndiyo yatapata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa, kwanza nawapongeza sana watu hawa wa *NHC* yaani Shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Mchechu, pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini pia ni masikitiko kuona nyumba hizi wanazozijenga, hivi kweli wanajenga kwa maslahi ya Watanzania au wanajenga kwa maslahi ya nani? Kwa mfano, nyumba za Medeli zilizojengwa, nyumba hizi wakati wa ufunguzi tuliambiwa kwamba zimetumia

milioni 60 gharama zake za ujenzi. Baada ya kuwekwa miundombinu ya maji machafu, maji safi barabara pamoja na umeme zilifikia milioni 80, nyumba hizi zimeuzwa milioni 100 kabla ya *VAT* ukiweka na *VAT* zinakuwa ni milioni 118.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye nyumba zilizojengwa Mchikichini, Ilala, nyumba hizi ni sawa na nyumba zilizojengwa Medeli, yaani nyumba ya vyumba vitatu, kule Mchikichini nyumba ni sawa na hizi, miundombinu ile ile iliyotumika kujenga nyumba hizi, lakini nyumba hizi wanaziuza milioni 168, kabla ya *VAT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaulize, kule Medeli mlisema kwamba kulikuwa hakuna miundombinu ya maji, umeme, barabara na maji machafu. Je, hizi za Mchikichini tatizo ni nini? Mpaka zikafikia kuuzwa milioni 168? Sasa nataka nijue hizi nyumba zilijengwa kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania au zimejengwa kwa ajili ya kuwasaidia matajiri na mafisadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa mie Mbunge sina uwezo wa kununua nyumba hizi, hivi ni mfanyakazi gani wa kawaida anayemudu kununua nyumba hizi? Sasa naomba watufafanulie, nyumba hizi zimejengwa kwa ajili ya watu wa daraja gani au hazikujengwa kwa ajili ya Watanzania, watuambie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza hapo, naomba kidogo nimuulize Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atufafanulie alisema kwamba kutajengwa *seat park* hizi ambazo zitajengwa katika mabonde ya Msimbazi na alisema watazijenga kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kinondoni pamoja na Halmashauri ya Ilala. Sasa kwa kweli

hatujajua hizi *park* zenyewe zitakuwaje? Hata sisi Wabunge tukiulizwa na watu jamani tunasikia mnataka kutujengea sehemu za kupumzikia jioni na nini, lakini hatuwezi kuwafafanulia hebu waki-*wind up* watuambie hizi *seat park* zitajengwa jengwa vipi ili na sisi tuweze kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kuna eneo lile la *beach* kule wanaita *Oystebay beach*, eneo lile limefanana kidogo na eneo lililoko Forodhani Unguja, lakini bahati nzuri sana kule Forodhani wao wamejenga vibanda vya kuuzia biashara, sehemu za kupumzikia watu na sehemu za ku-*park* magari, lakini eneo hili lililopo hapa Dar es Salaam ni kama halina mwenyewe. Unakwenda unawakuta watu wana-*park* tu magari yao kiholela, biashara zinauzwa uzwa pale uchafu tu sehemu yote imechafuka utafikiri haina mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa na wao waje Zanzibar waangalie jinsi watu wanavyotengeneza sehemu za kupumzikia jioni ili pale wajenge vibanda vya biashara, waweke sehemu za kupumzikia na sehemu za *parking* ya magari, eneo ni kubwa hata lile la Zanzibar ni dogo, linatosha kabisa. Kwa hiyo, nawashauri sana pale ambapo mmeona hapa mmeteleza mjifunze kupitia wenzenu, nchi hii ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niishie hapa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwa umeokoa muda wangu, basi naomba nimpe nafasi fupi Mheshimiwa Abood amalizie wakati huo Mheshimiwa Ndugulile tutafuatia katika

lile suala mahususi, Mheshimiwa Naibu Waziri itabidi ufuate. Mheshimiwa Abood. *(Makofi)*

Kabla ya Mheshimiwa Abood, nakuona Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako chini ya kanuni ya 47, ambayo naomba shughuli za Bunge ziahirishwe ili tujadili...

**NAIBU SPIKA:** Naomba uisome.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Kanuni ya 47(1), baada ya muda wa maswali kwisha na naamini maswali yameshakwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, kanuni hiyo inatumika baada tu ya kipindi cha maswali kwisha na hakuna maswali ambayo yamekwisha hivi sasa, kwa hiyo tunaendelea, Mheshimiwa Abood!

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba ya maendeleo ya Makazi. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Morogoro Mjini kwa kuendelea kuniamini kwa kuwatumikia. Pia nachukua fursa hii kuwapongeza Naibu Waziri na Makamishna wote wa Wizara ya Ardhi, kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Waziri anaidai Halmashauri ya Morogoro milioni 50, nitamfanyia kazi ili hizi pesa kurudi. Pamoja na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Waziri, matatizo ya ardhi ni makubwa sana katika nchi yetu pamoja na Jimbo langu la Morogoro. Matatizo haya yanawafanya mpaka wananchi wengine wanakuwa maskini kwa ajili ya tatizo la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Morogoro Mjini kuna wananchi walikuwa na mashamba ambalo tatizo hili lilielezwa na mradi wa *EPZ*, mashamba yamechukuliwa mpaka sasa toka mwaka 2010, lakini mpaka leo wananchi hawajui hatima yao ya kulipwa fidia, imekuwa nenda rudi tu. Maeneo hayo ni Ngerengere, Kyegeya B, na Kipera. Sasa nataka kupata jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuwa je, hawa wananchi wataendelea kulipwa au mashamba yao yarudi yafanyiwe kazi nyingine, ili wajue maisha ya mbele yanavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mashamba ambayo yamechukuliwa na yamefanywa viwanda huko Lukobe, Kyegeya na Mgulu wa Ndege, baadhi ya watu wamelipwa, lakini kuna wengine mpaka sasa hawajalipwa na bado wanaendelea kuwa maskini na wanaendelea kupoteza gharama zao za kwenda huko na huku kudai haki yao. Namwomba Mheshimiwa Waziri hili jambo ni la muda mrefu leo ni mwaka wa sita wanahangaika, ni wananchi karibu 700 wanasumbuka, atakapopita aje na azungumze na wananchi hawa, atayasikia mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashamba ambayo yalitolewa mwaka 1967 kwa ajili ya kilimo, wakati kilimo ni uti wa mgongo, katika Wilaya yetu ya Morogoro Mjini

wananchi hawa wanatoka nje na kwenda kulima, walipewa mwaka 1967 mashamba hayo ili walime. Eneo linaitwa Mgongora, wanalima kwenye bonde ambalo ni bonde la mbunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kule wanapokwenda wananyanyasika sana wanafukuzwa badala yake na mashamba yenyewe yanachukuliwa wanapewa wafugaji ambao wenye uwezo wa kuweza kufanya wanavyoweza na kupata hati miliki wanapata. Haya mashamba ni toka mwaka 1967 na Waziri Mkuu analijua suala hili lakini mpaka leo hatima yao haijulikani, wanapokwenda kulima wanafukuzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mwaka huu wamepata hasara kubwa sana hawakuweza kulima, nadhani namwomba Mheshimiwa Waziri tupate ushirikiano ili wakulima hawa waweze kulima mpunga na kuweza hata kuwekewa na wawekezaji mashine ya kukoboa mpunga na kuweza kuuza hata nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wetu wa Morogoro unakua sana, tunategemea tuwe Jiji lakini kuna mashamba ya katani bado yapo mjini yamezungukwa na mji, namwomba Mheshimiwa Waziri haya mashamba sasa wakati wake basi. Tuwape nafasi sasa wananchi waweze kujenga na mji uweze kupanuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli viwanja vinatoka, lakini bei inayotolewa ni kubwa mno, wananchi wengi wa hali ya chini wanashindwa kupata ardhi. Nashauri tungekuwa na mpango vile vile wa kuweka baadhi ya viwanja kwa ajili ya watu wenye hali ya chini. Ambao wakisajili hata kuuza

atashindwa, ni yeye tu na ni kote Wizarani zinakuwepo mtu hata akiuza tunazuia. Kwa hiyo, ningeomba mpango huu ungekuwepo ili wananchi nao waweze kupata kwa sababu leo kiwanja ukinunua tu ukienda Halmashauri unapata kwa milioni sita, mtu wa hali ya chini atapata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye bei ya kupima viwanja, nayo ni kubwa mno, wananchi wengi wanashindwa, wanaweza wakapata kiwanja wakaishia kupata kiwanja bila kupima. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kwa sababu tunaloliangalia tunaanzia kwa wananchi wa chini kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija *National Housing*, kweli *National Housing* wanafanya kazi nzuri, lakini majengo mengi sana bado ni machafu na majengo mengi ambayo ni *flats* wanakaa watu ambao ni wastaafu, walikuwa wanalitumikia Taifa hili mpaka leo wapo, kuna wajane ambao walikuwa wanafanya kazi Serikalini, lakini majengo haya bado ni machafu mno. Kwenye Jimbo langu kuna *flats* ziko Kilakala, kuna flats ziko *Forest Hill* zote zile ni chafu na wajane wamejaa katika *flats* hizo. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili ili tuweze kurekebisha haya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii ya kukushukuru kwa kunipa fursa hii na naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abood, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowaambia mapema sasa tuko kwenye kipindi maalum kidogo, nitampa dakika zisizozidi tano Mheshimiwa Ndugulile ili kuzitumia kufuatana na ombi la lalalamiko na tuhuma zilizotolewa na Madiwani

wanne, nilizozisoma leo asubuhi ambao walilalamikia maneno aliyoyasema Mheshimiwa Mbunge Daktari Ndugulile jana wakati akichangia kwenye Wizara ya Ardhi. Maneno ambayo nimejiridhisha kwamba ni kweli aliyasema Mheshimiwa Ndugulile na nilinukuu hapa alichokisema kwamba:

"Huu utaratibu ambao Wizara na Waziri ameanzisha wa kuwahonga Waheshimiwa Madiwani kwa gharama ya Serikali kuwaleta Dodoma, nikwambie kabisa pasipo ushirikiano wa Mbunge hutoweza." Mwisho wa kunukuu.

Kwa hiyo, hawa Madiwani wamemtaka Mheshimiwa Mbunge ama athibitishe tuhuma hizo mbele ya Bunge Tukufu ama aombe radhi. Unazo dakika tano Mheshimiwa Ndugulile kutuongoza katika jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FAUSTIN E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze tu kwa utangulizi kwa kusema kwamba, kimsingi jambo hili ambalo tunajadili leo mradi wa mji mpya wa Kigomboni ni batili, umekiuka Sheria ya Mipango Miji, Namba Nane (8) ya mwaka 2007, wananchi wa Kigamboni hawatokubali, tunataka mchakato uanze upya na wananchi wa Kigamboni endeleeni kujenga sheria inawalinda na Mbunge wenu nitawatetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa katika hoja kuhusiana na tuhuma zilizoletwa hapo mbele yako kuhusiana na hoja yangu ya jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati nachangia, sikutaja majina ya Madiwani katika Halmashauri ya Temeke. Tuna Madiwani 43. Sasa labda ungetupa mwongozo kwamba ni Madiwani gani ambao walinishtaki, kwa sababu wakati nachangia, mimi sikuwataja. Sasa inawezekana kwamba ni Baraza la Madiwani ya Manispaa ya Temeke wamelalamika, ama kuna baadhi ya Madiwani wa Temeke wamelalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana baada ya kuhitimisha kipindi cha maswali na majibu wakati Mwenyekiti anatambulisha wageni, naomba kunukuuu *Hansard*:

"Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 11 wa Prof. Anna Tibaijuka - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambao ni watoto wake; Kemi Tibaijuka na Kayankinza Tibaijuka; na Madiwani wanne pamoja na wananchi watatu kutoka Kigamboni wakiongozwa na Mheshimiwa Suleiman Mathew - Diwani Kata ya Vijibweni."

Mheshimiwa Naibu Spika, napata mashaka sana, Mheshimiwa Waziri ni Mbunge kama mimi, na jana alikuwa anawasilisha bajeti ya Wizara ya Ardhi, na suala hili anajua kabisa wananachi wa Kigamboni wana tatizo nalo. Kwa nini awaalike Madiwani kutoka Kigamboni? Kwa nini asiwaalike Madiwani kutoka kwake Muleba? Lengo lake ni nini? Maana yake katika mazingira ya kwetu, unaposema kwamba ni mwenyeji wa hawa Madiwani, lakini vilevile ninavyofahamu Manispaa ya Temeke leo kuna ziara ya Madiwani kwenda Moshi kwa ziara ya Mafunzo, Madiwani hawa wapo hapa Dodoma; ninaposema mwenyeji katika

mazingira ya kwetu, mwenyeji unaweza ukamlipa malazi, ukampa chakula na usafiri na kitu chochote.

Sasa sisi katika Sheria ya TAKUKURU siyo lazima mtu umhonge fedha, lakini kuna yale mazingira ambayo yanapelekea kuonyesha kwamba hapa mambo hayajakaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kifungu Na. 71 (1) na naomba kunukuu:

"Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 na 101 ya Katiba, Mtu yeyote ambaye si Mbunge ambaye atajisikia kuwa amepata athari hasi kutokana na kauli au maneno ya shutuma yaliyotolewa Bungeni kuhusu yeye binafsi, anaweza kupeleka malalamiko yake pamoja na kujitetea kwa Spika."

Kifungu cha pili: "Baada ya Spika kuwa tayari, ataiomba Kamati ya Haki, Maadili na Katiba, ya Bunge kuweza kukaa na kujadili hilo."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni yale mazingira yaliyokuwepo ambayo yanaonyesha kwamba kuna jambo ambalo linaweza likaleta tafsiri mbaya, ni hilo ambalo tulilipelekea sisi kusema yale ambayo tulikuwa tumesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba labda tu utumie busara na hekima yako ili suala hili tu-*refer* kwa kutumia kifungu 71 ili basi tupate muda vizuri wa kuweza kwenda kulijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Nimekupa nafasi na haki ya kuweza kulirekebisha jambo hili na wewe umenithibitishia kwamba ni kweli ulisema na ulidhamiria, na kwa kuzisoma kanuni ukajua kabisa kwamba mimi hapa mamlaka yangu ni ya kukupeleka kwenye Kamati ya Maadili tu, na kwa kupima uzito huo, basi ukaamua kufanya kama ulivyofanya. Sasa na mimi meza yangu ni pana, naamua kwamba katika mambo haya ya utaratibu, nitazame lipi hasa ambalo linakufaa, kama ni kwenye hiyo Kamati au mahali pengine.

Sasa, kwa sababu hukuthibitisha tuhuma za kwamba kuna gharama za Serikali zimetumika Wizara inahusika na Waziri, Mwenyekiti na Madiwani hawa wameomba, ama uthibitishe, ama uombe radhi, ambayo hukuiomba; sasa mimi ninatumia kanuni ya 73(3). “Endapo Mbunge yeyote atatakiwa kuthibitisha ukweli wa maneno aliyoyasema na hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa, (ambao nilikupa dakika tano) amekataa au ameshindwa kutoa uthibitisho huo, Spika anaweza kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie vikao vya Bunge vipindi vitano.

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti hapewi taarifa. Kaa chini tafadhali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hata kama unapotoshwa?

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini! Nasema kaa chini! Siyo tabia nzuri hiyo, ninapokuwa nimesimama, wewe acha nimalize, kisha nitakupa nafasi kama unataka kusema. Hakuna Mbunge ambaye mimi nakuwa Mwenyekiti nakosa kumpa nafasi, hiyo mikono haisaidii, naipuuza kwa sababu nashughulika na mtu mwingine na wananchi wa Kawe mnaona mlivyochagua kituko.

Sasa naendelea kumalizia, kwamba, Mheshimiwa Ndugulile nakutoa nje ya Bunge, ndiyo adhabu ninayokupa kwa vikao vitano mfululizo. *Sergeant-at-Arms,* mtoeni Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, vikao vitano mfululizo asionekane hapa. Hiyo ndiyo adhabu ninayoitoa. Mara moja hilo lifanyike sasa hivi, na utaratibu ni ule ule mpaka nje ya geti la Bunge.

*(Hapa Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile Alitolewa Nje ya Eneo la Bunge)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli za Bunge, na nirudie tena, Mheshimiwa Halima Mdee tutafuata taratibu za Bunge. Kama una jambo la kusema, utasimama mahali pako, nitakupa nafasi, lakini utaratibu wa kuropoka, si wa Kibunge, popote pale duniani! Nikiwa nimesimama, huruhusiwi kuzungumza. Utasimama mahali pako. Taarifa sipewi mimi, bali taarifa unampa Mbunge mwingine. Soma kanuni. Unanipa taarifa ya nini? Ni Mwenyekiti wa Kamati wa kikao gani anapewa taarifa? Hilo halipo!

*(Hapa Mheshimiwa Halima Mdee alikuwa akiongea kichini chini)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, nakusamehe kwa mara nyingine, tabia yako ni tabia isiyokubalika hata kidogo! Ni tabia inayotia aibu, tafadhali achana na tabia hiyo. Najua unataka umaarufu, nikufukuze na wewe, ili kesho uandikwe katika magazeti. Sifanyi hivyo! Lakini wewe ninachofanya ni kupuuza tu.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuipongeza Wizara ya Ardhi hii kwa ubunifu mkubwa wa masuala ya ujenzi na uendeshaji wa Wizara hii. Pia pongezi hizi apewe Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa *NHC. Team* hii ni nzuri, tatizo ni uwezo wa Serikali kukosa fedha za kutosha, na hii yote ni ukosefu wa vipaumbele kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, kumekuwa na ukiukwaji mkubwa sana wa kisheria juu ya ardhi. Tatizo kubwa ni ukosefu wa uaminifu kwa watendaji wa ngazi ya Kata wa Ardhi. Vijana wengi wanayo tamaa ya fedha, na hii inafanya wananchi wasiamini tena Wizara nzima, wakati wachache ndiyo wabaya. Ni vyema wakati wa kuwapa watu madaraka, viangaliwe sana tabia na uwezo wa mtu husika kama ni mwaminifu, bila hivyo, itakuwa ngumu sana Wizara hii kuonyesha uwezo wake wa kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa, Wizara hii huingiliana na Wizara karibu zote na matokeo yake kukitokea tatizo, kila Wizara inajitoa na matokeo yake migogoro haiishi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini msiunde Baraza la pamoja au Tume Maalum ya kusimamia migogoro inayoingiliana moja kwa moja na Wizara ya Ardhi? Mfano, suala la Missenyi na vitalu vya wawekezaji, ni Wizara mbili zinahusika. Mpima ardhi ni Wizara ya Ardhi, lakini mgawa ardhi hiyo au muuza ardhi ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati wanauza ardhi hiyo kwa wawekezaji, waliuziana na wananchi na nyumba zao na mashamba yao na watoto wao. Jambo hili ni aibu kubwa sana. Mpima ardhi anajua kabisa ameingilia ardhi ya wananchi na huku akiona watu wamo humo, bila kujali kuwa watu wako hapo. Hilo ni kosa. Wizara ya Ardhi kupima, huku wapo watu ndani, na Wizara ya Kilimo na uvuvi wakawauzia wawekezaji, na hawa wawekezaji bila kujali wameingia na kuanza kuwapiga, kuchoma nyumba zao na hata kuwaua. Kesi hizi bado hazipewi uzito kwa sababu, nani awajibike, kati ya Wizara ya Kilimo na uvuvi na Wizara ya Ardhi? Lakini kama kungekuwepo chombo cha kuunganisha, Wizara hizi tatizo lisingelikuwepo. Chombo kingechukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, suala la Narco Missenyi siyo la kiungwana hata kidogo. Ni dhuluma tupu! Naomba wakati Waziri anahitimisha hotuba yake, nipewe majibu ya hatima ya wananchi wa Kata za Kakunyu na Nsunga, maana wananchi wamechoka.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia na mazoea ya Maafisa Ardhi katika Halmashauri mbalimbali kutokuwa na nidhamu ya kazi, kupokea rushwa, kupima, kuuza maeneo ya wazi na kuzitolea hati na kufanya *double allocation* ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara iangalie kwa upya uwajibikaji wa Maafisa Ardhi na wawajibishwe kwa wakati pale inapothibitika wanafanya *double allocation* ambayo husababisha kuendeleza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Sheria No. 5 ya Ardhi ya mwaka 1999 inatambua Hati za Kimila zinazotolewa na vijiji husika. Hati zimekuwa haina uzito wa kisheria pale wahusika (wamiliki) wanapokwenda kuomba mikopo katika Benki au Taasisi nyingine za fedha, hawapati, kwa kuwa hati hizo hazina uzito wa Kisheria. Je, Serikali inatoa mwongozo gani kwa mabenki na Taasisi za fedha kuridhia na kuzitambua Hati za Kimila?.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ipitie kwa upya na kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi. Ukitizama sheria No. 4, inaelekeza kuwa, mtu anatambulika kuwa na umiliki kwa hati inayotolewa na *commissioner;* na Sheria No. 5 inatambua Hati za Kimila. Kwa kuwa Sheria husika inaonyesha usawa kwa hati mbili hizo, lakini inapotumika katika Benki na Taasisi za kifedha, hati inayotolewa na *commissioner* ndiyo inakuwa na nguvu ya kisheria. Nashauri Serikali ilete Muswada wa marekebisho ya Sheria za Ardhi ili kuleta usawa kwa wananchi wote mbele ya Sheria na ili kuondoa mkanganyiko wa Sheria hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, kuna urasimu na mlolongo mkubwa wa mwananchi kupata hati miliki. Urasimu huu hupelekea mwananchi kukosa haki yake ya kushindwa kupata *title deed* ya eneo lake. Hata hivyo, kwa kuwa utaratibu huu husababisha rushwa kwa Maafisa Ardhi katika Wilaya ambao ndiyo huanza na huhusika katika maandalizi ya awali ya kupata hati kabla ya kwenda kwa *commissioner* kwa hatua za mwisho, naishauri Serikali kufanya upya utaratibu huu ili kuondoa urasimu na kupunguza ushawishi wa rushwa inayotolewa na wananchi na kupokelewa na Maafisa ardhi ili mwananchi apate hati kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, natambua migogoro ya ardhi ni changamoto kubwa nchini na zinahitaji jitihada zaidi za kukabiliana na zitafanikiwa kukiwa na ushirikiano wa pande zote, kwa maana ya wananchi, Watendaji wa Ardhi (Serikali) na Viongozi wa Kisiasa. Migogoro mikubwa ya ardhi ipo katika Mkoa wa Arusha na hasa Wilaya ya Karatu, ikijumuisha ubadilishaji wa matumizi ya ardhi ambao hufanywa na wawekezaji wanaomiliki ardhi nchini. Hivyo, kutumia vibaya ardhi ya Watanzania ni kuipotezea Serikali mapato mengi. Naishauri Serikali iunde Tume Huru ya Kuchunguza Mgogoro wa Ardhi Nchini na hasa Mkoa wa Arusha.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kwamba kesi za ardhi zihamishiwe Mahakamani na Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria waajiri Mahakimu 133 kwenye kila Mahakama ya Wilaya ili wawe wanashughulikia migogoro ya ardhi tu, kwani

Mahakama hizi za ardhi ziko kwenye baadhi ya Mikoa, na ni vigumu watu wa Vijiji kushughulikia matatizo yao ya ardhi kutokana na umbali na gharama kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matatizo ya kupima ardhi moja kwa watu wawili hadi watatu. Naomba Serikali iwachukulie hatua Maafisa ardhi wanaofanya mchezo huu mchafu, kwani umekuwa unaliingiza Taifa kwenye matatizo na hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la matatizo ya ardhi Kibondo Mjini. Mji wa Kibondo ulioko Jimbo la Muhambwe, Maafisa Ardhi wamepima viwanja hovyo hovyo eneo la stendi mpya na kusababisha migogoro kwa wananchi. Napenda kupata majibu, mgogoro huu utatatuliwa lini?

Mheshimiwa Spika, Kibondo ni Wilaya iliyo mbali na Mkoa takribani kilomita 300 jambo ambalo siyo rahisi kupeleka malalamiko ya ardhi Mkoani. Wananchi wanaomba Serikali ipeleke Baraza la Ardhi huko.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua hatua ya kuanzishwa kwa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kasulu. Ni ajabu kuona Mkoa mzima wa Kigoma ukiwa na Baraza la Wilaya moja la Kigoma, tena ambalo linatajwa kuwa na mwamuzi wa migogoro mmoja au wawili. Mkoa huu unakadiriwa kuwa na wakazi kati ya milioni mbili hadi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni haki kwa Manispaa ya Kinondoni inayotajwa kuwa na waamuzi wawili wa migogoro ya ardhi? Aidha, Manispaa hiyo inatajwa kuwa na asilimia 50 ya migogoro yote nchini. Serikali inatoa kauli gani kutatua tatizo hilo la uhaba wa waamuzi wa migogoro ya ardhi Kinondoni, kutoka wawili kama ilivyo hivi sasa, lakini pia pamoja na kutatua tatizo hilo kwa maeneo mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ishughulikie tatizo la uhaba wa Maafisa Ardhi. Hili ni tatizo kubwa, naomba Serikali ihakikishe kila Wilaya iwe angalau na Maafisa Ardhi wawili. Hapa nasisitiza pia Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa la raia kupewa ardhi kwa mujibu wa sheria, lakini maeneo wanayopewa ni hifadhi ya ardhi. Tatizo hili ni kubwa nchini, Serikali ni moja, iweje Wizara mbili zigongane?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba uwekezaji mkubwa uangaliwe. Tufuate mfumo wa Uganda ambapo wakulima wadogo wanapewa 2/3% ya eneo la uwekezaji wa shamba kubwa. Hii itaondoa dhana ya mabepari kupora nchi yetu, lakini zaidi, ni njia ya kujenga uchumi wa raia.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara kwa bajeti nzima, lakini pia kwa jitihada mpya zinazoonekana. Nampongeza Waziri kwa shughuli ya kupanua eneo letu la bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza, tunaomba Makazi mapya ya Utawala yatekelezwe ili makazi ya maeneo mapya ya utawala yajengwe vizuri, kila mara Serikali iwe na *“ahead of the people”* wasijenge bila ya kupimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wageni, wananchi na Serikali, Wizara/Idara iwe macho ili wageni wakubwa na wadogo wasichukue visivyo halali maeneo ya ardhi katika maeneo ya mipakani. Watu ambao sio Watanzania wamechukua ardhi. Hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali/Wizara iendelee kupima viwanja na kuwapa wananchi kwa wao kurudisha gharama kama ilivyofanya Bunju, Mwongozo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kwanza kwa kuwapongeza Waziri na Naibu waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kutokana na umuhimu wa ardhi nchini. Napendekeza Wizara iwe na mpango wa muda mrefu kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kuongeza kasi ya kugawa vijiji nchini na kutoa hati miliki kamili kwa wananchi kumiliki ardhi zao. Ni muhimu sana kuwe na mwendelezo wa *land use plan* ili maeneo ya mashamba yasigeuzwe miji (mahali ambapo ukaribu wa mashamba husika unasaidia *greenery* katika eneo husika,

na kusaidia uzalishaji wa chakula, mboga na mboga na mahitaji mengine ya wananchi).

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kutoa mwongozo jinsi ya kupima na kupanga Miji midogo na matumizi ya ardhi katika maeneo yanayozunguka Miji hii midogo. Pia Miji midogo iendane sambamba na miundombinu ya umeme na maji kwa ajili ya wakazi na ongezeko la wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Singida Kaskazini, naomba sana vijiji vyote vipime na hati miliki zitolewe kwa wananchi ili iwe kichocheo cha kukua kwa maendeleo ikiwa ni pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uendelezaji wa upangaji wa maeneo haya uende sambamba na mpango wa Taifa wa umeme vijijini na miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuchangia katika sekta hii muhimu ya ardhi, kwani ardhi ni mali, ardhi ni kila kitu na ndiyo maana kutokana na umuhimu wa ardhi kumekuwa na mauaji na migogoro isiyokwisha. Naomba Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe taratibu zinafuatwa ili wananchi wapate haki zao za umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wabunge wote kulalamikia suala la migogoro hii, bado Serikali haichukulii kwa umuhimu na kuzipatia fedha Wizara ili waweze kupima ardhi na kutoa hati kwa kuwa ardhi ndiyo mkombozi wa

wananchi, hasa wale wa kipato cha kati na chini ili kupata mikopo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukosefu wa vifaa vya upimaji ni jambo linaloshangaza na limerudisha nyuma sana mipango mizuri ya Wizara. Ni matumaini yangu tatizo hili litapungua kama si kwisha kabisa katika kipindi kifupi nikiamini Wizara itaipa kipaumbele kitengo cha upimaji na ramani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linaloshangaza ni kwamba wananchi wameshaelewa maana ya ardhi na thamani yake. Hivyo, hapa ndipo Wizara ingeweza na nina uhakika Serikali ingekusanya fedha nyingi kwa malipo ya upimaji na hati. Ni vyema Serikali itambue umuhimu huu na kutoa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba ni maisha na bila makazi unakuwa huna tofauti na mnyama. Nichukue fursa hii kuwapongeza watendaji wa *NHC* kwa mwono wao wa mbali *(visionary),* lakini pamoja na utaratibu wao wa *menu* kama hotelini, bado nyumba ni za bei ya juu.

Kwa utafiti kidogo inaonesha kuwa bei zinakuwa hivyo kutokana na *VAT* kuwa juu. Suala la kujiuliza, kama Serikali inatoa misamaha ya kodi kwa Makampuni ya nje ya madini kwa mabilioni, ni vipi ishindwe kutoa msamaha kwa wananchi wake kuishi katika makazi bora kupitia *VAT* katika vifaa vya ujenzi? Wakati huo huo ilani ya CCM inasisitiza umuhimu wa wananchi kuishi katika makazi bora.

Mwisho, Serikali inapoanzisha mradi, isiwabughudhi wananchi kabla ya muda wake kuanza. Imekuwa ni jambo

la kushangaza Serikali kuwaondoa wananchi halafu eneo haliendelezwi.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wanavyojikita kwa dhati kusikiliza kero za ardhi na kuzitafutia majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa, bado kuna mapungufu mengi sana katika utendaji wa Maafisa wa Wizara ya Ardhi na kuwa sehemu ya migogoro. Mfano halisi ni Msajili, anajiingiza sana kwenye matatizo kwa kusimamia sehemu ya migogoro.

Mheshimwa Naibu Spika, nina ushahidi wa kutosha, na mara ya mwisho Naibu Waziri, ninamshukuru sana na kumpongeza sana alikuwa mkweli na muwazi kabisa, lakini pamoja na maelekezo aliyopewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, bado ameendelea kuwa sehemu ya mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafute pesa za kutosha kwa ajili ya kupima viwanja vya makazi na biashara, wasingoje mpaka wananchi wajenge kiholela, kwani inakuwa taabu sana kupata miundombinu ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo ambayo Serikali inakuwa ni sehemu ya migogoro, mfano Wilaya ya Mufindi. Miaka ya 1970 Serikali ilichukua maeneo makubwa kwa ajili ya kupanda miti, bila kufuata utaratibu takribani hekta 135,000 ambazo hazijatumika zote. Leo hii idadi ya wananchi imeongezeka na hawana ardhi kwa ajili

ya uzalishaji mali. Naomba Wizara ya Ardhi itusaidie kusudi Serikali iruhusu sehemu ya ardhi ambayo haijatumika irudi kwa wananchi waendelee kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie sana, kwa baadhi ya maeneo ya ardhi yetu kununuliwa na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali yetu iangalie sana Mahakama/Mabaraza ya ardhi kuwa sehemu ya kero za ardhi na kesi zao zinachukua muda mrefu mno sababu tu Mahakimu/Wenyeviti kuwa sehemu ya matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Serikali inatakiwa kulifanyia kazi ni suala la kulipa fidia kwenye maeneo yanayochukuliwa na Serikali, liwe la haraka na tathmini iwe halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kulifanyia kazi suala la leseni za makazi, zitambulike na ziweze kutumika kuwasaidia wananchi kupata mikopo, kwani kuna baadhi ya Taasisi za Kibenki hazitambui hizi leseni za makazi. Hii ni kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, natambua uwezo, hari na pia nia ya dhati ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri katika kuiongoza Sekta hii ya Ardhi, na naunga mkono bajeti ya Wizara ya Ardhi asilimia kwa 100.

**MHE. SLYVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali ione haja ya kuyafanyia kazi maboresho Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya ngazi za vijiji na Kata kwa kuwajengea uwezo Wajumbe wa Mabaraza

ya Ardhi na Nyumba sambamba na Makatibu wa Mabaraza hayo ili uwezo huo uwawezeshe kuzitafsiri sheria ili haki stahili ziweze kutendeka na kuonekana kwa pande zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri pia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba, ya Kata yaruhusiwe kuyasikiliza madai ya ardhi yanayozidi ekari 31, kwa kuwa sheria za sasa, ardhi yenye zaidi ya ekari 30 Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya ngazi ya Kata hayaruhusiwi kusikiliza madai ya kipande cha ardhi kinachozidi ekari 30. Mabaraza ya ardhi na nyumba ya ngazi ya Kijiji na Kata Kimsingi ni Mabaraza ya usuluhishi.

Hivyo, kwa kiasi kikubwa yanaongozwa pamoja na mambo ya kimila ya eneo husika. Kwa sababu hiyo, wenyeji wa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ngazi ya Kijiji na Kata huwarahisishia Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ngazi ya Kijiji na Kata huwarahisishia Wajumbe wa Mabaraza na Makatibu wa Mabaraza hayo kuubaini ushahidi unaotolewa dhidi ya madai ya ardhi na nyumba na hivyo uamuzi unaotolewa huwa na haki kwa pande zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ibadilishe utaratibu uliopo hapa nchini wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba wa kutoa hukumu/uamuzi kwa lugha ya Kiingereza na kuzitaka/kuyataka Mabaraza hayo kutoa uamuzi wa madai yaliyosikilizwa na kuamuliwa kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi walio wengi waweze kuujua na kuutafsiri uamuzi huo ili kama madai ama mdaiwa asiporidhika, iwe rahisi kwake kuukatia rufaa uamuzi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iwaone Makatibu wa Mabaraza ya Kijiji na Kata kama wadau muhimu katika jamii. Hivyo kwa umuhimu huo, Serikali inatakiwa iwawekee mishahara ili kuwaepusha katika ushawishi wa rushwa kulingana na kutokuwa na mshahara. Washauri wazee wa Mabaraza ya Ardhi na Madiwani wa kila Halmashauri ya Wilaya, kwa kuwa Madiwani ni miongoni mwa Wazee wa Mabaraza hayo, hivyo watakaochaguliwa kuwa washauri wa Mabaraza hayo watakuwa wanawajibika kwa wapigakura, hivyo uaminifu utakuwa mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wana Mbeya ambao ardhi yao ilichukuliwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe, nahitaji kauli ya Serikali ni lini wananchi hawa watalipwa fidia zao na kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbeya Mjini tunahitaji Waziri sasa atutembelee au atume timu yake anayoiamini ije Mbeya kushughulikia vilio vya wananchi ambao wana malalamiko ya ardhi zao kuporwa na Serikali ya Jiji. Wako wananchi wameporwa mpaka ekari 10 na walipokwenda kulalamika kwa wahusika waliahidiwa kupewa fidia ya kupewa *just* kiwanja kimoja tu ambacho ni chini ya ekari moja. Sasa hii siyo halali na haikubaliki kwa malalamiko haya ya wananchi kuporwa ardhi kwenye maeneo ya Ilomba *(VETA)* Mwakibete.

Mheshimiwa Naibu Spika, orodha ya majina ya wananchi wanaolalamika ninayo, na niko tayari kuisaidia Serikali/Wizara iwapo itakuwa na dhamira ya dhati ya kutatua vilio hivi vya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, na nasubiri Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya hoja zangu zote mbili wakati wa majumuisho.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hotuba nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi, nyumba, na maendeleo ya makazi ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya Watanzania. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa ardhi nzuri na eneo kubwa na tunajivunia kuwepo hapa Tanzania. Pamoja na kuwa na ardhi kubwa, bado changamoto ni kubwa sana katika suala la mipango miji na vijiji. Mara nyingi kumekuwa na ujenzi holela ambao unasababisha makazi yasiyo rasmi katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Geita kuna vijiji ambavyo sasa vimefikia hatua ya kuwa Mji kutokana na ukuaji wa haraka. Mfano, Katoro, Rwamgasa, Nyarugusu na Bukoli, lakini hakuna mpango wowote wa kuondokana na makazi holela. Kwa vile katika hotuba ukurasa wa 47 umetoa maagizo kwa Halmashauri zote nchini kwamba zihakikishe kuwa zinapima na kuvigawa viwanja kwa wananchi, naomba kuwe na usimamizi wa utekelezaji wa

maagizo haya, pamoja na usimamizi wa maagizo, pia Serikali ipeleke fedha kwenye Hamashauri hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yao. Kuna upungufu wa watumishi katika sekta ya ardhi. Naomba Serikali iweke kipaumbele katika kuongeza watumishi ili waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nyumba, naiomba Wizara iwekeze katika Mkoa mpya wa Geita. Katika hotuba, nimeona jinsi ambavyo *NHC* imepanga miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi na majengo ya biashara itakayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa katika mwaka 2012/2013. Sijaona Mikoa mipya, kwa kuwa Mikoa mipya ikiwemo Geita inahitaji miundombinu muhimu ikiwemo nyumba. Naiomba Serikali iweke kipaumbele katika Mikoa hii, maana uhitaji wa nyumba ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba Serikali iyazingatie na kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 80 wa hotuba ya Waziri, unasema jumla ya mapato ya Serikali ni Sh. 99,816,438,480/= na jumla ya matumizi ni Sh. 101,731,722,000/= ambapo kuna upungufu wa Sh. 1,915,283,520/= katika mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kama mapato ya Serikali ni Sh. 99,816,438,480/=, inawezekana vipi matumizi yakawa Sh. 101,731,722,000/=? Je, upungufu wa mapato ya Serikali wa Sh. 1,915,283,520/= unalipwa toka mfuko gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Waziri asikubaliane nami kuwa watu waliomilikishwa mashamba kipindi cha ubinafsishaji na hawajayaendeleza hadi leo, yataifishwe, yarejeshwe Serikalini na kisha wapewe Watanzania/wawekezaji wenye nia ya dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mashamba gani na mangapi ambayo hayaendelezwi mpaka sasa?

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza hotuba ya Wizara kwa vile imefafanua kwa kiasi kikubwa nini Serikali ilifanya mwaka 2011/2012 na yale yatakayofanyika kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013. Zaidi, nawapongeza Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka - Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi Wakuu wote wa Wakala zilizoko chini ya Wizara kwa jitihada zao katika kushughulikia masuala ya ardhi na makazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu kuwalipa fidia kwanza wananchi mahali popote nchini ambapo ardhi inahitajika kwa matumizi ya umma ili kuzuia migogoro ambayo inaweza kujitokeza. Hivyo, napongeza juhudi za Serikali za kuanzisha mfuko wa fidia ya ardhi na chombo cha kusimamia hazina ya ardhi. Kwa msingi huo, ni muhimu Sheria husika iletwe haraka Bungeni, kwani kwa miaka mingi wananchi wamedhulumika katika ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza suala la migogoro ya viwanja hasa mijini, yafaa pawe na mkakati madhubuti wa kuhakikisha kuwa kunakuwa na uhakika wa viwanja ili kutambua *"double allocation"* zilizopo, kwani haya yanatokea kwa sababu aidha ya uzembe au rushwa miongoni mwa baadhi ya Watendaji wa Idara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu ardhi kubwa ambayo haiendelezwi na wahusika ambao wanahodhi maeneo makubwa bila kuyaendeleza kwa malengo tarajiwa. Nashauri maeneo hayo yatwaliwe na Serikali na kuruhusu watu wengine kugawiwa kwao upya. Nafahamu kuna hatua zimeanza, lakini kasi iongezeke zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Shirika la Nyumba la Taifa kwa kuamua kujenga nyumba za kisasa katika maeneo mbalimbali nchini, kwa ajili ya kupangisha au kuziuza. Hata hivyo, nashauri Shirika lijenge nyumba ambazo miundombinu yake inazingatia mahitaji ya wananchi wenye ulemavu ili endapo familia zitakazonunua nyumba hizo na wanafamilia wenye ulemavu isiwe tatizo kwao. Nasisitiza Mainjinia wa Shirika wakumbuke suala hili kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikuwa na mpango wa kujenga kituo cha kuchukulia picha za *satelight* ili kusaidia kupunguza tatizo kubwa la kupima ardhi na kutoa hati ambapo ingesaidia Mikoa mingi. Je, Wizara imefikia wapi kufanikisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua na tunaona jitihada za Wizara kuwavunjia watu wanaojenga kwenye maeneo ya wazi na ambayo hayaruhusiwi kujengwa hasa katika eneo za fukwe na baadhi ya watu wanaohusika ni baadhi ya Wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri alitembelea na kuamuru maeneo hayo yavunjwe. Mbali na kwamba zoezi linaendelea, lakini nyumba hizo zimeachwa. Nini kigugumizi cha kuacha kuendelea kubomoa nyumba hizo, kwa watu hao wanaotumika nafasi zao za kisiasa na nguvu za fedha kuvunja sheria na amri halali ya Wizara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imejipanga vipi kuondoa urasimu wa baadhi ya Maafisa Ardhi ambao sio waaminifu, kuwazungusha kwa lengo la kutaka rushwa kwa Watanzania wanaohitaji viwanja?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatambua hati za Kimila, lakini Watanzania waliomilikishwa hati za Kimila, kushindwa kutumia hati hizo kupata mikopo, kwa kuwa Mabenki hayazitambui hati za Kimila: Je, Wizara imejipanga vipi kuwasaidia?

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Dodoma Mjini wana matatizo makubwa ya ardhi na Jeshi la Magereza katika Kata ya Msalato na Makutupora. Jeshi la Magereza wameporwa ardhi ya wakulima, wala hawataki kupisha maeneo hayo, na wala hawana vibali vya kukalia ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa namba kwa nyumba, pia una kasoro. Baadhi ya nyumba zinapewa namba, baadhi wananyimwa. Jambo hili linaleta hofu kubwa sana kwa wale wanaonyimwa namba. Ili kudumisha utawala bora, na kuondoa hisia mbaya ambazo zimejengeka kwa wananchi dhidi ya Serikali yao, naomba yafuatayo yafanyike:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ashirikiane na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kuliamuru Jeshi la Magereza kurejesha ardhi ya wakulima wetu wa Kata za Msalato na Makutupora na Mbalawala, na kuwapa onyo waache kabisa tabia ya kupora ardhi *(land plundering, Zionism and Expansionism),* ambayo wanajitwalia pasipo kibai cha mamlaka za Miji zilizokasimiwa na Mamlaka kugawa ardhi kwa wanajeshi na raia wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile zoezi la kuweka namba kwenye nyumba lifanyike kwa nyumba zote bila ubaguzi. Nchi zilizoendelea kama Afrika ya Kusini, walifanya zoezi la kugawa namba. Walizigawa namba hizi kwa watu wote wenye maeneo yaliyopimwa na yale ambayo bado hayajapimwa. Kisha, wale ambao hawajapimiwa, walipimiwa. Aidha, maboresho yalifanyika na maeneo yote ya Miji yameendelea kuwa safi na yenye kuvutia sana baada ya maboresho kufanyika.

Kwa kuhitimisha, ni kazi ngumu sana kwa Mbunge wa Dodoma Mjini kuendelea kuulizwa maswali juu ya mambo yaliyojificha ambayo hata mimi Mbunge eti sitakiwi kujua: Je, niseme nini kuhusu ardhi inayoporwa na Jeshi la

Magereza? Je, niseme nini kuhusu nyumba zinazopewa namba na zile zinazonyimwa namba hapa Dodoma Mjini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa nini tuwe na sera Kiziwi *(vague policy)*? Kwa nini Serikali isieleze maana ya mtu kupewa namba na kunyimwa namba? Kwa nini tuwafanye wananchi wetu kuishi katika hali ya heka heka wakati wote? "*Honesty is the best policy",* Msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Serikali ifafanue maana ya mtu (nyumba) kupewa namba, au kunyimwa namba ili watu wajue, na kama ni kuhama, wajiandae mapema. Jeshi la Magereza pia lirudishe ardhi waliojitwalia Msalato, Makutupora na Mbalawala, pasipo kibali cha Serikali, huu ni ubabe. Majeshi yetu ni majeshi ya wananchi na kwa ajili ya wananchi, na wala siyo majeshi ya kibabe ya kunyanyasa wananchi.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza hotuba nzuri iliyotolewa na Wizara na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri kwa Wizara kwamba ichunguze Watendaji wake, kwani wamekuwa kikwazo na kuwa na njama za kuuza viwanja bila Wizara au mamlaka kuwa na habari, hivyo kufanya shughuli zote hizo kuwa udanganyifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hati za ardhi zinachelewa sana bila sababu ya msingi. Hivyo Wizara ijipange upya kuona na kufupisha muda wa kupata hati. Hati zinachukua miaka zaidi ya mitano; *why*?

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya uwekezaji ni tatizo linalokumba Wizara mtambuka, lakini ni tatizo kubwa kwa wakazi wa eneo hilo. Tunaomba wananchi wapewe umuhimu sana, na huko tuendako kuna tatizo kubwa sana. Ushirikishwaji nchini bado ni mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba *NHC* ije Wilaya mpya ya Buhigwe wajenge nyumba za watumishi kukabiliana na uhaba mkubwa wa nyumba za watumishi. Wizara ya ardhi iwe na kipaumbele na kitu cha kuanza kufanya, kwani matatizo ya Wizara hii ni mengi. La sivyo, hatutaona kipi kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo matatizo ya migogoro ya ardhi, hati za ardhi, ujenzi holela, pango la nyumba, msongamano wa nyumba, nyumba duni, na nyumba za watumishi wasio waaminifu. Nashauri muwe na kipaumbele, la sivyo, pamoja na uchapakazi wa Mawaziri, hamtaweza kufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri aangalie Watendaji wa Ardhi, wengi hawako chini yake, hii itakugharimu wasipoweka mfumo wa Utawala ndani ya Halmashauri. Tuangalie utendaji wetu wa kutoa viwanja kama inavyotokea ubomoaji wa nyumba za *Mbezi Beach*. Tujichunguze, na Waziri tunakuomba uwe mkali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakutakia mafanikio mema katika kazi ngumu sana, lakini jipe moyo.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la wenye nyumba kuendelea kuwanyanyasa wapangaji kwa kuwatoza kodi kubwa bila mpangilio na

kuwataka walipe kodi ya mwaka na mara nyingine kwa kulipa kodi kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wanaotaka Serikali ilete Muswada wa Sheria ili Bunge litunge Sheria itakayoweka utaratibu mzuri wa upangishaji majengo/nyumba ikiwa pia na Serikali kupata kodi ya thamani kwa wenye nyumba ambao kwa sasa wanatoza kodi kubwa, lakini Serikali haipati kodi yake, yaani *(VAT).* Ni vyema Sheria itungwe ili kuwepo na haki kwa pande zote na Serikali iweze kukusanya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maafisa Ardhi kwenye Halmashauri kufanya wanavyotaka na kuendeleza migogoro ya ardhi na Wizara kushindwa kuwachukulia hatua. Ni vyema sasa Serikali ikaona umuhimu wa Maafisa Ardhi kuwa chini ya Wizara ya Ardhi kuliko ilivyo sasa ambapo Maafisa Ardhi hao wako chini ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi inashindwa kuwachukulia hatua za kinidhamu pale wanaposhindwa kutimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Anna Tibaijuka – Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa asilimia mia kwa mia na ninawapa *hi!*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee na ujenzi wa Mji mpya wa Kigamboni. Hii ni hazina ya nchi hii, lakini zaidi ni heshima kwa nchi, kwako Mheshimiwa Waziri na familia yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee na *program* yake ya kuwashughulikia wavamizi wa maeneo. Mwananchi sasa anadai nyumba, siyo kiwanja, kubomoa maeneo ya fukwe za Pwani kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Waziri. Asimamie upimaji wa viwanja na maeneo kwa uhakika, kwani kuna madalali ndani ya Wizara yenyewe, ambao huwa wanawaelekeza wageni kuomba na kuwapatia maeneo kwa muda mfupi kuliko Mtanzania mzawa. Mheshimiwa Waziri angalia vyema katika Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za *NHC* ni ukombozi mkubwa kwa maendeleo ya nchi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla, kwani tatizo kubwa kwa mwanadamu, ni nyumba ya makazi. Ukiwa una makazi ya uhakika, basi hata wizi na rushwa nchini vitapungua, kwani ni kweli kabisa kuna haja ya kuwa na nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iendelee kutunza, Mji tulionao, lakini ijitahidi kupanua maeneo nje ya Mji kwa kupunguza *congestion* iliyopo mjini. Miji ninayopendekeza pembezoni mwa Miji mikubwa, kama vile Miji ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na mingineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *duplication* ya kutoa hati katika Halmashauri, jambo ambalo linashusha hadhi ya Wizara yako, na ni vyema kwa Wakurugenzi na Watendaji wanaofanya makosa ndani ya Halmashauri na hata Wizarani wadhibitiwe na kuchukuliwa hatua kwa maana ya Waziri kuwawajibisha ili kulinda heshima ya Tanzania.

Mheshimiwa Waziri, endelea, *(aluta continua).*

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya kuuza viwanja vinavyopimwa ipunguzwe ili vijana nao waweze kununua viwanja hivyo na kumiliki ardhi ili hatimaye waweze kujenga na kuishi kwenye nyumba bora na pia waweze kutumia rasilimali hiyo kupata mkopo Benki na kuweza kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Uwekezaji ya *EPZ* na mingineyo inayohusisha kuchukua ardhi ya wananchi kama miradi ya uchimbaji wa madini. Serikali lazima itazame upya sera ya uwekezaji ili wananchi waweze kufaidika na ardhi yao na thamani ya mali inayopatikana katika ardhi. Nashauri wananchi wanapoondolewa, ili kupisha uwekezaji wajengewe nyumba bora na huduma za afya kwenye maeneo ya makazi mapya, wanapopelekwa pia wapewe hisa za umiliki kwenye miradi hiyo na itambulike kabisa kuwa wao ndio wamiliki halali wa ardhi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za *National Housing*, napongeza mradi wa ujenzi wa nyumba hizo na kulifanya Shirika kuwa na mabadiliko makubwa ikilinganishwa na hapo awali. Nashauri nyumba hizo ziondolewe kodi ya *VAT* na kwenye vifaa vya ujenzi ili wananchi waweze kununua nyumba hizo kwa bei nafuu, kwani sasa nyumba hizo zinauzwa bei kubwa sana, zaidi ya Shilingi milioni 120 jambo ambalo, ni kweli hakuna

mwananchi wa kawaida mwenye uwezo wa kuzinunua ikiwemo wafanyakazi katika Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba hizo zitanunuliwa na matajiri wenye fedha na wafanyabiashara wakubwa na Mafisadi katika Sekta ya Umma, kwani hata Mbunge hana uwezo wa kununua nyumba hiyo. Ikumbukwe kwamba katika mshahara wake, ameshakopa fedha kununua gari ili aweze kutekeleza majukumu yake ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Pili, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalamu wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhudumia Watanzania kupitia Sekta ya Ardhi. Pamoja na pongezi hizi ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa katika Wizara hii ni kupima ardhi Mjini na Vijijini na kuimilikisha kwa wananchi. Upimaji huu utarahishwa na kuharakishwa iwapo Serikali itakamilisha haraka mradi wa kujenga kituo cha kupokea picha za *satellite*. Ushauri ni kwamba Serikali itafute fedha popote ili kukamilisha mradi huu, kinyume chake, upimaji wa ardhi utachukua miaka mingi na hivyo kuchelewesha maendeleo ya nchi yetu na wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji wa mashamba Wilayani Manyoni, Wizara na MKURABITA mlianzisha mradi wa kupima ardhi za mashamba katika Wilaya ya Manyoni mwaka 2009/2010 ambapo Kata tatu zilinufaika, lakini mradi huu umesimama. Ombi ni kwamba,

mradi uendelee katika Kata zilizobakia. Aidha, katika vijiji vilivyopimiwa mashamba na hati za Kimila zitayarishwe *(customary righ of occupancy),* bado hati hizo hazijakabidhiwa kwa wananchi kwa wakati ule kwa vile vijiji havikuwa masijala za ardhi, kwa kuwa baadhi ya vijiji kama Chikuyu, Mbwasa, Kilimatinde, Sanjarundi na kadhalika, tayari wemejenga Masijala za Ardhi. Sasa Wizara ifanye utaratibu wa kukabidhi hati hizo kwa vile wananchi wanazihitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kuanzisha Baraza la Ardhi Wilaya ya Manyoni. Jengo la Baraza linakamilishwa kukarabatiwa, hivyo tunaomba Watendaji wa Baraza (Mwenyekiti na Wazee wa Baraza) waanze kutafutwa ili Baraza hilo lianze kufanya kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la kuyafunga Mabaraza ya Ardhi, siyo sahihi, na halifanani na hali halisi kwamba Mahakama za Kawaida za Mwanzo na Wilaya zinazidiwa sana na mahali pengi Mahakama za Mwanzo ama hazipo au hazina Mahakimu. Sasa iwapo Mabaraza ya Ardhi yataondolewa, hali itakuwa mbaya sana. Ombi ni kwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na TAMISEMI itenge fedha za kutosha kuwezesha Mabaraza ya Vijiji vyote na Wilaya, yafanye kazi kwa ufanisi, lengo liwe kuimarisha Mabaraza hayo na siyo kuyafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba ni moja ya mahitaji muhimu ya binadamu, hivyo Serikali ione uwezekano wa kuondoa kodi katika zana/vifaa vya ujenzi kama vile *cement*, bati na kadhalika, kama ilivyoondoa kodi katika elimu, afya, kilimo na kadhalika.

Shirika la nyumba linafanya kazi nzuri, lakini ili lijenge nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa kawaida ambalo ndilo jukumu lake la msingi, ni muhimu Serikali iliwezeshe kutekeleza azma hiyo kwa angalau kuondoa kodi ya *VAT* katika nyumba za watu wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupata nyumba ya kuishi kwa Mtanzania mwenye kipato cha chini, ni tegemeo la kila Mtanzania. Hivyo nyumba hizi inabidi ziwe na bei ndogo kabisa ili kila mwananchi aweze kununua na kuzimiliki. Hivyo, kodi za ongezeko la thamani *VAT* na kodi ya ongezeko la mtaji zinaongeza bei za nyumba hizi na kuwafanya wananchi washindwe kuzinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Mkurugenzi wa Shirika la nyumba, wachuke hatua za haraka ili kupunguza na ikiwezekana kuondoa kodi hizi kabisa ili kupunguza bei za nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wimbi kubwa la watu wanaovamia maeneo matupu na hata maeneo ya watu katika Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine iliyomo nchini, ingawa Mheshimiwa Waziri amesema siyo kazi ya Wizara kulinda maeneo haya, lakini imethibitishwa kuwa vibali hivyo vinatolewa na Maofisa wa Wizara hiyo, hivyo hawezi kukataa dhamana zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa likisababisha uvunjifu wa amani, vurugu na kujazana kwa kesi za madai katika Mahakama ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri awachukulie hatua kali sana Maafisa wote wanaotoa vibali batili ambavyo vinawapora wananchi viwanja vyao.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi – Mheshimiwa Tibaijuka na Naibu wake Mheshimiwa Ole-Medeye kwa kazi nzuri wanayoifanya tokea wakabidhiwe majukumu ya kuiongoza Wizara hii. Nawapongeza pia Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha MKURABITA kwa shabaha ya kuwasaidia wananchi hasa wa hali ya chini kwa kurasimisha mali zao na hasa ardhi ili waweze kunufaika na mali zao. Aidha, waweze kupata dhamana ambayo itasaidia kukopa katika mabenki na kujiletea maendeleo. Tatizo ni kubwa, hadi sasa ardhi haijapimwa kwa visingizio vya uhaba wa fedha na wataalam. Zoezi hili kwa Singida Magharibi, yaani vijijini halijatekelezwa. Napenda kujua lini upimaji utafanyika na mali za wananchi zirasimishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanashindwa kupata viwanja vinavyotangazwa kwa sababu gharama zinazotozwa ni kubwa na wananchi wa kipato cha chini hawawezi kumudu kulipa gharama hizo. Hili ni tatizo kubwa. Nashauri Serikali itazame upya suala hili ili kupunguza gharama kwa wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera/Sheria ya kuwa na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ni nzuri, inatazamiwa kupunguza mlolongo wa kesi katika Mahakama za juu. Vilevile kasi ya kusikiliza kesi au migogoro ya ardhi ingeongezeka, kwa hiyo ili yote hayo yapatikane, nashauri Mabaraza haya yapewe elimu kwa kufanyiwa Semina za mara kwa mara ili kuimarisha utendaji wa kazi wa Mabaraza haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mpaka ni kubwa ndani ya nchi na nje ya nchi. Ugomvi wa mipaka kati ya Wilaya na Wilaya umekithiri, lakini vilevile ugomvi kati ya vijiji na vijiji nao ni mwingi na inasikitisha kuwa migogoro hiyo haipatiwi ufumbuzi kwa muda mrefu. Hili lisipoangaliwa mapema, uvunjifu wa amani unaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Napongeza jitihada zinazofanywa na National Housing za ujenzi wa nyumba, hata hivyo bei ya kuuza nyumba hizo ni kubwa ambazo wananchi wa kipato cha chini hawawezi. Tutakuwa tunawadangaya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Tibaijuka na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa umakini na kujiamini. Nami nasema, njooni na Jiji la Mwanza kufuatilia hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa tatizo la ardhi husababishwa na Maafisa wa Ardhi kwenye kila Halmashauri kutokana na kupenda kitu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale mwanzo, katika maeneo mengi, watu ardhi yao imechukuliwa na hawajalipwa fidia zao. Mfano eneo la Kiseke Kata ya Ilemela, Bugarika Kata ya Pamba; pia kuna maeneo mengine kama Luchelele, Kamama, Nyanguku na mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri hupima viwanja kwenye mashamba ya watu, vikatoka viwanja zaidi ya vitatu, hufikia hadi viwanja saba, lakini mwenye ardhi hupewa kiwanja kimoja na vingine vikauzwa, lakini hata kiwanja kimoja hicho alichopewa ni lazima akinunue. Malipo anayolipwa ni kidogo, lakini hata hicho kiwanja alichopewa akinunue tena. Hii ni hatari sana. Tunaomba Sheria ya Ardhi iwe wazi na wananchi weielewe na kama kunahitajika marekebisho ya ardhi iletwe, kwani mtu ametunza ardhi miaka nenda rudi, lakini inapopimiwa mtu aliyekuwa anaitunza ananyanyaswa na ardhi hiyo. Sasa ni wakati wa kuwaangalia walinda ardhi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunaamini kwamba kupanga ni kuchagua. Siamini kama tunachagua kumrudisha Mkoloni kwa lugha ya kumpamba na kumwita mwekezaji, lakini wawekezaji hawa kuna na kuchukua ardhi kubwa na wananchi ambao walikuwa na ardhi hiyo kuwa hawana haki na wanaonekana wakorofi. Napenda kujua kama utatoa haki miliki kwa Mwekezaji, siku atakayoshindwa kuwekeza itakuwaje? Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kiongozi, hati yako unaweza kuipata kwa mwaka mmoja, au miwili, nanyi husema ndani ya miezi mitatu hadi sita. Lakini mwananchi wa kawaida huchukua miaka miwili hadi zaidi. Tunaomba mtilie msisitizo kwa watumishi wa ardhi ambao wanashughulikia suala la hati miliki. Mwasisitize kwamba hati ichukue muda gani ili itoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoongelea ardhi, ni lazima utagusa mambo mengi. Cha mno, ni bora katika Majiji yanayopanuka kwa kasi, ardhi ipimwe na ijulikane kwamba ardhi hii ni ya nini na hii ni ya nani. Mfano, Wilaya ya Ilemela katika Jiji la Mwanza, ardhi kama itapimwa na ikajulikana wapi magorofa, wapi Hospitali wapi nyumba za kawaida, wapi viwanja vya shule na mengineyo, tutapanga Mji katika mpango wa kuridhisha sana, kwani ardhi bado ni tatizo kubwa sana. Tutoe pesa ya kupima ardhi ili kuiweka ardhi kwenye mpangilio mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuandaa mikakati 15 ya kutatua changamoto kumi zinazoikabili Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kurejea changamoto ya pili, hivi sasa mara nyingi kumekuwa na tabia ya kuwaondoa wananchi katika maeneo yao Mijini na Vijijini kwa sababu au ya kupisha uwekezaji au kuanzisha maeneo ya mipango Miji. Katika zoezi hili kuna wanaolipwa fidia na wengine hawalipwi fidia. Wananchi hawa wanapohama ni dhahiri kwamba wanakwenda kuanzisha ujenzi holela mahali pengine. Mpango wa Taifa wa matumizi ya ardhi

bado haujaanza. Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kusitisha zoezi la kuwahamisha wananchi mpaka mpango huu utakapokamilika? Je, ni kwa nini wawekezaji wasipelekwe katika maeneo mapya au mipango ifanyike katika maeneo mapya kama ilivyofanyika Wilaya ya Mvomero na Uyui ili kuepusha usumbufu kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikumbuke kwamba kuwahamisha wananchi hasa maeneo ya vijijini kunaweza kuathiri suala la Kilimo Kwanza, kwani wananchi wengi hulazimika kuacha mashamba yao ambayo yako karibu na huduma za jamii kama umeme, maji na barabara na kuhamia maeneo yasiyo na huduma. Kwa hali hii, usafirishaji wa mazao unakuwa mgumu, pia kwa mazao kama mpunga, huweza kupanda bei na kuongezeka bei ya mchele kutokana na kukosekana huduma za kukoboa mpunga katika maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu kwa Serikali ni kwamba kama italazimika kuhamisha wananchi, basi ihakikishe inaandaa kwanza maeneo yenye mazingira mazuri kwa shughuli za Kilimo na nyingine ambazo walengwa walikwishazizoea.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NHBRA* inafanya kazi nzuri sana na inastahili pongezi, lakini kweli kasi yake ni ndogo sana na inaonekana hawana fungu la fedha za kutosha kwa ajili ya kueneza matokeo ya utafiti. Naishauri Serikali iongeze fungu la fedha ili wananchi wengi waweze kufaidi matokeo ya utafiti wa nyumba bora na za gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu

wake kwa uchapakazi wao wa kuridhisha. Mungu awabariki sana.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu wa maandishi katika Wizara hii katika maelezo ya Waziri katika ukurasa wa 51 pale aliposema kwamba, nanukuu: "Wawekezaji wa ndani na nje watapewa maeneo ya kuanza kujenga makazi ambayo yatatumika kuwahamisha wananchi watakaopenda kubaki Kigamboni."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Serikali kuona kwamba kipaumbele katika ujenzi huu kimewekwa zaidi kwa wawekezaji wa ndani kuliko wawekezaji wa nje ili kutoa nafasi kwa Watanzania wazawa kupata za ajira za muda, lakini kuhakikisha kwamba fedha nyingi zinabaki nchini kuliko kwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni Wizara ambayo ina umuhimu mkubwa katika nchi; ndiyo Wizara ambayo itatulindia ardhi au itatuuzia ardhi, ndiyo Wizara ambayo itatujengea mazingira mazuri ya kutuletea mipango Miji katika Wilaya, Mikoa, Miji na Majiji katika Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe. Wawekezaji kutoka nje mara nyingi huangalia zaidi maslahi ya nchi zao na siyo maslahi ya Watanzania na vile vile hufanya uchunguzi juu ya namna gani nchi zao zitafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la maendeleo ya makazi linapatikana kwa kuwa na eneo la

ardhi. Tanzania ni nchi ambayo ina eneo kubwa la ardhi, hata hivyo ujenzi wake ni holela kiasi kwamba tunapoteza hadhi na heshima ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikaangalia vyema Sheria ya ugawaji na uuzaji wa ardhi kwa wananchi ili ihakikishe kwamba Sheria ya ugawaji wa ardhi haziendi kinyume na sheria husika. Vilevile sheria itoe kipaumbele katika umiliki wa ardhi kwa Watanzania kuliko watu au wawekezaji kutoka nje. Lolote lenye maslahi na nchi, Mtanzania kwanza, na wageni baadaye.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, na nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo rasilimali muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa watu wote na hasa waishio vijijini. Hivyo, ni lazima kuwepo na *Land Tenure security* kwa raia wa Tanzania wote. Ardhi ibaki ni *Bona Fide Right* ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa Sheria za Ardhi Na. 4, na Na. 5 bado una matatizo mengi. Nashauri Wizara iboreshe eneo hili na kuweka *checkes and balances.* Aidha, nashauri Mabaraza ya Ardhi yote ngazi ya Kijiji, Kata na Wilaya yaimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe agizo kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia Sheria kuhakikisha kuwa vijiji vinatumia kanuni ya 76 ya kuhakikisha kuwa wanapotoa ardhi, apewaye awe ni

Raia wa Tanzania na apewe ardhi isiyozidi hekta 21, na pia Wilaya itoe ardhi isiyozidi hekta 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iunde *Interministerial Committee* na ipewe hadidu rejea *(TOR),* ambayo pamoja na mambo mengine itaandaa mkakati wa kumalizia migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima, wananchi na wawekezaji, wananchi na wachimba madini na wananchi na hifadhi.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kodi ya nyumba za *NHC,* ni ghali sana hasa kwa wafanyakazi wa kima cha chini. Je, wakaishi wapi? Kuanzishwa kwa *NHC* ni kwa ajili ya kusaidia watumishi, siyo wafanyabiashara. Pia vipi eti wanajenga nyumba kusaidia walalahoi na vipi nyumba ya vyumba viwili ya ukubwa wa *square* mita 56, yaani mita 7 x 8 = 56 kwa Sh. 42,000,000/=, wapi na wapi? Hivyo bei ya ajabu kabisa! Huoni ni kutaka mtumishi asimiliki nyumba?

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia leo oneo la Sinza lilipimwa, lakini leo hii wanajenga hata kuziba barabara, kila nyumba leo Sinza imepora barabara na kufinya barabara zote za Sinza, na wataalamu wako, Sinza sasa inakuwa kama Manzese au Vingunguti. Hakuna tofauti yoyote ile! Vilevile katika Wilaya ya Nkasi kuna baadhi ya wafanyabishara na baadhi ya watumishi wamepora ardhi kubwa na kuwakosesha wananchi ardhi. Pia tunaomba sana watusaidie kupima ardhi kwa ajili ya wananchi kupata hatimiliki hata za Kimila ili kuondoa ugomvi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii majumba ya *NHC* ya kuishi yamefunguliwa mabaa na mengine ni *RAGI* tu lakini hakuna maji mabomba yote yalikwishaoza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa na migogoro ya ardhi nchini inatokana na uadilifu mdogo wa Watendaji wa Wizara hasa ngazi ya Halmashauri. Pia uhaba wa Watendaji wa Kata na Vijiji unaotokana na uelewa mdogo wa Sheria ya Ardhi ya vijiji. Cha kushangaza, hata Wakuu wa Wilaya huingilia migogoro hiyo kwa kutoa uamuzi au amri zilizo kinyume na sheria, wakati mwingine viongozi wanaagiza ngazi za chini na zinakaidi. Naomba nitoe mfano na niombe Mheshimiwa Waziri achukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgogoro wa ardhi katika Kata ya Izimbya katika eneo Kyabalamba, Miziku, Kanyatembe na eneo lote la Guno Izimbya. Ardhi iliporwa tangu mwaka 2009. Kijiji kiliuza ekari 600 bila ridhaa ya wanakijiji kwa vigogo. Vigogo hawa walilipa zaidi ya Shilingi millioni sita kwa *VEO* Izimbya. Wananchi walilalamika na baada ya malalamiko, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba alimhamishia mahali pengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 11/03/2011 alifanya ziara Izimbya na kupokea malalamiko na kuagiza Wilaya ishughulikie suala hili. Wilaya iliunda Tume ambayo ilifanya kazi na kukabidhi taarifa yake tarehe 1/10/2011 ambayo ilibaini ukiukwaji wa taratibu katika utoaji ardhi hiyo. Tarehe 17/11/2011 Mkuu wa Wilaya Bukoba aliagiza kusimamishwa shughuli zozote katika ardhi hizo, lakini *WEO* na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji ambao ndio waligawa kinyume, wanakaidi agizo. *RAS* wa Kagera na *DAS* wana taarifa

iliyotolewa kwa tarehe 20/6/2012 kuwajulisha juu ya vikao vinavyofanywa kubadili maandishi, ionekane watu hao wamekodishwa. *DAS* aliandika barua yenye Kumb. Na. KAGR/BK/T/L.20/10/26 ya kuzuia, lakini bado ngazi za chini zinakaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama mlolongo wa malalamiko ya wananchi na muda wa hatua kuchukuliwa ni mrefu na ukaidi wa kutekeleza maagizo ya ngazi za juu unaoimarishwa na vigogo wenye fedha kwa upande wa ardhi unahitaji hatua kubwa ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Izimbya wanahitaji msaada wako Waziri. Nakuomba usaidie mgogoro huu ambao hata wanakijiji wenzao wanatishwa, vigogo hao ni wazito, wawili kati yao ni Mheshimiwa Jaji Gabriel Rwakibalila na Bwana Josiah Mwesiga ambaye alikuwa Mkuu wa Chuo cha *CCP* Moshi.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri na yenye mikakati thabiti na inayotekelezeka endapo mtapata pesa za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa ni mchapa kazi na ana uzoefu mzuri kwenye nyumba na maendeleo ya makazi. Tuna imani naye tangu alipokuwa *UN-Habitat.* Tunakuomba mama uchape kazi, usiangalie nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Naibu Waziri, ni mwelewa, mchaka kazi na akiahidi kitu anafanya. Mheshimiwa Naibu Waziri amesaidia sana kurudisha amani katika Kijiji cha Pande B.

Naomba atakapofanya majumuisho aelezee mgogoro huo, utatatuliwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naandika hili kwa masikitiko makubwa sana. Tanzania bado hakuna udhibiti wa uuzaji/ununuzi wa ardhi, holela. Suala la ununuzi/uuzaji wa ardhi Tanzania liko kiholela sana, tena sana kwa sababu hakuna utaratibu/mfumo wa kisheria unaoeleweka wa kudhibiti hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye pesa/mitaji mikubwa wamekuwa wakiwadanganya/dhulumu wananchi wa chini kwa kununua ardhi yao kwa bei ya chini na kuwaachia masikini. Hata wageni wanatumia fursa hii kwa wananchi wa chini, na mbaya zaidi ni kupitia viongozi wa kijiji, Kata na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ukija kufanya majumuisho, uniambie: Je, unafahamu huu uuzwaji/ununuzi wa ardhi kwa wageni kiholela? Je, ni hatua gani Wizara yako inajipanga kuzichukua? Chonde chonde, ardhi yetu inakwisha. Kwa mfano, Tanga, ardhi yetu imenunuliwa sana na Wakenya kwa kupitia Mombasa. Hali inatisha na inasikitisha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuwa mlinzi wa ardhi ya wananchi wa chini kwa kuweka utaratibu au mfumo wa kisheria ambao hata walaghai wakiwaendea wananchi, siyo rahisi kuwadanganya au kuwadhulumu. Mbaya zaidi, kinachonichanganya, hata wageni toka nje tena wengi wanatumia mwanya huu wa uuzwaji wa kiholela kununua ardhi kiulaghai kwa sababu wana pesa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano dhahiri, miongoni mwa mifano mingi ni katika Mkoa wa Arusha hasa maeneo ya Sanawari, Mianzini, Ngaramtoni na maeneo ya karibu. Naibu Waziri anafahamu zaidi maana ni Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie, hivi anafahamu kweli kama Gerezani yote Kariakoo, imenunuliwa na Wasomali na inaitwa *Somali Land*? Mtaa huu wa Gerezani Wasomali wamenunua wote. Ni hatari sana, kwani sijui wametumia utaratibu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuwa Rais ndiye msimamizi mkuu wa ardhi Tanzania na anaweza kufanya maamuzi yoyote juu ya ardhi bila kuhojiwa na kuomba. Mheshimiwa Waziri achukue nafasi hiyo kutufikishia maombi yetu kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga, tunayoomba kufutwa kwa hati kumi za mashamba ya Mkonge na shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na usimamizi mdogo wa ardhi, leo hii kuna migogoro mingi sana, mojawapo ni mgogoro baina ya *CDA* na Manispaa ya Dodoma unaotokana na Mkanganyiko huu wa usimamizi wa ardhi. Wakati *CDA* ina ardhi, Halmashauri ya Manispaa ina ushawishi mkubwa kwa watu kupitia Madiwani. Mara kadhaa hili limepelekea kuibuka migogoro isiyo ya lazima, na mbaya zaidi ni kucheleweshwa kwa miradi ya maendeleo kutokana na ubishani baina ya Taasisi hizi mbili. Mgogoro uliopo ni wa kisheria, maana kimsingi Manispaa ndiyo iliyopaswa kumiliki ardhi na wala siyo *CDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Waziri ajitahidi kutatua migogoro hii ya ardhi ambayo ni mingi.

Nina imani yangu kwamba Serikali ikidhamiria inaweza. Suala la ardhi ni nyeti sana na ardhi ndiyo nguzo kuu ya maisha, kwani vingine vyote iwe maji, madini, mazao na vinginevyo hutegemea rasilimali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba na maendeleo ya makazi ni kiashiria kimojawapo *(indicator)* kinachotumika kupima maendeleo ya nchi baada ya kipato, elimu na mengine. Hivi ni kwa nini Shirika la nyumba la Taifa *(NHC)* limeshindwa kujenga nyumba kwa ajili ya watu wa chini na watu wa kati? Kinachoshuhudiwa sasa ni Shirika hili kuzidi kuwakumbatia wenye uwezo (matajiri) huku ikiwaacha wale wenye uwezo wa kati na chini. Mfano halisi ni watumishi wa Shule za Sekondari na Msingi pamoja na wengine wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa heshima na taadhima alete huo Muswada wa pango la nyumba, ni muhimu sana kwa Watanzania hasa wa kipato cha chini.

**MHE. ADAM K. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Anna Tibaijuka- Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Goodluck Ole Madeye – Naibu Waziri kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na kupewa dhamana ya Wizara hii nyeti, kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri kwamba utata wa umiliki wa ardhi na Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi hasa kwenye masuala ya madini na kilimo yana umuhimu wa kipekee kwa sababu migogoro yake ina athari

kubwa za kiuchumi na kijamii hasa kwa wananchi wa kipato cha chini. Mara nyingi hasira inayojengeka ni kwamba, leseni ya madini au kibali cha uwekezaji wa kilimo kikubwa *(commercial agriculture)* kina haki na umuhimu zaidi kuliko *small scale mining* au *small holder farming land*, na hivyo kupelekea wadau wa uchimbaji mdogo au kilimo kidogo, unapojitokeza, harakati za uwekezaji mkubwa, wanatengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri haki za wananchi zinazohusiana na umiliki wa ardhi zinapoingiliana na shughuli kubwa za uchumi zielezwe vizuri ili zieleweke kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasiliana mara kadhaa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Makazi kuhusu tatizo sugu la Mkoa wa Dar es Salaam kujiongezea maeneo kinyemela. Manispaa za Dar es Salaam zimechukua maeneo ya Wilaya ya Mkuranga (Manispaa za Temeke na Ilala), Wilaya ya Kisarawe, Kibaha na Bagamoyo; naomba maelezo ya kina yatolewe kuhusu suala hili kwa kuwa hakuna mabadiliko yoyote ya mipaka yaliyofanywa tangu mwaka 1974. Tabia inazuka ya kuonekana kwamba upanuzi wa makazi na viwanda unakua kila siku kutokana na kukua kwa uchumi wetu. Watu wa Pwani hawastahili kuwa sehemu ya uzuri huo. Hali hii imekuwa jambo la kero na huzuni kwa wakazi wa Pwani wa Wilaya zote zinazopakana na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atamke kuhusiana na haya yafuatayo:-

Kwanza, kurejea mipaka ya 1974 ya Dar es Salaam na Pwani, na kuitisha Mkutano wa *Waziri wa Aardhi, Naibu Waziri wa Ardhi, Ma-RC* wa Dar es Salaam na Pwani, Waheshimiwa Wabunge, Ma-*DC* na wataalamu wa Ardhi ili tumalize suala hili na tuafikiane.

Pili, kutambua haki ya Mkoa wa Pwani kupokea kodi na malipo husika/stahili yote yanayotokana na shughuli za uchumi zinazofanywa ndani ya Mkoa wetu kwa mipaka ya mwaka 1974.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Wizara iteue Kamati Maalum ya kuchora na kubainisha mipaka ya Wilaya mpya zote nchini. Hali hiyo itaondoa migogoro isiyo ya lazima kati ya wakazi wa Wilaya hizi. Mfano wa hili, ni migogoro mikubwa na inayotishia kupanuka kwa migogoro ya mipaka ya Wilaya ya Mkuranga na Rufiji. Maeneo ya Lukanga, Malenda, Nyamato mpaka Nkamba-Kiseguse. Aidha, kuna migogoro mikubwa ya Mkuranga na Kisarawe hasa kwenye mipaka ya Kata za Panzuo, Bupu na Tambani. Naomba Wizara ichukue hali hii kuwa ya udharura mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na nasisitiza, naomba ufumbuzi wa migogoro yetu ya ardhi kama ilivyojieleza. Naunga mkono hoja.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii ya Ardhi nyumba na Makazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi Tanzania ni ubovu wa sheria inayosimamia ardhi, ambayo inatoa

haki upande mmoja na kunyima haki kwa mwananchi kwa upande mwingine, pamoja na kuwa na uso wa ardhi katika nchi wenye kilometa za eneo 848.200 (Tanzania), bado 75% ya ardhi haikaliwi au vigumu kutumika kutokana na maumbile ya kiasili ya kijiografia, (mlima, mabonde, majangwa na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki wa ardhi umepelekea kundi la wanawake kama sehemu ya jamii kutotambulika kama wamiliki wa ardhi hasa maeneo ya vijijini. Tunaona jinsi gani wanawake hasa vijijini wanapomiliki ardhi kupitia migogoro ya waume zao au koo alikoolewa japo sheria hiyo hiyo imetamka kama ana haki za kumiliki ardhi kwa upande mwingine. Tatizo la Sheria za Mirathi, pia linawaumiza sana wanawake katika kumiliki ardhi na kuonekana hana haki ya kumiliki ardhi. Hali hii inapelekea kufurahia ardhi kama ilivyoainishwa kikatiba kama kutumia ardhi kupata mikopo benki, kuuza na kupata pesa na kurithisha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria za Tanzania zipo wazi kabisa kwamba kama Serikali inataka kuchukua sehemu ya ardhi ya mtu/watu, basi tathmini ya malipo ya kuhamishiwa eneo husika yalipwe kwa gharama za thamani ya ardhi ya wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la kuthaminisha ardhi kwamba watu wanathaminiwa ardhi yao leo, huwa wanakuja kulipwa baada ya muda wa miaka mitano kwa wengine. Hali hii inapelekea wananchi kulipwa kiasi kidogo sana kwa kuwa thamani ya ardhi wakati watakaokuja kulipwa itakuwa kubwa.

Mfano, ni tathmini na malipo kwa wakazi wa Kipawa Dar es Salaam huko Kondoa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi huwa hawashirikishwi katika maamuzi ya ardhi hasa vijijini hasa linapokuja suala la kuwekeza hali hii, hupelekea watu wachache kuuza ardhi ya vijiji kinyume cha utaratibu na sheria. Mfano, ni uwekezaji wa *NAFCO* na *NARCO* katika Mikoa ya Morogoro na Arusha. Mwekezaji alipewa ardhi bila idhini ya wananchi. Mfumo huo ndiyo unaopelekea machafuko na kupoteza maisha ya watu hasa wananchi wanapokuja kudai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfumo mbaya wa utoaji ardhi kwa wawekezaji katika maeneo mengi ya Tanzania yanapochukuliwa na mwekezaji au umiliki wa ardhi hiyo. Kwa wenzetu kama Angola ardhi, inapowekezwa kisheria, lazima mwananchi aliyepewa eneo lake awe na hisa na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna migogoro ya wakulima na Serikali. Mara nyingi Serikali imekuwa ikikiuka Sheria na utaratibu katika kuchukua ardhi toka kwa wananchi, maeneo ambayo Serikali ilitangaza kama hifadhi, mbuga, msitu wa Taifa au urithi wa dunia, wananchi wamekuwa wakinyanyasika kwenye malipo au kuhamishwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1957 Serikali ilianzisha pori la akiba la Mkungunero Wilayani Kondoa na wananchi wakawa wanatumia kwa kilimo, uwindaji, uzalishaji na kadhalika uliruhusiwa. Mwaka 1995 Tume ya Ardhi, Upimaji na Ramani ya Taifa ikishirikiana na Halmashauri ya Kondoa

waligawa eneo hilo kwa vijiji vya Ikengwa, Keikei na Idindiri (Kisodoko) na kuchimbia *beacon* (alama ya mipaka ya vijiji) mwaka 1996 Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamini Mkapa alitangaza maeneo ya Pori la Akiba yawe hifadhi. Lile la Mkungunero halikuwepo, lilikwishagwiwa vijiji mwaka 1995. Mwaka mmoja kabla ya tangazo la Mheshimiwa Mkapa la mwaka 1996 lililofuatiwa na uwekaji *beacon* mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwepo pia migogoro ya wakulima na wafugaji wakinyang'anyana maeneo ya ardhi ya ufugaji na ulimaji. Sasa Serikali iangalie kuboresha na kutatua migogoro yote, kwani ni aibu kwa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi –Prof. Anna Tibaijuka na Naibu Waziri wake – Mheshimiwa Ole-Medeye na wataalamu wao kwa kuandaa hotuba nzuri liyowasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, lazima nikiri kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zinazokabiliwa na changamoto nyingi. Changamoto kubwa kabisa ni migogoro mingi ambayo inahusisha umiliki wa ardhi au wamiliki (wananchi) kuchukuliwa ardhi yao bila fidia stahiki. Baadhi ya migogoro imetajwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, lakini migogoro yote ya ardhi iliyo kwenye ngazi zote ilifahamu na kuandaa mkakati wa kuimaliza katika kipindi kifupi ili kuwe na amani na utulivu katika sehemu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri, Wizara imefanikiwa hadi sasa kuweka Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Wilaya 42 tu. Wilaya zilizobaki hazina Mabaraza hayo. Kadhalika, katika sehemu nyingi, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Kata hayana uelewa wa Sheria za Ardhi na Nyumba. Hali hii husababisha matatizo, hasa kukiwa na maslahi binafsi. Wizara ifanye juhudi ili kuhakikisha kuwa kila Wilaya iwe na mwanasheria wa ardhi atakayekuwa na Ofisi katika Mahakama ya Wilaya ili ashughulikie migogoro ya ardhi kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi hapa nchini yana migogoro baina ya wakulima na wafugaji inayohusu matumizi ya ardhi. Mara nyingi, wafugaji wamekuwa wakivamia maeneo ya wakulima yenye mazao au ambayo kwa wakati huo hayana mazao. Tatizo hili liko mahali pengi, hata jimboni kwangu Bukombe. Kiini cha tatizo ni wafugaji kutotengewa maeneo ya malisho mahali pengi. Wizara imejiandaaje kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee mpango wa maendeleo wa Makongo juu, Jimbo la Kawe Dar es Salaam. Mpango huu una lengo zuri la kuibadilisha Makongo iwe ya Kisasa. Hata hivyo, tayari mpango umeshaanza kuzua maneno. Baadhi ya maswali yanayoulizwa ni kwamba, kwa nini Makongo walipie maeneo yao wanayoyamiliki wakati maeneo mengine, mfano, Kigamboni, Mikocheni na kwingineko hawalipii maeneo yao? Kwa nini Serikali isigharimie kiasi kikubwa cha gharama, na wakazi wa Makongo wakatoa kiasi kidogo kilichobaki? Hofu ni kwamba kwa mpango huo, wakazi wasio na uwezo wa Makongo hawataweza gharama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wanamakongo Juu hawana imani na baadhi ya wataalamu wa ardhi wanaohusika na mradi huu kwa kuwa ni hawa hawa ambao wamekuwa chanzo cha migogoro ya ardhi kwa muda mrefu. Pendekezo ni kwamba, zoezi zima liwe wazi, lizingatie maslahi ya Wanamakongo Juu bila ubaguzi, lisiwe na ujanja ujanja ambao umekuwa ni mazoea katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Shirika la Nyumba la Taifa, lina mipango mingi ya kujenga nyumba za kuuza na kupangisha. Limeandaa mkakati mzuri wa kuingia kwenye biashara ya nyumba *(real estate).* Katika Semina iliyopita, iliyoendeshwa na Shirika la Nyumba la Taifa, Viongozi wa Shirika waliwaeleza Wabunge kuhusu mipango mizuri na mafanikio na changamoto. Pamoja na mipango mizuri na mafanikio ya Shirika, bado ni Shirika lililojikita katika kuboresha makazi kwa Majiji na Miji, ambalo ni lengo zuri. Bado Shirika halijawa na mpango wowote wa kushughulikia makazi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa, Shirika hili ligawanywe ili liwe Mashirika mawili (a) Shirika la Nyumba la Taifa Vijijini na (b) Shirika la Nyumba la Taifa Mijini. Shirika la Nyumba la Taifa Vijijini kwa sababu huko kuna changamoto nyingi za makazi, ili tuweze kuboresha maisha ya watu vijijini. Kuna haja ya kuwa na Shirika la namna hii ili makazi yawe bora, Waziri alitolee ufafanuzi jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea wazo alilotoa Mheshimiwa Waziri hivi karibuni hapa Bungeni kuhusu majina ya Mitaa katika Miji na Miji midogo nchini. Alielekeza

kuwa majina ya Mitaa/barabara yajumuishe waanzilishi wa TANU. Wazo ni zuri kwa sababu ni jambo la maana kuwaenzi walioshiriki katika ukombozi wa nchi hii. Lakini napendekeza kuwa, Wizara iandae sera ya majina ya Mitaa/barabara mjini na vijijini ili kuwe na sera pana zaidi, ili majina ya watu maarufu katika maeneo husika (sekta ya tiba, elimu, utawala, siasa na kadhalika) yaweze kutumika kama majina ya Mitaa/barabara. Jambo hili lina umuhimu wake hasa tukizingatia kuwa Taifa lina mpango wa anwani za makazi na *symbol* za Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najielekeza Jimboni kwangu, nitataja mifano michache tu ya migogoro iliyo Jimboni. Migogoro iliyopo chanzo chake hasa ni Halmashauri kuchukua maeneo kwa ajili ya huduma za jamii na kadhalika. Lakini fidia kwa wamiliki wa maeneo inakuwa taabu, hasa kwa kuwa Halmashauri haina fedha ya kutosha. Mfano, eneo kubwa la uhamiaji lilichukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Polisi, Ofisi za CCM na kadhalika. Hadi leo fidia kwa wamiliki haijakamilika, kesi bado iko Mahakamani. Wizara isaidie kutatua mgogoro huu.

Chanzo kingine cha migogoro ni utovu wa uadilifu wa Watendaji/Wenyeviti ngazi ya Kata na Vijiji. Mifano ni migogoro ya ardhi ya Kijiji cha Lyobahika (Kata ya Uyovu) na Kabagore (Kata ya Bosonzo) imeanziswa na Watendaji/Wenyeviti. Cha kushangaza ni kuwa aliyehusika katika kuchukua maeneo ya wananchi wa Lyobahika anafahamika, hata Mkurugenzi Mtendaji na viongozi wengine wanamfahamu, pamoja na ushahidi wa wazi, lakini hadi sasa hajachukuliwa hatua kwa sababu ni Diwani wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri anipe majibu kwa masuala niliyoyaongelea.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uelewa wa kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali na ni heshima kwa maendeleo na ustaarabu wa nchi yoyote ulimwenguni, hivyo ni lazima Serikali itoe kipaumbele cha juu katika kuipima na kuithaminisha ardhi kwa maslahi, manufaa na maendeleo ya nchi pamoja na watu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, inavyoonekana, kuna mgongano wa kimaslahi kati ya Wizara ya Ardhi na Manispaa au Halmashauri katika usimamizi wa ardhi nchini. Hili ni tatizo na lazima lipatiwe ufumbuzi wa haraka. Sehemu za wazi ambazo ni muhimu kwa ustawi wa jamii husika ya eneo hilo zinauzwa bila aibu, kwani Watendaji wa Wizara na Watendaji wa Halmashauri wanagombea uuzaji wa maeneo hayo ya wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana pia kwamba, Wizara haina nguvu za kisheria kuwadhibiti Wakurugenzi wa Halmashauri katika kuuza sehemu za wazi. Pia Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kukosekana sheria ya kubana na huwa wanahamishiwa kutoka Halmashauri moja na kupelekwa nyingine inakuwa ni fursa nyingine kwa Wakurugenzi hawa kuendelea kufanya ufisadi wa kuuza maeneo ya wazi kiholela, kwani wanakuwa hawana uchungu na Halmashauri wanazopelekwa kufanya kazi.

Nashauri Serikali ishughulikie jambo hili haraka na pia Wakurugenzi wawe ni wananchi wa asili wa Halmashauri husika. Hii itasaidia wazee wa Halmashauri hiyo kuweza kumdhibiti Mkurugenzi wao katika Mabaraza ya ardhi, kwani atakuwa ni mtoto wa nyumbani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *National Housing* na Ujenzi wa nyumba. Juhudi za ujenzi wa nyumba mpya ni jambo zuri, lakini *National Housing* wamefanya tamaa sana ya kutaka faida kubwa sana na kujisahau kuwa ni Shirika la Umma, linalotegemewa kuangalia maslahi ya wananchi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa nyumba za ghorofa, *(apartments)* za Medeli Dodoma, nyumba hizi zina vyumba vitatu vya kulala, wakati wa ufunguzi wa nyumba hizi tuliambiwa kuwa imegharimu Shilingi milioni 60 na zilitarajiwa kuuzwa kwa Shilingi milioni 80, ambao ni bei ya kiasi kulingana na nyumba yenyewe ilivyo. Shirika lilitoa dharura *(Excuses)* na kusema kuwa eneo la Medeli halikuwa na miundombinu ya barabara, umeme, maji safi na machafu. Hivyo Shirika la *National Housing* lililazimika kujenga lenyewe miundombinu hiyo. Hivyo kuongeza gharama za nyumba hizo kutoka Shilingi milioni 60 hadi kufikia Shilingi milioni 80 na kulazimika Shirika kuuza nyumba hizo kwa Shilingi milioni 100 bila *VAT* bei ambayo ni faida ya asilimia 25 *which is reasonable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kushangaza ni nyumba zinazojengwa Mchikichini Ilala, Dar es Salaam ambazo ni sawa na nyumba za Medeli Dodoma. Nyumba hizi za Mchikichini, Ilala Dar es Salaam zinauzwa Shilingi milioni 168 bila *VAT*. Kwa nini waweke faida ya zaidi ya

asilimia 100, *profit.* Hali ya kuwa hata zile *excuses* za Medelii hapo hazipo? Mchikichini kuna miundombinu yote!

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Serikali ikiondoa *VAT*, bado nyumba hizi hazinunuliki. Ikiwa nyumba iitwayo ya *medium cost,* Mbunge hawezi kuinunua! Mtu wa kipato cha kati ni nani? Ni lazima Serikali kupitia Wizara hii ishughulikie pia ku-*re-adjust* bei za nyumba hizi ili waliokusudiwa waweze kuzinunua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna hoja *(Logic)* ya kuzipandisha bei nyumba za Mchikichini Ilala Dar es Salaam kwa zaidi ya asilimia 100 kwa kuwa tu zipo Ilala Dar es Salaam. Ardhi iliyojengwa nyumba hizi ni mali ya *National Housing* ya kurithi. Siyo kama ardhi wameinunua kuwa ndiyo itaongeza bei, hawajanunua!

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iweke *"flat rate profit percentage"* kwa nyumba zinazojengwa *National Housing* ili kuepusha maslahi binafsi ya Watendaji kwa kushirikiana na mafisadi wachache wenye nia ya kuzinunua nyumba hizi na kisha kuzikodisha badala ya kuwafaa wananchi waliokusudiwa. Asilimia 20 hadi 25 ya faida ni *reasonable and acceptable*, lakini siyo faida ya *more than 100%.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Public beaches* kama *Oysterbay Beach*, ziboreshwe na zijengwe bustani na *bench* za kukaa na kupumzika wananchi badala ya kukodishwa kwa watu binafsi na kutoza viingilio kwa wananchi wa kawaida. Huku ni ku-*re-colonise* nchi. Wananchi watapumzika wapi baada ya kazi ngumu za kujitafutia maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri *Public Beach* zote ziwe ni *Public beaches!* Zisiuzwe wala kukodishwa ili wananchi na vijana wetu wapate sehemu za kupumzikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana, timiza wajibu wako. Ahsante sana.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa Afya na fursa kuchangia Bungeni leo. Naipongeza Serikali kwa kuanza kuboresha Sera na kusimamia sheria na rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nichangie suala la Sera na Sheria ya Fidia. Sheria hii ina upungufu makubwa. Sheria inatamka kwamba fidia ikichelewesha kulipwa pindi unalipwa unaongezewa fidia ya asilimia sita kwa kila miezi sita. Sasa kama mtu atalipwa baada ya miaka mitano atapata asilimia 60 juu ya ile fidia. Mfano, ardhi ya Babati - Komoto walifidiwa kwa Sh. 300,000/= kwa ekari moja na baada ya miaka mitano atatakiwa kulipwa Sh. 480,000/= wakati kipindi hicho ardhi ina thamani ya Shilingi millioni tano hadi saba na Halmashauri wakitoa viwanja vya kati *(medium density)* wanauza kiwanja kimoja kwa Sh. 2,850,000/= na ekari inatoa viwanja vinne. Kwa hiyo, wanapata Sh. 11,400,000/=, gharama ya upimaji kiwanja Babati ni Sh. 80,000/=. Kwa hiyo, ekari moja ni Sh. 320,000/=. Kuandaa hati ni Sh. 90,000/=, kwa hiyo, viwanja vinne ni Sh. 360,000/=. Kwa ujumla, kufidia eneo ni Sh. 480,000/=, ukijumlisha yote ni Sh. 1,160,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri au Manispaa au mtu binafsi (mwekezaji) kupata fidia ya Sh. 11,240,000/=, kama mwananchi angelipwa fidia hiyo au ile Shilingi millioni saba, akalipa *capital gains tax.* Itamfanya Mwananchi wa kipato cha chini mwenye haki kwenye ardhi husika asingelalamika na kutomfanya maskini. Kwa sheria ya leo miradi yenye manufaa Kitaifa, upanuzi wa Miji imekuwa laana kwa wananchi.

Pili, nashauri Serikali iangalie namna ya kuweka Mabaraza ya Ardhi chini ya Wizara moja ngazi zote. Mabaraza ya Wilaya, Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Vijiji, yote chini ya Wizara ya Ardhi ili kuleta ufanisi. Pia Wenyeviti wa Mabaraza ya Wilaya wawe wamesomea Sheria na hasa Sheria za Ardhi *(specialization).* Pia Serikali iangalie namna ya kurudisha Maafisa Ardhi wawe chini ya Wizara kuongeza ufanisi. Leo hii wako chini ya Serikali za Mitaa, hawawajibiki kwa Wizara ya Ardhi na kunakuwa na mgongano wa Kimaslahi. Mfano, Wizara ya Ujenzi imefanikiwa kwa sababu wana mtandao hadi ngazi ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi katika Mabaraza ya Ardhi, kesi zinachukua muda mrefu, haki kwa wanyonge kwa sehemu kubwa inapotea. Pia Mabaraza hayashirikiani na wataalamu wa Ardhi kubaini mipaka kisheria na kwa kutumia vifaa vya kitaalamu. Tungependa kuona Mabaraza haya yawe yanatumia wataalamu zaidi wa Ardhi, maeneo yenye hati na yamepangwa kisheria. Pia wanapokea malalamiko bila kuangalia kama ni mgogoro halali, na aliyeshitaki ana haki na nyaraka zote. Tunashauri Mboreshe haya Mabaraza na yawe chini ya Wizara moja.

Tatu, naipongeza Serikali kwa kuweka mpango wa kuwa na mtambo wa kupokea picha za digitali *(satellite imaging technology)* na kuwa na vifaa vya kupima ardhi katika Halmashauri zetu. Mtambo huu utasaidia kujua maeneo yetu yote na pia kuondoa udanganyifu unaofanywa na Maafisa wa ngazi ya chini. Nchi za jirani pia wanaweza kutumia mtambo wetu. Husaidia kuona wavamizi katika maeneo ya hifadhi ambako siyo rahisi kufika kila siku. Tutakuwa tunakwenda na wakati, pia itarahisisha Halmashauri zetu kuwapimia wananchi, hatimiliki za Kimila kwa gharama nafuu. Pia itasaidia wanafunzi wa Vyuo, hasa Chuo cha Ardhi kufanya mazoezi kwa vitendo *(practicals)* na kuwa wazoefu badala ya kusubiri na kufanya kwa vitendo akiwa kazini.

Nne, Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali hasa Wizara ya Ardhi kwa kufanya Maboresho katika Shirika la Nyumba la Taifa, *(NHC)* na kuleta mtazamo mpya. Tunashauri wasaidie kuleta kwanza elimu hiyo kila Wilaya na pia uteuzi wa nyumba iwe katika kila Mkoa hasa Mikoa mipya. Tunashauri katika nyumba za kuishi wasipandishe kodi sawa na kodi za bei ya soko, dhana nzima ya Shirika la nyumba la Taifa, *(NHC)* ni kusaidia wale wenye kipato cha chini na kuweka sawa mfumko wa bei wa kodi za nyumba mkiwa sawa na bei ya soko, basi bei zitaendelea kuwa juu. Tunapongeza Uongozi wa *NHC*.

Tano, suala la migogoro ya Ardhi, napenda kuishauri Serikali wajitahidi kumalizia migogoro katika Mkoa wa Manyara hasa Wilaya ya Babati. Tuna migogoro ya muda mrefu zaidi ya miaka 25 iliyosababisha wananchi wawekezaji kuishi kwa hofu na kutokuwa na amani. Bonde la Kiru limekumbwa na migogoro ya ardhi kwa miaka mingi.

Tume mbalimbali zimeundwa na la mwisho chini ya Mawaziri watano waliotumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini hadi leo hakuna jibu, na wananchi na wawekezaji hawajui kinachoendelea.

Tulipendekeza kwamba, ili kutatua mgogoro, Shamba la *Breweries* -Sigino na la Rivacu - Dareda zingetoa ekari 600 ili wananchi walioko eneo la kiru *Valley estates* wahamishwe hapo. Pia mmiliki wa *Hamir Estate* apewe eneo lililosalia katika shamba la maendeleo ekari takribani 300 na yeye aachie eneo lililokaliwa katika Shamba la Kijiji cha Kirudiki, pia mipaka ya vijiji na mashamba yawekwe bayana na suala la mifugo lidhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni mgogoro ya Tarangire na vijiji vya Gidefabong, Ayamango na Gedemar. Wananchi hao wanaendelea kupata mateso kwa sababu walikuwa hapo Kihalali, wametakiwa kuondolewa hapo, lakini fidia wanayolipwa ni ndogo na haimkidhi hata kidogo mwananchi huyo kuweza kujikimu na pia hawajapatiwa eneo mbadala hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alisema sheria inataka Kijiji kisigawe eneo zaidi ya ekari 50 (HA 28), lakini huko Babati vijijini bila wao kutambua wamemilikishwa Rivacu na sasa *Rivacu* wamekwenda Mahakamani. Tunaomba Wizara isaidie kuitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashamba ambayo hayaendelezwi na wamiliki wanakodisha kwa watu mbalimbali; moja, ni Shamba la *Breweries* na lingine ni shamba la Rivacu *(Dareda Estate).* Wote wana migogoro na vijiji wanavyopakana navyo, vijiji vya Sigino, Dohom,

Endasagu, Arri, Managha, pamoja na Uongozi wa Wilaya na Mkoa kupendekeza baadhi ya maeneo yapewe kumaliza mgogoro wa Bonde la Kiru. Shamba la *Breweries* limebadilishwa mmiliki kutoka Shirika la *Breweries* na kupewa mtu binafsi mwaka 2011, kinyume na utaratibu na tayari anataka kwenda Mahakamani kushitaki vijiji nilivyotaja hapo juu.

Pia *Rivacu* yenye mashamba katika Mkoa wa Manyara na Arusha hawaendelezi mashamba yao, bali kukodisha kinyume na utaratibu wa sheria. Tunashauri wafutiwe hati yao na kupewa wananchi wenye tatizo kubwa la ardhi hasa Wilaya ya Babati. Wao pia wameshitaki wananchi walioingia katika maeneo yao sababu ya kutoendeleza miaka mingi na kuendelea kukodisha mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, tunaomba elimu juu ya Sheria ya Ardhi na haki ya mwananchi iendelee kutolewa ili kupunguza migogoro. Wizara ya Ardhi ishirikiane na Wizara ya Mazingira, Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na Wizara ya Ujenzi ili kudhibiti na kuweka matumizi bora ya ardhi na kutunza hifadhi ya misitu, hifadhi ya barabara, hifadhi nyingine na vyanzo vya maji.

Mwisho, tunaomba mlete mabadiliko ya Sheria ya Uuzaji holela ya ardhi, kwani wananchi wenye kipato cha chini huuza ardhi yao na baadaye kuwa tatizo kwa nchi. Wanauza kwa wenye uwezo kwa kutegemea kwamba ardhi nyingine ipo. Mfano, India ni vigumu mtu yeyote ambaye hana historia ya kuwa na eneo la kilimo, hawezi kununua eneo la kilimo. Inadhibiti eneo la kilimo kupotea, na kubaki wachache wenye uwezo.

Mheshimiwa Spika, leo hii maeneo mengi muhimu yenye rutuba yamegeuzwa kuwa za makazi na eneo mbadala la kilimo (hupotea) kukosekana. Tuwe na sheria inayozuia maeneo ya Kilimo kutopotea. Tunaweza kujenga katika maeneo yasiyo na rutuba na vyanzo vya maji na maeneo ya milima na kupeleka miundombinu mbalimbali katika maeneo hayo kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutenga maeneo ya maalum kwa ajili ya mifugo ili migogoro kati ya wakulima na wafugaji isiwepo, miiundombinu ya wafugaji, yaani mabwawa na malambo pamoja na majosho. Itasaidia wafugaji kutohamahama na kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa Wizara ya Ardhi sasa imepata Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na viongozi wote wa Wizara wenye mtazamo mpya na nia ya kutatua matatizo ya ardhi. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mwendelee na moyo huo huo na msibadilishe msimamo.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa kuandaa bajeti na hotuba nzuri ambayo tunaichangia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja na suala la alama za Kimataifa. Ili kulinda mipaka ya nchi yetu, naishauri Wizara ijitahidi sana kuweka mipaka (alama) inayoeleweka kati ya nchi yetu na nchi za jirani. Kwa

mfano, katika Wilaya ya Rorya na Tarime hakuna alama yoyote ile inayotambulisha mpaka wa Tanzania na nchi ya Kenya. Hali hii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu, na kwa kuwa katika Wilaya hizi mbili kuna mwingiliano wa jamii ya Wakurya na Wajaluo (Tanzania) na halikadhalika kuna jamii hizi toka Kenya, hali hii husababisha wizi, ujambazi, uhasama na kadhalika. Hivyo, inakuwa ni vigumu kuwatambua wahalifu hao wametoka nchi gani, ili kuondokana na adha hii. Naishauri Wizara iweke haraka iwezekanavyo alama za mipaka ya Kimataifa katika eneo la mpakani baina ya Tanzania na Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni la kushughulikia haraka ni rushwa katika Wizara hii hasa katika Sekta ya Ardhi. Kuna rushwa ya kutisha katika Mabaraza ya Ardhi, Halmashauri zetu, Manispaa zetu na hata katika Wizara yenyewe. Swali la kujiuliza, sijui kama Waziri anafahamu juu ya uozo uliopo katika Manispaa ya Kinondoni Mkoani Dar es Salaam? Je, anafahamu kuwa kuna rushwa ya kutisha katika kitengo cha upimaji ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli hadi sasa kwa nini maeneo mengi hasa ya Mijini hayajapimwa mpaka sasa? Maeneo ya *Mbezi Beach,* Salasala na kadhalika, kwa nini hayajapimwa? Je, Wizara ina mpango gani juu ya maeneo haya? Kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Shirika hili, lakini bado kuna kasoro ndogo ndogo kama vile: upangishaji wa nyumba za Shirika hili haujawanufaisha watu wa kipato cha chini. Hali hii inapelekea matajiri kumiliki nyumba hizi na hivyo kulipa kodi kidogo kwa Shirika, lakini huku wamewapangisha walalahoi kwa kodi kubwa. Fikiria maeneo yote yaliyozunguka Kariakoo na Mitaa yake. Naishauri Wizara ifanye utambuzi

upya ili kubaini watu wa aina hii ili waweze kuchuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuisemea ardhi na Sekta ya Madini. Swali muhimu kwa Waziri: Je, wawekezaji wa Sekta ya Madini wanalipia kodi ya ardhi? Je, kama wanalipa, wanalipa kiasi gani kwa hekta/kama hawalipi ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri kwa kuonyesha uzalendo wa kuomba kuongeza kilometa za mraba 61000 katika bahari ya Hindi. Namwomba afuatilie kwa haraka ili tuweze kumiliki eneo hili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshauri Waziri ahakikishe kuwa sheria kuhusu hakimiliki ya ardhi iandikwe kwa lugha nyepesi ya Kiswahili na kuielewa vizuri. Hali hii itawapatia ufahamu wa kuielewa sheria inayotawala ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naungana na wenzangu kushauri kuwa Mabaraza ya Ardhi ya Kata, Wilaya na kadhalika kwa kipindi hiki cha Sayansi na Teknolojia hayana nafasi, kwani rushwa imekithiri sana. Hivyo, nashauri yavunjwe na badala yake majukumu ya Mabaraza haya yahamishiwe kwenye Mahakama za Mwanzo na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naishauri Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Ardhi zishirikiane ili kupima na kutoa hatimiliki kwa shule zote za Kata za Sekondari na Shule za Msingi ambazo bado hazijapata hatimiliki. Hali hii

itasaidia sana kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima baina ya shule hizo na wenyeji wanaozunguka shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upimaji wa ardhi katika Wilaya ya Tarime ni nyeti sana ili kuepukana migogoro isiyo ya lazima katika Wilaya ya Tarime. Ifahamike wazi kuwa migogoro, vurugu na mapigano ya koo na koo katika Wilaya ya Tarime kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na suala la ardhi.

Hivyo, ili kuepukana na tatizo hili, naomba sana Wizara kupima viwanja/ardhi ili kila ukoo ufahamu mipaka yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la hati za Kimila kwa kila mwanakijiji Wilayani Tarime, swali la kujiuliza ni: Je, kwa nini Wilaya ya Tarime haimo katika mkakati na mpango wa kupima ardhi ili kutoa hati za Kimila? Wizara haioni kuwa kuna faida nyingi za kuondoa vurugu, migogoro, uhasama na vita isiyo ya lazima kwa kupima hati za kimila?

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji Miji midogo ya Sirari, Nyamwaga, Nyamongo, Komasawa na kadhalika, naishauri Wizara ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kwa lengo la kupima Miji midogo ya Sirari, Nyamwaga, Nyamongo, Komaswa kwa lengo la kuepusha ujenzi holela katika Miji hii inayokua kwa kasi sana. Pia upimaji wa Miji hii utasaidia kuboresha maisha ya wananchi wetu kwa kuweza kutumia hati zao kuchukulia mikopo benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalopenda kulizungumzia hapa ni tatizo la mgogoro wa ardhi Wilayani Tarime baina ya wananchi wa Rosonti na Jeshi la Wananchi

wa Tanzania. Naiomba Serikali iangalie upya suala la mgogoro huu, kwani inatia aibu Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linahitaji ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Je, suala la mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Nyamongo na vigogo wanaomiliki ardhi Wilayani Tarime limeshughulikiwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naiomba Wizara iangalie upya suala la mgogoro wa ardhi katika Kijiji cha Gibaso. Baada ya hapo naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu katika maeneo machache ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa utayari na bidii yake katika kushughulikia kero za ardhi. Makazi ambayo kweli ni tatizo kubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kuweza kumudu maisha yao nasisitiza Serikali iharakishe upimaji wa mashamba au viwanja na kutoa hati miliki ili wananchi waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na vyombo vya fedha, Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kuhusu upatikanaji wa hati miliki za kimila itolewe mara kwa mara kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri zetu ziweze kutoa huduma ya upimaji na kutoa hati miliki kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kuwa mabenki yanakubali hati milki za kimila kuwakopesha wananchi. Kinyume chake kama ilivyo sasa kwa kweli ni vigumu kwa wananchi wetu kuondokana na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la makazi, napenda kushauri Serikali kuangalia bei ya vifaa vya ujenzi kama sementi, bati, misumari, nondo na kadhalika. Vifaa hivi viweze kupatikana kwa bei nafuu ili wananchi waweze kujenga nyumba bora na kuweza kupambana na maisha hasa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia juu ya matatizo ya Ardhi, Mipaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi hiyo, Vijiji vya Sositeli, Kitete, Kambi ya Simba, Rhotra, Tloma, Endamaglag, Olpiro na kadhalika. Hali ambayo inasababisha migogoro ya mara kwa mara, kwa mfano, kubambikiziwa kesi wananchi wa maeneo yao, kuweka sumu kwenye mboga ili kuwa na tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, TAMISEMI na Halmashauri zinazopakana na hifadhi hii pamoja na *TANAPA* kukaa pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kudumu kwa migogoro hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wapate haki yao na watambue kuwa tembo, maliasili hiyo ni yao na kwa faida yao hivyo waitunze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwe na mikutano ya ujirani mwema kwa wahusika wote. Suala kubwa ninaloona kuleta shida au migogoro ni kutoshirikishwa kwa wadau katika kuweka *Buffer zone* kwa kuwa wananchi walizoea kutumia maeneo hayo kupata kuni, kulishia mifugo, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kutatua migogoro ya Ardhi inayowakabili wananchi wa Murus – Endabash ambao ardhi yao imepokwa na inaendelea kupokwa baada ya dhahabu kugunduliwa. Haki ya wananchi wa eneo hili iko mashakani, naomba Serikali itoe kauli yake ili kuwahakikishia wananchi usalama wa ardhi yao.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto nyingi ambazo zimeikumba Wizara hii, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa namna wanavyokabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndio rasilimali kuu ya nchi na ndiyo ambayo inaweza kutumika vizuri italeta maendeleo na iwapo haitokuwa katika mpango mzuri wa kuimiliki na kimatumizi inaweza kuleta maafa ya mauaji na hata vita baina ya mtu na mtu, familia au hata nchi na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri aharakishe zoezi la uwekaji mipaka ya vijiji, mashamba, maeneo ya wazi na maeneo ya machimbo kwa kutumia teknolojia ya *satellite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi na ukaguzi wa mara kwa mara kupitia kikosi kazi cha ardhi kuangalia udhibiti wa uvamizi katika maeneo ya wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na sheria au kitengo kimoja tu nchini ambacho kitakuwa na mamlaka kamili ya utoaji vibali vya umiliki wa ardhi pia ujenzi wa nyumba, ambacho kitaondoa mgongano baina ya maofisa wa Ardhi katika Halmashauri ambao wako chini ya TAMISEMI ambapo Afisa wa Ardhi wa Wizarani anakosa mamlaka juu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Makazi katika maeneo mengi katika nchi yetu hususan vijijini ni duni sana kutokana na uwezo mdogo ambao unawakabili wananchi wetu. Vile vile ujenzi holela, usio katika viwango ambao unafanyika katika miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mipango miji ni tatizo kubwa na linahitaji ufumbuzi wa haraka, ufumbuzi ambao unahitaji matumizi makubwa ya fedha ili kuhakikisha tunapata maendeleo katika suala zima la makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha hotuba yake atoe ufafanuzi juu ya mradi katika Bonde la Msimbazi ambapo Wizara yake itashirikiana na Halmashauri ya Ilala na Kinondoni. Mradi huo wa *City Park* ni budi wananchi waelezwe na waelewe

ni nini hasa Serikali imekusudia kufanya. Pia ni vyema kuelewa mipaka ya mradi huo, vile vile thamani ya mradi huu ni lini mradi huo unategemewa kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yako na ufafanuzi wako pia utasaidia kutoa uelewa hata kwetu sisi Wabunge na tutaelewa namna ya kuwaeleza wananchi wetu pale tunapokutana nao.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri na kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuboresha maendeleo ya watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na napenda kuwashauri Waheshimiwa Wabunge waunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba na kuishauri Serikali iondoe *VAT* katika uuzaji wa nyumba zake, kufanya hiyo ni kuweza kuwasaidia wananchi wa Tanzania wazalendo kuweza kununua nyumba za *NHC* zilizo bora na wakati huo huo kupatia Serikali faida kubwa kwa sababu nyumba zitaweza kununuliwa kwa wingi kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuweza kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya upimaji wa viwanja kwa sababu ardhi kubwa haijapimwa, jambo ambalo linasababisha mkutano mkubwa kwa wananchi na kupelekea hasara kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilosa na hasa Jimbo la Kilosa ina ardhi yenye rutuba nyingi sana na sehemu nyingi hazihitaji mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya mashamba mengi makubwa yanamilikiwa na matajiri ambao hawayaendelezi na wengi wao wako nje ya nchi na wala hawana haja ya mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kampeni, mwaka 2010, wananchi wa Jimbo la Kilosa na hasa Kata za Msowero, Dumila na Magole, wananchi walimwomba Rais Kikwete aingilie kati suala hili ili ardhi wanayohodhiwa na matajiri bila kuendelezwa, igawiwe kwa wananchi wa maeneo hayo ili wapate mashamba walime. Mheshimiwa Rais anaahidi kulifanyia kazi tatizo hilo. Ninavyokumbuka viongozi wa Mkoa wa Morogoro walishalifanyia kazi suala la *re-survey* ilifanyika na hata *RCC* ilizungumzia tatizo hili kwa Mkoa mzima wa Morogoro. Sina hakika kama kuna hatua yoyote imechukuliwa na kama wananchi wangu wa Jimbo la Kilosa walioibua tatizo hili wamejulishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi atoe kauli wakati wa majumuisho ya hoja yake ili mimi Mbunge wao niweze kukazia ahadi za Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya vijijini hayajapimwa na hivyo kuwafanya wananchi hao kushindwa kupata hati miliki za ardhi na kushindwa kupata mikopo katika mabenki kwa kukosa dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Wilaya ya Kiteto na Kondoa ambapo mgogoro huo umesababisha vifo. Naomba Serikali ichukue hatua ya haraka kuondoa tatizo ambalo ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashauri Wizara ya Ardhi kupitia Shirika lake la nyumba kujenga nyumba katika Wilaya mpya zote nchini ili kuondoa adha ya watumishi wapya watakaoajiriwa kufanya kazi katika Wilaya hizo na si vibaya mkaanza na Wilaya ya Chemba Mkoani Dodoma. Ahsante.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi katika nchi hii kwa muda mrefu sasa na inaelekea kuna hali fulani ya kuhujumu juhudi zinazofanywa na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ili kumkatisha tamaa, urithi wa pekee ambao hata wale watu au Watanzania walio maskini kabisa wangeweza kuimiliki, lakini tofauti na hilo Watanzania wamekuwa kama wageni katika nchi yao huku tukishuhudia wageni wakimilikishwa ardhi kubwa tena kwa muda mrefu. Hii sio sahihi kabisa, tunamtaka Waziri alishughulikie hili mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kigamboni ni tata kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Namba 8 ya mwaka 2007 haikufuatwa kwa maana kwamba wananchi hawakushirikishwa katika kuiridhia *The New Kigamboni City*, lakini pamoja na hayo bado fidia zilizotolewa kwa baadhi ya wananchi hazilingani na thamani ya mali walizokuwa nazo. Kwa hiyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri aonane na wananchi wa Kigamboni awasikilize na ndiyo utawala bora, kwa kufanya hivyo watafikia muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kurasini al-maarufu maji machafu ni la kusikitisha sana na tatizo hili linajulikana. Namwomba Waziri wa Ardhi kwa mara nyingine tena akaonane na wananchi hao wanaoishi Kurasini Maji Machafu awasikilize kilio chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii si lelemama na tunamtaka Waziri ajifunge kibwebwe, akaze buti kwani anapambana au kukumbana na vikwazo vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Tanga kuna mashamba ambayo hayaendelezwi kabisa. Baadhi ya mashamba hati za umiliki ziko mezani kwa Mheshimiwa Rais, kwa kufanya Jimbo la Korogwe Vijijini kuna shamba la Toronto *Sisal Estate*. Shamba ambalo lina takriban hekta zaidi ya 6,000. Sehemu ambayo inalimwa mkonge ni ndogo, kubwa imepandwa majani ya ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Magunga *Sisal Estate* yenye hekta 6,500. Sehemu inayoendelezwa ni 19% na ni wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halemruazi *Estate* lenye hekta 4,000 ambazo zinazotumika ni hekta 1,100. Eneo lote halitumiki. Kwashemshi *Estate* haliendelezwi, Hale Mwakinyumbi *Sisal Estate* haliendelezwi wala halina mkonge. Shamba la Kerenge *Sisal Estate* nalo haliendelezwi. Shamba la Gomba *Estate* haliendelezwi. Shamba la Magoma Kulasi, baadhi linaendelezwa baadhi haliendelezwi. Mazinde *Estate,* shamba hili eneo dogo sana ndio linaloendelezwa. Mswaha *Estate,* nalo hili ni msitu mtupu haliendelezwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mashamba haya wawekezaji wameshindwa kuyaendeleza na kwa kuwa baadhi ya mashamba haya hati ziko mezani kwa Rais na kwa kuwa Waziri aliyepewa dhamana ya Wizara hii ni msikivu, naiomba sasa Serikali itamke rasmi kufuta hati hizi za mashamba yasiyoendelezwa ili iwapatie wananchi maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maeneo mengi ya Jimbo hili yameathirika kwa kiasi kikubwa na mashamba haya yasiyoendelezwa, naomba jambo hili lipewe umuhimu na kipaumbele cha hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumpongeza

Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kutumikia nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala ambao linaeleweka kwamba Wizara ya Ardhi ni Wizara nyeti sana. Aidha, nyumba ni miongoni mwa mahitaji ya lazima kwa kila mwananchi, hivyo kutumikia wananchi wote wa Tanzania kuwaridhisha kuwapatia viwanja, nyumba kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Wizara hii kuna umuhimu wa kupanga mikakati na mipango ya muda mrefu kuhakikisha kwamba matumizi ya ardhi na haki za umiliki wa ardhi kisiwe chanzo cha migogoro na mauaji ya wananchi wa Tanzania wakiwemo wafugaji na wakulima wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba fedha iliyotengwa kwenye bajeti hii ni ndogo kwa kufanya kazi hiyo, lakini kupanga ni kuchagua. Kwa msingi huo ni vema Wizara yako ikaliangalia suala hili na kulipa kipaumbele na kuishauri Serikali namna ya kulikabili kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeona umuhimu wa ardhi na naomba niipongeze kwa maamuzi yake na msimamo wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kutotaka kuingizwa kama suala la Jumuiya, aidha, kutokuwa tayari kuuza ardhi kwa wageni, huu ni mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho atueleze Watanzania ni lini Wizara

itafanya juhudi ya makusudi kuueleza umma mpango wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kuona kwamba Watanzania wanaelewa kwamba haki yao ya ardhi ipo na haitaporwa na Watanzania wenyewe ndio watafaidika na haki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa Waziri anaweza kutumia muda huu katika chombo hiki cha Bunge kuelimisha Watanzania na kuwapa imani na uhakika wa namna gani watafaidika na haki yao ya matumzi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imekuwa na tabia ya wafanyakazi ambao si waaminifu kuuza viwanja mara mbili hususan viwanja vya wanyonge na kutengeneza hati za miaka ya nyuma. Je, Waziri ana taarifa juu ya malalamiko haya na anayatatuaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la utoaji *form* wa viwanja na wananchi wanatoa pesa, mwisho wa siku hakuna uuzwaji unaoendelea. Je, huu si wizi kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma Manispaa ya Kigoma Mjini hawana Afisa Ardhi kwa takriban miaka mitano mfululizo baada ya kulalamika tumeazimwa yule Afisa Ardhi wa Mkoani. Je, ni lini Serikali inatuletea Afisa Ardhi wa Manispaa ya Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la wachimbaji madini, baada ya kumaliza huacha mashimo hayo wazi na hivyo kusababisha mmomonyoko wa ardhi. Je, Waziri ana mkakati gani wa kutatua tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na urasimu wa kutafuta au kuchelewa kupata hati Wizarani. Je, Waziri anaweza kutuambia kwa nini Mtanzania anatumia zaidi ya miaka miwili kupata hati na tukiangalia hati hizi husaidia wananchi kupata mikopo. Je, Waziri haoni Wizara yake inachangia kukuza umaskini Tanzania? Je, pia anaweza kutuambia *process* ya kupata hati inachukua muda gani? Hii ni kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za ununuzi wa nyumba za *National Housing* ni kubwa sana, wananchi wa kawaida hususan vijana wanaoajiriwa mara tu baada ya kumaliza skuli hawana uwezo wa kununua nyumba hizi, hivyo ni vyema Wizara ingejaribu kuwa *fair* kwa Watanzania ambao ni maskini.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme wa Upepo unaotazamiwa kuendeshwa na Kampuni ya *Power Pool (East Africa) Limited,* unatazamiwa kuchukua ardhi za wananchi wa Vijiji vya Kisasida na Januka katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida. Katika kutekeleza mradi huo, Maafisa Ardhi wa Manispaa walifanya tathmini ya maeneo yatakayoathiriwa na mradi huo. Hata hivyo, wananchi wa maeneo husika wamelalamikia zoezi zima la tathmini hiyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi ambao maeneo yao yamewekewa *beacon* kwamba yako ndani ya mradi hawajafanyiwa tathmini yoyote na wala hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa Kata ya Kisasida (Mheshimiwa Diwani) na Kijiji cha Jamuka wamehujumu zoezi zima la tathmini kwa kuweka majina ya ndugu na jamaa zao wa karibu kwenye orodha ya walipwa fidia wakati watu hao hawana maeneo yaliyoko kwenye mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia iliyolipwa ni kwa ajili ya ardhi na miti tu. Fidia ya upotevu wa faida, usumbufu na usafiri haijalipwa kinyume na matakwa ya Kanuni za Ardhi za Vijiji za mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini imefanywa na wathamini ardhi wa Serikali wakati Serikali haikuwa na wajibu kisheria wa kulipa fidia husika bali ni wajibu wa mwekezaji au anayehusika yaani *Power Pool (East Africa) Limited*. Hii ni kinyume na matakwa ya Kanuni za Ardhi za Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho ya hoja za Wabunge alitolee tamko suala hili na aeleze kama Serikali itafanya uchunguzi wa suala hili.

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao kwa hotuba nzuri ya bajeti ya 2012/2013. Nawatakia utekelezaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache kwa nia ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie sana tatizo la migogoro ya ardhi katika vjijiji vyetu. Suluhisho lake ni kuhimiza uwepo wa mipango ya matumzi bora ya ardhi pamoja na uanzishwaji wa Masijala za Ardhi Vijijini ikienda sambamba na upimaji wa ardhi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutambua mapungufu ya Mabaraza ya Ardhi katika ngazi zote. Ikiwezekana kitafutwe chombo mbadala kama Serikali imeazimia kuhakikisha wananchi wanapata haki katika masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana Shirika la Taifa la Nyumba *(NHC)* kwa utendaji uliotukuka. Naomba waisaidie Serikali kujenga nyumba katika Wilaya na Halmashauri mpya. Hatua hii itasaidia kupeleka huduma karibu na wananchi kama ilivyokusudiwa. Nawakaribisha Mvuha, Makao Makuu ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafute mwarobaini wa kuondoa au kukomesha rushwa iliyokithiri katika Idara za Ardhi na Mipango Miji katika Halmashauri zetu. Hii ni kero kubwa sana inayochangia kukosa haki ya umilikaji halali wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kwamba miji yetu sasa inapangwa vizuri kwa kupima viwanja vya kutosha na vya bei nafuu ili kila mwananchi aweze

kununua. Maeneo ya *Squatter* sasa yatafutiwe uwezekano wa kuboresha maeneo haya ili kupunguza athari za Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali irudishe maeneo ya wazi pamoja na viwanja vya michezo. Kutokuwepo kwa viwanja kunawanyima watoto haki ya kucheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isitishe ofa ya shamba la Serikali ambalo lilipwa Halmashauri ya Morogoro kwa ajili ya uwekezaji shamba hili lipo katika kijiji cha Usungura Kata ya Mkulasi. Naomba wananchi wapewe mwekezaji ambaye atatoa hisa asilimia 25% kwa Halmashauri. Hivi sasa *TIC* imeamua kushirikisha Halmashauri ya Wilaya pamoja na Serikali ya Kijiji. Naomba wafuate taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kwamba Shirika la Nyumba la (*NHC)* katika gharama zake liondokane na kujumlisha gharama za barabara, maji na umeme – hivyo ni vitu vinavyotakiwa kufikishwa au kupelekwa maeneo yanayojengwa nyumba hizo na Serikali Kuu kupitia Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ukipunguza gharama hizo utakuwa umewasaidia wanunuzi wa nyumba hizo kununua kwa bei nafuu vile vile shirika liwe tayari kutumia *low cost material* kama vile tofali la udongo na mbao za

*cyprus* kwa kutengenezea *furniture* ambazo kama zitatumika vizuri zinaweza kuishi hadi miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia isisahaulike kwamba kwa vile nyumba hizo zikijengwa zifuate masharti ya sheria za zimamoto ili watakaonunua wawe huru na salama katika suala zima la zimamoto sambamba na mambo hayo wasisahau kujenga katika dhana nzima ya kuwafikiria walemavu. Suala la matumizi ya njia zote mbili yaani umeme na gesi lipewe kipaumbele ili yatakapofika matumizi ya gesi waweze kupata huduma hiyo kirahisi. *NHC* isisahau na Zanzibar wanahitaji huduma yao na soko lipo, hivyo nako huko kupelekwe huduma hii.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu huu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuweza kuandaa bajeti hii na kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu. Wizara hii ina changamoto nyingi, lakini naamini kwa msimamo wa Waziri na Naibu wake wataweza kurudisha imani iliyokwishapotea kwa Watanzania kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa sana katika masuala ya ardhi katika nchi yetu mpaka kumesababisha vifo kutokea. Niiombe Serikali kupitia Wizara hii kuhakikisha inatoa fedha za kutosha kuwezesha zoezi la upimaji ardhi katika maeneo ya nchi yetu yafanyike na kutenga maeneo mfano, kilimo, ufugaji, makazi na

maeneo mengine muhimu. Naamimi tukifanya hivi na Wizara hii ikisimamia kwa umakini na uadilifu nchi yetu itaachana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la uvamizi wa maeneo wazi katika maeneo ya nchi yetu ambapo imesababisha hata watoto wetu kukosa maeneo ya kuchezea. Tatizo hili liko hasa kwenye Manispaa ya Kinondoni kutoa maeneo kwa watu bila kufuata taratibu na hii ni kwa sababu ya rushwa. Wako wananchi waliozuiwa kujenga katika maeneo hayo wakakimbilia Mahakamani na kushinda kesi lakini pamoja na kushinda walitakiwa wapate kibali cha ujenzi kutoka Manispaa ya Kinondoni hawakufanya hivyo wakaendelea na ujenzi bila kibali hicho. Je, Wizara inasema nini juu ya watu hao ambao hawakufuata utaratibu huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie utoaji wa ardhi kwa wawekezaji. Sisi kama nchi tunawahitaji wawekezaji lakini tuchukue tahadhari kwa watu hawa wanaojiita wawekezaji kwa sababu tumeona wanavyowanyanyasa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara hii kusimamia kwa makini suala hili ili Watanzania wafaidike na ardhi waliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii, naomba yafanyiwe kazi niliyoyaeleza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa jitihada kubwa wanazofanya katika

kuisimamia Wizara hii, ambayo sote tunajua inachangamoto nyingi sana za kiutendaji na kimfumo. Ni Wizara ngumu sana, lakini vile vile Wizara muhimu kwa mustakabali wa maisha ya Watanzania na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali ardhi ina umuhimu wa kipekee kwa uhai wa maendeleo ya binadamu, wanyama, mimea na viumbe vyote. Kwa uchumi wa Taifa letu ambalo wananchi walio wengi wanategemea sana kilimo kama sekta muhimu katika kukidhi mahitaji ya kila siku; rasilimali ardhi inakuwa na umuhimu wa kipekee, kiasi kwamba ni haki ya kila mwananchi kuipata, kuimiliki, kuitumia na kuitunza. Kimsingi raslimali ardhi inahitajika ili kuendeleza sekta nyingine za uchumi, kama vile viwanda, biashara na hata kwa makazi ya binadamu ambayo hutegemea ardhi kwa ujenzi wa nyumba, barabara na matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na ukweli huu rasilimali ardhi inabeba sifa ya kuwa haki ya kila Mtanzania na kwamba kumnyima Mtanzania yeyote haki ya kumiliki na kuitumia ni uvunjaji wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbi la kuwepo kwa migogoro ya mipaka na uvamizi wa ardhi katika maeneo ya vijiji limekuwa tatizo kubwa katika nchi yetu. Tatizo hili ni kikwazo kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Migogoro hii imeendelea kusababisha upotevu wa mali, vifo na kuendeleza uhasama kati ya jamii na jamii na hivyo kuwafanya wananchi kubaki maskini na kuishi maisha duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa sababu zinazochangia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa migogoro hii ni kasi ndogo ya upimaji ardhi, wataalam wa ardhi kutowashirikisha wananchi wakati wa uwekaji mipaka na kutowaelimisha wananchi juu ya mipaka iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa wataalam wa ardhi wanawashirikisha na kuwaelimisha wananchi wakati wa uwekaji wa mipaka. Vile vile Wizara iongoze kasi ya upimaji ardhi ili kuzuia wajanja wachache kuvamia maeneo pasipo viongozi wa vijiji kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji imeendelea kuwa chanzo cha machafuko na umwagaji damu nchini. Lazima kasi yetu ya kutenga maeneo maalum ya wafugaji na wakulima iandamane na utungaji wa sheria kali utakaozuia uvamizi wa maeneo unaofanywa na pande hizi. Aidha, kuwepo kwa mashamba makubwa yasiyoendelezwa ni chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wetu wa kufuta milki ya ardhi isiyotumika ipasavyo kwa mujibu wa makusudio ya umiliki wa ardhi husika unatoa mwanya wa watu wachache kuhodhi ardhi bila kuitumia na kuwaacha wananchi wengi kutaabika kwa kukosa ardhi. Ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili, ni vema Serikali ikaiangalia upya sheria ya umiliki ardhi ili tuweze kuwa na mfumo utakaowezesha mashamba yaliyotelekezwa kuweza kufutiwa hati za umiliki mara tu yanapothibitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine linalopaswa kufanyiwa kazi kwa haraka ni kupitia upya viwango vya fidia na kodi ya ardhi vinavyolipwa na wawekezaji. Viwango hivi kwa sasa ni vya chini mno; lazima viwango hivi viongezeke ili kuwezesha wananchi na Serikali kufaidika na rasilimali ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mkinga, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ziara aliyoifanya katika Wilaya yetu. Ujio wake katika Wilaya yetu umeleta matumaini makubwa na kuijengea heshima Serikali ya Chama cha Mapinduzi miongoni mwa wananchi walio wengi. Wilaya ya Mkinga ni miongoni mwa Wilaya zinazokabiliwa na migogoro ya umiliki wa ardhi na mashamba yaliyotekelezwa muda mrefu. Kwa nyakati tofauti Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga na mimi binafsi tumewasilisha Wizara ya Ardhi mapendekezo ya Wilaya husika utatuzi wa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mapendekezo ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga yaliwasilishwa Wizara ya Ardhi tangu mapema mwaka 2007 wakati huo Mkinga ikiwa bado ni sehemu ya Wilaya ya Muheza; ofisi yangu iliwasilisha tenda maombi hayo kupitia barua Kumb. MB/MKN/Ardh 01/2011 ya tarehe 17 Novemba, 2011. Napenda kuikumbusha Wizara juu ya maombi haya ambayo kimsingi yamechukua muda mrefu kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la Kilulu ndipo palipojengwa Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga. Shamba hili kwa mara ya kwanza lilimilikishwa kwa Bwana

Van Brandis na Bibi Van Brandis hadi 31.10.1959 ambapo umiliki ulihama kwenda kwa Bwana Akberali Walii Jiwa. Mmiliki huyu hakuendeleza shamba hili lenye ukubwa wa ekari 5,699.9 hadi umiliki wake ukafutwa mwaka 1972. Baada ya kufuta umiliki, Serikali ililipa fidia na shamba likawa chini ya Serikali.

Baadaye Wilaya ya Muheza ilipokea maombi ya kumilikishwa shamba hilo toka kampuni ya *M/S Arusha Farms Limited (CHAVDA)*. Taratibu zote zilifanyika na alimilikishwa ekari 2,699.9 na ekari 3,000 walipewa wananchi wa vijiji jirani vya Vuo Mwachala na Parungu Kasera waliokuwa na shida ya ardhi. *M/S Arusha Farms Limited* walipewa barua ya toleo *(Letter of Right of Occupancy)* ya tarehe 10/5/1991 ambayo ilisajiliwa na Msajili wa Hati aliomba mkopo kutoka *CRDB* kwa kuweka rehani barua ya toleo. Aidha, alishindwa kurejesha mkopo huo na *CRDB* waliuza shamba kwa *M/S Mbegu Technologies Limited* tarehe 27/3/2004 ambao walilipa mkopo huo. Lakini pia hakuweza kuliendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Bwana Akberali Jiwa licha ya kunyang'anywa shamba hilo na kulipwa fidia aliwasilisha ombi lake la kurejeshewa umiliki wa shamba hilo. Ombi lake liliwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Kugawa Ardhi tarehe 10/10/1996 na iliazimiwa liwasilishwe katika Kamati ya Ushauri wa Ardhi Mkoa. Kamati hiyo chini ya Uenyeviti wa Mkuu wa Mkoa aliridhia Bwana Akberali Jiwa apewe shamba hilo kwa vile *M/S Arusha Farms Limited* wameshindwa kuliendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Muheza ilitoa barua ya toleo kwa miliki ya miaka 99 kuanzia tarehe 1/10/1998 kwa Akberali Jiwa kwa jina la Kampuni ya Kilulu (2000) *Limited*. Baada ya tatizo hilo la *double allocation* kujitokeza, Halmashauri ya Muheza iliandika barua Kumb. Na. *MUDF*/3844/63 ya tarehe 2/4/2007 kwenda kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya kuomba kufuta milki hizo. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri hadi leo Halmashauri haijapata majibu yoyote licha ya ufuatiliaji uliofanywa wa mara kwa mara. Naiomba Serikali ifute milki hizo kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la Moa lina ukubwa wa ekari 15,739.60 na linamilikiwa na Mkomazi *Plantations Limited* wa S.L.P. 2520 Dar es Salaam kwa hati Na. 4268, 9780 & 9781. Halmashauri ya Wilaya ilituma notisi ya kuwafutia hati miliki yao kwa kutoendeleza na kutolipia kodi. Baada ya hapo Halmashauri ya Wilaya iliwasilisha barua ya mapendekezo kwa Kamishna wa Ardhi yenye Kumb. Na. *MKG/LD/F*/2/54 ya tarehe 28/7/2009. Taratibu za ufutaji hati milki ziliendelea Wizarani, lakini Halmashauri ilipokea barua ya mmiliki akieleza kuwa jina la umiliki lilibadilika na kuwa *Moa Plantation & Agriculture* wa S.L.P. 364, Dar es Salaam na kwamba wanataka kuendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilikwishawasilisha Wizarani, barua ya mapendekezo ya kufuta hati miliki, ililazimika kumwandikia Kamishna wa Ardhi barua yenye Kumb. Na. *MKG/LD/F/*2/56 ya tarehe 9/6/2011 kumweleza kupokea barua hiyo na kwamba shamba hilo lina vijiji vinne ambavyo vimeanzishwa na kusajiliwa (Moa, Ndumbani, Mayomboni na Mahandakini).

Aidha, vijiji hivyo tayari vina huduma za jamii kama shule, zahanati, barabara na kadhalika. Katika maeneo hayo, hivyo aendelee na taratibu za ufutaji hati miliki au kama atasitisha ufutaji, basi wamiliki wakubali kumega maeneo yanayokaliwa na vijiji na kuendelezwa na wananchi. Hadi sasa Halmashauri ya Wilaya inasubiri uamuzi wa Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwele *Seed Farm* lina ukubwa wa hekta 964. Mmiliki ni Wizara ya Kilimo. Halmashauri ya Wilaya iliandika barua kwa Kamishna wa Ardhi Kumb. Na. *MUD/ASF/Vol. VI*/35 ya tarehe 21/9/2007 ya kupendekeza kumegwa kwa vile uendelezaji wake ni mdogo sana na kodi hailipwi. Shamba hili linapakana na kijiji pekee katika Wilaya ya Mkinga ambacho kimekosa hata eneo la kujenga shule ya msingi. Aidha, shamba hili linapakana na Mji Mdogo wa Maramba ambao hauwezi kupanuka. Hadi sasa Halmashauri ya Wilaya inasubiri jibu la Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Maramba J.K.T. ukubwa wake ni hekta 2,445 na linamilikiwa na jeshi. Eneo kubwa halitumiki na halilipiwi kodi. Barua iliyoandikwa kuhusu Mwele *Seed Farm* iliunganisha pia mapendekezo ya kumega shamba hili ili wananchi wa Mji Mdogo wa Maramba waweze kupata eneo la kujenga makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja nikiamimi kwamba Serikali imesikia kilimo cha watu wa Mkinga na itayapatia ufumbuzi matatizo niliyoyaainisha.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote na wafanyakazi kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu migogoro ya ardhi inayoendelea kati ya wakulima na wafugaji. Tatizo hili kwa kiasi kikubwa linachangiwa na kutokuwa na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi *(good land use plans)* hata pale ambapo mipango hiyo ipo, kuna uhaba wa huduma muhimu zinazotakiwa, kwa mfano, maeneo ya malisho ya mifugo yanayopaswa kuwa na mabwawa na mabirika ya kunywesha maji mifugo. Aidha, hata malisho (nyasi) zinatakiwa kuwepo zisichomwe moto na katika maeneo maalum zinaweza kupandwa na hata kumwagiliwa maji kwa kifupi. Tunahitaji kuwa na maandalizi ya mipango mizuri ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya migogoro ya ardhi inajitokeza kwa sababu pande zinazohusika zinaingia makubaliano bila kuihusisha Wizara ya Ardhi na migogoro inapoibuka ndipo Wizara inahusishwa. Nashauri wananchi na wawekezaji wa aina yoyote ile wawe wanaihusisha Wizara ya Ardhi katika mipango yao. Nasema hivi kwa sababu uwekezaji wa aina yoyote unafanywa juu ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara imalize mgogoro uliopo kati ya mwekezaji wa shamba la Kapunga na wanakijiji wanaomzunguka. Tayari nimekwishaleta maelezo ya kina ya mgogoro uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana wafanyakazi wote wa *NHC* kwa mashirikiano yao mazuri wanayoshirikiana na Mkurugenzi wao pia kuweza kujenga nyumba za kununua wananchi ili wapate makazi yenye uhakika. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuchangia kuhusu Kigamboni mpya, naiomba Serikali ifanye jitihada za haraka sana ili wananchi wa huko wajue hatima yao kwa sababu hivi sasa wanaishi bila kujua nini kinaendelea. Pia naomba wajulishwe kila kinachoendelea kuhusiana na hiyo Kigamboni mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndio rasilimali mama katika maisha na maendeleo ya kila raia wa nchi husika, sera yetu ya ardhi bado haijatoa fursa kwa raia kumiliki ardhi na kumiliki kilichomo ndani. Kama kuna madini ambayo ni mengi Serikali huchukua ardhi hiyo bila ya kutoa tathimini halisi ya fidia kwa mmiliki wa ardhi hiyo yenye mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ibadilishe sera ya umiliki wa ardhi kama ilivyo Ulaya na Arabuni ambayo ukimiliki ardhi ni pamoja na rasilimali zilizopo. Kama ushauri huu utafuatwa Watanzania wengi wataondokana na umaskini kwani wataweza kufaidika na ubia wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi, pamoja na juhudi za Serikali za kupima na kutoa kati ya umiliki.

Naishauri Serikali iendelee na juhudi hizo kwa kufanya program maalum ya kuhakikisha kuwa kila kaya imepimwa ardhi na kupewa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya ujenzi wa nyumba za kipato cha chini, kati na juu iendelezwe kwa kasi zaidi ila nashauri, nyumba zote zitengenezwe *land scaping*, uvunaji na maji ya mvua na pia kutumia teknolojia ya ujenzi inayoweza kujenga *min city* kwa gharama nafuu.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi japo nikipata nafasi ya kuongea pia nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kuipongeza Wizara hasa katika kusimamia sheria na kuanza kuvunja nyumba kwa wale ambao wamekiuka taratibu halali za ujenzi katika maeneo yanayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi ni zuri japo limechelewa sana kufanyika, napenda sasa kuona sheria hii haibagui matajiri na maskini maana wapo watu wengi wakubwa wamejenga ufukweni na mfano, mzuri ni *Slipway* na pia ipo hoteli ya kitalii ya *Golden Tulip*, kama hawa hawatachukuliwa hatua naiona hatari ya mgawanyiko hapo mbele kuhusu suala hili, maana tayari minong'ono kuhusu suala hili limeanza kujitokeza na napenda sana wakati Waziri au Naibu Waziri akifanya majumuisho basi aeleze kwa kina kabisa kuhusu maeneo hayo mawili ambayo nimeonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vizuri sasa kuendana na sayansi ya kisasa katika ujenzi wa majengo baharini na pwani ya bahari kama *Burj Arab* ya Dubai na *Jumlirah Beach* ni majengo ambayo siyo tu yapo pwani ila pia yapo mita chache ndani ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni muda muafaka sasa wa kuwaelewesha na kuwafundisha watu wetu kuhusu ujenzi huu wa uwekezaji wa majengo ya kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana pia kutoa pongezi za dhati kwa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, kwa ubunifu mkubwa na wa kisasa katika ujenzi wa nyumba. Wazo ni zuri sana ila tatizo bado gharama za manunuzi ni kubwa sana kulinganisha na kipato cha Watanzania wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipendekeza shirika liwe na timu yake yenyewe ya ujenzi yenye wataalam wa kutosha kwa ajili ya ujenzi kuliko kuwapa wakandarasi. Pia ni vizuri shirika likaomba msamaha wa kodi katika kuingiza vifaa vya ujenzi kwenye nyumba za wananchi wa hali ya chini sana ili kuzipunguzia gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waziri atakubaliana na mimi kuwa tayari kuna makazi holela na yasiyopimwa hasa katika Mkoa wa Mara, Wilaya ya Musoma Mjini, eneo la Nyakato ambalo upimaji wake ni mgumu ila kama Wizara itawaelimisha watu hao na jinsi gani ya kuwasaidia wataalam, hali hiyo ya makazi itaendelea kuwa duni na utoaji wa anuani ya makazi itakuwa na changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza basi kama kuna uwezekano mimi mwenyewe na hata kwa kushirikiana na Halmashauri, basi eneo la Nyakato liwe ni eneo la mfano katika maeneo yaliyokuwa siyo makazi rasmi na kwa kuwa makazi tayari yamepimwa ili iwe mfano kwa maeneo mengine Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependekeza eneo hili kuwa la mfano kwa ajili ya kuwa Mara kumekuwa na migogoro mikubwa sana ya ardhi na kama tukifanikiwa katika eneo hili, basi hakuna eneo ambalo Serikali itashindwa kama ikifanikiwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo la mwisho napenda sana kushauri kuhusu uharakishwaji wa kupima ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Musoma iliomba wataalam wa Wizara ambao wana vifaa vya kisasa na utalaam hasa ukizingatia katika Halmashauri nyingi wataalam wa ardhi bado wanatumia mbinu na vifaa vya kizamani sana. Dar es Salaam tulikwishalipa na kufunga mikataba, lakini cha ajabu hadi leo hakuna mwelekeo wa haraka wa wapimaji kuja kutupimia viwanja hivyo. Naomba sana katika majumuisho basi Waziri atuambie wapimaji hao wapo kwenye hatua gani na pia ningeomba Waziri atoe wito kwa Halmashauri zote zihamishe watu wetu kuhusu upimaji na upatikanaji wa hati ili kuondokana na migogoro mikubwa ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nipende kutoa shukrani kwa watendaji wa Wizara na Waziri

mwenyewe pia Naibu wake kwa kuifanya kazi hii ngumu kwa maslahi ya nchi.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa upande wa ardhi. Tatizo kubwa la nchi yetu ambalo linasumbua wananchi wengi ni ardhi. Tatizo la kwanza, wananchi hawana hati za kumiliki ardhi yao ili iwe rasilimali yao katika kupata mikopo ya benki. Ingawa kuna hati za kimila zinazopaswa kutolewa, lakini bado walio wengi hawana kwa wale wa mijini kuna gharama kubwa ya kupima viwanja. Kwa hiyo, kwanza naishauri Serikali itafute pesa za kutosha ili ardhi yote ya Tanzania ipimwe na wamilikishwe Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni tatizo la viwanja. Viwanja vinapatikana kwa tabu na mara nyingine rushwa inabidi itumike ili upate kiwanja kwa ajili ya kujenga nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa tatizo hili ambalo linatokana na uchache wa viwanja, Serikali ijitahidi kupima kuvigawa kwa wananchi pesa zitakazopatikana zitasaidia kupima viwanja vyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyumba pia ni kubwa sana katika nchi hii. 80% ya Watanzania wanaoishi vijiji hawana nyumba nzuri za kuishi, lakini hata wanaoishi mijini, wengi wanaishi katika nyumba za kupanga, tatizo

kubwa ni vipato vya wananchi haviruhusu wananchi kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* linajenga nyumba za bei nafuu. lakini bado unafuu unaozungumzwa haumwezeshi Mtanzania wa kawaida kukopa. Naishauri Serikali kuwapatia wananchi wa kawaida mikopo ya fedha za muda mrefu kupitia benki zetu ili waweze kujenga nyumba za kisasa.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya makadirio ya Wizara kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Pia napongeza juhudi zote zinazofanywa na viongozi wote wa Wizara wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na viongozi wote wa idara na vitengo.

Mheshimiwa Spika, kazi zinazofanywa na Shirika la Nyumba *(NHC)* zinastahili pongezi kubwa. Wilaya ya Chamwino ni moja ya Wilaya mpya ambayo inajenga Mji wa Makao Makuu ya Wilaya kule Bwigiri ambako hivi sana tunapima viwanja na kuvigawa kwa matumizi mbalimbali. Tungeomba Shirika la Nyumba lishirikiane na Wilaya yetu kuendeleza Mji wetu wa Makao Makuu ya Wilaya kwa kupata viwanja na kujenga nyumba kwa matumizi mbalimbali. Naomba maafisa wa *NHC* waje wapate viwanja tujenge Wilaya yetu mpya ya Chamwino ambako na Ikulu yetu ya Chamwino imo ndani ya Wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya mipaka liko katika maeneo mengi hapa nchini ikiwemo ile ya Kijiji kwa Kijiji, Kata kwa Kata, Wilaya kwa Wilaya na Mikoa kwa

Mikoa. Migogoro hii mahali pengine imesababisha umwagaji damu, upotevu wa mali na kucheleweshashughuli za maendeleo. Chanzo cha migogoro mingi inatokana na mivutano ya viongozi wa maeneo husika kugombania maeneo. Wizara ya Ardhi ndiyo chombo pekee ambacho kinaweka mipaka ya maeneo yote nchini na inapotokea migogoro hii haipati ufumbuzi wananchi wanashindwa kuelewa kama kweli Wizara inalisimamia suala kwa stahili yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumaliza suala la migogoro ya mipaka, nashauri Wizara iandae program maalum ya kuipatia mipaka yote ya Vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa na kuandaa ramani ya kudumu itakayoeleweka kwa wananchi wote kupitia kwa viongozi wao. Program hiyo pia iandaliwe sambamba na utoaji elimu kwa wananchi juu ya matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwemo kilimo, mifugo, makaazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi wa Idara ya Ardhi Wilayani. Matatizo mengi yanayotokea Wilayani yanatokana na kukosekana kwa maafisa ardhi kwenye Wilaya. Kutokana na kupanuka kwa mahitaji ya matumizi ya ardhi kwa wananchi wengi nchini, ni vema Wizara iangalie upya suala la kuajiri watumishi wa Idara ya Ardhi wa kutosha na kuwasambaza Wilayani. Lakini ili waweze kuwajibika kiutalaam, napendekeza watumishi hawa wasimamiwe na Wizara moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongezeni nyote, nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni uvamizi na ugawaji wa viwanja katika maeneo ya wazi. Kwa kuwa kumekuwa ni tatizo sugu la uvamizi na ugawaji wa viwanja au maeneo yaliyoachwa wazi kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo michezo na shughuli za mikusanyiko mbalimbali. Ni kwa nini Serikali imekuwa ikikaa kimya mpaka ujenzi unafanyika kwenye maeneo hayo na baadaye kuleta usumbufu mkubwa wa kuyashughulikia maeneo hayo ikiwemo maswala ya kisheria? Ni kwa nini maeneo haya ya wazi yasiwe yanalindwa na pindi yanapovamiwa au kugawiwa kwa watu wenye fedha sheria isichukue mkondo wake na kuwanyang'anya wahusika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi za Sekondari hazina viwanja vya michezo ambavyo ni vigezo mojawapo vya kusajili shule. Hii ni kwa sababu viwanja hivi huwa aidha vimevamiwa au kugawiwa kwa wawekezaji kwa ajili ya shughuli zingine. Ni kwa namna gani tutawafanya watoto wetu wawe na afya bora kwa kutokucheza maana michezo ni afya na tunafahamu kwamba wanafilosofia wakubwa (*Plato*) waliwahi kusema kwamba michezo ni muhimu kwa ukuaji wa akili na afya ya mtoto, *a health mind is a health people*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu ugawaji wa viwanja kwa zaidi ya mtu mmoja; kumekuwa na matatizo makubwa yanayosababishwa na watendaji wa ardhi ya kugawa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa wanunuzi

ikiwepo kudai haki zao Mahakamani. Ni kwa nini Wizara imekuwa ikiwafumbia macho watendaji hawa ambao si waaminifu? Ni kwa nini kiwanja kimoja kigawiwe mara mbili au zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni ufuatiliaji wa hati za viwanja; kumekuwa na urasimu mkubwa sana katika kufuatilia hati za viwanja, zoezi hili limekuwa likigubikwa na mlolongo mrefu wa ufuatiliaji kuanzia *survey* mpaka hatua ya kupewa kiwanja. Ni kwa nini Wizara isipunguze hii *bureaucracy* ya kupata hati kama ni kweli mtu anastahili hati hiyo kihalali? Zoezi hili mara nyingi limekuwa likiambatana na rushwa na upotevu mkubwa wa muda wa kazi. Naiomba Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili ni lini Serikali itatoa mwongozo unaoeleweka kuhusu hati za kimila hasa huko vijijini ambako wananchi wengi wanamiliki mashamba, lakini hawawezi kupata mikopo katika taasisi za kifedha kutokana na wao kutokuwa na hati. Hati za kimila zimekuwa hazitambuliwi vema, hivyo ni busara kwa Wizara kutoa maelezo ya kina na ufafanuzi kuhusu hati hizi na namna ambayo zinatakiwa zikubalike katika taasisi za kifedha. Ili kuepusha usumbufu wanaopata wananchi wa vijijini na pia kuweza kuwatendea hati ya kupata mikopo ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, kwanza nilipongeze shirika hili kwa kuonesha kwamba Watanzania wakiamua kufanya maamuzi magumu wanaweza na ndivyo uongozi wa *NHC* ulivyoweza kuchukua hatua za kuwafukuza wadaiwa sugu ambao walikuwa wanaishi kwenye nyumba bila kulipa, walikuwepo

watumishi wa Wizara na idara mbalimbali za Serikali, hivyo nashauri mashirika mengine zikiwepo mamlaka za maji nchini kuweza kufanya maamuzi magumu ya kulipwa fedha zao na wadaiwa sugu ambao ni majeshi, JWTZ, JKT, Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo nitoe rai pia kwa kuwa *NHC* imeamua kuwajengea nyumba zenye bei nafuu wananchi, iangalie kwamba ni kweli lengo hilo linatumia na kweli wananchi wenye kipato kidogo wanapata fursa ya kuzinunua na isije ikaja kutokea wenye fedha wakazinunua na kuanza kupangisha kwa wananchi wenye kipato kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo bei za nyumba hizo pia ziangaliwe, maana kwa hali halisi mwananchi wa kawaida na mtumishi wa Serikali hawezi kumudu kununua nyumba ya zaidi ya shilingi milioni 590 na kuendelea. Naomba shirika hili liangalie namna nyingine bora ya kuwasaidia wananchi wenye uwezo wa kati kuwasaidia wananchi wenye makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Morogoro Manispaa unakuwa kwa maana makazi ya watu yanapanuka katika mji. Tatizo lililopo ni mashamba ya mkonge ambayo bado yapo mjini na mji umekua na makazi ya watu yanapanuka. Naishauri Serikali kuyafuta mashamba hayo na kuacha maeneo hayo kuendelea kugawiwa kama viwanja ili wananchi waendelee kupewa nafasi za kujenga na kuwa na nafasi katika makazi ya watu, mjini badala ya kubanana sehemu moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mashamba ambayo nayo yako kati kati ya mji mashamba ya *SUA*. Naishauri Serikali iyatoe kwa wananchi ili yawe viwanja na kuwa makazi ya watu ukizingatia *SUA* wana ardhi kubwa katika Manispaa ya Morogoro. Kuna maeneo ya Morogoro Manispaa ambayo yalikuwa mashamba ya wananchi wa manispaa yamechukuliwa na kuwa makazi ya watu, lakini wenye mashamba hayo hawajalipwa fidia mpaka sasa waliolipwa ni wachache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi inasajili maeneo hayo bila kujali kama wananchi wamelipwa fidia au la, wananchi hawa wa Kiyegeya, Mgulu wa Ndege, Lukobe, wamedhulumiwa fidia zao. Naishauri Wizara ya Ardhi, kwa maana tunaomba Waziri aje kuongea na wananchi waliodhulumika na kuona maeneo yenyewe na kuwapa majibu lini watalipwa fidia zao ambazo imekuwa ni hadithi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nyumba za *National Housing* Manispaa ya Morogoro lakini ni chafu mno na hasa *flats* wanazokaa wananchi wa hali ya chini katika maeneo ya Kilakala ambazo zinatambulika kama Kilakala, Kata ya *Forest,* hizi *flats* ni chafu mno na wala hazishughulikiwi. Katika nyumba hizo pia kuna wastaafu wajane ambao wanakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majengo ya *NHC* ambayo wanapewa watu binafsi kubomoa na kujenga maghorofa. Utaratibu huo ni mzuri, lakini *NHC* wana watu ambao wanawapa majengo hayo badala ya kutoa kwa *tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, hao watu wapo wawili wakienda *NHC*, wanapewa majengo hayo, lakini wengine wakienda wanaambiwa msubiri *tender* na wakati huo hakuna *tender* wanatoa sababu tu ya kukwepa na kuwapa watu wengine watakaoweza kujenga kwa ubia na *NHC* hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Je, hawa watu kuna manufaa gani katika *NHC* na hawa watu. Wenye uwezo wa kupewa na kuingia ubia na *NHC* kujenga kama upo lakini isiwe *NHC* wanawapa watu wao tu kwa maslahi yao binafsi na sio wananchi.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua Mji wa Kigamboni kuwa mji wa kisasa kwa kuanza kujenga upya katika makazi ambayo kwa hivi sana tayari wananchi walishakuwa na makazi yao ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu ni mzuri kwa maendeleo ya nchi yetu na wakazi wa Mji wa Dar es Salaam kwa ujumla. Mpango huu toka umetangazwa kwa sasa imefika mwaka wa nne, lakini hakuna jambo lolote ambalo wananchi wanaona linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kigamboni wamesimamisha shughuli zao za kuendeleza makazi yao kwa kusubiri Serikali itoe utaratibu nini kinaendelea, lakini kwa masikitiko makubwa wananchi hawa wapo hewani tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu unaleta usumbufu mkubwa na kero kubwa kwa viongozi na

wananchi kwa ujumla. Naishauri Serikali kwa dhati kabisa kwa kuwa Shirika la Nyumba lina eneo kubwa huko Kibada, Kigamboni na ni eneo zuri lipo karibu na eneo litakapojengwa daraja la Kigamboni, ni vema sasa tukaacha kutumia gharama kubwa kwa kulipa fidia na kuwatafutia makazi wananchi hawa wa Kigamboni, ni vema mji huo mpya ukaenda kujengwa eneo la Kibada kwenye eneo ambalo liko wazi na zuri sana na bado mji huo tarajiwa utakuwa Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni zuri kuwasaidia wananchi wake, lakini kwa kuwa Serikali ilikuwa bado haijajipanga vizuri, ni vema sasa kuwe na maamuzi ya dhati na yenye kuondoa kero na chuki kwa wananchi kwa kuachana na eneo hili au kukaa upya na wananchi kuwaelimisha nini kinaendelea ili na wao watoe maamuzi au ushauri kwa Serikali ili pande zote mbili ziwe na msimamo wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM tuliahidi kuondoa kero kwa wananchi, naomba tuitekeleze ilani hii kwa vitendo, vinginevyo eneo la Kigamboni pamoja na nia nzuri ya Serikali yetu, kisiasa litaathiri sana chama chetu. Naomba hili litekelezwe kwa umakini mkubwa sana kwa manufaa ya Taifa letu.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi bado inaendelea hasa kwa wale wawekezaji, tunashuhudia kila siku wananchi wanagombana na wawekezaji na husababisha hata kuhatarisha amani kwa nini Serikali haiwi makini kwenye suala hili? Kwa nini Serikali haiji na mfumo mzuri wakati wa

kupata ardhi wa uwekezaji na kuepukana na migogoro ya kila siku. Naishauri Serikali iwe na mfumo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa hati miliki, nazungumzia hizi hati zinazotolewa kwenye Halmashauri za Dar es Salaam, kuipata ina usumbufu kila siku, hivi sasa utaratibu una mzunguko mkubwa wakati wa kupata hati miliki, inachukua hata miaka miwili bado hujapata hatimiliki na kwa mfumo huu unapelekea rushwa itumike ili uweze kupata hiyo hati miliki yako. Naishauri Serikali pale tu unapofika Halmashauri unapotaka kupata hati miliki, gharama zote zinatakiwa kwa njia ya kuwapa risiti na mambo yote yafanywe na Halmashauri na itapokuwa hati yako tayari upigiwe simu kuja kuchukua hati miliki yako na kwa mfumo huu mwananchi hatohangaishwa na pia tutaziba mianya ya rushwa.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi imezidi kushamiri mpaka kupelekea maafa na haya yote yanatokana na Serikali kutokupima ardhi na kuweka mipaka. Ofisi nyingi za ardhi katika Wilaya zetu nyingi hazina watumishi wa kutosha na la muhimu zaidi hawana vifaa vya kutendea kazi, mfano, hawana vifaa vya kupima darubini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina eneo kubwa sana kutoka Wilaya mpaka Vijijini na hata mbali kutoka kijiji kimoja mpaka kiingine ni mbali sana hivyo ni vigumu kwa wapimaji kuwafikia au kufika sehemu ya kupima sababu hawana usafiri. Je, Serikali ina mikakati au mipango gani ya

kuhakikisha upatikanaji wa watumishi vifaa pamoja na usafiri angalau hata pikipiki kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa hati, pamekuwepo tu na matatizo ya maafisa wa hati kutoa hati mara mbili. Ni kwa nini hati zitolewe mara mbili? Kwa eneo moja tena kutoka kwa maafisa hao hao wanatoa hati? Hati kutolewa kwa muda wa miaka 99 na miaka 33, hii ilikuwa enzi ya ukoloni ili kuwakandamiza wazawa, ni aina fulani ya ubaguzi, cha kusikitisha mpaka leo hii mtindo huu bado upo kwa baadhi kupewa hati ya miaka 99 na 33. Je, ni sababu zipi zinazotumika kwa ubaguzi wa kuwapa wananchi wengine hati ya miaka 99 na wengine 33? Naomba jibu kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya malipo ya fidia, pamekuwepo na malalamiko mengi yanayohusu kulipwa fidia kwa wananchi ambao aidha, Serikali imeyachukua kwa upanuzi wa barabara na kadhalika. Aidha, tathmini inachukua muda mrefu na fidia inachukua muda mrefu sana bila sheria kufuatwa. Ni lini wananchi hawa mfano wa Kigamboni na sehemu nyingine katika nchi hii watalipwa fidia zao? Sababu ni kuwatesa wananchi ndani ya nchi yao. Hii huleta mfarakano hata kupelekea vifo kwa baadhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* lilianzishwa ili kuweza kusaidia wananchi kwa kujenga nyumba za bei nafuu kwa wale wenye kipato cha kati na kuachwa duniani masikini. Badala yake shirika hili kwa sasa linajenga nyumba nyingi sana ambazo ni jambo zuri, lakini bei zake ni za juu sana. Je, mwananchi wa kawaida unajengea nyumba ya milioni 30,000/= ukizingatia

wananchi wengi hawana dhamana, nyumba hizi zisingejengwa kwa wenye uwezo tu? Ikumbukwe Serikali inataka kuwa na amani kwenye makazi ya watu, hii ni njia mojawapo ya maendeleo, ni pamoja na kuondokana na nyumba za tembe. Je, kwa bei hizo za juu wataweza?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kusikitisha, Shirika limekuwa likipandisha kodi zake za pango bila kuwaarifu wadau (wapangaji) na bei hizi zinapandana mara mbili. Ikumbukwe siyo watu wote ni wafanyabiashara wakubwa, hivyo vipato ni vidogo, ni vizuri kupandisha bei kwa kuangalia hali ya uchumi inaendeleaje. La sivyo huu ni ukandamizaji na unyanyasaji kwa wananchi wenye kipato cha chini. Nashauri pia tozo ya *VAT* kwa ununuzi wa nyumba zifutwe kwa kuwa tayari ujenzi wa nyumba ile ulishalipiwa *VAT* kwa vifaa alivyotumia kwa kujengwa wakati akivinunua.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia eneo la kuanzishwa hazina ya ardhi, endapo Wizara itakamilisha uanzishaji wa hazina ya ardhi hakika Watanzania wengi sana watanufaika na mpango huo. Endapo kutakuwa na chombo cha kusimamia utoaji wa ardhi kwa wawekezaji kwa kuzingatia kuingia ubia na wawekezaji hasa wale wanaotoka nje ya nchi ni matumaini yangu kuwa haki itakuwa inatendeka kwa wananchi wa Tanzania ambao wengi wao ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wataweza kunuifaka kwa kupata hisa zitakazotolewa kwa uwiano na dhamana ya mtaji wa mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ilete haraka Muswada wa Sheria ya kuanzisha rasmi chombo hicho ili watanzania waanze kunufaika na ardhi yao badala ya kuendelea kuwanufaisha wageni.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu katika Wizara hii ni suala zima la upatikanaji wa hati za kimila za kumiliki ardhi zinazotolewa na Serikali ya Kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni kuwa ardhi ndiyo mali pekee ambayo wananchi wengi wa kawaida wa vijijini ndiyo wanayoimiliki na hivyo wananchi wengi wanategemea mali yao hiyo ardhi iwasaidie kwa namna mbalimbali. Ili kuweza kuifanya ardhi iwanufaishe wananchi wa vijijini ni lazima wananchi hawa wapatiwe hati za kumiliki. Ardhi hiyo na kisha utaratibu huu ufanyike kuwezesha hati hizi za kimila zitambulike katika taasisi kadha za kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi ambazo ni muhimu zitambue hati hizi za kimila ni pamoja na taasisi za kifedha na taasisi ambazo zinatoa huduma za mikopo hasa kwenye pembejeo za kilimo kama mbolea, matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuzifanye ardhi za wananchi wa vijijini ziwe na thamani inayotambulika kifedha iwapo tunataka kweli kuwakomboa wananchi wetu wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza kuwa ardhi ndiyo mali kubwa na pekee ambayo wananchi wetu wa vijijini wanamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Wizara kwa mikakati yake ya kuboresha mandhari ya Jiji la Dar es Salaam hasa kwa kutilia mkazo uanzishwaji bustani za kijamii za Jiji. Namwomba Waziri pia alishughulikie hili katika Majiji mengine kama Tanga ambako kuna sehemu nyingi zilizostahili kuwa bustani za kijamii ambazo nyingi zimeshikiliwa bila kutumiwa ipasavyo na watu wachache. Mfano wa hili ni hekta 63.852 zilizozungushiwa ukuta katikati ya eneo la hadhi ya juu ya Jiji la Tanga kule Raskazoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutoa mwongozo wa kuwaenzi wapigania uhuru waasisi wa nchi hii kwa kuipa mitaa ya miji majina yao. Kule Tanga tumeliona hilo na tayari tumeanza kuliongelea kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, ardhi ndiyo rasilimali namba moja ya nchi kwani kila rasilimali nyingine inatokana na ardhi. Hivyo, mipangilio kabambe inahitajika kuhakikisha kuwa ardhi yetu inaendelea kuwa ni hazina ya Watanzania wote na inatumika vizuri na vyombo, taasisi na wananchi ambao wako tayari na wana dhamira ya kuitumia kwa maendeleo yetu sote na sio kiulanguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, walanguzi wa ardhi wapo na kila uchao wanajitokeza. Ni wajibu wa Serikali kuzuia hilo na

kuthamini kwa kupangilia vile ardhi yetu yote itatumikaje kwa kuipangia matumizi kikamilifu. Uvamizi wa ardhi unafanyika kwa mbinu nyingine hata kujiegemeza kwenye sheria. Wamiliki wanaoshindwa kuitumia ardhi waliyokabidhiwa hasa mashamba wamekuwa wanabadilisha umiliki ili waendeleze kuwanyima wananchi wengine ambao wanaishi kwenye sehemu hizo. Haiyumkini kuwa kijiji kizima cha Kichangani kule Maweni Tanga kiwe kinamilikiwa na mtu ambaye hana shughuli yoyote ya sehemu hiyo na kuwafanya wananchi hao wawe wanaishi hapo kwa ridhaa ya mtu huyo. Huoni mfano mmoja tu wa mifano mingi ambayo ipo katika Wilaya ya Tanga likiwemo shamba la Mkembe, Kata ya Marungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa viwanja vinavyopimwa unaofanywa na Maafisa Ardhi nalo ni jambo lingine ambalo linaendelea kule Tanga na Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi pale alipotembelea Tanga na kukumbana nalo. Namshukuru kwa jinsi alivyolishughulikia hili na kuwezesha mama mmoja aliyedhulumiwa kiwanja chake na Afisa Ardhi kurejeshewa kiwanja chake. Hata hivyo, maafisa hawa hawaonekani kuchukuliwa hatua, jambo ambalo linawapa nguvu ya kurudia kufanya ubadhilifu wao huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa mbinu wa eneo la mwambao wa pwani umekithiri. Naomba Serikali ilishughulikie hili ili maeneo hayo yarejeshwe Serikalini au na vijijini kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za Shirika la Nyumba zinavyouzwa na kupangishwa pia imekuwa ni changamoto nzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano ya matatizo ya ardhi yaliyopo Wilaya ya Tanga ni mengi na yanayogusa kila aina ya matatizo ya ardhi. Namwomba Mheshimiwa Waziri aende Tanga akayaone na ayashughulikie ili yampe uzoefu kamilifu wa kuyatatua, atueleze uzoefu kamilifu wa kuyatatua na atueleze atakuja lini nasi tunamuahidi ushirikiano kamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo ningependa kuliongelea ni ulipaji wa kodi ya ardhi na nyumba. Kwa kweli kodi inayokusanywa ni ndogo mno ikilinganishwa na maeneo ya ardhi pamoja na nyumba zilizojengwa. Ni vyema sasa Wizara ije na mkakati kwa kushirikiana na Manispaa ya Halmashauri zetu. Haiwezekani takwimu za makusanyo ya *property tax* na kodi za ardhi zikawa kwa viwango vilivyopo na bado wamiliki wanashindwa kulipia katika Manispaa mfano, maeneo ambapo majengo makubwa yamejengwa, lakini kodi inayotozwa ni ya ardhi tupu wakati eneo lina maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni *derivative right* inayotolewa na *TIC,* ni vyema wawe makini na msimamie kuhakikisha kwamba wawekezaji hawa wametimiza vigezo. Aidha, Wizara ijitahidi kuboresha

huduma kwa wateja ili wananchi wapate vyeti, nyaraka na vibali mbalimbali kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia Waziri atakapofanya majumuisho yake atueleze Mfuko wa *Housing Revolving Loans*, unatoa mikopo nafuu kwa watumishi, umefikia wapi? Tangu ulipoanza umeshahudumia watumishi wangapi kwa kuwapatia mikopo? Kwani Mfuko huu umekuwa ukilalamikiwa kwamba hauko wazi, haufahamiki na wengi na kwamba mikopo inatolewa si kwa uwazi na kwamba watumishi wenye vyeo vya chini wengi hawajanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Serikali itafute mkopo mkubwa wenye riba nafuu utakaowasaidia watumishi kunufaika nao na kupewa mkopo wa kujenga nyumba kamili kuliko sasa ambapo mtu anapewa kiwango cha juu cha shilingi milioni sita, halafu anaomba tena na hana uhakika wa kupata. Hii haiwezi kumkomboa mfanyakazi hata kidogo. Hivyo Wizara itoe mkopo mkubwa ambao utaweza kukopesha wafanyakazi wote wenye kuhitaji kwa masharti nafuu ili waweze kuwa na nyumba na makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mji wa Kigamboni limekuwa likiuliziwa sana. Je, mpango huu utafanya kazi? Ni lini utaanza na kukamilika? Sambamba na hilo, kwa maeneo ambayo yataainishwa kuwa makazi je, wamiliki wazawa wataweza kuendelea na nyumba hizo au watapata fursa endapo watahitaji kutafuta wawekezaji wabia?

Mheshimiwa Spika, eneo la upimaji na ramani ni muhimu sana. Ni vyema idara hii ikaangaliwa kwa kina na uadilifu wa watumishi wake maana wengine wamekuwa wakibadili michoro bila kufuata utaratibu na baadaye kusababisha migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba watendaji wake wengi wamekuwa wakituhumiwa kwa ukosefu wa uadilifu na wengi wamekuwa na utendaji usioridhisha. Ni vyema sasa watu hawa wakachukuliwa hatua kwani wanatia doa Serikali yetu na utoaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetaarifiwa kwamba ziko Halmashauri kadhaa ambazo zilikopeshwa kwa ajili ya mpango mzima wa mradi wa viwanja 20,000. Hata hivyo kati ya hela hizo zilizokopeshwa bilioni 1.22 hazijarejeshwa. Ni vyema ufuatiliaji wa kina ufanyike na ikibidi Hazina kuzikataa Halmashauri ili maeneo mengine yaweze kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kufahamu kutoka kwa Waziri ni lini itakamilisha utoaji wa hati katika maeneo ya Mbezi Jogoo, Dar es Salaam. Aidha, ningependa kufahamu ni lini vijiji vilivyopo katika Wilaya ya Same watapatiwa hati za kimila? Kwani ukiangalia kwa takwimu za Mkoa wa Kilimanjaro imeachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuligusia ni uwekaji wa rehani. Wako watu wamekuwa wakikopesha watu fedha na watu hao wamekuwa wakichukuliwa hati zao na wanaposhindwa nyumba na ardhi zao zimekuwa zikiuzwa bila ya

mwanandoa kuwa aliridhia mali au ardhi yao kuweka rehani. Ni vyema sasa watendaji wa Wizara ya Ardhi ambao si waaminifu wakaacha kupokea rehani ambazo mwanandoa hajatoa ridhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara yako iangalie upya gharama za upimaji wa ardhi ambazo ni kubwa kuliko uwezo wa wananchi na inasababisha wananchi wengi kushindwa kupata ardhi na kuwa ni nafasi ya wenye uwezo pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ikamilishe taratibu za utoaji hati miliki za ardhi katika kila Halmashauri ili iwe rahisi kwa wananchi kupata kwenye Halmashauri zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaonesha vijana wenye utaalam wa upimaji ili kila Halmashauri iwe na Afisa Mpimaji wake ili kupunguza gharama za kukodi Afisa Mpimaji kutoka eneo lingine kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ABDALLA HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Naanza mchango wangu kwa kusema kwamba ardhi katika nchi yoyote ni rasilimali muhimu sana

kwani ardhi ndiyo mambo yote. Tumekuwa tukishudia migogoro, ugomvi, maafa na hujuma mbalimbali zinazowapata wananchi kutokana na migogoro ya ardhi. Migogoro hiyo inahusisha kati ya wananchi na Serikali; wananchi na wawekezaji; wananchi na mashirika ya uhifadhi, lakini pia wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa yote haya yanasababishwa na matumizi mabaya ya ardhi nchini petu. Ushauri wangu kwa Serikali ili kuyaepusha hayo ni kwamba, Serikali iongeze bidii ya kusimamia vyema hazina hii ya ardhi katika hali ya kupima ardhi na kuigawa inavyostahiki kwa walengwa hasa maeneo ya kilimo yatengwe na yale ya ufugaji, maeneo ya hifadhi, mipaka iwe wazi na kuwabana waliopakana na hifadhi kutii sheria za maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi bila kutunzwa haiwi ardhi endelevu na yenye kuzalisha. Hivyo, Serikali ijikite zaidi katika kusimamia uharibifu unaofanywa na binadamu kama kukata na kuchoma misitu, kuharibu vyanzo vya maji na shughuli za kuchoma mkaa. Yakidhibitiwa haya na mengineyo hali inaweza ikaboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la nyumba na makazi; nyumba ni miongoni mwa mambo yanayosisitizwa na Serikali kwa wananchi wote kuishi katika nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kupitia Shirika lake la nyumba la Taifa *(NHC)* wamedhamiria na wana nia ya dhati kuwasaidia wananchi kupata nyumba bora na za bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa kupitia Shirika hili ilipe Shirika la Nyumba ushirikiano wa dhati kabisa. Ikumbuke kwamba ina wajibu mkubwa juu ya kwasaidia wananchi kupata nyumba bora za bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwamba ili unafuu kwa ununuzi wa nyumba za Shirika upatikane kwa wanunuzi na wapangaji, kuna mambo ambayo Serikali kwa kushirikiana na wahusika wengine yanaweza kuleta unafuu na wananchi nao wakajisikia kwamba nao ni sehemu ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwao ni suala zima la kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)*, Serikali iweze kusimamia na kuridhia kuondoa kodi hii ili shirika lipate nafasi ya kuuza nyumba hizi kwa bei muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lalamiko lingine ni suala zima la miundombinu katika maeneo mapya. Naishauri Serikali kuwataka wahusika wa maji, umeme na barabara, mfano, Shirika la *TANESCO, DAWASCO* na *TANROADS*, yawajibike ili hizi gharama ziwaondokee Shirika ili watoe wasaa mzuri juu ya bei za nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naiomba Serikali isikubali kabisa kuwafumbia macho wananchi wanaojenga katika maeneo yasiyoruhusiwa na baadaye kusubiri majengo tayari na kuanza kubomoa kama zoezi linavyoendelea Dar es Salaam. Hii haileti picha nzuri na inaweza kuleta chuki kati ya Serikali na wananchi. Hivyo, maeneo yalindwe na yasijengwe kabisa.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara hii kwa mambo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu migogoro ya ardhi. Mwaka jana katika hotuba ya bajeti 2011/2012, nilianisha migogoro ya ardhi iliyopo katika Jimbo la Mvomero. Kwa upande mmoja migogoro hii ni matokeo ya wamiliki kutelekeza mashamba kwa muda mrefu bila kuyatumia na wananchi kuyatumia na baadaye wamiliki kuyadai maeneo hayo na migogoro mingine inasababishwa na wamiliki kukosa sifa za kumiliki. Narudia tena kuiomba Wizara itoe kauli, ahadi ya kuyafikia maeneo hayo na kutoa maelekezo ili kuepusha migogoro. Maeneo niliyoomba yatafutiwe ufumbuzi ni:-

(i) Newland (Kata ya Mtibwa), kumbukumbu sahihi za historia zinaonesha eneo hili si sehemu ya Mtibwa *Sugar* mpaka mwaka 1992. Mheshimiwa Ole-Medeye aliahidi kufika eneo hili na ikibidi kumshauri Rais abadilishe na kuwapa wananchi. Naomba kauli ya Serikali.

(ii) Kinyenze (Kata ya Mlali) mgogoro huu ni wa muda mrefu, mwekezaji wa sasa amemega eneo la wananchi, mazao ya wananchi yameharibiwa na amefunga njia. Haya yote ni sehemu ya unyanyasaji. Kwa hali ilivyo ni wakati muafaka kuangalia upya umiliki wa sasa ili tuwatendee haki wananchi wa kitongoji hiki.

(iii) Shamba la *BEE* na Bonde la Mgongola (Kata ya Hembeti) eneo hili linajulikana kama shamba la *Bee,* lina mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na mmiliki wake. Kwa muda mrefu wananchi wamelima na kuwekeza katika eneo hili, lakini cha kushangaza ametokea mmiliki na

kuathiri kilimo kwa wakazi wa eneo hili. Naomba Waziri kufika eneo hili ili ajionee kilio cha wanachi wa Kata ya Hembeti.

Aidha bonde la Mgongola nalo lina mgogoro na lina wakulima toka maeneo mbalimbali, wengine toka miji mingine kuendelea kutumia eneo hili bila ridhaa ya Kijiji cha Kabala. Naomba hili nalo lipatiwe ufumbuzi.

(iv) Njenla (Kijiji cha Mziha, Kata ya Kaga) kumezuka tatizo la wanunuzi wa ardhi kununua maeneo makubwa pasipo wananchi kushirikishwa, *DC* Fatuma Mwasa aliwahi kuingilia suala hili lakini malalamiko bado yapo. Halmashauri ya Mvomero haijaweza kutatua tatizo hili. Naomba Waziri afikie eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu viwanja vilivyopo Makao Makuu ya Wilaya; historia ni kwamba Serikali ilitenga hekta 3,000 kwa ajili ya ujenzi Makao Makuu ya Wilaya na makazi. Halmashauri imevuka mipaka mpaka Kijiji cha Sokoine na kuwaondoa wakazi na kuwapa viwanja watu wengine. Mwaka jana nilichangia, Ofisi ya Waziri Mkuu na ilielekeza wananchi wa Kijiji cha Sokoine na Wami Luhindo wasiondolewe bali wapewe kipaumbele cha kiwanja. Hivi karibuni kumetokea malalamiko tena ya wananchi wa Kitongoji cha Kanisani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atoe agizo la kutowahamisha wananchi wa Sokoine na Wami Lulindo, badala yake wapewe kipaumbele katika kupimiwa viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE: GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuleta kilio cha wananchi wa Wilaya ya Karagwe kwa shabby eneo la Wilaya ya Karagwe limemegwa na mipaka ya Wilaya za Muleba, Bukoba Vijijini, Misenyi na Ngara. Malalamiko haya yanahusu Vijiji vya Rugera, Kata ya Rugera inapakana na Wilaya ya Bukoba Vijijini. Malalamiko mengine yanahusu Vijiji vya Kibogoizi, Rubale, Kata ya Ihembe. Malalamiko mengine yanahusu Kijiji cha Ruhita, Kata ya Rugu inapakana na Wilaya ya Muleba, malalamiko mengine yanahusu Kijiji cha Nyakasimbi, Kata ya Nyakasimbi inayopakana na Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hii ilitokana na wataalam wa Idara ya Ardhi kutoshirikisha viongozi na wazee wa maeneo husika ya mipaka ya awali ikiwa ni pamoja na kubadili ramani ya zamani. Mfano Wilaya ya Ngara mpaka wa zamani ulikuwa Kanyamasongo katika mapori ya akiba ya Kimisi na Burigi mpaka umesogezwa takribani kilomita 30 kuingia ndani ya Wilaya ya Karagwe. Mfano mwingine ni wa Kijiji cha Ruhita, Kata ya Rugu mpaka wa zamani ulikuwa sehemu ijulikanayo kama Nyakato, kwa sasa mipaka mipya imewekwa Katahanamwa takribani kilomita 25 toka mpaka wa zamani kuingia Karagwe, Rwembilizi kilomita15, Nyanetojo kilomita 25, Nyarubungo kilomita 30, Chamengo kilomita mbili (2),

Bunywangiri kilomita 30 na Kigasha mto Mwisa kilomita 35 na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hii inaumiza sana wananchi wa Karagwe, tunaomba itatuliwe haraka kwa kutumia hekima na busara ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mortgage* za *NHC* ni za gharama ya juu riba za kibenki ni kubwa, kwani riba inayotolewa ni ya kibiashara *mortgage finance* duniani kote ina riba ya *single digit almost* 3% yetu ni *above* 18% na zaidi, ni hatari nyumba hazikopesheki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karagwe tunashukuru kupata Baraza la Ardhi la Wilaya. Tunaomba lianze haraka na majengo yajengwe. Wilaya ya Karagwe hasa Kata ya Nyakakika ardhi yetu imevamiwa na wahamiaji toka nchi jirani. Nimeshalisema sana hapa Bungeni, tunaomba Serikali isaidie kuwaondoa na kurudisha ardhi hii kwa Kijiji cha Nyakasimbi, Kata ya Nyakasimbi. Vile vile pori la akiba Kimisi na Burigi Wizara ya Ardhi na Wizara ya Maliasili na Utalii zishirikiane kuhakikisha pori hili linakuwa hifadhi ya wanyamapori kuliko lilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipango miji, idara inayoshughulikia mipango miji imezorota, iboreshwe kwani miji yetu mingi haijengwi kwa kufuata mipango miji iliyowekwa au iliyopangwa hali inayopelekea maeneo mengi kujengwa kiholela. Sasa hivi upo mpango wa Serikali kuweka majina ya mitaa na anwani zake pamoja na namba za nyumba. Je, Serikali

itatekelezaje hili hali ya kuwa miji yetu na vijiji vyetu vingi havikujengwa kwa mpangilio unaofaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hati miliki za ardhi, hati miliki za ardhi upatikanaji wake ni mgumu kwani mwananchi anatumia muda mrefu sana kupata hati yake pale anapoomba. Wizara imeamua kujenga ofisi ya ardhi ya Kanda ya Magharibi itakayohudumia Mkoa wa Tabora, Katavi, Rukwa na Kigoma. Wazo hili halikuzingatia hali halisi ya miundombinu yetu. Kwa kuwa upatikanaji wa hati ni mgumu kwa kutegemea tu ofisi za ardhi zilizopo katika Halmashauri zetu, kuna wakati wananchi mfano wa Kigoma hulazimika kwenda kufuatilia hati miliki katika ofisi ya Kanda, Tabora wananchi walikuwa wanafuata hati zao Mwanza. Naomba Serikali itueleza baada ya wananchi kuomba hati miliki katika ofisi za Idara ya Ardhi katika Halmashauri zetu. Je, Maafisa Ardhi ndio watakaozifuatilia huko ofisi za Kanda au wananchi wenyewe. Kama ni ofisi ndio itakayofuatilia muda wa upatikanaji wa hati hizo utakuwa wa kiasi gani mwezi au miezi mingapi baada ya kuomba?

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji na ugawaji au uuzaji ardhi uende sambamba na uwekaji miundombinu muhimu. Ugawaji viwanja usifanyike mpaka miundombinu ya barabara, maji, umeme, simu maji taka na vyote muhimu viwe vimekamilika ndio watu wauziwe. Tuige mifano ya nchi nyingine ikiwemo Rwanda, hii itasaidia kumpunguzia mwananchi gharama za ziada za kujivutia maji safi na maji taka na umeme. Vile vile viwanja vikiuzwa wakati vina miundombinu iliyopangwa vizuri itapandisha hadhi ya maeneo husika. Naishauri Wizara hii iwasiliane na ishirikiane na Wizara zingine ili kufanikisha hilo. Iwe ni sheria ili viwanja visiuzwe tena bila kuwa na miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vingi vimetokea kutokana na migogoro mingi ya ardhi. Vyombo vya habari leo hii vimeripoti mauaji Mkoani Tabora yaliyotokana na mgogoro wa ardhi, rejea migogoro ya Kilosa na maeneo mengi nchini. Ni vyema Serikali ipange vizuri matumizi ya ardhi ili wafugaji wapewe maeneo yao na wakulima pia wapewe maeneo yao ili migogoro ipungue au iishe kabisa na maeneo ya wafugaji yawekewe miundombinu inayofaa kwa ufugaji. Vile vile Wizara itoe adhabu kali kwa wafanyakazi wa Idara ya Ardhi wanaomilikishwa kiwanja kimoja wa mtu zaidi ya mmoja. Hii pia itapunguza migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linafanya kazi nzuri, lakini tatizo lililopo nyumba zinazojengwa zinauzwa bei ya juu sana. Mfano, katika semina yao kwa Wabunge nyumba ya vyumba viwili wanavijenga kwa milioni 23 wanauza milioni 48 na zaidi ya vyumba vitatu milioni 57, bado ni kiasi kikubwa waangalie jinsi ya kurekebisha hilo ili liwe Shirika kwa ajili ya Watanzania ambao wengi kipato chao ni cha kawaida au wastani na wengine kipato ni kidogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi iondolewe kwenye vifaa vyote vya ujenzi ikiwemo simenti ili wananchi wakae nyumba bora kama Wizara hii inavyoshauri. Ifikie wakati Serikali kupitia Wizara ya Fedha iondoe kodi ya vifaa vya ujenzi na itafute vyanzo vingine ili Wizara hii ipunguze bei ya vifaa vya ujenzi vyote. Tuige mfano wa nchi za wenzetu ikiwemo nchi ya Rwanda, wao wana mkakati wa kuondoa nyumba duni zote na nyumba zote zilizojengwa kwa nyasi.

Mwaka huu wanayo kampeni ya ondoa nyumba duni za nyasi, kwa nini sisi tushindwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanikiwa Wizara itakuwa *reflected* vizuri, maendeleo ya makazi yataonekana. Hivyo jina la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi litaendana na hali halisi ya makazi yatakavyokuwa yakionekana. Sasa hivi jina la Wizara haliendani na hali halisi ilivyo ya makazi ya watu. Suala hili linawezekana kama *political will* ya Serikali itahitaji au itaona umuhimu huo wa kupunguza *bill* ya vifaa vya ujenzi kwani vyanzo vipo vingi tuanze na kupunguza misamaha ya kodi isiyo lazima ili ifidie kodi itakayoondolewa kwenye vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inijibu yote niliyohoji.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya mipango ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 inatekelezeka pamoja na uhaba wa fedha uliopo. Hata hivyo, Wizara yako iendelee kusimamia sheria zilizopo ili miji yetu ivutie na iwe endelevu pamoja na kuondoa kabisa migogoro ya ardhi huko Wilayani. Mheshimiwa Waziri aendelee na juhudi ulizoanza nazo na namwahidi ushirikiano wote atakaouhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi bado ni kitendawili ni *confusion,* tupu juu ya wapi hasa yanawajibika Wizara ya Ardhi, TAMISEMI

au Wizara ya Sheria na Katiba? Aidha, wananchi wanalalamika kuwa kuna rushwa kwenye uendeshaji wa Mabaraza haya. Aidha, hata watu wasiohusika katika maeneo husika (kijiji) ndiyo wamepewa nafasi ya kuongoza Mabaraza hayo kwa kupitia rushwa. Kwamba watu wa maeneo mengine ambao hata hawajakaa muda mrefu wanapata nafasi kwenye Mabaraza haya na hivyo kupata nafasi ya kuwapora wenyeji wa maeneo hayo ardhi yao. Naishauri Wizara hii iyafanyie uchunguzi Mabaraza haya na kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna utata juu ya hati ya kumiliki ardhi kama kweli ni *authentic* kwa maana ya kutumika kukopa kwenye mabenki hapa nchini. Naomba kupewa mfano wa Benki zilizokwisha wakopesha wenye hati hizi. Naona suala hili ni kama la kisiasa zaidi kuliko kibiashara. Aidha, MKURABITA wapewe nafasi ya kujipanua zaidi ili wapime ardhi za wanavijiji kwa kasi zaidi. Rasilimali watu na rasilimali fedha ziongezwe ili wafikie malengo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa jitihada zao. Nia zao ni nzuri ila tatizo la rushwa kwenye sekta hii ni adui yao na yetu. Watendaji wala rushwa kwenye masuala ya ardhi watoswe haraka ili kusafisha jina la Wizara na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iharakishe upimaji wa viwanja katika Mji Mdogo wa Itigi na *Land Rent and Recurrent Expenditure fee* ya shilingi 200,000/= iwe *reviewed* na kupunguzwa kwa sababu ni kubwa sana kwa mwananchi wa kawaida na ni chanzo pia cha kuchelewesha upimaji wa viwanja. Namwomba Mheshimiwa Waziri mwenyewe au Naibu wake wafanye

ziara Manyoni na Itigi kuhamasisha shughuli za Wizara hii na sekta nzima ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawatakia heri na naomba majibu juu ya maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja ila naomba ufafanuzi.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ina umuhimu mkubwa sana na kama ardhi haikupangwa vizuri basi mifarakano, magomvi katika jamii hutokea. Ugomvi na mapigano kati ya wakulima na wafugaji kati ya wakulima na wafugaji, kati ya wananchi na wawekezaji, wananchi na Hifadhi za Taifa na kadhalika. Kwa maana hiyo upimaji wa ardhi wa mipango ya matumizi ya ardhi lazima utiliwe mkazo. Hata hivyo, inasikitisha kuwa bajeti ambayo Wizara ya Ardhi inapata ni ndogo sana na hata haitajwi katika yale maeneo ya kipaumbele. Ni muhimu sasa Serikali ikatambua hivyo na kufanya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna utaratibu wa kubakisha fedha zilizokusanywa na Wizara *(retention),* utaratibu huu unataka baada ya fedha kukusanywa na Wizara zirudi kwanza hazina na ndipo asilimia ya Wizara irudishwe, utaratibu huu umeleta usumbufu mkubwa na hii ndiyo iliyofanya mradi kadhaa kutotekelezwa, kwa kuwa pamoja na Wizara kukusanya fedha ilikuwa vigumu kwa Hazina kuwarudishia fedha hizo. Inafaa suala hili liangaliwe

upya na kuwa na uwezekano wa kubakisha fedha pale pale na kupeleka Hazina kiasi kinachotakiwa kupelekwa yaani *retention at source*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ugawaji viwanja bila ya kuweka miundombinu si mzuri viwanja vingi vilivyogawiwa kwa utaratibu huu bado kuendelezwa na hata ile sheria ya mtu kuendeleza kiwanja kwa muda uliowekwa haiwezekani na kama Wizara ya Ardhi ingefuata hili basi wengi wangenyang'anywa viwanja. Ni muhimu kuwa na ushirikiano na Wizara zingine na Wizara hizo zione ni jukumu lao kufanya hivyo, mfano, Wizara ya Maji Nishati, Ujenzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lilianzishwa ili kuwapatia nyumba wananchi wa kipato cha chini. Shirika limepanuka na hivi sasa linajenga nyumba nyingi mwanzo kwa ubia na baadaye wenyewe, pia kwa wananchi wa kipato cha kati na cha juu. Ni muhimu wakati hili linafanyika *National Housing* isipoteze lile lengo la awali. Ni muhimu kuweka *balance* nzuri katika ujenzi ili nyumba za bei nafuu ziweze pia kujengwa. Hivi sasa inaonekana nyumba za aina hii ni chache ukifananisha na zile za wenye vipato vya kati na juu. Isije ikajikuta inajenga nyumba nyingi kwa wananchi wa kipato cha juu na baadaye kukosa soko kwani wawekezaji binafsi nao wanafanya hivyo hivyo na wanunuzi ndio hao hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mikopo ya nyumba ndio utakuwa ukombozi wa Watanzania kuweza kujenga nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu huo, tatizo kubwa ambalo itabidi Serikali kufuatilia sasa ni riba kubwa zinazotozwa mikopo huu ni wa miaka zaidi ya kumi, lakini kama riba itakuwa ya tarakimu mbili itakuwa vigumu kuweza kulipia. Serikali lazima ikae na mabenki kama inavyofanywa katika nchi nyingine ulimwenguni ili riba iwe chini na ya tarakimu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, natamka tena kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii ya Waziri. Najua kazi ya upimaji ardhi ni juhudi za Wizara hii, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupima eneo tunataka kujenga Makao Makuu ya Wilaya ya Wagingambe pale Igwachanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Njombe mjini kuna shamba kubwa sana la Tawwat, eneo hili lina milki ya miaka 99. Hoja yangu kubwa, baada ya Njombe kuwa Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Njombe, naomba eneo hili lipunguzwe ili wananchi wapate maeneo ya kujenga, naomba Mheshimiwa Waziri atupe utaratibu ambao tunahitajika kufuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Serikali inapaswa kulifanyia marekebisho ni kodi ya ardhi. Mpaka sasa hivi wanalipa shilingi 200 kwa eka wakati mwananchi akihodhi ardhi kwao wanalipia si chini ya 25,000/= kwa eka. Wawekezaji wengi kama wa Kapunga, Mbalali na

penginepo hununua mashamba kwa bei ndogo na wao kufanya biashara ya kukodisha kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mwananchi akishapimiwa ardhi na kupata hati ya kimila. Je, Serikali ya kijiji ina mamlaka yapi ya kubadilisha matumizi ya eneo hilo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kuhusiana na ardhi na nyumba. Kabla ya kuanza napata faraja kuona mipango mizuri sana kwa maendeleo ya nchi yetu kama ilivyoanishwa kwenye kitabu cha bajeti pamoja na kusomwa kwa ufafanuzi na Waziri Mheshimiwa Anna Tibaijuka. Hivi kama kweli hii mipango itatekelezwa natoa pongezi kwa Mawaziri pamoja na watendaji wote chini ya Wizara waliofikiri na ku-*suggest* mambo haya mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuongelea migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikidumu katika Wilaya ya Tarime na Tanzania kwa ujumla. Mwaka jana niliuliza swali la msingi kuhusiana na raia wa Kenya kumiliki ardhi kinyume na Sheria ya Ardhi na kwa mujibu wa Kanuni ya 76 ya Sheria za Ardhi za Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliainisha kuwa kuna Wakenya wanamiliki ardhi kwenye eneo la Matongo ambalo linapakana na Kijiji cha Ikoma na eneo hili la Matongo lipo katika Vijiji vya Nyabirongo na Kiongera kwenye Kata ya Susuni ambapo kuna majibu ya Naibu Waziri aliahidi kufuatilia suala hili kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani (Uhamiaji).

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha Waziri hakufanya hivi na hivi karibuni kwenye Bunge hili la Bajeti, Mheshimiwa Mbunge wa Rorya aliuliza juu ya Wakenya hawa ambao wanapelekea vita za koo na alitaja Vijiji vya Ikoma, Nyamhonda na Nyabirongo lakini hatua hazijachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kauli ya Serikali juu ya hili, kwa nini kuna Watanzania wamenyang'anywa ardhi yao ambapo waliwazika baba, mama na ndugu zao na ndio walikuwa wakitumia kama mashamba yao kuweza kupata kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kujua ni lini sasa wananchi wa maeneo ya Ronsolti watalipwa fidia zao ambazo ni stahiki ili waweze kwenda maeneo mengine na kuendelea na shughuli za maendeleo. Kwa sababu mwaka jana akijibu swali langu Mheshimiwa Tibaijuka, Waziri wa Ardhi alisema wameshatenga fedha kwenye bajeti ya 2011/2012 na kwamba sasa wananchi hawa watalipwa ili kupisha JWT kuendelea na shughuli zao. Pia kutoa fursa kwa wananchi hawa kutafuta maeneo mengine ili waweze kujiendeleza kiuchumi kwani ni takribani miaka zaidi ya tisa hawa wananchi wapo tu, hawaruhusiwi kujenga au kufanya shughuli zozote zile hata za kilimo cha msimu. Hii si haki, hivyo ningependa kupata majibu ni kwa nini Serikali haijalipa watu hawa kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kujua au kupata majibu ni juu ya mgogoro wa ardhi uliopo kati ya wananchi wa Buhemba shuleni *(FDC)* ambapo Wizara wana taarifa juu ya mgogoro huu. Je, ni hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kuzungumzia kwa masikitiko makubwa kabisa juu ya fidia wanazopewa wananchi wetu ili kupisha matumizi mengine ya ardhi, inasikitisha kuona mwananchi analipwa shilingi 200,000/= au 300,000/=. Sasa najiuliza kiukweli kabisa huyu mwanachi akiji-*reallocate* ataweza vipi kuji-*establish*? Hii imekuwa ni kero kubwa na kuwakatisha tamaa kabisa wananchi wanaotakiwa kuhama. Hivi ni viwango ambavyo wamekuwa wakilipwa baadhi ya wananchi Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kiwango kipi huchambuliwa kulipa fidia kwa wananchi na hapa wanamaanisha malipo yanayofanywa kwenye mgodi wa *North* Mara ambapo kwenye kitabu cha bajeti 2012/2013, Waziri ametaja Nyamongo na Nyakunguru kama maeneo ambayo watalaam wake wamefanya tathimini. Hivyo basi, nataka kujua ni viwango vipi vinatumika kuwaondoa wananchi kwenye maeneo yao hasa yale ya Nyamongo ambayo yamejaa dhahabu.

Leo hii unamlipa shilingi 4,000,000/= milioni nne, saba au kumi. Hivi kiuhalisia kwa maisha ya sasa huyu mwananchi unayemhamisha atapata wapi ardhi aamue ajenge na ku-*establish* maisha yake. Huu ni unyanyasaji kabisa kwa hawa wananchi. Hivyo, naomba nipatiwe majibu ni viwango vipi vimewekwa kama malipo ya chini kabisa kwa wananchi, wenye eneo lisiloendelezwa na yule aliyejenga na kuwa na mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate majibu ya haya yote.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kusema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miji yote mikubwa hapa nchini kama vile Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na kadhalika, ina maghorofa mengine marefu hata kufikia ghorofa 50; na kwa kuwa wanaomiliki majengo hayo huwa ni watu binafsi au makampuni au mashirika ya umma au binafsi; na kwa kuwa umilikaji wa majengo hayo huwa unatokana na kuwa na hati miliki ya ardhi kama vile *right of occupancy* na kadhalika. Je, Serikali haioni umefika wakati mwafaka kuleta Bungeni Muswada maalum ili kutunga Sheria mpya ya Ardhi ya aina ya *Commonhold* ili iweze kukidhi mahitaji ya watu wanaomiliki ghorofa moja au mbili na zaidi katika maghorofa hayo? Nchi nyingi duniani wana *system* ya *Commonhold* ambayo hutumika kwenye umilikaji wa majengo marefu mijini. Naishauri Serikali ilete Bungeni Sheria ya *Commonhold* ili irekebishe hali halisi ya umilikaji wa majengo mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kwa kazi nzuri anayoifanya hasa kwa kujiamini na kuwa mkweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kuhusu Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye mauzo ya nyumba zinazojengwa na *NHC*. Pamoja na nia nzuri ya kuwapatia Watanzania fursa ya kununua nyumba kwa bei nafuu lakini kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*

kunaleta bei ya nyumba inapouzwa na Shirika kuwa kubwa hivyo kusababisha unafuu kutoweka. Hali hii haimsaidii Mtanzania kununua nyumba kwa bei nafuu na kuishi kwenye nyumba nzuri. Napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara hii pamoja na Wizara ya Fedha wakati wa kufanya marekebisho ya Sheria ya *Finance Bill* itakayoletwa Bungeni siku za mbeleni na Sheria hii irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda Wizara ya Ardhi yenye dhamana ya Shirika la Nyumba *(NHC)* ifahamu kwamba, ule mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi katika eneo la Medeli Mkoani Dodoma ambazo wakati wa uzinduzi wa mradi huu na Mheshimiwa Waziri Mkuu tuliahidiwa kwamba kwa wale wanunuzi wa nyumba hizo watakaolipia gharama ndani ya miezi mitatu ya mwanzo watakabidhiwa nyumba zao ifikapo mwezi Marchi 2012. Cha kusikitisha hadi leo Julai, 2012 nyumba hazijakamilika kujengwa na haijulikani nyumba hizo zitakamilika lini. Hakuna mawasiliano yoyote baina ya mnunuzi na Shirika kueleza maendeleo ya ujenzi wa nyumba, mbaya zaidi kwa wale tuliomaliza kulipia malipo ya nyumba ndani ya miezi mitatu, muda uliopangwa hakuna mkataba wowote uliokwishasainiwa na pande zote mbili. Matarajio ya kuwa na makazi hapa Dodoma ilipofika March 2012 hayapo tena, Shirika *(NHC)* linasemaje kufidia hasara hii tangu mwezi wa ahadi March 2012 na kuendelea?

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka huu Serikali iliahidi hapa Bungeni kuleta Sheria ya Kudhibiti Shughuli za Upangishaji Nyumba mara baada ya kumaliza Sera ya Nyumba. Ahadi hii ilitokana na Hoja Binafsi niliyoleta Bungeni nikitaka Serikali ilete Sheria hii ili kuondoa manyanyaso dhidi ya wapangaji na kuleta

nidhamu katika shughuli nzima ya upangaji. Kwa kuwa Sera ya Nyumba imekuwa kwenye matayarisho tangu mwaka 2007, Sera hiyo ikamilishwe mapema ili Sheria iletwe Bungeni kama ilivyoahidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikal ianzishe Mamlaka ya Udhibiti wa Biashara na Nyumba *(Real Estate Regulatory Authority - RERA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali idhibiti uongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ambalo viongozi wake wamejielekeza kwenye *PR* zaidi kuliko ubinadamu na ufanisi wa shughuli za Shirika na bado kuna rushwa na upendeleo mkubwa katika kugawa nyumba.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilieleza katika mchango wangu wa mwaka 2011 wakati wa kujadili makadirio ya mwaka 2011/2012, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni sekta muhimu kwa uchumi wananchi na maisha ya wananchi. Hata hivyo, mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yanaonyesha kuna tofauti na ahadi ya Waziri Mkuu ya kuhakikisha Wizara inaongezewa fedha mpaka Juni 2012 hata fedha kidogo zilizotengwa zilikuwa zinapatikana kwa asilimia 68.1 tu yaani shilingi bilioni 34.65 huku fedha za maendeleo zilizotumika zilikuwa shilingi bilioni sita (6) tu sawa na asilimia 28 tu ya bajeti ya maendeleo. Serikali inapaswa kutoa maelezo kuhusu hali hii pamoja na kuongeza fedha kwa mwaka 2012/2013 za miradi ya maendeleo ya shilingi bilioni 71 tu, ni kidogo kulinganisha na unyeti wa sekta ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nyingi zinazofanywa na Wizara, nieleze masikitiko yangu ya Waziri wa Ardhi kutokutekeleza ahadi ya kutembelea Kata za Kwembe na Kibamba kwa ajili ya mgogoro wa fidia ya ardhi na mipaka Kwembe, Kisopwa na Mloganzila pamoja na uendelezaji wa mji wa Lungumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nieleze masikitiko yangu zaidi kwa kutokujibiwa kwa barua zangu ambazo niliandika kwa Wizara kuhusu masuala husika. Hivyo naungana na maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kutaka majibu ya Serikali kuhusu uvamizi wa maeneo ya umma Dar es Salaam. Pamoja na kushukuru Wizara na Waziri kwa kuweka mabango Kata ya Sinza na kwa kuwa muda wa notisi umepita, Serikali ichukue hatua ya kurejesha viwanja husika na kutekeleza mapendekezo ya ripoti ya mwaka 2010 ambayo iliainisha maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamoja na majibu ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, tarehe 29 Juni 2012; Wizara ieleze ni kwa nini wananchi wa Mloganzila, Kisopwa na Kwembe 1919 wanaopaswa kuhama kupisha ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya (*MUHAS*)wameelezwa kuwa hawatalipwa fidia ya ardhi wakati ambapo Serikali iliahidi katika mikutano na wananchi wa eneo husika mwaka 2010 kuwa watalipwa fidia ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuhusu Mji wa Luguruni, pamoja na kauli ya Serikali kuwa mwendelezaji mweza (*co-master developer*) ameshapatikana, ni muhimu Serikali ieleze kampuni hiyo binafsi ni ipi imeingia

makubaliano kwa masharti yapi na uendelezaji unaanza lini? Serikali ieleze pia ni lini mgogoro wa mipaka kati ya Manispaa ya Kinondoni na Halmashauri ya Kisarawe katika maeneo ya Kisopwa na Mloganzila utapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Wizara imeeleza kuwa katika mwaka 2011/2012 imeshirikiana na Manispaa ya Kinondoni kuandaa mpango wa uendelezaji upya eneo la Manzese. Naomba kupatiwa nakala ya mpango husika na maelezo kwa kuwa eneo hilohilo kulitekelezwa mipango mingine kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kupatiwa taarifa ya uhakiki wa urasimishaji Mbezi Makabe, Mshikamano, Malamba Mawili na Msigani.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana Waziri Tibaijuka na timu yako yote pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kwa ubunifu aliokuja nao wa kuwapatia Watanzania nyumba bora za kuishi kwa kununua, kupangisha au hata kwa kukodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kero zifuatazo za ardhi katika Wilaya ya Ngorongoro zitafutiwe ufumbuzi. Mipaka ya ardhi ya vijiji ipimwe na kupewa hatimiliki. Vijiji pekee vilivyopimwa na kupewa hatimiliki ni Ololosokwan na Engaresero.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga matumizi bora ya ardhi itaondoa migogoro na mapigano (kuuwawa) kati ya Wamasai (wafugaji) na Wabatemi au Wasonjo (wakulima). Mgogoro huu ni mkubwa na hatua iliyofikia inahitaji

‘*intervention’* ya Serikali Kuu. Uongozi wa Wilaya na Mkoa walijaribu mara kadha kutatua tatizo hili lakini mafanikio ni kidogo na ya muda mfupi. Naomba *intervention* ifanyike kabla mapigano na mauaji hayajaibuka tena. Naomba fedha ya kupima mipaka ya vijiji na mashamba ili kuondoa tatizo hili na kusimamia sheria na utaratibu uliowekwa. Aidha, maeneo ya malisho ya mifugo na kilimo yabainishwe na kusimamiwa na uongozi wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la wawekezaji nalo litambuliwe na kubainishwa. Maeneo ya wanyamapori halikadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ipitiwe upya ili sheria hiyo iweke na itamke bayana kuwa wananchi waishio katika Tarafa ya Ngorongoro ambayo pia ni hifadhi mseto (*multiple land use*), wana haki juu ya ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Chiligati alipokuwa Waziri wa Ardhi aliahidi kutupa fedha ya kupima vijiji na matumzi bora ya ardhi. Mheshimiwa Profesa na ndugu yangu Ole-Medeye, nisaidieni katika hili na nilikwishawaalika Ngorongoro ili kujionea wenyewe maana kuona ni kusadiki.

**MHE. NEEMA M HAMID:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie maeneo manne katika hotuba hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuzungumzia suala la ucheleweshwaji wa kupimwa viwanja maeneo mengi nchini hususani Jiji la Dar es Salaam. Serikali inachelewa

kupima viwanja wakati mahitaji ya watu ni makubwa hivyo kupelekea watu kuvamia maeneo na kuanzisha makazi ambayo baadaye Serikali inakuja kuwahamisha na kuwavunjia. Ombi langu kwa Serikali, wadhibiti ucheleweshwaji wa upimaji wa viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujengaji wa nyumba na kuuza ni wazo zuri na ni mpango mzuri lakini nyumba nyingi zinauzwa kwa bei ya juu sana wakati mpango huu unalenga kusaidia watu wa hali ya nchini. Hivyo, naiomba Serikali iangalie kwa ukaribu zaidi mpango huu na kuhakikisha kuwa na watu wa hali ya chini wanafaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la Mji Mpya wa Kigamboni. Serikali imechukua muda mrefu sana kujenga Mji Mpya wa Kigamboni. Mji Mpya wa Kigamboni umechukua muda mrefu sana kiasi ambacho wananchi hawaelewi cha kufanya na wanashindwa kuendeleza maeneo yao. Hoja yangu ni kwamba kama mpango upo basi uendelezwe na wananchi wawe wanapewa *feedback* kuhusu mradi unavyoendelea hatua kwa hatua. Hii ndio itatatua matatizo baina ya Serikali na wananchi. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho anieleze mradi huu utaaanza lini rasmi na utachukua muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutaka kuchukua Madiwani wa Kigamboni kuwapeleka nchi za nje ili kupata fursa ya kuona Majiji ya wenzetu lakini namkumbusha Mheshimiwa Waziri usisahau kuwa Wabunge pia washirikishwe sababu Wabunge nao ni sehemu ya Madiwani.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kodi zinazotozwa nyumba zilizojengwa mjini, ukibahatika kupata kiwanja mjini, ukajenga nyumba, utapambana na kodi zifuatazo, *land rent* na *property tax* na endapo utaipangisha itabidi ugawane pesa hizo na Serikali. Natambua kwamba kodi ni lazima zitozwe ili zimuendeleze mwananchi lakini kama kodi zenyewe zinakuwa kero kwa mwananchi huyohuyo, ni muhimu Serikali ikaliangalia upya suala hili. *Land rent* na *property tax* unalipwa na kila mtu aliye na nyumba haijalishi hana ajira, ni mstaafu au haipangishi, kosa lake ni kwamba amejenga nyumba mjini. Kodi hizi zinalipwa ofisi tofauti, hii inaleta usumbufu mkubwa kuzisaka ofisi hizi sehemu mbalimbali mjini. Ukadiriaji wa *property tax* ni *arbitrary,* nyumba zinazofanana na ziko eneo moja kodi zao zinatofautiana. Sijui uzoefu wa Wizara unasemaje kuhusu '*compliance'* katika ulipaji wa kodi hizi? Nina imani matatizo madogo madogo yakirekebishwa watu wengi watalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na naunga hoja mkono.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu na Watumishi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wafahamu kuwa ardhi ni rasilimali na haki ya msingi ya mwananchi ambaye yupo mjini na wengi wapo vijijini. Sehemu kubwa ya ardhi ipo mikononi mwa Serikali za Mitaa na Vijiji. Hata hivyo, viongozi wa vijiji na mitaa hawana uwezo wa ku-*manage*

hali ilivyo hivi wameanza kuchukua hatua za kuuza ardhi na Wizara inabariki wakati mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua, je, Sheria Na. 2 ya 1999 ya Ardhi Vijijini kama imetungiwa kanuni, kama kanuni hazijatungwa, sheria inatekelezwa vipi? Naomba nifahamishwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kupongeza Wizara kwa kazi nzuri. Mapema mwaka 2011 nilimwita Mkurugenzi wa *NHC* ili katika kuwawezesha wananchi wa kawaida, aone namna atakavyoweza kuongea na wakazi wa Manzese, Buguruni, Keko na pote penye nyumba ambazo zimejengwa holela waweze kuachia maeneo hayo ambayo yako kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za *NHC* kwa baadaye wao kuachiwa nyumba za kuishi na moja ya *income generation* bure. Katika kufanya hivyo *NHC* itakuwa imeshiriki ipasavyo kuwaondolea wanyonge umaskini wa makazi, pato na kwa ujumla na wakati huo kujenga nyumba kwa ajili ya ama kuuza ama kupangisha kwa Watanzania wengine, naomba Waziri anipe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Babati ni Mji Mkuu wa Mkoa mpya wa Manyara, hivyo kutakuwa na nyumba chache hasa kwa wafanyakazi, naomba *NHC* itoe kipaumbele kwa Mji kama Babati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umeme wa msongo wa kutoka Mtera kwenda Shinyanga umepitia katika ardhi za wananchi wa vijiji vya

Mkiwa, Issuna A na B, Nkuli, Ulyampiti, Muungano, Ikungi, Ighuka na Kipumbuiko katika Jimbo la Singida Mashariki. Wilaya mpya ya Ikungi, njia ambayo umeme huu umepitia ni sehemu ya ardhi za wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi za Vijiji 1999.

Kwa mujibu wa sheria ya Ardhi za Vijiji na Kanuni za Ardhi za Vijiji 2011, ardhi za wananchi zilitakiwa kutwaliwa na Rais kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na kufanyiwa tathmini ya ardhi husika kwa lengo la malipo ya fidia. Hata hivyo, hadi sasa wananchi wote ambao mashamba na mifugo yao yamepitiwa na njia ya umeme hawajatathiminiwa ardhi zao kwa mujibu wa Kanuni za Ardhi za Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fidia ya haki timilifu na ya wakati muafaka haijalipwa kwa wenye ardhi husika. Fidia inayozungumziwa hapa sio fidia ya maendeleo ya kudumu tu bali pia ni fidia ya ardhi yenyewe na maendeleo yaliyofanyika kwenye ardhi yenyewe, fidia ya upotevu wa faida, usumbufu na usafiri ambazo zote zimeelekezwa kwenye Kanuni za Ardhi za Vijiji. Naomba nipatiwe maelezo juu ya mpango wa Serikali kama upo wa kuwalipa wananchi fidia kama iliyoelezwa na ni lini fidia hiyo italipwa?

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze kasi au ianzishe sasa upimaji wa miliki za mashamba Shinyanga na Simiyu. Hotuba ya Waziri imeonyesha upimaji wa miliki za mashamba ni zero katika Mikoa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Meatu ina vijiji takribani 200 lakini ni vijiji 45 tu vilivyopata vyeti vya vijiji mbaya zaidi hakuna hata hati za kimila ambazo zimetolewa. Serikali iliangalie hili ili wananchi wa Meatu wapate haki yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa ardhi katika nchi yetu na kutokana na kuwa ardhi ni mali, kilichojitokeza ambacho watu wanashangaa sana na kuwafanya waichukie Serikali yao ni kwamba:-

(a) Serikali kupitia Wizara na taasisi husika haifanyi wajibu wao katika kusimamia ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi iliyopo.

(b) Watendaji katika maeneo yote kuanzia Serikali Kuu mpaka Serikali za Mitaa wamekuwa madalali wa ardhi wanaozingatia maslahi yao bila kujali matokeo ya baadaye.

(c) Wananchi wanapewa ardhi na viongozi wanaohusika, wanaanzisha ujenzi mpaka wanahamia na familia zao, ndipo Serikali Kuu inawavunjia wananchi, huu ni udhalilishaji.

(d) Hata kwa wale ambao Serikali imewamilikisha ardhi bado kunakuwepo na usumbufu mkubwa wa kupata hatimiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matokeo yote hayo ambayo yanawasababishia shida kubwa Watanzania

lakini haionekani kwamba Serikali inachukua hatua kwa wanaoisababishia nchi hii kuingia katika mizozo isiyokwisha kati ya Serikali na wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba, matarajio ya walio wengi hapa nchini ni kuona kwamba Shirika hili lisaidie pia sio tu kusimamia ujenzi wa nyumba na ukarabati wa nyumba za Serikali ambazo pia wafanyakazi wanapangishwa, lakini jambo lingine ni kujenga na kuwapatia wananchi nyumba zenye gharama nafuu lakini ni kinyume kabisa na matarajio hayo. Wizara hii kupitia Shirika la Nyumba nimechangia sana kuhusu kuwa la kibiashara zaidi kuliko kusaidia wananchi, nyumba sio nafuu ila ni balaa na mzigo mzito kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua ardhi ya wananchi katika eneo la Mabwepande na wakawaweka watu waliopatwa na janga la mafuriko Dar es Salaam. Si vibaya lakini Serikali walikuwa wana jukumu la kuwalipa wananchi hawa fidia ya ardhi yao. Naomba wananchi hawa walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imekuwa ya ajabu sana, inaonekana kwamba wote katika Serikali hii wana ndevu (kambare) baba ndevu, mama ndevu, kaka ndevu, dada ndevu, sasa haieleweki ni nani mkubwa anayestahiki kusikilizwa kauli yake. Kuna mashamba kadhaa ambayo yalikuwa yamekabidhiwa wawekezaji lakini kwa kuwa mashamba hayo baada ya kutelekezwa na wawekezaji hao, wananchi walikuja juu na kiongozi mkuu wa nchi hii (Rais) alitoa agizo kwamba mashamba hayo yarejeshwe kwa wananchi na hadi leo bado wananchi wangali wanasumbuliwa na agizo la Rais pia halikuheshimiwa. Sasa

mimi nauliza ni nani ambaye katika nchi hii anastahili kuheshimiwa kama Rais amedharauliwa kwa kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu wa kupeana nafasi kisiasa, kushindwa kuwajibishana na kuridhishana kisiasa, nchi hii kupiga hatua za kimaendeleo ni ndoto na hatutafika kwa mtindo huu wa kila anayepata nafasi kuchukua chake mapema bila kujali wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole-Medeye, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Wizara hii sasa ianze kupunguza migogoro na malalamiko kutoka kwa wananchi hasa kutokana na baadhi ya watendaji wa Wizara kushirikiana na madalali wa viwanja. Haya malalamiko ni makubwa sana. Baadhi ya watendaji hutafuta maeneo ambayo wananchi wana *offer* za viwanja na kuyauza mara mbili au tatu na kusababisha wananchi wenye haki kupoteza haki zao. Huu ni uonevu wa hali ya juu, naiomba Serikali ijaribu kubuni njia ya kurudisha imani kwa wananchi waliopoteza imani na utendaji mbovu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo ni sugu katika Wizara hii, ni tathimini na malipo ya fidia. Inasikitisha kuona mwananchi ananyanyasika kutokana na ardhi

aliyoimiliki kwa miaka mingi anadhulumiwa haki yake kwa kufanyiwa tathimini ya malipo ya fidia kienyeji wakati tunao wataalam wanaozijua sheria na ukiukaji wa taratibu kwa makusudi na kufanya zoezi hili kienyeji kwa ajili ya kutaka kujinufaisha wenyewe. Hili jambo, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia wakati wa kuuza viwanja wale wamiliki wa eneo wangefikiriwa kwanza na pia hakuna utaratibu mzuri wa ugawaji viwanja, pia gharama ni kubwa sana za ukadiriaji wa viwanja hivyo. Matokeo yake viwanja hivyo kumilikiwa na watu wenye pesa. Naomba Mheshimiwa Waziri na watendaji wasome kwa makini jambo hili na tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki wa kiwanja *block 8 Saruji Corporation.* Michoro ya mipango miji katika Jiji la Dar es Salaam, je, inatambua uwepo wa *block 8* chini ya umiliki wa kampuni ya Saruji ambayo kwa hivi sasa haipo? Je, eneo katika *block* hiyo ambalo liliachwa kwa ajili ya huduma za jamii kama vile Kanisa, Misikiti makaburi, benki ya posta, maji na kadhalika, mmiliki halali wa nyumba zilizo katika *block* hiyo ni nani na ziko katika hatua gani ikizingatiwa kuwa kuna ujenzi wa Kanisa mahali hapo?

Baada ya sehemu ya upande wa magharibi kumegwa na kupewa *Dawasco* na hivi sasa tayari tanki la maji limejengwa, je, kibali cha ujenzi wa tanki hilo *Dawasa* walipata wapi? Kwa kuwa Kanisa Katoliki wameshindwa kuendeleza eneo hilo walilopewa na kiwanda kutokana na hati ya umiliki wa eneo hilo kuwa chini ya kiwanda au kampuni ambayo kwa hivi sasa haipo, je, Wizara inaweza kufuta umiliki huo ili upimaji ufanyike upya na Kanisa

waweza pia kuomba *Dawasa* kwa ajili ya matumizi tengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, majengo ya iliyokuwa *Saruji Corporation,* kiwanda cha Twiga, Shirika la Reli yaliyopo eneo la Wazo, yanamilikiwa na nani? Kwa kuwa sasa kuna wapangaji ambao hata hawajui kodi alipwe nani kwa kuwa majengo haya yalichukuliwa na *PSRC* na wajanja wachache walichukua fedha na kuweka mifukoni. Pia kwa hivi sasa inasemekana majengo hayo yapo chini ya *TBA*, je, ni kweli na kama ni kweli, je, ni kwa nini watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa hata wa Kiwanda cha Saruji kukosa sehemu za kupanga wakati nyumba zipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mzungu amekodisha karakana iliyokuwa *Saruji Training Instute*, je, naye kodi analipa wapi? Pia ameyageuza kuwa gereji, kwa nini zile maabara zisitumike kwa ajili ya shule ya sekondari ya Twiga ambayo iko jirani kwa kuwa tunao uhaba wa maabara katika shule zetu? Je, Serikali inafahamu hilo? Kama inafahamu, je, ni kwa nini hatua zisichukuliwe mapema ili kunusuru nyumba hizo ambazo Serikali ya kwanza ilijenga kwa nia njema? Naomba Mheshimiwa Waziri ayatolee majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utaratibu gani unaotumika kupima maeneo ambayo tayari yana majengo kwa kuwa katika Halmashauri ya Iringa kuna maeneo ya Kata ya Mkwawa, *Don Bosco* na Itamba bado mpaka sasa hivi hayajapimwa. Ni vizuri Wizara ikawa na mkakati kuhakikisha yanapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba pia hizi hati za leseni za makazi ziongezwe muda wa umiliki kuliko ilivyo hivi sasa. Kwa kuwa kuna baadhi ya Benki sasa hivi zimekubaliwa kuwa rehani kwa ajili ya kuchukulia mikopo na ndio nia ya Serikali kwamba wananchi wanufaike kwa leseni hizo. Pia Serikali itoe tamko ili Benki zinazokataa leseni hizi sasa zihalalishwe.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2004 mpaka 2009 mradi wa barabara ya Nangurukuru – Lindi – Mingoyo ulipita Mjini Lindi na kubomoa maeneo kadhaa ya mji huo ambapo malipo ya fidia kwa wananchi hao hayakukidhi kanuni, sheria na taratibu za ulipaji fidia. Malalamiko ni mengi kwa wananchi hao na wameshindwa kupata makazi mapya baada ya kubomoa nyumba zao kwani malipo hayastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ujenzi ndiyo iliyohusika na bomoabomoa hiyo na kuweka "X" katika maeneo hayo lakini Wizara ya Ardhi ndiyo iliyotoa hatimiliki kupitia Halmashauri ya mji wa Lindi. Wizara ya Ardhi imenyamaza kimya wakati wananchi waliopatiwa hatimiliki wakivunjiwa makazi yao kwa mujibu wa sheria hiyo. Hatimiliki zilizotolewa na Wizara ya Ardhi hazina thamani tena. Inaonyesha Wizara ya Ujenzi inaweza kufanya maamuzi katika ardhi ambayo haina mamlaka nayo kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba yaliyotelekezwa, kuna mashamba ya mkonge 12 katika Manispaa ya Lindi, ambayo hati zao zina utata, ni za muda mrefu na wenyewe hawajulikani waliko. Tunahitaji Wizara iangalie upya

hatimiliki za mashamba haya na wananchi wapewe maeneo ya kilimo.

**MHE. YUSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima. Nakushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uongozi wako uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imegusa sehemu nyingi muhimu lakini pia na uwasilishi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi ni muhimu kwa Taifa lolote duniani, kwa maendeleo ya nchi na watu na Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimebarikiwa kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba kwa maslahi ya Taifa, inapaswa itunzwe kwa juhudi kubwa sana. Kumekuwa na uharibifu wa ardhi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu ambapo unasababishwa na watu katika shughuli zao za kutafuta maisha. Mfano uchimbaji wa mchanga wa kujengea, ukataji wa miti ovyo, ufugaji wa makundi makubwa ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zifuatazo zichukuliwe kwa ushauri wangu, kutolewa elimu ya utunzaji ardhi, itolewe elimu ya umuhimu wa ardhi, wananchi wenye tabia ya kukata miti kwa ajili ya kuni ama mkaa wawezeshwe ili kumudu shughuli mbadala za kutafuta maisha. Lakini pia Serikali ni lazima ibuni njia mbadala ili tuondokane na matumizi ya kuni na mkaa kwa matumizi ya kila siku kwa kupika chakula. Tukiweza kufanya hivi, tutapunguza mmomonyoko wa ardhi (*erosion*) na ardhi yetu itadumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumzia migogoro, nchi nyingi duniani zenye utajiri wa mafuta, gesi, madini na mali mbalimbali, huingia katika migogoro mikubwa ya ardhi mpaka kupelekea vita, mara nyingi husababisha wanyonge walio wengi kunyimwa na kukosa haki ya kumiliki ardhi au masharti magumu ya umiliki yaliyowekwa na Serikali. Mali zinazovunwa kutoka ardhi yao wao hawafaidiki. Wanaishi katika maisha duni, wanakosa maji, barabara, *dispensary*, yote haya huchangia migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni baya zaidi, Serikali kukumbatia makampuni makubwa na matajiri, hivi wananchi hujihisi serikali yao imewatelekeza, hivyo migogoro ya ardhi huendelea na kujenga chuki na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa ardhi katika maeneo ya wazi au ardhi za Serikali. Maeneo haya yamekuwa yakivamiwa sana katika sehemu mbalimbali nchini. Tatizo hili ni kubwa na linahitaji ufumbuzi wa mapema sana. Mamlaka zinazohusika zichukuwe hatua mapema sana kabla wavamizi hawajajiimarisha. Si vizuri mtu anavamia katika ardhi ya Serikali, anapima, anachimba msingi, anajenga nyumba yote tayari anaishi na familia ndio Serikali inashtuka na kubomoa nyumba zenye thamani kubwa. Hili si jambo zuri na linajenga chuki baina ya raia na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, maeneo yote yasiyoruhusiwa kujengwa basi Serikali iweke ulinzi madhubuti. Lakini pia wako watendaji wengine si waaminifu na ndio wao wanaotoa vibali vya ujenzi katika sehemu za

wazi, vyanzo vya maji na sehemu nyingine lakini Serikali haichukuwi hatua yoyote kwa watendaji wake.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukupongeza kwa kazi kubwa na nzuri unayofanya wewe na timu yako hapo Wizarani na ninakutakia kila la kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unahusu Sheria mpya ya Barabara yaani hifadhi ya barabara ambayo awali ilikuwa mita 25 na sasa sheria hiyo mpya imeongeza eneo la hifadhi ya barabara toka mita hizo 25 hadi 30 kwa sasa. Sasa Mheshimiwa Waziri, kwa vyovyote vile kuongezwa kwa eneo hilo kunagusa eneo la ardhi ya wananchi na pahali pengine inagusa makazi ya watu kama tunavyoona alama za barabarani zimesogea katika ardhi inayomilikiwa na wananchi na pia tumeona alama za "x" ambazo zimewekwa katika nyumba zote ambazo sheria mpya inazigusa ili kufikia kiwango cha sheria mpya ya hifadhi ya barabara kufikia mita 30 kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najua sheria hiyo inasimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Ujenzi imeanza kutimiza wajibu wake kwa kusogeza alama zao ndani ya ardhi ya wananchi na kuweka alama za "x" katika nyumba zote zinazoguswa na sheria hiyo mpaka katika Jimbo langu la Bahi. Jambo hili limefanywa bila wahusika walioathirika na sheria hiyo kulipwa fidia kutokana na ardhi yao kumegwa au nyumba zao kutiwa alama ya "x" hata kama bado hajabomolewa. Jambo hili limeathiri sana wananchi waliomegewa ardhi yao au kuwekewa ya "x" kwani sasa hawapati wapangaji au wanashindwa

kuendeleza maeneo yao kutokana na hofu ya sheria hiyo mpya ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujua mambo matatu toka Wizara ya Ardhi juu ya jambo hili, Wizara inatamka nini juu ya zoezi hili kuendelea kienyeji bila wahusika ikiwemo Wizara ya Ardhi kushirikishwa na kuandaa mpango mzuri wa utekelezaji wa zoezi hilo hatua kwa hatua badala ya kuathiri nchi nzima kwa wakati mmoja? Kwa kuwa zoezi hili linaendelea bila wananchi kulipwa fidia, je, Wizara inasema nini juu ya jambo hilo hasa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi ili wananchi walipwe fidia sambamba na utekelezaji wa zoezi hilo? Je, Wizara ipo tayari kushirikiana na Wizara ya Ujenzi kuandaa mpango wa pamoja wa kuliandaa zoezi hili kisayansi na tija ili wananchi mara wanapofikiwa na zoezi hilo walipwe mara moja na kama bado hamna fidia waachwe kwanza?

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa jitihada zake za kuweka utaratibu mzuri Wizarani. Si vema kuacha kupongeza viongozi wengine waandamizi Wizarani hapo kwa jitihada zao za dhati za kutumikia umma na kujenga mfumo rasmi ulio wazi wa kusimamia kugawa ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Makamishna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba kwa kugusa maeneo muhimu ya kiuchumi na uboreshaji miji na vitongoji, uharibifu wa mazingira, ugawaji makazi, ufanisi wa kiutendaji (vifaa na utaalam).

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ardhi Mkoani Tanga hususani Korogwe Mjini, maeneo yaliyotelekezwa na

iliyokuwa Mamlaka ya Mkonge, ni vema sasa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi iingilie kati. Ieleweke kuwa mji wetu uko chini ya vilima vya Usambara na mita chache kutoka eneo letu, ni mapitio ya mto Pangani, ni mita chache tu pembezoni mwa mto huu kuna mashamba makubwa ya mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu wa maneno na maandishi katika kujadili bajeti ya Wizara hii, tuliomba timu ya wataalam ipite Wizara ya Kilimo, Ardhi na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Korogwe unakua kwa kasi sana kiasi cha kufanya maendeleo mahsusi kama eneo jipya la hospitali kuwa na maeneo ya kubarizi kama sehemu ya uboreshaji miji midogo. Tunaomba Serikali ifike Korogwe mjini na kusaidia kupanga mji huu upya. Vijiji na vitongoji na mitaa vilivyomo ndani ya yaliyokuwa mashamba ya mkonge vimekuwa sana na raia wa nchi hii ni vema sasa wakatambuliwa na kugaiwa ardhi hii kwa makazi na shughuli nyingine za kujiongezea kipato. Asilimia 80 ya ardhi nzuri ya Mkoa wa Tanga inamilikiwa na watu wachache chini ya mfumo wa kilimo cha mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aliahidi kuwa atafuatilia mgogoro wa ardhi ya mkonge kwa kweli wawekezaji wameshindwa na kinachofanyika ni usanii tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umakini katika kujenga sekta hii unarudishwa nyuma na kuwepo Maafisa Mipango na Maafisa Ardhi wanaokiuka taaluma zao na kushiriki vitendo vya ugawaji ardhi bila kufuata taratibu. Wakati umefika sasa tuwajibishane, hofu ya wananchi hasa eneo la

Mikoroshini-Kilole pale Korogwe Mjini. Wenye mashamba na wenyeji wakitimuliwa bila fidia wala kugaiwa maeneo ya kuishi, inasikitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzembe na uzoroteshaji maendeleo hata uwekezaji unarudishwa nyuma na watendaji waliopo katika Manispaa, Miji na hata Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo Korongwe na hata makazi, imekuwa ikisuasua na kutokana na tabia zisizofaa za watalaam pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la mipango miji na vijiji, ni mpango mzuri wa Serikali wa kuweka makazi mazuri ya wananchi lakini mipango hiyo inasititishwa na watendaji wa Serikali kwa maslahi yao binafsi. Hivyo, namshauri Waziri kusimamia ipasavyo suala hili ili wananchi wa Tanzania waishi maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa viwanja, Serikali imekuwa na utaratibu wa utoaji viwanja kwa njia ya kutoa fomu kupitia afisi za Serikali lakini hata hivyo utaratibu huo umekuwa ukiwapa matatizo wananchi wanaochukua fomu kwa kutopata viwanja hivyo na badala yake viwanja vingi vinachukuliwa na watendaji wa ardhi na baadaye kuviuza kwa bei ya juu. Sasa utaona lengo la Serikali la kuwezesha wananchi kupata viwanja halipo. Hivyo namshauri Waziri

atupie macho sehemu hiyo ya utoaji fomu na ugawaji viwanja.

**MHE. DKT. TEREZYA P.L. HUVISA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri inayofanyika katika kutekeleza Sera ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuzidi kushirikiana na ofisi ya Makamu wa Rais ili kulinda maeneo oevu. Maafisa wa Ardhi katika ngazi zote za Halmashauri na Serikali Kuu waone umuhimu wa kutokupima viwanja katika maeneo yote oevu, kwenye mikoko na vyanzo vya maji ili kuepuka au kupunguza madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Maeneo oevu ufukweni mwa bahari ni kuiwezesha bahari ipate sehemu za kupumulia. Hivyo ni vizuri Maafisa wa Ardhi wakaona umuhimu huo ili kupunguza madhara ya mafuriko, Tsunami na menginenyo yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya sekta zote kwa wananchi yanategemea sana matumizi bora ya ardhi. Naomba tuzidi kushirikiana kwa maendeleo na uhai wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Tibaijuka na Naibu Waziri, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye kwa kuubeba mzigo mzito wa majukumu ya Wizara hii. Aidha, nawapongeza watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Ndugu Patrick Rutabanzibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Wabunge wote walioiunga mkono hoja hii. Aidha, napenda kutoa ushauri ufuatao; Wizara itunge Sera ya Ardhi ya kupiga marufuku uuzaji au ukodishaji ardhi kwa kipindi kirefu mfano miaka 99 kwa wageni. Taarifa za uhakika ni kwamba ifikapo 2050 mahitaji (*demand*) ya chakula yatazidi, uzalishaji na hali hii itasababisha bei ya vyakula duniani kupanda sana. Wageni wanalijua hilo na wameanza kufurika nchini kununua na kukodisha mashamba kwa fedha kidogo sana. Miaka 40 kuanzia sasa watakuwa wamechukua ardhi kubwa sana na watawauzia Watanzania chakula katika nchi yao. Ushauri, Sera itamke waziwazi kuwa uwekezaji katika kilimo ufanywe kwa ubia kati ya wazawa na wageni. Ni uamuzi utakaopokelewa vizuri na wananchi lakini utakaolalamikiwa na wageni lakini kama Dubai walivyolazimisha ubia katika uwekezaji na Tanzania ikilazimisha ubia badala ya wageni kuikimbia Tanzania wataongezeka pale wanapoona Watanzania wanaingia ubia nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilete Muswada hapa Bungeni wa kurudisha katika Serikali mapori yaliyochukuliwa na wanaojiita wawekezaji wazawa au wageni na kuyaacha bila kuyaendeleza miaka lukuki. Matokeo ya kuhodhi ardhi hii ni mawili. La kwanza, wanaohodhi, wanasubiri bei ipande ili wayauze, hivyo kujenga dhana iitwayo *'artificially high demand'. This speculation only fuels inflation in food items, leading to an overall increase in inflation*. La pili, kuhodhi huku kunawazuia wawekezaji wa kweli katika kilimo kushindwa kuwekeza *leading to food shortage and higher inflation in food items*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, maadam Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya ku-*revoke land ownership*. Wizara ifanye tathmini ya mapori haya na kumshauri Mheshimiwa Rais ipasavyo. Yale mapori ambayo yatathibitika kutokuwepo na mpango wa kuyaendeleza yachukuliwe mara moja na kuwekwa kwenye *'land bank'.* Serikali ya CCM tusingoje Wapinzani walipigie kelele hili maana mantiki yake sote tunaifahamu. Tukitoa japo 'notisi' hawa wenye mapori watayaendeleza kwa kuhofia kunyang'anywa na matokeo yake chakula kitaongezeka na bei za vyakula zitashuka hivyo kusababisha maisha kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kufanya urasimishaji wa baadhi ya vijiji vya Jimbo la Moshi Vijijini. Ombi langu ni kuwa kasi hii iongezeke ili vijiji vyote vipate kufanyiwa urasimishaji, jambo hili litatusaidia wananchi wa Moshi Vijijini kuweza kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha kusukuma maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Mwalimu wangu Profesa Anna Tibaijuka.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji limechukuwa sura mbaya baina ya pande mbili hizi ambapo baadhi ya wakati kunapelekea mapigano ya pande hizi. Imedhihirika kuwa asilimia tisini ya ardhi yetu haijapimwa hivyo kero la kumilikishwa wananchi limekuwa likisuasua, hivyo ushauri wangu kwa Halmashauri na kuongeza fedha hata za dharura ili kuongeza kasi ya

kutatua kero ya migogoro ya mipaka ya ardhi kwa kupimwa na kumilikishwa wananchi kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Mji Mpya wa Kigamboni, umekuwa na matatizo makubwa na umegubikwa na usiri mkubwa ambao wananchi wa Kigamboni wanajiuliza maswali kadhaa yasiyo na majibu huku wakiwa hawamini mchakato mzima unaoendelea kwa Serikali ambapo hauwashirikishi wananchi wake kikamilifu na ni muda wa miaka miwili sasa tangu Serikali ifanye tathimini ya wenye nyumba. Naishauri Serikali kujipanga upya na kukaa kitako na wananchi ili uhalisia upatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* limekuwepo zaidi kibiashara kuliko kuwasaidia wananachi wa kawaida. Pango la nyumba za Shirika la Nyumba linaongezeka siku hadi siku kutoka shilingi 200,000/= hadi laki 350,000/=ni kiwango kikubwa sana, hivi ni kweli maskini wa nchi hii ataweza vipi kumudu kupanga nyumba hizi zinazoitwa za shirika la Serikali? Naishauri Serikali kuandaa mazingira ya kujifunza kwa kupata ujuzi nchini Morocco na Uturuki ambako nyumba zinauzwa kwa bei nafuu kwa ajili ya maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amegusia tatizo la migogoro ya mipaka kati ya nchi yetu na Burundi. Ni dhahiri alama za mipaka (*beacons*) zimeondolewa na watu wanajulikana. Alama za mipaka kati ya Tanzania na Zambia kule Tunduma zimeondolewa na ni dhahiri ni suala mtambuka kwa Wizara, Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa (JKT) pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje kwa kushirikiana na nchi ya

Zambia. Ni lini '*beacons*' hizo zitarejeshwa mbona muda umekuwa mkubwa sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, alama za mipaka (*beacons*) kati ya Tarime (Tanzania) na Migori (Kenya) zimeondolewa. Vijiji vya Ronche, Kirongwe, Ikoma, Danyakoo, Kagoje na Nyamhunda, je, Serikali yetu na ile ya Kenya zina mikakati gani ya kurejesha alama hizi? Kuvumilia na kuchelewa kurudisha alama za mipaka kati ya nchi na nchi, ni hatari sana kwa usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kwa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, *filing system,* katika ofisi za ardhi ni *more traditional.* Manispaa ya Kinondoni imepoteza mafaili yangu ya kuomba kupimiwa ardhi mara tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimu na rushwa kukithiri kwa watendaji wa Halmashauri na Ardhi. Nimefuatilia kibali cha kupimiwa ardhi Manispaa ya Kinondoni kwa miezi tisa sasa bila mafanikio bila sababu zozote. Mbunge miezi tisa mkulima ni miezi mingapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, wakubwa mfanye ziara za kushtukiza pale Manispaa za Dar es Salaam mtabaini madudu ya kutosha, nchi inateketea hasa inateketezwa na Maafisa wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maskini nchi yangu Tanzania wachache wanaturejesha nyuma.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa Wizara, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa juhudi kubwa za kuleta maendeleo ya makazi na kupanga ardhi na matumizi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo tatizo pale mwananchi anapohitaji kupata hatimiliki inamchukua muda mrefu kupata hati pamoja na kuwa amekamilisha taratibu zote. Ni kwa nini Kamishna wa Ardhi anachelewesha sana kusaini hatimiliki? Wapo wananchi wameomba hati wana karibu mwaka hawajapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mji Mpya Kigamboni, nawapongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa, ongezeni kasi mji mpya ujengwe kwa maanufaa ya Watanzania wote angalau na sisi tuwe na Singapore ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NHC,* nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mkurugenzi Mkuu na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuboresha nyumba na kujenga mpya. Naiomba Serikali iondoe (*VAT*) kwa nyumba zinazojengwa na *NHC* kwa ajili ya kuwauzia wenye kipato cha chini ili nao waweze kununua nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni usumbufu wanaopata wananchi kwenye Mabaraza ya Ardhi Wilayani, ni vyema Serikali ikaliangalia hilo kwa sababu kesi zinacheleweshwa makusudi hivyo kuchukua muda mrefu kutolewa maamuzi lakini pia kuna upendeleo wa wazi katika Mabaraza hayo baadhi hivyo kuleta kero kubwa kwa

wananchi. Baadhi ya Wenyeviti wa Mabaraza hayo kujiona ni Miungu watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri ya bajeti na yenye mwelekeo mzuri. Pamoja na hongera hizo, nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni migogoro ya ardhi. Kwa muda mrefu kumekuwepo na migogoro mingi ya ardhi baina ya watumiaji wengi. Tukumbuke ardhi ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya nchi yoyote ikiwa na pamoja na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya migogoro mikubwa ni ile inayohusu wakulima na wafugaji ambayo sasa imetapakaa maeneo mengi nchini na kuleta madhara makubwa kwa wahusika. Eneo lingine ni migogoro kati ya Hifadhi za Taifa na maeneo yanayozunguka ambako kumekuwa na migogoro mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa kasi kubwa ikiwa ni pamoja na ongezeko la mifugo na wanyamapori. Ni dhahiri kwamba migogoro hii itazidi kuwa mingi. Kwa kuwa Wizara nyingi zinahusika na matumizi ya ardhi, nashauri kuundwe *Interministerial Task Force* ili waje na mikakati ya muda mrefu ili kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wananchi wengi wangependa sana kupimiwa ardhi yao ili watumie kwa kupata mikopo kwa maendeleo yao. Kwa bahati mbaya gharama ya kupima ardhi ni kubwa sana na wananchi wanashindwa kumudu.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaunga mkono mia kwa mia. Hongera sana kwa taarifa nzuri ya bajeti ya ardhi. Hongera sana vilevile umesoma vizuri sana ahsante sana mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hoja yangu ipo katika kodi za nyumba kwa Serikali. Ni kweli kwamba tulitunga sheria sisi wenyewe Wabunge kuhusu kodi hiyo ya majengo lakini inaonekana kuwa kwa kweli wenye nyumba wenyewe hawawezi kulipa kodi hizo. Naomba Wizara itoze kodi zile nyumba kubwa za kibiashara lakini kutoza nyumba za makazi ni kumuonea mwananchi kwani atakuwa hana uwezo wa kulipa kodi ya majengo. Naomba yafanyike marekebisho ya Sheria ya Kodi za Majengo ili nyumba za makazi zisitozwe kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho na mimi ninaomba kiwanja kule Madaba au Kivukoni. Ahsante sana.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya Kongwa ina watumishi watatu tu katika Idara ya Ardhi. Hivyohivyo Halmashauri zote nchini. *Trainning* iko chini ya Wizara, ongezeni idadi ya wanafunzi vyuo vya Morogoro, Tabora na Ardhi ya Dar es Salaam. Wataalam wa Mipango Miji ni wachache mnomno, Mji Mdogo wa Kibaigwa hauna afisa huyo hata mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu na ukiritimba uliomo katika *process* ya kutaka kumiliki ardhi na ama kuhamisha miliki kutoka mmiliki A kwenda mmiliki B ni ngumu na ndefu sana. Serikali inakosa mapato mengi sana hasa mijini kwa kaya ambazo miliki zimehama lakini hayuko aliyetayari kuja kwenu aidha kuanza ukiritimba wa *process* ya kuhamisha miliki. Ushauri ziangalieni taratibu hizo zifupisheni.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba niungane na Mheshmiwa Waziri kumpongeza sana Mkurugenzi Mkuu na timu yake yote. Sisi Wabunge wa Dar es Salaam tulitembelea miradi baada ya kupata maelezo ya kina. Ni wazalendo na wanachapa kazi, wameokoa nyumba za shirika ambazo kuna wezi walikwishazigeuza zao kwa hila ndogondogo. Mimi nasema wapewe '*support'* wafanyakazi na kama wakiendelea hivi wanaweza kutoa jawabu la matatizo makubwa ya nyumba nchini hasa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini narudia kuwaambia bado waangalie bei ya nyumba kama alivyoripoti kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri anasema walengwa wa nyumba hizi ni wananchi wa kati. Hawa walio wengi ni vijana, wasomi waliohitimu karibuni, Mainjinia Walimu, Madaktari, Wafamasia, Manesi, Wanasheria na kadhalika lakini pia wapo wafanyabiashara wa kati. Mishahara yao ni kati ya shilingi 450,000 mpaka 900,000 kabla ya kodi ni vipi ataweza kulipa shilingi 250,000 mpaka laki 400,000 kwa mwezi? Au tunataka kuwafundisha ufisadi mdogo mdogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesikia malalamiko yao juu ya kodi kubwa, mimi naomba nitoe ushauri waende kujenga '*affordable houses*' wenzetu wa Ethiopia nadhani

sasa hivi wana viwanda vitatu vya kutengeneza *'building material'* kwa kujengea *'affordable houses'. Material* hii ni *water proof, fire proof, earth quake proof'* inajenga nyumba mpaka ghorofa tano bila vyuma. Kwa sababu ni *panels* ujenzi wake ni wa haraka. Gharama ya ujenzi inapangua kwa asilimia 33. Waende wakaangalie, naweza kuwapa *website* na Serikali iwasaidie kujenga kiwanda kitaokoa fedha nyingi sana na Watanzania wanaweza kupata nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliyoyasema kwa Kigamboni ninasema hivyohivyo kwa Ilala, Kata za Segerea, Kinyerezi, Msongola na Chanika na Majibe na kwa Kinondoni Kata za Goba, Mabwepande, Kwembe, Saranga na kadhalika. Natumaini Serikali itatafakari na kutoa uamuzi wa busara ili tusiwatumbukize wananchi kwenye dimbwi la umaskini.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu na Watendaji wote kwa namna walivyoanza kushughulikia matatizo sugu ya Wizara hii, naiomba kasi hii iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo matatu, naomba yabaki kama mchango wangu. Kwanza ni namna urasimu ulivyo katika kupatikana hati za kimila na za kawaida kwa wananchi. Tatizo hili ni kubwa kwani wananchi wa kipato cha chini hawamudu kabisa kupata hati kutokana na urasimu wa gharama zilizopo, naiomba Serikali kuangalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, gharama za nyumba zinazojengwa na kuuzwa na *NHC* ni kubwa. Kama yapo mambo yanayosababisha gharama kuwa kubwa kwa maana ya *VAT* na gharama za vifaa vya ujenzi, Serikail

iangalie kuondoa matatizo haya. Aidha, niiombe *NHC* kufika na kujenga nyumba za gharama nafuu kwenye Wilaya zinazoanza kujenga miji yake kama vile Sikonge na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niombe Serikali iwezeshe Halmashauri na Wilaya zipate vifaa vya kutosha vya upimaji na pia kuhakikisha wataalam wa kutosha wanapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya ili upimaji kwenye Halmashauri zetu za Wilaya uwe na kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja.

**MHE. ZAHRA ALI HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili binadamu apate heshima na athaminiwe basi awe na makazi ya kudumu. Tatizo tulilonalo kubwa ni kuwa wananchi wengi katika nchi yetu uwezo wa kupata heshima ya kuwa na makazi yao inakosekana. Kipato cha kila siku cha mwananchi hakitoshelezi matumizi ya lazima seuse kujenga nyumba?

Mheshimiwa Naibu Spika, mabenki yaliyohamasika kutowa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba yana masharti magumu sana ambayo hayampi mwananchi wa kawaida hasa wa vijijini kuyamudu. Mabenki haya yana urasimu mkubwa na kuna riba kubwa sana mara nyingi bei za nyumba ni kubwa na mara nyingi zinauzwa kwa dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze juhudi zinazofanywa na Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) kwa kazi nzuri ya kujenga na kuuza nyumba kwa wananchi. Pamoja na juhudi hizo, kuna ukweli kwamba hali

bado ni ngumu, bei za nyumba hizo ni kubwa sana na wananchi wengi hawawezi kuzimudu. Kutokana na hali hii bado naendelea kuiomba Serikali iendelee kulipa uwezo Shirika la Nyumba Tanzania (*NHC*) pamoja na Wakala wa Ujenzi wa Nyumba za Serikali (*TBA*) ili taasisi hizi ziweze kuwa na dhamana ya kujenga nyumba na kuuza kwa wananchi kwa njia ya mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali itizame kuondoa *VAT* kwa Shirika la Nyumba ili liweze kujenga na kuuza nyumba kwa wananchi kwa bei nafuu ambazo wananchi wanazimudu kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kugusa maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dukuduku ni eneo lililomilikishwa kwa kampuni ya Sum-Biofuels ya Uingereza. Eneo hilo limechukuliwa katika vijiji kumi na moja vya Wilaya ya Kisarawe. Mwekezaji alitumia mbinu ya kuwarubuni wananchi kwa ahadi ya kujenga miundombinu ya afya, elimu, maji na barabara sambamba na utoaji wa ajira kwa wananchi. Kibaya zaidi mwekezji huyo alipewa hatimiliki kinyume cha sheria kwani hata fidia iliyokusudiwa haikutolewa. Je, ilikuwaje mwekezaji apewe hatimiliki bila kulipa fidia? Jambo hili lililazimishwa na kinyume cha sheria. Hivi sasa kampuni hiyo imehodhi eneo hilo na hivi sasa

alikuwa katika mchakato wa kuuza hisa kwa kampuni nyingine ikiwemo *thirty degree east*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utapeli mkubwa uliofanyika, naiomba Serikali ifute hatimiliki ya mwekezaji huyo na eneo hili kurudishwa kwa wananchi kwani hivi sasa kuna mgogoro mkubwa kutokana na mwekezaji huyo kufanya utapeli mkubwa. Wanakisarawe hatutokubali katika jambo hili. Naiomba Serikali ifute hatimiliki ya mwekezaji huyo, haiwezekani ardhi yetu itumike kuwa kitega uchumi cha wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kibong'wa hawajalipwa fidia toka mwaka 2005. Viwanja vimeshapimwa lakini hadi leo hawajalipwa fidia. Ni muhimu kupata majibu ya kina katika mgogoro wa Kibong'wa ndani ya Kijiji cha Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Wilaya ya Kisarawe eneo la Kisarawe Mjini walitoa maeneo yao kwa ajili ya Mipangomiji kwa bahati mbaya toka mwaka 1982 hadi sasa watu hao wamekosa stahili zao zilizotathminiwa. Naiomba Serikali ihakikishe kwamba wazee hawa wanalipwa fidia zao kwani wengine wamefariki bila kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iharakishe zoezi la hati miliki za kimila katika Wilaya ya Kisarawe. Hati hizi zitawasaidia sana Wanakisarawe kupata mikopo ili kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho, naomba nielezwe ni lini Serikali itafute hati ya Mwekezaji wa

*Sunbiofuels* kwa Wilaya ya Kisarawe pamoja na taratibu za fidia za wananchi waliodhaminiwa maeneo yao kwa ajili ya mipango miji ya mwaka 1982.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi ya mwaka 2012/2013. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti ambayo imetayarishwa kwa umahiri na utaalamu na inalenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayosisitiza kukuza uchumi madhubuti na endelevu katika matumzi bora ya ardhi na kuendeleza mpango wa kurasimisha ardhi na makazi. Mpango huu unalenga kumpa heshima mwananchi kwa kuwawezesha kumiliki ardhi na kuwa na makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango mizuri ya Wizara, bado kuna matatizo mengi katika umilikishaji ardhi ikiwa ni pamoja na urasimu katika zoezi zima la utoaji wa hatimiliki, uvamizi wa maeneo ya wazi, ujenzi holela wa maduka na sehemu za biashara zilizoshamiri katika maeneo ya makazi, ujenzi wa nyumba katika maeneo ambayo hayajapimwa, ujenzi wa nyumba za kuishi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda na biashara, ujenzi wa viwanda katika maeneo ya makazi, migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji waliomilikishwa ardhi kwa matumizi mbalimbali na migogoro ya kugombea mipaka kati ya wakulimia na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana katika mchango wangu wa maandishi kwa Wizara hii, nilishauri namna

Serikali inavyoweza kujipanga katika kuweka mipango mizuri itakayoboresha miji yetu. Pia nilitoa ushauri namna wataalamu wetu wa Chuo Kikuu cha Ardhi wanavyoweza kutumika kuanzisha miji ya kisasa katika Mikoa ambayo haijaathiriwa na ujenzi holela na pia kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa mingi ina maeneo ambayo ardhi yake bado haijakaliwa na wananchi wengi na kwa hivyo yapo maeneo ambayo yakipimwa na kuwekewa mipango mizuri yatakuwa na mwonekano na mandhari nzuri. Nasikitika kutoa mfano na kusema kwamba Dar es Salaam kwa ukweli umejengwa kiholela sana, hata maeneo yao mpango miji yaliyopimwa miaka ya karibuni kuanzia mwaka(1980) kama Mikocheni, Mbezi Beach, Kijitonyama na Sinza majengo yanaonekana kusongamana sana na hata ujenzi wa nyumba zake hauko katika mpangilio unaoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kwenda kwa mkazi wa maeneo hayo unapata shida sana ya kufuata maelekezo kwani hakuna barabara za kueleweka, mitaa haina majina na hii pia inafanya huduma za jamii kama barabara, mabomba ya maji safi na maji taka, nguzo za umeme na njia za mawasiliano ya simu kuwafikia kwa shida sana. Katika kupima maeneo haya haikuzingatiwa kuwepo kwa maeneo ya huduma kama vituo vya usalama na polisi, zahanati, shule na maeneo ya michezo na kama yalikuwepo basi yaliuzwa au yalivamiwa. Maeneo kama Tandale na Manzese ndio usiseme kabisa. Naishauri Serikaili kuwa makini katika maeneo mengine ambayo hayajajengwa kiholela ili kuweka mipango miji itakayokuwa na mvuto kwa maana ya kuweka masharti ya ramani za

majengo, kuweka huduma za jamii kabla ya kugawa viwanja ili mtu anayetaka kiwanja anunue pamoja na ramani ya nyumba inayoelekeza ujenzi na upande itakayoelekea alipie huduma zitakazokuwa zimejengwa kama miundombinu ya barabara, maji, umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini wako tayari kabisa. Serikali ifanye majaribio ya ujenzi wa mji wa mfano utakaokuwa unaonyesha mipangilio ya barabara, mitaa, huduma za jamii na kadhalika katika Miji Mdogo wa Mlandizi na maeneo mengine ambako ardhi bado ni kubwa ambapo utekelezaji wake utasaidia kusukuma maendeleo ya Jimbo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kila mtu anakuwa na heshima katika jamii kama ana nyumba na mji wake. Kipato cha kila siku cha mwananchi hakitoshelezi mahitaji yake na kumwezesha kujenga nyumba bora. Mabenki yaliyohamasishwa kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, yana masharti magumu sana ambayo hayampi nafasi mwananchi wa kijijini kuyamudu. Mabenki haya yanahitaji dhamana na yanatoza riba kubwa sana. Wakati mwingine hata kama una dhamana, urasimu wa kupata mkopo ili uweze kujenga au kununua nyumba ni ndoto. Bei za nyumba nazo ni kubwa sana, mara nyingi utakuta nyumba zinauzwa kwa bei ya pesa za kigeni ambazo mwananchi wa kawaida, mkulima, mfugaji au mfanyakazi hawezi kuzimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze juhudi zinazofanywa na Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* kwa kazi nzuri ya kujenga na kuuza nyumba kwa

wananchi. Pamoja na juhudi zao pia kuna ukweli usiofichika kwamba hali bado ni tete, bei za nyumba hizi pia ni kubwa sana na wananchi walio wengi hawawezi kuzimudu. Kutokana na hali hii, bado naendelea kutoa kilio kwa Serikali iendeleze na kuzipa uwezo Shirika la Nyumba Tanzania *(NHC)* pamoja na Wakala wa Ujenzi wa Nyumba za Serikali *(TBA)* ili taasisi hizi ziweze kuwa na dhamana ya kujenga nyumba na kuuza kwa wananchi kwa njia ya mkopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *rent increaments*, 2001- Sh.68,000 *per month,* 2005 – Sh.116,000 *per month*, 2007 – Sh.187,000 *per month*, 2009 – Sh.299,000 per month, 2012 – Sh.662,830 *per month to be paid quarterly*. Ongezeko la kodi katika miaka mitatu ni asilimia 69 yaani ongezeko la mara mbili zaidi. Ongezeko la kodi katika kipindi cha miaka kumi yaani 2001 – 2012 ni zaidi ya asilimia 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali kubinafsisha sekta ya nyumba mnamo 1971 ni kuwapa wananchi makazi nafuu, kujenga nyumba nafuu kwa mfano Magomeni, Ilala, Kinondoni na Temeke kufuatana na Sera ya TANU wakati huo. Serikali ilipangisha nyumba za msajili kwa wafanyakazi wa Serikali, Taasisi za Serikali na Mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuuzwa nyumba za Serikali, Mashirika na Taasisi, mnamo mwaka 2003, Serikali ilipitisha mpango wa kuuza nyumba za Serikali, Mashirika na Taasisi kwa wapangaji waliokuwa wanaishi kwenye nyumba hizo. Serikali pia kupitia agizo la Rais Mkapa na Rais Kikwete ilipendekeza Shirika la Nyumba liwauzie wapangaji wa *NHC*. Agizo hilo hadi leo limewekwa kapuni. Sisi wapangaji wa *NHC* tunaonewa na Shirika la Nyumba. Iweje Serikali iwauzie

wafanyakazi wake na sasa ikatae kuuza nyumba hizohizo za Serikali kwa wapangaji wa *NHC*? Hii ni *"double standard"* na inapelekea manung'uniko na chuki kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupandisha kodi kiholela, uongozi wa Shirika la Nyumba katika miaka ya karibuni imegeuka kuwa 'mbogo' kwa wapangaji. Ongezeko la kodi ya nyumba ya hivi sasa ni uonevu mkubwa wenye dhamira ya kuwafukuza wananchi kwenye nyumba hizo. Ongezeko la kodi la hivi sasa ni ishara wazi Shirika halina muda wa wapangaji maskini. Wote wataondoka na watabakia wenye hela. Je, hii ndiyo sera ya CCM? Tunaomba Serikali kupitia Bunge lako Tukufu kusitisha ongezeko hili ambalo linaashiria harufu ya ubepari na tangu lini Serikali ikajikita kwenye biashara kuwakandamiza wananchi wake?

Mheshimiwa Naibu Spika, yote yanawezekana tukidhamiria, naunga mkono hoja.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, lakini pamoja na kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia katika eneo moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kutumia Mabaraza ya Ardhi limeshindikana. Utaratibu huu, umeongeza mlundikano wa kesi za ardhi katika Mahakama Kuu hadi kufikia 6,000 hivi sasa. Kesi hizi zote zinatokea kwenye Mabaraza ya Ardhi kama Rufaa Mahakama Kuu. Rufaa hizi zinaletwa Mahakama Kuu kwa sababu ya uendeshashaji mbovu wa kesi katika Mabaraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuwa Mabaraza haya yavunjwe ili utoaji wa haki katika migogoro ya ardhi urejeshwe Mahakamani kama ilivyo katika masuala mengine yote ya utoaji wa haki. Katiba ya nchi inaeleza wazi kuwa Mahakama ndiyo chombo pekee kitakachotoa haki hapa nchini. Naiomba Wizara ifikirie kwa makini *alternative* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niongeze mchango wangu juu ya hotuba hii ya Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi hii. Wizara hii inauhusiano mkubwa sana na mikakati ya maendeleo ya nchi hii. Tunapozungumzia kuondoa umaskini tunazungumzia kukuza uchumi kwa kuboresha uzalishaji katika kila sekta. Hii inahitaji sana uwekezaji wa ndani na nje katika sekta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ni sehemu kubwa sana ya uwekezaji na ili watu wakope ni lazima wawe na hati za umiliki wa rasilimali kubwa ikiwa ni pamoja na ardhi. Kwa hivyo, ni muhimu sana shughuli zote za usimamizi na uhakiki ardhi na mambo yote husika yafanyike vizuri. Nataka kuiomba Serikali irudishe uratibu wote wa masuala ya ardhi Wizarani hususani udhibiti wa ukiukwaji unaofanywa na Halmashauri zetu nyingi. Hili ni muhimu kwa sababu tumeona jinsi gani Wizara ya Ardhi imeshindwa kuwadhibiti viongozi wa Halmashauri wanaokiuka sheria na taratibu za ardhi. Mfano wa Idara ya Polisi inaratibiwa na Mkuu wa Polisi ingawa ngazi za uongozi mbalimbali zipo, ngazi hizi hazijitegemei kama vile Halmashauri zilivyoachiwa kufanya wanavyotaka. Kwa kuwa Sheria ya Ardhi ni za

Kitaifa basi usimamizi wake pamoja na ukiukwaji wake uachiwe Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakubali kabisa kuwa Wizara imetengewa fedha kidogo katika bajeti lakini naamini kwa *mandete* ninavyoipendekeza hapo juu itawapa pia uwezo wa kuongeza mapato yao kwa zile shughuli zinazolipiwa na wananchi. Katika bajeti vilevile Serikali ikope kwa ajili ya kukamilisha kazi za maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mono hoja.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuchukua nafasi hii kuchangia Wizara hii kwa maandishi. Kwanza kabisa, tukumbuke usemi wa hayati Baba wa Taifa alisema ili tuendelee tunahitaji mambo manne ambayo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali na ardhi ni mtaji lakini Serikali imejisahau kutunza thamani ya ardhi badala yake ardhi imekuwa mgogoro mkubwa hapa nchini. Sheria hazifuatwi bali kila kiongozi ana maamuzi yake katika ardhi. Naiomba Serikali kupitia Wizara iweke mikakati ya kumalizia migogoro ya wakulima na wafugaji na ikibidi wakulima wasimiliki hekta zaidi ya mia moja ili kuwapa nafasi wafugaji nao kwa ajili ya kulishia mifugo yao. Naishauri Serikali ihakikishe inatenga maeneo ya wafugaji na wakulima ili kuokoa wananchi wanaopigana na kuuwawa kwa ajili ya migogoro ya maeneo ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabaraza ya Kata; Mabaraza ya Kata yametelekezwa mno na kuyaacha

yajiendeshe, hakuna motisha yoyote ambayo Serikali inatoa ili kuzuia tamaa ya kupokea rushwa, kutopewa maslahi yoyote na Serikali, ni kutoa mwanya wa rushwa kwa Mabaraza haya na ndiyo maana haki zinapindishwa kwa wananchi. Kesi zisizozaa matunda kwa kuonewa na kunyang'anywa mashamba au maeneo yao. Serikali iliangalie suala hili la motisha kwa Wazee wa Mabaraza ya Kata ili wasirubuniwe na vipesa na kupindisha haki. Tunakokwenda matokeo yake yatakuwa mabaya sana. Naomba suala la ardhi lipewe kipaumbele sana kulinda heshima ya Mtanzania kwani mwananchi wa Tanzania mtaji wake mkubwa au ajira yake kubwa ni ardhi, Wizara isipokuwa makini tutasababisha vita au mauaji yatakayokula Watanzania wengi kwa jambo linalowezekana kuzuiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namalizia kwa kusema naomba Waziri anihakikishie kunijibu maswali yangu yafuatayo:-

(a) Serikali sasa itachukua hatua gani kwa Maafisa Ardhi wanaogawa kiwanja mara mbili kwa watu wawili tofauti ili kupunguza migogoro iliyopo sasa hivi? Naomba Mheshimiwa Waziri suala hili unifafanulie kwa faida ya Watanzania wanaopambanishwa kwenye kiwanja kimoja, fedha zinachukuliwa kwa watu wawili tofauti.

(b) Viwanja vinavyogawiwa kwa wananchi ambao wanachelewa kuvijenga miaka mingi na kusababisha vichaka mijini, je, Serikali kupitia Wizara yako inasemaji kwa hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuchangia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la migogoro kati ya wananchi na wawekezaji, migogoro mingi inatokana na wawekezaji kupewa maeneo makubwa ya ardhi kinyemela kwa kutofuata sheria na hata hivyo maeneo hayo wamekuwa hawayaendelezi na kuifanya Serikali kutopata mapato ya kutosha na wananchi ambao wamezunguka sehemu hizo hawana sehemu za kulima na kusababisha migogoro mikubwa na wawekezaji pamoja na Serikali. Pamoja na kuwa baadhi ya mashamba mengi Rais ametoa kibali cha kuyafuta, je, kwa nini kumekuwa na kigugumizi cha utekelezaji mpaka leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko ya wakulima wadogowadogo kutokupimiwa mashamba yao na zoezi limekuwa la muda mrefu kiasi mpaka wengine wanadhulumiwa na matajiri maeneo yao. Ni lini Serikali itaharakisha kuwapimia mashamba yao ili kuondokana na matajiri kuwanyanyasa wakulima wadogowadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la migogoro ya ardhi kwenye Halmashauri, Watendaji wa Halmashauri wamekuwa si waadilifu na kupelekea migogoro ya ardhi kwenye Halmashauri kati ya wanavijiji na Watendaji hawa wa Halmashauri na hata wamekuwa wakiuza ardhi bila ridhaa ya wananchi na kupelekea migogoro mikubwa. Naiomba Serikali kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa lengo la kuwezesha Halmshauri, kuajiri watumishi wa sekta ya ardhi wenye sifa moja kwa moja kutoka vyuoni ili kuendelea kutoa elimu kwa umma na

kwa watumishi kuhusu sera na sheria za sekta ya ardhi ili kuepuka migogoro isiyokuwa na sababu na kuhakikisha tunaimarisha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi katika ngazi za Vijiji na Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika ngazi za Wilaya. Hii itaepusha wajane wengi kutodhulumiwa ardhi na wasiokuwa na uwezo wa kifedha na kuepusha migogoro Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la makazi vijijini, wananchi wengi wanaoishi vijijini hawana makazi bora. Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(NHBRA)* ana mchango mkubwa hasa katika kufanya utafiti na ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu ili kuinua na kuboresha viwango vya nyumba na kuongeza ubora wa maisha ya wananchi vijijini na mijini. Kwa kuwa pamoja na umuhimu wa Wakala huu kwa Taifa bado kumekuwa kukikabiliwa na changamoto na uhaba wa fedha hasa za maendeleo, zinahitajika kwa ajili ya utafiti kuanzia mwaka 1984 mpaka sasa utafiti haujawahi kutengewa fedha zozote za maendeleo, hivyo kukwamisha jitihada za Wakala katika kutekeleza majukumu yake ya msingi. Je, Serikali mwaka huu wa bajeti wa 2013 imejipangaje kuhakikisha Wakala hawa wa Taifa wanapata fungu la kuendeleza miradi hiyo vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa, limekuwa likidai Serikali na Taasisi zake kodi za pango kwa muda mrefu sasa. Hadi kufikia Juni, 2012, Serikali imekuwa ikidaiwa na Shirika kiasi cha shilingi bilioni 2.4. Endapo Serikali ingekuwa inalipa kodi hii kwa wakati muafaka, Shirika la Nyumba la Taifa lingeweza kujenga makazi mengine zaidi na wafanyakazi wengine wa Serikali ambao wanaishi pembezoni wangeweza kupata makazi ya

kukaa na kufanya kazi zao kwa utulivu. Je, ni lini Serikali itahakikisha inalipa pesa zote kwa Shirika la Nyumba la Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujengaji holela Dar es Salaam, Mheshimwa Waziri limekuwa ni tatizo sugu kwa wakazi wa Dar es Salaam, viwanja vya wazi ambavyo vinasaidia wananchi kupaki magari vimekuwa vikijengwa holela na wananchi wengine kujenga karibu na fukwe za bahari na wanavyobomolewa na Serikali wanarudia tena kwenda kujenga. Je, Serikali inawachukulia hatua gani wananchi ambao wamekuwa wakikiuka Sheria hii ili iwe fundisho kwa wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujengaji wa maghorofa Kariakoo yamekuwa yakijengwa holela na mara nyingi kumekuwa na malalamiko kuhusu viwango vya ujenzi huo, hata nyakati fulani yamekwishatokea maafa kwa kuanguka kwa hayo maghorofa. Je, wakati wa ujenzi wataalamu kutoka Jiji (Wahandisi) huwa wanakuwa wapi mpaka ujenzi unafika hatua ya mbali sana bila ya usimamizi? Inapotokea hivyo Wahandisi husika huwa wanachukuliwa hatua gani? Mpaka sasa ni Wahandisi wangapi wameshachukuliwa hatua za kinidhamu kuhusiana na ujenzi huo ulio chini ya kiwango?

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza sana Mheshimwa Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji fasaha. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Viongozi wa Wizara na watumishi wote kwa maandalizi mazuri ya bajeti ya Wizara, Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri na Uongozi wa Wizara wamesimama kidete kutekeleza Sera ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, waendelee kushika uzi huo huo, juhudi zao zinaonekana na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni ni hatua ya maendeleo kwa wananchi wa Kigamboni na kwa wananchi wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla. Ni muhimu miji ya nchi yetu ikapangwa vema ili kutupa mandhari nzuri na kuwezesha shughuli za maendeleo zikafanywa kwa ufanisi mkubwa. Wizara isirudi nyuma katika mradi huu, wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali watakuwa tayari kushirikiana na Serikali yetu kuwekeza katika mradi wa Mji Mpya Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni, Wizara isisahau kuweka mkakati wa kupanga miji yetu inayokuwa; mfano, Arusha, Mwanza, Mbeya, Moshi na mingine. Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili kuweza kufanikisha mkakati huu. Pia Wizara isisahau miji mingine mizuri inayochipukia, Mji wa Bagamoyo ni mmoja wa miji hiyo. Bagamoyo inakuwa kwa kasi kubwa sana lakini bila mpangilio mzuri. Wizara ilikopesha fedha za kupima viwanja mara moja tu na haijarudia tena. Viwanja vilipimwa bila kutenga maeneo ya matumizi ya umma kama Polisi, Makaburi, *Open space* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Bagamoyo limekumbwa na migogoro mingi ya ardhi, binafsi nimekwenda Wizara ya Ardhi na kuwasilisha migogoro yetu kwa Mheshimwa Waziri. Nimefanya vikao mara mbili na Mheshimiwa Waziri, migogoro hii ni pamoja na wenye

mashamba makubwa ambao hawajatumia ardhi hizo kwa miaka inayozidi 20 na sasa kuwanyima nafasi wananchi kutumia ardhi hiyo kwa maendeleo yao. Pia niliwasilisha migogoro mingine kadhaa. Namwomba Waziri aharakishe tupate maelekezo ya utatuzi wa migogoro tuliyowasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya mwaka jana ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, ilielezwa kwamba Serikali ingefungua Ofisi ya Baraza la Ardhi Wilayani Tunduru. Hii inatokana na umbali uliopo toka Tunduru hadi Songea (Mkoani) ambapo ni km. 276.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba walalamikaji wengi (takriban 90%) ni wanyonge wasio na uwezo wa kumudu gharama za nauli pia malazi. Kwa kukosa huko uwezo, wengi wao hukata tamaa na kupoteza haki zao japo kama wangefuatilia kwenye Baraza la Ardhi Mkoa wangeweza kupata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kukumbusha hili kwa kuwa hadi nawasilisha mchango huu hakuna lolote lililofanyika katika kuanzisha Ofisi ya Baraza la Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri atakapokuwa anatoa hitimisho atueleze kwa nini hadi leo Ofisi hiyo haijafunguliwa na kuna maandalizi gani ya kuifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimwa Waziri kwa kutuletea bajeti ambayo na mimi naomba kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Waziri kujitahidi katika utendaji wa kazi katika Wizara yake bado Wizara hiyo ina changamoto nyingi sana tena zinazowagusa wananchi wengi wa hali ya kati na ya chini kabisa. Hata hivyo, changamoto nyingi zinachangiwa sana na watendaji wake ambao hupenda kukaa sana Maofisini badala ya kutembelea sehemu mbalimbali nchini zinazokabiliwa na matatizo ya ardhi. Pia katika Ofisi/Wizara yake wapo watendaji ambao siyo waaminifu na pengine huwa chanzo kikubwa cha baadhi ya matatizo katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka jana 2011/2012 na katika nyakati mbalimbali nimeongelea sana suala la migogoro ya ardhi inayosababishwa na kutojulikana vyema kwa mipaka kati ya hifadhi za misitu na wananchi wanaoishi jirani kati ya Wilaya na Wilaya, Kata na Kata, pamoja na watu wanaovamia sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Waziri kuwa ameanza kutatua mgogoro wa ardhi katika Kata ya Chanika Nzasa kwenye msitu wa Kazimzumbwi, Wizara yake ilitoa taarifa katika vyombo vya habari kuwa eneo lililobomolewa lilikuwa ni la wananchi, lakini napenda kumweleza Mheshimwa Waziri kuwa bado wananchi wananyanyaswa na Maaskari na kuzuiwa kufanya shughuli za kiuchumi katika maeneo yao. Mimi naomba Waziri aniambie katika majumuisho ni lini Wizara yake itafika Nzasa

kuonyesha mipaka kati ya wananchi na hifadhi ya misitu ili jambo/mgogoro huu uweze kuwa umemalizika kabisa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama nilivyosema kwa nyakati tofauti nimekuwa hapa Bungeni naongelea kuhusu migogoro ya mipaka kati ya Wilaya ya Ilala, Temeke na Kinondoni mfano mzuri Kata ya Kitunda na Temeke, Kivule na Mbagala (Temeke) na kadhalika. Hivyo namwomba Waziri aje na majibu kuwa ni lini watendaji wake watatoka maofisini kuja kuainisha mipaka ya maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha nikitegemea majibu ya hoja zangu wakati wa hitimisho.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi kubwa inayoifanya Katika Mkoa wa Arusha hususani Wilaya ya Arumeru. Wananchi wa Oldonyosambu walichukuliwa maeneo yao kwa ajili ya matumizi ya Kijeshi na waliahidiwa kupewa eneo lingine. Kwa bahati mbaya, wananchi hao hawajapata maeneo hayo na hivyo kusababisha usumbufu kwa wananchi hao. Maeneo yaliyotengwa awali yamechukuliwa na Watendaji na baadhi ya wavamizi wengine wakati wananchi wa Oldonyosambu wakibaki wanatangatanga. Je, Serikali inasemaje juu ya kadhia hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaiomba Serikali ichukue maeneo yaliyouzwa bila kuendelezwa wapewe wananchi hawa kwani mpaka sasa hata maeneo ya kuzikia hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono hoja mpaka nitakapopata ufumbuzi utakaotolewa na Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, ahsante.

**MHE. MAULIDAH A. V. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, naomba kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kurudi Bungeni na kuendelea na majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ni Wizara muhimu sana na ni ya mtambuka kwani ardhi ni kila kitu, ardhi ni uhai, ardhi ni uchumi, ardhi ni maendeleo, ardhi ni tumbo linalozaa madini na ardhi unapoitumia ipasavyo huondoa shida zote na hata kutoa dawa za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha kuona mpaka sasa miaka 50 ya uhuru Serikali inashindwa kuitumia ardhi nzuri yenye rutuba na iliyojaa vivutio vya kila aina na mali nyingi, lakini sijui tunashindwa wapi kuitumia ardhi yetu na tuepukane na umaskini uliokithiri katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kutoa ushauri wangu kwa baadhi ya mambo ambayo nayaona hayaendi vizuri katika matumizi ya ardhi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanapojikuta wapo kwenye ardhi kwa uhai wao na wakati wa kulipima eneo hilo na kugawa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi, Serikali au Halmashauri watoe kipaumbele kwa wenyeji kwanza.

Kwa mfano, itoe viwanja kwanza kwa wale waliohodhi ardhi husika, wanapotoa viwanja hivyo waangalie uwezo wa wale waliopo pale au wamiliki wa eneo husika kwa kuwapa bei iliyo muafaka ambayo wataweza kumudu kulipa, sio kuwalazimisha walipe mamilioni ya fedha wakati hawana uwezo huu, kwa kweli huu ni uonevu. Mmiliki kama ana watoto basi apatiwe viwanja ambavyo ataweza kuwapa watoto wake ili na wao waweze kuendelea kuwepo eneo husika kwani pale ndio walipozaliwa au tuseme ndio kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwapa wawekezaji ardhi ili wawekeze, si jambo baya kwani ardhi tuliyonayo ni kubwa sana, lakini angalizo ya hili ni kama ifuatavyo:-

Kwanza lazima kuangalia mwekezaji huyu amekuja na nini, fedha ngapi kaingia nayo nchini hususani ninavyoelewa kwa sheria ya utoaji *permit* za kuwekeza nchini yaani *class A permit* ili aweze kuishi hapa, lazima awe ameweka fedha benki zenye kiwango Fulani, aambatanishe makabrasha yanayoonyesha idadi ya fedha kwenye *account* yake ndipo apewe *permit* husika. Leo inakuwaje mwekezaji apatiwe kibali cha kuishi na kuwekeza nchini bila ya kujulikana amekuja na fedha ngapi za mradi husika? Apewe ardhi ya Watanzania na yeye si Mtanzania, aombe mkopo kwa kutumia ardhi hiyo na apewe mkopo huo kwa kutumia ardhi hiyo, je, huu si ujambazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanajitwalia ardhi bila idhini ya wananchi na kwa sababu mwekezaji ana pesa basi hapo inaonekana kabisa kwamba ni uonevu kwani wananchi huhamishwa kwa kutumia nguvu, kupigwa, kuvunjiwa vyombo vyao, kunyanyasika kwa kina mama na

watoto wadogo na wengine kati ya hao huwa wajawazito, kutolewa kwa nguvu, kwa kweli ni jambo baya sana sana.

Hali hii ni mbaya na inaashiria kwamba wananchi walio maskini kwenye maeneo yao hawana haki kabisa. Nasisitiza sana kutoa haki kwanza kwa wananchi halafu ndio wageni kwani tuna pori la kutosha kama ni lazima wapeni maeneo ambayo hayajaendelezwa waende huko wakaendeleze sio maeneo ambayo wananchi wameshaishi kwenye eneo hilo na wanajiendeleza kwa kuweka maisha yao hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, ni Shirika la wananchi na wao ndio wangepewa nafasi ya kwanza katika kumilikishwa nyumba hizo na kuuziwa kwa bei nafuu. Nyumba hizo zilitaifishwa katikati ya miji ambapo zilikabidhiwa kwa Msajii wa Majumba wakati huo na kutoa nafasi ya kuwapangisha wananchi ili na wao wafaidike kukaa au kuishi mijini. Leo hii Shirika la Nyumba *NHC* wanapandisha kodi kiholela tena bila taarifa yoyote, au kutuma meseji kwenye simu za wapangaji na kuwataarifu kodi imepanda na mpangaji kuambiwa kwenye meseji hiyo aende akalipe kabla ya tarehe fulani la sivyo atahamishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba ilikuwa ikilipwa kodi ya shlingi laki moja na sitini unaambiwa ukalipe laki tatu na elfu hamsini hapo bado hujalipa maji, hujanunua umeme na pia hata hujalipia takataka, nani mwenye uwezo wa kulipa kodi kubwa hivyo? Je, mnataka matajiri ndio wakae mijini na wanyonge maskini waende wakaishi porini, mkumbuke hawa ndio wananchi wenye nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana ndio Taifa la leo, wamejaa mijini na shughli muhimu wanayofanya, wanageuka meza na makabati ya biashara kwa kujibebesha mizigo ya biashara mwili mzima wakipita njiani kuuza biashara hizo, hii si halali hata kidogo, naomba kutoa rai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi imetuzunguka na kuna kipindi ambacho tulipatia taarifa ambayo ilieleza kwamba ardhi yetu imepimwa na kuangaliwa na tukaambiwa imeshaonekana wapi panafaa kwa kilimo bora, sasa basi tunasubiri nini tusitumie ardhi hiyo kwa kuwapeleka vijana kwenda kuwafunza kilimo bora na hasa kwa vile tuna Mabwana Shamba wa kutosha na nguvu kazi ni hao vijana? Je, hatuoni kwamba tutaweza kupunguza mfumuko wa vijana kukimbilia mijini na kupata matunda mazuri ya kilimo na hasa hiyo kauli mbiu ya Kilimo Kwanza? Tukubali kutumia fedha ili tupate fedha, hii ni kipindi cha mwaka mmoja au miwili tu na baada ya hapo tutavuna vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naiomba Wizara kuhakikisha hatimiliki za viwanja zinatolewa kwa muda mfupi, kwani kwa kweli hivi sasa unapohitaji *Title Deed* huwa ina urasimu mkubwa mpaka kusababisha mwananchi kama anahitaji hati hiyo kwa haraka kupata kishawishi cha kutoa rushwa, naomba tuangalie utaratibu ambao utaleta uharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia hapa kwa kuwaombea ndugu zetu hawa nikianza na Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, bila kumsahau Mkurugenzi Mkuu na wasaidizi wake wa *NHC*, Mwenyezi Mungu awalinde, awape hekima na

busara ili waweze kulitumikia Taifa hili kwa ukweli na uaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba nafuu. *UN Habitat* waliwashawishi wananchi katika kijiji cha Basotu kujengewa nyumba 100 na masharti kujenga nyumba moja ya mfano kwa kushirikiana, lakini matokeo yake hawakujengewa hizo nyumba mpaka leo tangu mwaka 2000. Mheshimiwa Waziri utawasaidiaje wana wa Hanang kijiji cha Basotu wakati huo wewe ulikuwa *Habitat*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za *NHC* ziko juu sana, wananchi wa kima cha chini hawatamudu kununua nyumba hizo. Gharama za vifaa vya ujenzi itolewe kodi ili bei ishuke. Pia gharama za ujenzi kwa *contractors* iko juu sana, kwani nyumba kama hiyo ni imara ikijengwa na mafundi binafsi gharama zao ziko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, upimaji wa viwanja unasuasua sana mara nyingi mwaka unapita bila upimaji au ugawaji kufanyika; fidia kutolipwa kwa wenye ardhi ambao wamepitiwa na ramani ya mji toka mwaka 1995 hadi leo wanadai lakini hakuna malipo; ugawaji holela wa ardhi bila kikao kukaa cha ugawaji na waliofanya hivyo hawakuchululiwa hatua pia kugawa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya watumishi wa Serikali/Halmashauri, Mheshimwa Waziri tembelea Hanang kutatua kero za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yamepita nyaya za umeme au gridi ya Taifa wananchi walioathirika kutolipwa fidia na maeneo yaliyoongezeka kwa barabara kutolipwa fidia. Kwa kuwa wananchi huzungushwa sana na Taasisi hizo ni vema Wizara iingilie kutatua hizo kero za ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya mipaka, vijiji vya Hanang viliweza kupimwa lakini kuna migogoro ya mipaka ya vijiji na vijiji, kitongoji kwa kitongoji, tunaomba hiyo migogoro ingetatuliwa mapema. Mgogoro wa mipaka ya Singida na Manyara kuna sehemu ilirejeshwe Manyara lakini mpaka leo hatuoni utekelezaji wenyewe hata huduma za kiutawala bado zipo Singida, Mdida, Mwanga, hilo analifahamu Naibu Waziri. Naomba kufahamishwa utekelezaji wake.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ilete na kutoa elimu kwa umma kuhusu sera, sheria na kanuni za ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi kupitia program ya elimu kama mlivyoeleza kupitia hotuba hii ukurasa wa 11(V). Aidha, naliomba Shirika la *NHC* litekeleze adhma yake ya kujenga nyumba za kutosha kwa ajili ya kuuza na kupangisha kwa watu wa vipato mbalimbali Jimboni/Wilayani Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana *NHC* kwa kazi nzuri wanayoifanya na tunaiomba Wizara itusaidie kutatua tatizo la masijala ya Ardhi Wilayani Sengerema

kutokuwa na vifaa pamoja na *master plan* yetu kutopitishwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Kwanza naunga mkono hoja hotuba hii asilimia mia moja (100%), ila nina maoni kuhusu mambo yanayojitokeza Wizara ya Ardhi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya ardhi, watumishi wasio waaminifu waliopo Wizarani na kwenye Halmashauri wanashiriki kwa makusudi kusababisha migogoro kwa kutoa viwanja zaidi ya mara moja kwa watu tofauti pia kushiriki kuuza viwanja halali kwa waliopewa kwa watu wengine. Pia baadhi ya watendaji wa Wizara hushirikiana hata kuhalalisha *document* zisizo halali ili kudhulumu watu waliopewa kihalali na kuwafanya wananchi wa kawaida kukosa haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu gharama za kulipia ardhi. Katika suala hili, kumejitokeza malalamiko juu ya upandishwaji wa gharama za kujua anayemiliki kiwanja (*search*) na gharama za usajili. Hili litazamwe upya ili wananchi wa kawaida wasiumie kutokana na uwezo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Kigamboni, suala hili Serikali ilitazame kwa umakini kwa kuwa wananchi wanaumizwa kwa kutotekelezwa kwa mradi kwa takribani miaka minne sasa. Wananchi wanateseka, wamepata

hasara kwa kusimamisha ujenzi wao, mradi ni mzuri sana ila maandalizi ya utekelezaji wake hauko sawa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la bomoabomoa. Napongeza juhudi zinazoendelea za kuhakikisha sheria zinaheshimiwa. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri *(keep it up).* Tatizo lililopo ni watendaji kutozuia mapema ujenzi pale wanapoona uvunjifu wa sheria unapoanza kutokea, tusisubiri wananchi wajenge halafu tubomoe baadaye. Maafisa Mipango Miji ambao maeneo yao yanakiuka taratibu kwa muda mrefu wachukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kuondolewa kuongoza Idara pale anapoongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, uwepo wenu na utumishi wenu pale Wizarani umeleta tumaini jipya kwa Watanzania na maendeleo makubwa na kimbilio na ahueni kwa wanyonge wanaonyimwa haki kuhusiana na masuala yanayohusu ardhi, nyumba na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ije na mkakati ambao utarahisisha upatikanaji wa hati za nyumba na mashamba. Utaratibu wa hati za kimila nao unasuasua sana, ungeweza kusaidia, mpango ulioanzishwa na MKURABITA wa kurasimisha mali, nyumba na ardhi za wanyonge nao unasuasua sana. Pengine Mheshimwa Waziri ungependa kuelezea kidogo hatua iliyofikiwa na mpango huu wa MKURABITA wakati una *wind-up.* Utaratibu uliotumika kwa *un-surveyed settlement* katika eneo la

Gongolamboto na Ukonga wa kutambua makazi kama yalivyo kupitia ramani zilizotokana na kupigwa picha toka angani (kwa ndege) ungeweza pia kutumika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa ardhi katika Wilaya ya Ulanga, Mkoani Morogoro unafadhiliwa na *TANAPA* kwa ajili ya mnyama mmoja anayeitwa Sheshe, utafutiwe dawa nzuri ya kudumu haraka inavyowezekana. Mimi ni mdau kwa kuwa nina shamba la mpunga maeneo hayo na mwaka huu (mwezi huu) nimevuna magunia 250 yenye debe nane kila moja.

Mheshimiwa Ngasongwa pia ana shamba kubwa na msimu huu (hivi sasa) amenunua *combine harvester* ambayo imesaidia sana wakulima wa eneo lile kwa kupunguza *drudgery* ya kuvuna mpunga. Mgogoro huu ulipelekea watu sita kuuwawa kufuatia mapigano baina ya wananchi (wakulima na wafugaji) na Polisi (wa Serikali na wa *TANAPA*). Wananchi walipewa fursa ya kulima mara ya mwisho msimu huu na hivi tunavyoongea wamepewa notisi wawe wamevuna mazao yao ifikapo mwisho wa mwezi wa August mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utata wa mipaka halisi ya eneo la hifadhi husika, mpaka leo wananchi hatuna uhakika mpaka halisi uko wapi ili wale ambao hawako ndani ya hifadhi waweze kupanga kilimo cha msimu na waweze pia kupanga aina ya uwekezaji wanaoona unafaa. Eneo linalohusika ni kubwa sana kiasi kwamba lote likichukuliwa, hatua hii itakuwa inapingana na azma ya Serikali ya kuufanya Mkoa wa Morogoro uwe *National Granery* kwa zao la mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mikoa/maeneo ambayo yana *population* kubwa sana kama Mwanza, je, Serikali haioni umuhimu wa kuja na ubunifu wa kutenga ardhi maalum katika maeneo ya nchi hii yenye *lowest population density* ili waweze kuhamishiwa huko kama ilivyowahi kufanyika kwa wakazi wa Kisiwa cha Ukara (Wilaya ya Ukerewe) pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi yake, kwa mwaka 2012/13 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naanza kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka (Waziri), kwa uwasilishaji na utendaji wake makini na wenye ujasiri tangu alipochaguliwa kuiongoza Wizara hii. Napenda kumpongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Goodluck Ole Medeye, kwa ushirikiano mzuri nasi na utendaji wake bila kuchoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Hotuba hii kukidhi mahitaji, lakini napenda nami nitoe mchango wangu kwa uchache, kwa maeneo machache pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba hii nimeona kuna mpango uliobuniwa na kuanzishwa ili kutoa msukumo

wa upimaji wa ardhi kwa kutumia *GPS* na Wizara imesisitiza sana Halmashauri zote nchini zihakikishe zinatenga fedha kwa ajili ya zoezi hili na ununuzi wa vifaa vya kisasa. Naomba Waziri afikirie upya agizo hili kwa kuzingatia uhalisia na uwezo wa Halmashauri zetu kwa sasa. Pamoja na umuhimu wa upimaji kwa maeneo mengi, lakini ikumbukwe kuwa Mikoa ya Lindi na Mtwara ina upekee kwa kuwa hivi sasa limekuwa kimbilio kubwa kwa wawekezaji kutokana na uvumbuzi wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ardhi katika nchi yetu ni kubwa sana, ipo haja sasa ya Serikali kuangalia upya namna ya kuboresha eneo hili kwa kuwa waathirika wakubwa ni wananchi ambao wana kipato cha chini. Nashauri Serikali iendelee kuboresha Mabaraza ya Ardhi ambayo yamesaidia kupunguza migogoro, lakini yanazidiwa na uwingi wa mashauri na pia kutokana na upungufu wa vitendea kazi kama Hotuba ya Waziri ilivyoonesha katika ukurasa wa thelathini, jitihada ziongezwe pia kwa kuhakikisha Mabaraza haya yanatoa haki kwa wakati. Mara kadhaa wananchi wamekuwa wakilalamika kuwa kuna ukiukwaji mkubwa sana kwa haki hasa kwa wale wasio na uwezo, lakini pia Mabaraza haya yamekuwa yakitumika kama chombo cha unyonyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie kwa makini sana utaratibu wa umiliki wa ardhi, kutokana na kuwa na malalamiko lakini pia lipo tatizo la uhamishwaji ovyo wa mali za umma hasa yaliyokuwa Mashirika au Taasisi za Serikali. Ikiwezekana, yawe yanatolewa matangazo kuwa umiliki unatoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mwingine kama wanavyofanya nchi nyingine. Hii

itaongeza sana uwazi na kuondoa yale yasiyo ya lazima kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba hii imeonesha kuwa zipo changamoto nyingi, mojawapo ikiwa ni utunzaji wa kumbukumbu, ambapo Serikali inakusudia zitoke mfumo usio unganishi kuwa ki-elektroniki. Hii ni muhimu na naiomba Serikali iweke mkazo na iharakishe ili kuondoa ghushi nyingi zinazojitokeza katika nyaraka za umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji inaweza kwisha au kutatuliwa kwa kuharakisha zoezi la upimaji wa ardhi. Hotuba ya Waziri, aya ya 43, amezungumzia upimaji wa vijiji. Ninaloliona ni kuwa kasi ni ndogo sana kupita kiasi cha kawaida. Lazima tutenge fungu la kutosha ili kuondoa kadhia hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la bomoabomoa limekuwa ni kero ya kwanza na ni la kipaumbele kabisa kwa nchi nzima, maana malalamiko ni makubwa. Naiomba Serikali isikie kilio hiki kwa kuzingatia haki. Mathalani katika Jimbo la Kilwa Kaskazini, wananchi wamejenga kabla hata Sheria iliyotajwa haijatungwa na kuridhiwa na Bunge ama kuidhinishwa na mamlaka husika.

Hili linathibitishwa na historia ya nchi yetu kwamba, Wakoloni wamekuwapo kuanzia Karne ya 18 na kabla ya hapo walikuwepo Waarabu na Washirazi katika maeneo ya Kilwa. Hivyo, sikubaliani kabisa kuwa uwepo wa wananchi hawa katika maeneo haya ni kuvunja sheria kwa tafsiri kwamba wamekuwepo kabla. Haitoshi, itakuwa pia Katiba inakiukwa kama Ibara ya 13(1) inavyotamka kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya

ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Mwezi Februari, 2011 tumejadili na kuridhia Hotuba ya Rais, ambayo aliisoma wakati wa Uzinduzi wa Bunge la Kumi. Katika vipengele kumi na tatu ameainisha kuwa Serikali itafanya kila iwezalo kuwawezesha wananchi. Je, wananchi wanawezeshwa vipi kwa kuwavunjia nyumba zao na kupoteza mali zao bila ya fidia? Naiomba Serikali katika hili itumie busara zake na usikivu wake na kuwasaidia wananchi na kuokoa mali zao ambazo wamezipata kwa jitihada kubwa na za muda mrefu ili tusiwakatishe tamaa na kuwaweka katika hali tata. Ifikiriwe namna hata ya kuwapa kifuta machozi kwani upande wa Serikali pia umechangia wao kuingia katika tatizo kwa maana Uongozi na Watendaji wa chini hawasimamii ipasavyo Sheria husika na kuruhusu wananchi kujenga holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia suala la migogoro ya ardhi isiyokwisha, ipatiwe ufumbuzi kwa njia ya haraka kwa maana tuimarishe upimaji na nyenzo za uhifadhi wa kumbukumbu za ardhi nchini. Sheria husika zisimamiwe kwa kuwa yote yanatokana na kutosimamiwa vizuri kwa sheria. Ofisi za ardhi ziongeze muda wa kutoa huduma hasa Makao Makuu. Kwa mfano, lipo eneo la Mwembe Yanga, Wanachama wa *Club* hii wamekuwa na mgogoro usiokwisha kwa miaka zaidi ya ishirini na tano sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la wageni kupewa na kumilikishwa ardhi limekuwa kubwa sana na likiachwa kama

lilivyo, litahatarisha usalama wa nchi yetu. Hii izingatiwe kuwa ardhi ni kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ucheleweshaji wa makusudi katika ulipaji wa fidia kwa wananchi pale ambapo inabidi kupisha miradi ya uwekezaji au miundombinu. Serikali iweke mfumo utakaoweka uwazi na uharaka wa wananchi kupata fidia na stahiki zao bila ya usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nashukuru na nawatakia kheri wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SEIF SELEMANI RASHID:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napongeza juhudi za Wizara katika kuendeleza makazi na usimamizi wa ardhi yetu nchini, ikiwa ni pamoja na kuongeza eneo la bahari, kuheshimu maeneo ya fukwe za bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwasilishe kutoridhishwa na Ofisi ya Kamishna wa Ardhi kwa kushindwa kutatua matatizo niliyoyawasilisha kuhusu migogoro ya umiliki wa maeneo Rufiji, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kanisa ndani ya eneo la shule kwa kupindisha ramani na kuweka nyingine mpya. Nyongeza ya hii niliwasilisha kwa maandishi, malalamiko ya Wanakijiji wa Nyamwage – Rufiji, ambao walitoa eneo kupitia Serikali ya Hamashauri toka 2005/2006 na hadi leo kwanza, wanakijiji hawa hawajalipwa fidia na pili, eneo hili halijaendelezwa kama walivyoomba eneo hilo ambalo *TIC* ilishalitoa kwa mwekezaji ambaye hayupo kwenye eneo husika. Mwekezaji huyo aliomba

kupata eneo kwa kilimo cha mahindi na hadi hivi sasa zaidi ya miaka sita hakuna cha maana kilichopo hapo; lakini pia kuna eneo dogo linaanza kupandwa miti aina ya mitiki, kinyume na kusudio la Mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iingilie kati na kutoa maamuzi sahihi kwa maslahi ya Wananchi wa Rufiji hasa maeneo hayo ya Utete na Nyamwage.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara iendeleze juhudi za kumilikisha ardhi kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na miliki za mashamba. Naiomba Wizara na isimamie utoaji wa usajili wa vijiji kwa haraka inavyowezekana. *NHC* lazima irudi kwenye lengo la awali la kuwawezesha wa kipato cha chini, wengi wao wakiwa Watumishi wa Serikali kumiliki nyumba na au kutoza kodi za pango yenye kulingana na mapato yao. Kodi ya laki tatu au nne ni kubwa kwa wafanyakazi na watu wa kipato cha chini. Naiomba Serikali itatue tatizo la ardhi Rufiji kama nilivyoeleza hapo juu, eneo la Shule ya Mapinduzi ya Utete lililomegwa kwa kujenga Kanisa na shamba katika Kijiji cha Nyamwage Kata ya Mbwera Rufiji lililomilikishwa kwa mwekezaji ambaye hajaendeleza kwa miaka sita sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru ahsante.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa Serikali ni katika eneo la Serikali na hasa Shirika la Nyumba la Taifa, ambalo limefanya katika eneo la ujenzi wa nyumba za

kisasa na za bei nafuu na kuziuza kwa wananchi na hasa wenye kipato kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira hii nzuri ya Serikali na Shirika la Nyumba la Taifa katika kumpatia Mtanzania nyumba hasa wa maisha ya kawaida hayatatimia kwa utaratibu uliowekwa na Shirika na Serikali kwa ujumla wa kutoza kodi ya ongezeko la thamani katika uuzaji wa nyumba zake ambazo nyingi zimelengwa kwa Watanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ni vizuri wakaangalia namna ya kushirikiana na Wizara ya Fedha, wakaangalia uwezekano wa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani ili nyumba zitakazouzwa bei ishuke ziweze kununuliwa na wananchi wengi ambao ndiyo Serikali na Shirika la Nyumba limewalenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine kwa Serikali ni kuona katika utaratibu ambao Shirika la Nyumba limejiwekea na mabenki katika utoaji wa mikopo kwa wanunuzi wa nyumba hizi ni vizuri Serikali ikaona jinsi gani mabenki yatashawishiwa kushusha riba katika mikopo hiyo. Riba ya asilimia 15 au 17 kumtoza mkopaji wa nyumba ni kubwa sana na itamfanya mnunuzi kuinunua nyumba hiyo kwa gharama kubwa na kumwumiza mnunuzi huyo. Riba za benki kwa mkopaji wa nyumba ingefaa iwe asilimia 10 au 12 kwani mkopaji huyu hakopi kwa biashara bali ni makazi; hivyo basi, kama mkopaji wa nyumba ya kuishi asilimia isiwe 15 au 17 na iwe asilimia 10 au 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi ambavyo amekuwa akijitahidi mno katika utendaji wa kazi katika Wizara yake na ifuatayo ni michango yangu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya au Mkoa kuanzia kwenye Kata wanapuuza haki za wanyonge na kukumbatia wenye fedha. Hii ni hatari kwa hatima ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri upimaji ardhi za vijiji na mwananchi mmoja mmoja utaongeza thamani ya ardhi kwa vile kila mtu atapenda kuiendeleza ardhi yake, itasaidia pia kumwezesha mnyonge kuthaminiwa na vyombo vya fedha (mikopo).

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo mali ya msingi kwa mwananchi huyu asiye na kitu kingine chochote. Sasa wananchi wameanza kuuza ardhi kwa wafugaji na wenye fedha na wanabaki hawana kitu, hii yote ni kwa sababu hawana fursa ya kukopa au kupata mtaji kwa ajili ya kuendesha maisha katika hali ya ushindani iliyopo na akishauza anamaliza vijisenti, anaathirika na hata kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ije na utaratibu ambao utamfanya huyu Mwananchi asiuze ardhi kirahisi, pawepo urasimu ambao hatimaye utamshauri au kumfanya asiuze au aweke ubia na anayetaka ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Nyumba, kwanza, naomba waje Nkasi tutawapa ardhi Namanyere.

Naipongeza *Management* ya Shirika kwa kazi nzuri inayofanywa na Shirika hili. Naomba Serikali iondoe kodi kwenye uuzaji wa nyumba hizi ili wananchi waweze kununua kwa bei ambayo ina unafuu, kwani ukiongeza kodi unaongeza gharama za uuzaji na hivyo ni mzigo kwa wananchi ambao ndiyo walengwa katika ujenzi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashirika mbalimbali ambayo yamekuwa na ardhi muda mrefu hawatumii kwa malengo yaliyokusudiwa. Ichukuliwe na wananchi wapewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi kubwa kubwa kwenye maeneo yenye shida ya ardhi, tafadhali wananchi kwanza kabla ya wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Baada ya kuunga mkono, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara na hususan Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* ihakikishe kwamba, kipaumbele kinatolewa kwa kujenga nyumba za Viongozi wa Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia uzoefu wa Shirika letu la Nyumba la Taifa, kwa kujenga nyumba zenye hadhi na gharama nafuu, kwa kuzingatia viwango kuanzia ramani zilizo za kisasa ambazo kama zikijengwa kwa

wananchi itakuwa ni rahisi kukopi ubora huu na kusambaa Mikoa na Wilaya Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile uhitaji wa makazi na ofisi ni wa muhimu kwa maendeleo na pia kulisaidia Shirika letu la Taifa la Nyumba kwenye soko lililo tayari na hivyo kulijengea uwezo ili liweze kutoa huduma ya nyumba bora kwa Tanzania nzima badala ya kujikita miji mikubwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Sumbawanga na Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Kalambo, wananchi wengi nyumba zao hazina hati, wameishia kupata *offer* kwa muda mrefu sana ambazo hazina manufaa kwani hazitambuliki kisheria hata pale ambapo anatakiwa kupeleka hati ya nyumba itumike kama dhamana kuweza kum-*bail out* mtu anayekabiliwa na kesi. Hali hii haishii tu kwenye Mahakama ambazo hazitanbui hati ambazo hazijakamilika kisheria kwa maana ya *offer* badala ya *title deed* hata taasisi za fedha hazitambui *offer* kama *security.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii haikubaliki kwani wananchi wanashindwa kufaidika na jasho la kazi za mikono yao katika kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi ya ardhi inatokana na kutokupimwa kwa ardhi na mashamba ili kuainisha ardhi na matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kodi hii ni ndogo sana na hivyo itachukua muda mrefu sana mpaka Wilaya zote za Tanzania ziwe zimefikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wimbi kubwa la wafugaji hususan kutoka Mikoa ya Wafugaji ya Shinyanga kukimbilia Mikoa ya Rukwa na Katavi na hususan Wilaya Mpya ya Kalambo, naiomba Wizara itoe kipaumbele kwa kuhakikisha ardhi ya Wilaya hii inapimwa na kubaini matumizi bora ya ardhi katika Wilaya hii ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalazimika kuomba majibu ya dhati kutoka Wizara hii baada ya kuuliza swali langu kuhusiana na mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka Shamba la *NARCO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba hili lilitolewa na wananchi bila kupewa fidia yoyote ile kwani walikuwa na imani kubwa na Serikali yao, kwa kuwa walishirikishwa kwa kuruhusiwa kuendelea kulima katika mashamba haya na huku wakipata elimu juu ya kilimo cha kisasa. Wananchi wa Vijiji vya Katapulo, Mbuluma na Mkowe, waliendelea kufaidika na elimu hii na hivyo kutokuwa na haja ya kutaka fidia kutoka Serikalini isipokuwa Vijiji vya Mkowe na Mbuluma waliopewa fidia. Wananchi wa Kijiji cha Katapulo hawakupewa fidia na wala hawahitaji fidia kwani wanachotaka ni kurudishiwa ardhi yao waweze kuitumia kwa kilimo cha ufugaji. Bahati mbaya sana ardhi hii amekodishwa mwekezaji ambaye badala ya kufugia analima na kufuga kidogo sana, kazi ambayo wananchi wanahitaji ardhi hii ili waweze kutumia kwa shughuli kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wameshindwa kutoa haki kwani nao ni sehemu ya

mgogoro. Nilienda na mtaalam aliyetumwa lakini akashindwa hata kubaini mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iingilie kati ili ardhi hii iwarudie wananchi waendeleze shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuvuna miti waliyopanda.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametufanya leo kukutana hapa katika Bunge lako Tukufu tukiwa wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali ambayo ametupatia Mwenyezi Mungu na kama tutatumia vizuri tunaweza kupiga hatua mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado makazi ya watu, hayajakaa vizuri, kwani hata miji yetu bado ipo ile ile ambayo tumerithi. Sasa ipo haja ya kuanzisha miji mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la watu kuhamia katika Jiji la Dar es Salaam, inadhihirisha kuwa mipango miji yetu bado ni ya kale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunataka tuwe na mipango miji mizuri, basi tuanzishe miji mbadala, yaani miji mipya na Serikali ninaiomba kuwa katika kila eneo la vijiji, wapatiwe viwanja vya kupimwa ili wawekewe pindi watakapopata uwezo wajenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pango la nyumba bado ni mtihani. Kumekuwa na unyanyasaji wa wapangaji kwa kutokuwa na Sheria ya Upangaji, kila siku wapangaji wanazidishiwa kodi na kuambiwa walipe kwa mwaka

mzima, ukiangalia uwezo wa mpangaji ni mdogo, nashauri kuwepo na Sheria ya Upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Timu ya Wataalam wa Wizara, inayoongozwa na Katibu Mkuu mahiri, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia vizuri rasilimali hii muhimu ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi ni rasilimali muhimu kwa wanyonge wanaoishi vijijini ni muhimu kwa Wizara kutoa elimu na miongozo nchi nzima, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ngara kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Ardhi ili wananchi wafahamu vizuri haki zao kuhusu umiliki wa ardhi. Wasiwasi wangu ni kwamba, elimu hiyo haijatolewa kwa Wananchi wa Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Ngara wanangojea kwa hamu kumilikishwa ardhi kupitia Hati Miliki za Kimila ili wafaidike na Mpango wa MKURABITA, ambao utawawezesha kurasimisha mashamba yao na wataweza kupata mikopo kutoka kwenye mabenki kwa kutumia Hati Miliki za Kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashari ya Ngara ina upungufu mkubwa wa Wataalam wa Ardhi ambao wangesimamia matumizi bora ya ardhi. Nitapeleka maombi ya Wataalamu huko TAMISEMI kama nilivyoshauriwa na Naibu Waziri, lakini nilidhani Wizara hii

ndiyo yenye Wataalam na ndiyo yenye *mandate* ya kuziwezesha mamlaka za upangaji zikiwemo Halmashauri za Wilaya na Vijiji kupanga, kutekeleza na kufuatilia uendelezaji wa mipango ya makazi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimefurahia mchakato wa Wizara wa kukamilisha uanzishwaji wa Chombo (Mfuko wa Fidia ya Ardhi) ili Chombo hicho kisimamie utoaji wa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje. Ardhi ndiyo tegemeo la wanyonge wa Tanzania baada ya madini kuendelea kuporwa na wawekezaji kutoka nje. Serikali imeshindwa kusimamia vizuri uchimbaji wa madini, tusifanye makosa kwa upande wa ardhi. Nauamini Uongozi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wakenya, Waganda na Wanyarwanda, wananyemelea ardhi yetu; kama tutawapatia ardhi basi iwe kwa nia ya ubia na Watanzania Wazalendo na isiwe kwa miaka 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngara kuna migogoro ya ardhi kati ya wafugaji kutoka nje ya nchi na wakulima. Ninaamini Wizara ikitusaidia kukamilisha matumizi bora ya ardhi baada ya kupata vyeti kwa vijiji vyote 73, tutaondokana na tatizo la wahamiaji haramu wanaovamia vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngara kuna mgogoro wa mpaka kati ya Burundi na Tanzania katika Kijiji cha Kasange, Kata ya Kirushya. Naiomba Wizara au Serikali, ishughulikie tatizo hilo la mpaka kwa kuwa na mazungumzo na Serikali ya Burundi ili kuimarisha alama za mipaka.

Nilimwandikia Waziri barua ya maombi ya Baraza la Ardhi mwaka jana, bado sijapata jibu. Wananchi wa Ngara wana kesi nyingi za ardhi na inabidi walalamikaji na walalamikiwa wafunge safari kwenda Wilaya ya Chato, kilomita 150, kusikiliza kesi zao. Tuna migogoro na Nyarubanja kama ya Bukoba na Karagwe. Tunaomba tupewe Baraza la Ardhi.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala wa ardhi, kila mwananchi ana umuhimu wa kumiliki ardhi katika uhai wake na kuiendeleza kwa maslahi yake na Taifa kwa jumla. Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mkakati gani au mpango gani wa muda mfupi, wa kati na mrefu, wa kuwawezesha wananchi kuanzia miaka 18 kumiliki ardhi popote pale walipo?

Je, ni lini Serikali au Wizara itamtendea haki mwananchi mnyonge ya kumlipa fidia stahili pale anapoondolewa kwenye ardhi ambayo ameimiliki au ameishi na kuiendeleza kwa miaka mingi?

Je, Wizara ina kauli gani kwa Wananchi wa Kigamboni; waendelee kujenga au wasijenge na sasa wafanye nini?

Wizara ina mkakati gani wa kupima ardhi na kupanga matumizi bora ya ardhi kulingana na mahitaji ya wanadamu ili kupunguza matatizo ya ardhi?

Je, Shirika la Nyumba lina mpango gani wa kuyakarabati majengo yake ili yaende sambamba na upandishaji wa kodi kwa kila mwaka ambazo hazizingatii gharama ya matengenezo ya mpangaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuwashukuru Waziri na Naibu Waziri, kwa kuboresha uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi vijijini wamekuwa wakichukuliwa ardhi yao bila ridhaa yao kwa sababu za kujenga shule, barabara, zahanati, vituo vya afya na kadhalika. Wananchi wengi wamechukuliwa ardhi yao bila hata kupewa ardhi nyingine mbadala na hivyo kukosa mahali pa kulima na makazi. Mifano ya wananchi waliotwaliwa ardhi yao bila fidia ya fedha wala ardhi mbadala ni Wananchi wa Vijiji vya Nansimo, Neruwa, Bulamba na kadhalika. Naomba nipate majibu ya kina ni jinsi gani wananchi hao watapatiwa fidia au ardhi mbadala. Sera ya Ardhi inasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ardhi ya Wananchi wa Kijiji cha Bunere ilitwaliwa kwa mabavu na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kulifanya kuwa eneo la mazoezi ya kivita ndani ya kijiji. Huu ni mwaka wa sita sasa, nimekuwa niikitaka Serikali na hasa kupitia maswali hapa

Bungeni na kuomba Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kuwa Jeshi lijiondoe katika ardhi ya wananchi kwani kuna mabaki ya mabomu yameachwa pale na madhara tayari yalishatokea kwa mwananchi mmoja wa Kijiji cha Namhula kuliokota na kumlipukia na kupoteza maisha. Nipate maelezo ni lini Jeshi litaachia ardhi ya wananchi kwani kilichowaleta hao Wanajeshi ni madini yaliyoko pale kwa kisingizio cha mazoezi ya kivita. Mazoezi ya kivita katikati ya kijiji ni mazoezi gani hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Kibara kilipandishwa hadhi na kuwa Mji Mdogo (Mji wa Biashara) na hivyo ardhi yake ikapimwa kwa kusimamiwa na Kamishna Ardhi kama Ardhi ya jumla *(General Land).* Aidha, mwaka 2010 mwanzoni Kibara iligawanywa katika vijiji vinne vya Kibara A, Kibara B, Kibara Stoo na Mwibara. Baada ya kutoka hadhi ya Mji Mdogo (Mji wa Biashara) na kuwa vijiji, Viongozi wa Serikali za Vijiji hivyo wameamua kupima ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi (Na. 5) ya Mwaka 1999. Kitendo hiki kimeleta mgogoro kati ya Kijiji cha Kibara na Idara ya Ardhi, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Katika mgogoro huu, Afisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya amewazuia Viongozi wasiondoke kupima na kugawa ardhi kwa wananchi wake kwa madai kwamba, ardhi hiyo ipo mikononi mwa Kamishna wa Ardhi. Sheria ipi ya Ardhi itumike katika kijiji hivyo ili kuepusha migogoro ya ardhi vijijini? Naomba nipate maelezo ya kuridhisha katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya katika mazingira yenye changamoto nyingi. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya ardhi inayosemekana imeuzwa kwa wawekezaji wa nje na wa ndani katika mazingira ya udanganyifu hususan vijijini na kwenye ukanda wa ufukwe kuanzia Tanga kwenye mpaka na Kenya mpaka Mtwara. Naomba kufahamu ni akina nani waliomilikishwa (kwa majina na *acreage* zao) na je, ni kweli kuwa maeneo makubwa yameuzwa kiasi cha kutia wasiwasi? Kama ni kweli je, kuna uwezekano wa kuwanyang'nya hao wawekezaji waliohodhi ardhi na walioipata kwa njia za kuwarubuni wananchi; kwa sababu hivi sasa wananchi waliogundua kuwa walirubuniwa wanalalamika?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza hatua za kubomoa majengo yaliyojengwa kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kisheria. Ili kukomesha hili, tunapendekeza nyumba zibomolewe na maeneo ya wazi yarudie hali ya asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara iweke mikakati maalum kwa ajili ya maeneo ya ardhi ya uzalishaji kwa vijana kupitia Serikali Vijijini na Halmashauri za Miji. Hii itawezesha vijana wetu kusaidiwa kuendesha miradi ya uzalishaji mali na kujiajiri ya kilimo, ufugaji, mifugo, samaki, usindikaji na shughuli nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mkakati huu utenge asilimia ya ardhi kwa ajili ya wanawake chini ya mkakati

mahususi wa kuwawezesha wanawake kupata ardhi kwa kupewa kipaumbele mkianzia na maeneo ya vijijini. Hii itawawezesha wanawake kuanzisha vikundi vya uzalishaji wa pamoja au mmoja mmoja na hii itahamasisha ukuaji uchumi vijijini kwa haraka zaidi, kwa sababu wanawake ni wazalishaji wakuu. Mkakati huu utarahisisha hata utoaji wa huduma kwa makundi haya ili kuwaboreshea shughuli zao na kwa hiyo kuleta maendeleo ya haraka na kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza tena sana na kuunga mkono hoja.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mgogoro wa ardhi kati ya Wananchi na Uongozi wa Kanisa la EFATA, ambapo wananchi wananyang'anywa ardhi yao bila haki kufuatwa na inaonekana Serikali inafumbia macho. Tafadhali, lazima Serikali ilitazame suala hili kwa makini ili haki itendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufugaji holela, wafugaji na mifugo yao wanaharibu ardhi wala hakuna anayeona dosari hiyo na kukemea; mifugo mingi kuliko hata ardhi ya kufugia. Tafadhali, Sera nzuri za Kutunza na Kuendeleza Ardhi ziheshimiwe na wawepo watu wa kusimamia sheria za kutunza au uendelezaji ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba waje Sumbawanga kujenga, tena waende na kule Namanyere Wilayani Nkasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUTABITA ianze kwenye ardhi ili wananchi waweze kutumia mabenki waboreshe maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima ardhi tuliyonayo tuifahamu ukubwa na matumizi yake ili tupange ipi itumike kufugia, ipi itumike kwa kilimo, ipi itumike kwa ujenzi wa nyumba, ipi ni akiba kwa wawekezaji kutoka nje, ipi itumike kwa Miradi ya Kimkakati Kitaifa kuendeleza wawekezaji wazalishaji na ipi akiba kwa mtazamo wa matumizi ya baadaye.

**MHE. LAMECK O. AIRO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono Bajeti hii ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba Serikali iingilie kati ya upangishaji nyumba kwani wapangaji wanapata shida kubwa sana. Mtu anapoajiriwa, mwenye nyumba anataka mkataba wa mwaka mmoja wakati huyu mpangaji ndiyo ananza kazi, naomba Serikali iingilie kati kuhusu bei ya upangaji na kuhusu ulipaji wa miezi 12. Iwepo Sheria ya mwenye nyumba kudai lazima kodi ilipwe mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Mwanza umezungukwa na milima yenye mandhari nzuri sana. Milima yote ya Mwanza imevamiwa na kujenga majengo kiholela. Nashauri Serikali ipime ile milima kisha iwalipe wananchi waliojenga bila utaratibu, wagawiwe wenye uwezo wa kuweka majengo mazuri ili Mji wa Mwanza uwe na mandhari nzuri na kuwavutia watalii wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *NHC* iwekeze katika Wilaya ya Rorya kwani ni Wilaya mpya, Wakuu wa Idara hawana majumba ya kuishi. Naomba sana *NHC* waje wawekeze katika Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri atembelee Rorya kwenye Kata ya Ikoma, Kijiji cha Ikoma, kuna migogoro ya ardhi na tayari baadhi ya wananchi wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rorya ina *centre* kama kumi kubwa za Shirati, Utegi, Ocuma, Buturi, Kinesi, Kogaja, Maumau, Ratia, Masonga, Kirongwe na Randa, tunaomba upimaji ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali muhimu sana kwa maisha ya binadamu. Ardhi ni msingi wa maendeleo yote ya kiuchumi na kijamii ya binadamu. Mpango wa matumizi bora ya ardhi ni jambo kuu na la msingi kutekelezwa ili kuhakikisha maendeleo endelevu yanakuwepo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali iongeze kasi ya kupima viwanja katika miji na vijiji vyetu ili wananchi wasiendelee kuvamia maeneo *(squatters).*

(ii) Maeneo ya vijiji yapimwe na kugawiwa kulingana na matumizi yaliyopangwa. Wafugaji na wakulima

wagawiwe maeneo maalum na wafundishwe stadi za kuzalisha na kuendeleza shughuli za maisha yao bila kuhamahama. Maeneo hayo yapimwe na kupewa hati miliki. Tukishughulikia suala hili vyema, tutapunguza tatizo la jamii za kifugaji kuhamahama.

(iii) Sheria ya Ardhi irekebishwe ili iwiane na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, inaelekeza kuwa, wananchi wanaohama kupisha ujenzi wa migodi ya uchimbaji wa madini, wafidiwe *(compensation)*; wajengewe makazi mapya *(relloction);* na wahamishiwe kwenye makazi mapya *(resettlement).* Wizara ya Ardhi na Wizara ya Nishati na Madini zishirikiane kurekebisha suala hili.

(iv) Watumishi na Watendaji wa Wizara ya Ardhi na Idara za Ardhi kwenye Serikali za Mitaa wadhibitiwe kwani wao ndiyo wanaosababisha migogoro mingi katika Sekta ya Ardhi. Watendaji hawa hujigawia viwanja vingi na kuuzia wengine. Watendaji wengi huwadhulumu wasio na uwezo na hasa wajane na wasio na uelewa mzuri wa masuala ya ardhi.

(v) Wizara isaidie kuondoa migogoro iliyopo katika Jimbo la Igunga. Katika Jimbo hili wananchi wengi Mjini Igunga wamedhulumiwa viwanja vyao. Maeneo yao yamepimwa lakini wengi hawakupewa fidia na wakalazimika kuhamia nje ya mji na kuanzisha makazi holela tena. Naomba Wizara ifuatilie dhuluma hizi.

(vi) Naishauri Wizara kwenye bajeti ijayo ya 2013/2014, itenge fedha za kutosha kufanya *mapping,* upimaji wa uchoraji wa ramani za hali ya nchi *(Topographic Maps).* Ramani zilizopo zimepitwa na wakati kwani zilitayarishwa

miaka ya 1950 na 1960. Wizara iandae Programu Maalum, itafute mradi wa kupima na kuchora ramani hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya *Surveys and Mapping* ipewe kazi ya kuandaa Mradi Kamambe wa Kitaifa wa kupima na kutayarisha ramani hizi muhimu kwa maendeleo ya nchi ili Wizara iweze kuishauri Serikali kutekeleza Mradi huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo, naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuirekebisha Wizara hiyo iwe ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. UMMY ALLY MWALIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa Sera, Mipango na Mikakati ya Nchi katika Sekta hii muhimu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa faida ya Watanzania hasa Wanawake wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutatua migogoro ya ardhi katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji langu la Tanga, nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Ole-Madeye, Naibu Waziri wa Ardhi, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kufuatilia au kushughulikia mgogoro wa ardhi katika Kata

ya Pande (Pande B). Pia amesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua mgogoro wa ardhi katika Wilaya ya Pangani na Mkinga (Kata ya Manza).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara iendelee kuyafanyia kazi masuala mbalimbali yaliyojitokeza na yanayojitokeza katika Jiji la Tanga, Mkinga na Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuomba Wizara ishughulikie kwa haraka maombi ya Halmshauri ya Jiji la Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Halmashauri ya Mji wa Korogwe na Korogwe Vijijini, juu ya kufuta hati za umiliki za mashamba ya Mkonge yaliyotelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itawezesha kwa kiasi kikubwa ardhi hiyo ipatiwe wananchi hasa wanawake ili waweze kuitumia kwa shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kazi nzuri na inayoonekana inayofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* katika kuboresha nyumba zake na kuwa na mipango ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa wananchi wa kipato kidogo. Haya yote ni matunda ya Uongozi bora wa Mkurugenzi Mkuu wa *NHC*, Bwana Nehemia Mchechu. Nitoe rai kwa *NHC* kuhakikisha nyumba nyingi zinajengwa kwa ajili ya makazi ya Watanzania wa kipato cha chini hasa wale wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Ardhi ya 1995 na Sheria za Ardhi (Namba 4 na Namba 5) za 1999 zinatambua na kusisitiza haki sawa ya wanawake na wanaume katika kumiliki na kutumia ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya ukweli huu bado Wanawake wengi wa Tanzania wananyimwa haki hii, aidha, kutokana na uwepo au kutumika kwa baadhi ya mila na desturi zinazowabagua wanawake au kukosekana kwa uelewa au elimu juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa Wizara kuwa na mipango na mikakati maalumu inayolenga kuchochea na kuwawezesha wanawake wengi hasa wa vijijini kumiliki ardhi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri anieleze ni mikakati gani imewekwa na Wizara kuhakikisha Sheria na Sera ya Ardhi juu ya haki za wanawake zinatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Vijiji na Kata hayawezi kufanya kazi zake vyema pale ambapo hakuna Baraza la Wilaya. Licha ya Serikali kupitisha na kuidhinisha uwepo au uundwaji wa Baraza la Ardhi la Wilaya Tunduru. Baraza hilo bado halijaundwa kwa maana ya kutokuwepo kwa watendaji, ofisi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa na kwa miaka mingi sana, mashauri yaliyopatiwa rufaa kutoka Mabaraza ya Kata yamekuwa yakipelekwa Songea – Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umbali (km 260) na ubovu wa barabara, wahanga wengi wamekuwa

wakipoteza haki zao kwa kushindwa kuhudhuria Baraza la Ardhi ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iiwezeshe Wilaya ya Tunduru kuanzisha shughuli za utendaji wa Baraza lake la Ardhi (W) kwa mpango wa dharura.

**MHE. ABDULSALAAM SELEMAN AMER:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nawapongeza sana kwa kazi wanayoifanya ili kuleta imani kwa wananchi na kwa Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko yangu ni juu ya Mashamba ya Mkonge yaliyotaifishwa tangu mwaka 1975. Baada ya Serikali kuyataifisha kwa nia ya kuyaendeleza kupitia Shirika la Mkonge, Mashamba hayo yalikuwa yakitoa ajira na kuwavutia wananchi ambao ndiyo chanzo cha kuja kwa wananchi katika maeneo hayo tena kabla ya Uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba mengi ya Mkonge yaliyopo Wilayani Kilosa ni mapori toka yabinafsishwe na kuvamiwa na wananchi tangu zamani baada ya Shirika la Mkonge Tanzania. Walijenga na kulima mazao ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba hayo kwa sasa yapo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, wanakodisha kwa wananchi kwa maslahi yao binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo mahususi kwa mwekezaji wa Shamba la Mkonge lililokuwa *Miyambo Estate*. Shamba hili linalimwa na wanachi wa vijiji vyote

jirani na Wakazi wa Kilosa Mjini. Suala la Shamba hili lilifika Ofisini kwa Waziri wakati huo Waziri alikuwa Mheshimiwa John Chiligati, 2000 – 2005. Mheshimiwa Chiligati, alishawahi kufika eneo husika na kuahidi kulishughulikia kwa haraka na alitoa ruhusa wananchi waendelee kulima mpaka ufumbuzi utakapopatikana. Wananchi walifurahi na waliweza kulima hadi msimu ulioishia Juni, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi huu wa Julai huyo mwekezaji alikuwa na Waraka wa kuwataka wananchi wote waliolima waondoke na kusababisha hao wananchi kulalamika. Nadhani huu utakuwa mzozo mkubwa sana na kuacha familia zaidi ya 2000 kukosa maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara au Naibu wake ili aweze kuongea na mwekezaji huyo, ikiwezekana Serikali imwombe angalau hata robo ya shamba hili wapewe wananchi waweze kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuja kwa wawekezaji ni maendeleo kwa nchi yetu katika kutoa ajira pia. Ningeomba hao wawekezaji wapewe maeneo ambayo hayajaguswa ni mapori, waweze kuyafyeka wao wenyewe na kufufua mashamba mapya ili kuondoa mzozo na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, historia itajirudia tena kwa wakati, kupitia watumishi tulionao maofisini, kwani maskini hata alichonacho atanyang’anywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoloni alikuka kututawala Tanganyika tukafaulu kumtoa kwa wema kupitia Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, 1961 akafunga virago akaruka kichura kurudi kwao Ulaya. Katika historia kujirudia inaingilia kwenye uwekezaji na hata katika Kitabu Kitakatifu imeandikwa "Mtanyang'nywa mashamba yenu na mazao yenu na nyumba zenu na hata kuuwawa na haki hamtapewa." Pia Biblia inasema: "Vumilieni mkijithibitisha ndani ya mioyo yenu kuwa mimi bwana niko karibu."

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja ana mashamba hayo yanayotolewa kwa wawekezaji, ieleweke wazi mateso tuliyoyapata Ukononi ni nafuu kuliko Utumwa tutakaouendea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenye akili zao zitapotea na ufahamu wa wenye busara utafichwa, hawataelewa kinachoujia ulimwengu, huu ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huo ndiyo utakaoleta tabu na maafa pia. Jambo hili liangaliwe lisije kuwa kitanzi kwa watu wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya ya uwekezaji siungi mkono hoja. Naomba niseme kwa ufupi, *NHC* si kwa ajili ya Watanzania kwani Watanzania wanahitaji nyumba zilizo ndani ya uwezo wao, hivyo ni vyema zijengwe nyumba pia za kiwango cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ardhi wanapoona kuna matatizo ya kiutendaji katika eneo fulani, wachunguze

kwa makini maana ule unakuwa ni mtandao kuanzia ofisini hadi Viongozi wa Kata au Kijiji nao huhusika katika jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupimiwa watu viwanja baada ya zoezi hilo kukamilika, naomba watoa ramani watoe zote tatu kwani ukipewa ramani ya viwanja vyako bado utahitajika kuambatanisha na *Master Plan* ya eneo hilo na ramani sijui vidudio! Baada ya kupimiwa viwanja, wengine tunaendelea kuvihangaikia ili tupate ramani zote tatu, lakini zoezi limekuwa likigonga mwamba na hivyo tunaendelea kujenga kiholela. Naomba nipewe jibu juu ya suala hili la mwisho hata kwa maandishi, mimi mwenyewe nimwone nani anihudumie nipate hati ya kiwanja changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011, mwezi Desemba, kulitokea mafuriko makubwa katika Jiji la Dar es Salaam na kuathiri mali na maisha ya wananchi wetu. Maafa makubwa yaliyotokea eneo la Kigogo Mbuyuni kwa kiasi kikubwa yametokea kutokana na ujenzi mkubwa wa uzio eneo la Kigogo Sambusa, ujenzi ambao Wizara imetoa vibali, hati na kumruhusu huyo anayeitwa mwekezaji kujaza kifusi na hatimaye kujenga uzio.

Eneo hilo lilikuwa linajaa maji kabla ya kuingia baharini na sasa maji yanajaa kwenye nyumba za wananchi wetu. Hivyo, kwa kuwa Serikali imeanza kubomoa nyumba zilizojengwa kandokando ya bahari ni vyema sasa hawa waliojenga Kando ya Mto Msimbazi akiwemo huyo aliyejenga Kigogo Sambusa, nao wavunjiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ningeomba Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu Watendaji wote waliohusika kutoa kibali cha ujenzi na hati miliki kwenye eneo hilo hatarishi hapo Kigogo Sambusa.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii Serikali inaendelea kufanya vizuri kwa upande wa ardhi na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ambayo yalikuwa kero kubwa kwa wananchi. Mfano, utoaji hati ulikuwa wa shida, sasa hivi hati inatolewa Makao Makuu Dar es Salaam na hata katika Ofisi za Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofa zilitolewa kwa watu wawili ofa moja *(double allocation).* Sasa hivi tatizo hili limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya wazi yalivamiwa sana. Sasa hivi yanalindwa na yaliyojengwa kinyume na taratibu, majengo yanabomolewa. Naipongeza Serikali, naomba uzi huo huo uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, yapo mambo mengi bado yanahitaji utekelezaji makini wa Serikali na ufafanuzi kwa ajili ya uelewa wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala mojawapo ni Leseni za Makazi; hivi karibuni Serikali ilitangaza Leseni hizi zinatolewa na Halmashauri za Wilaya. Bado kuna urasimu na kutokuwa na uwazi. Mfano, yupo rafiki yangu alihitaji leseni ya makazi Kimara; nilimwona Kamishna wa Ardhi Wizarani akaniambia

Kimara haipo katika Mpango wa Leseni za Makazi, ila Mipango Miji; hivyo, nitafute Wapima wa Manispaa ili wakampimie na kuwa itabidi achangie gharama. Nilipowafuata Wapima wa Manispaa waliniambia hapana, Kimara kuna Mpango wa Leseni za Makazi na ni lazima wakazi 10 mpaka 30, walipe gharama kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa, ambaye atapeleka Manispaa kulipa, ndiyo wapima wampangie siku ya kwenda kupima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kukusanya wakazi 10 mpaka 30 ni tatizo na pia fedha ikilipwa kwa Serikali za Mitaa nalo ni tatizo. Ninaomba Serikali iwaambie Wabunge na Wananchi ni lipi liko sawa; la Kamishna wa Ardhi au Idara ya Upimaji ya Manispaa? Nashauri Serikali iweke Dirisha katika kila Halmashauri la Leseni za Makazi ya Wananchi waelezwe kwa uwazi ni gharama kiasi gani. Pale ambapo ni Mipango Mjini na ni budi kutumia Wapima, nashauri Serikali pia iliweke wazi, iweke Dirisha, itaje ni kiasi gani ili wananchi wapimiwe maeneo yao. Hati na Leseni za Makazi, zitasaidia sana wananchi kupata mikopo ya Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lenye utata ni uchache wa Wapima wenye sifa (Surveyors). Mkoa wa Kilimanjaro, Halmashauri ya Moshi Vijijini, Halmashauri ya Mwanga na Rombo, hakuna wapima. Muhimu, Serikali ipeleke wapima ili kuwe na matumizi mazuri ya ardhi *(Land Use Plan)* na kuondoa manung'uniko ya wananchi wanaotaka ardhi yao ipimwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na uhaba wa wapima, kuna uhaba pia wa darubini ya kupima *(Total Station)* katika Halmashauri ya Wilaya. Kifaa hiki ni ghali, hivyo, Halmashauri nyingi nchini Tanzania hawana kifaa hiki.

Nashauri Serikali ifuatilie Halmashauri ya Wilaya, inawezekana kabisa Halmashauri za Wilaya zikaweka bajeti ya kununua *Total Station,* lakini kwa ufuatiliaji wa Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Sheria zilizopitwa na wakati. Sheria Namba 30 ya 1966 *(Rural Farm Lands – Acquistion and Regrant Act),* inaruhusu mashamba makubwa yalipe kodi ya ardhi Sh. 200 kwa eka moja. Wataalam wa Mkoani Kilimanjaro wananiambia yuko mwekezaji analima eka 320 za ardhi, analima maua na analipa Sh. 64,000 kwa mwaka kama maduhuli ya Serikali. Uwekezaji huu utatumaliza. Nashauri Serikali ilete Muswada wa Kurekebisha Sheria kandamizi kwa uchumi wa nchi yetu; angalau mashamba makubwa yalipiwe Sh. 5,000 kwa eka moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali itoe ufafanuzi katika hili, kwa nini mashamba makubwa yanalipishwa kodi kidogo sana na kuna mkakati gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kubuni mpango mzuri wa kuboresha nyumba za *NHC.* Bado gharama za nyumba hizo kubwa kwa wananchi wa kipato cha chini. Ile dira ya *NHC*, aliyoibuni Mwalimu Nyerere ya kusaidia watu wa kipato cha chini, inakuwa haitekelezeki. Azma ile inakuwa *eroded.* Kuna haja Serikali itafute namna ya kusaidia wananchi, pengine ifikirie kuondoa kodi ya *VAT* katika vifaa vya ujenzi kwa *NHC* ili waweze kupunguza bei ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Mimi naipongeza Serikali kwa kubaini chanzo cha matatizo ya makazi holela nchini mwetu kuwa ni ugumu wa kupata viwanja vilivyopimwa. Nashauri Wizara itunge Sera ya kuzitaka Halmashauri zote zipatiwe vitendea kazi na wataalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo ni kwamba, upimaji wa maeneo mbalimbali nchini mwetu una ugumu kutokana na ukosefu wa maafisa na vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ni watu wanaopenda kujenga makazi ya kisasa, matokeo yake wengi hulazimika kugombania maeneo machache yaliyopimwa na matokeo yake ni chanzo cha rushwa na pale wengine wanapoona wanacheleweshwa, hulazimika kwenda kujenga nyumba kwenye maeneo yasiyopimwa (makazi holela).

Wilaya ya Mbogwe na Mkoa Mpya wa Geita, tunaomba Serikali ianzishe utaratibu wa kuzisimamia Halmashauri zetu mpya ili zipimwe zisije zikakumbwa na ujenzi wa makazi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya au Jimbo langu la Siha, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, kwa hutuba yake nzuri na yenye msisimko wa hali ya juu, pamoja na uchambuzi wa kina

ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara yake. Naunga mkono hoja hii. Nampongeza pia Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Naibu Waziri wa Ardhi, kwa msaada wa hali ya juu ambao anautoa katika Wizara na hivyo kuifanya kazi ya Waziri kuwa nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Siha ni Wilaya mpya ambayo Halmashauri imeamua kujenga Makao Makuu ya Kisasa ambayo yatazingatia ujenzi wa Mji wa Siha wa kisasa na wa aina yake. Utakuwa ni Mji Mdogo wa Siha ambao utazingatia maelekezo ambayo Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka amekuwa akiyatoa toka aanze kushika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atusaidie kwa hali na mali katika kuhakikisha kwamba, njozi ya Wana wa Siha inawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi atusaidie utaalamu na rasilimali fedha ili tuupime Mji Mdogo wa Siha kwa ubora na Viwango vya Kimataifa. Halmashauri yangu itawasilisha rasmi ombi hili Wizarani ambalo litaonesha kiasi kinachohitajika kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia Hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza kwa dhati Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hatua kadha wa kadha zilizochukuliwa na ambazo zipo kwenye mipango, kwa hili nawaunga mkono angalau kuna ubunifu wa uthubutu wa kutosha kurekebisha makosa makubwa yaliyofanywa na watangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu ni kwamba kuna suala la Nyumba za Serikali zilizouzwa kwa bei ya kutupwa kwa Vigogo wa Serikali kwa kisingizio cha kwamba, hawana uwezo wa kujenga nyumba zao baada ya kustaafu, lakini ukweli ni kwamba hicho kilikuwa ni kisingizio tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukienda Oyster Bay, Masaki na kadhalika, inashangaza kuona Mahekalu yaliyojaa huko, kumbe kusema kweli walikuwa na nia ya ardhi kwenye *site,* yaani walikuwa na uchu wa kupata nafasi nzuri kwa ajili ya kujinufaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hasa vijana wana hoja ya kutaka Serikali iwarudishie Watanzania nyumba zao na waelezwe kupitia Wizara yako ni lini nyumba zao zitarudishwa bila masharti kwa Serikali (Wananchi).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuitaka Serikali iende zaidi ya hapa kwa kupima ardhi na kuiwekea miundombinu yote; yaani Serikali iwadhamini hawa vijana wanaomaliza vyuo wanahangaika kutafuta kazi hadi wanachakaa! Waunganishwe, ardhi isifuate mijini ambako kumejaa bali iwe nje kabisa ya miji huko mikoani na waunganishwe kwa kupewa maeneo ya kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na kadhalika, wawezeshwe na kupewa vifaa vya kuanzia maisha.  Suala hili linaweza kupangwa

kwa kushirikiana na Wizara husika maana ni suala Mtambuka ili kuwawezesha vijana kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ili kuwatendea haki wananchi ni muhimu kufikia upya gharama za nyumba hizi zinazojengwa, maana kusema kweli ni aghali mno. Hizi nyumba zipunguzwe kabisa bei yake iwe *realistic* kusudi ioneshe dhamira katika vitendo badala ya nadharia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la Watendaji wa Ardhi ambao wamesababisha migogoro mikubwa katika nchi na hivyo kuigharimu Serikali fedha nyingi sana. Je, hawa wakorofi waliotenda mambo haya ni wangapi angalau katika miaka kumi iliyopita? Je, wamechukuliwa hatua gani tangu wajulikane kuwa wameharibu taratibu za nchi? Zaidi ya hayo, pendekezo ni kwamba wengi wao hata wakifukuzwa kazi hawaumii kwani wao walijilimbikizia mali, hivyo hakomi na wengine watakaokuja watafanya hivyo hivyo. Ingefaa wachunguzwe na kuorodheshwa mali zao na kuzipima kama kweli walizipata kwa uhalali, ijulikane kuwa hawakufanya ufisadi waachiwe mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikidhihirika kuwa kuna ufisadi ndani yake wafilisiwe na kutangazwa ili liwe fundisho kwa wengine wanaoanza kazi wasije kufuata nyayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. naomba kuwasilisha.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayofanya. Changamoto kubwa ni:-

(i) Kuwa na mpango mkubwa katika Halmashari wa kupima viwanja na kila anayetaka kiwanja apate kiwanja.

(ii) Kila anayetaka hati ya umiliki apate. Hii itawezekana kama Maafisa Ardhi watakuwa waadilifu. Hawa ni wasumbufu maana bila rushwa siyo rahisi kupata huduma. Nimekuwa nikijaribu kupata hati katika Halmashauri ya Mkuranga lakini mpaka sasa bado; danadana nyingi na za kukatisha tamaa. Kama Mbunge anapata tabu namna hii; je, Mwananchi wa kawaida? Serikali iweke utaratibu mzuri wa kufuatilia ili wananchi wapate hati kwa wakati. Vijana hawa hutaka wafanye kazi kwa kisingizio cha kufanya kama *private.* Hii ni rushwa ile ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri akiangalie Kitengo cha Ramani. Mitambo yao imeharibika na hata *photocopy* tu inabidi mwananchi alipie wakatoe nje ya ofisi. Naomba akitembelee Kitengo hiki na kuona uwezekano wa kutatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona mipango mbalimbali, kumbukumbu aa ardhi na teknolojia za habari, mawasiliano, *ILMIS*, katika Wilaya nyingi lakini Wilaya ya Mbinga haimo. Ninaomba Mbinga nayo ifikiriwe na ule Mradi wa kujenga Ofisi za Ardhi katika vijiji uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Nampongeza sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri na Mkurugenzi Mkuu wa *NHC*, Ndugu Msechu na Watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia kuhusu maeneo ya wazi, maeneo haya yanakuwa yametengwa kwa ajili ya michezo na shughuli za kijamii. Tatizo lililopo hapa ni kukinzana kwa Sheria kati ya Maafisa wa Ardhi walioko Halmashauri ambao wapo chini ya TAMISEMI na Maafisa wa Ardhi walioko Wizarani, mara nyingi wanaouza maeneo haya ni Wakurugenzi wa Halmashauri wakishirikiana na Maafisa wao wa Halmashauri. Hawa Wakurugenzi mara nyingi huwa wanatoka maeneo mengine na kuletwa tu pale, wanakuwa hawana uchungu na ile miji wanayokwenda kwa sababu siyo kwao, wanafanya ubadhirifu na baadaye wanahamishiwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Serikali iunde Taasisi moja tu ambayo itashirikisha Wajumbe kutoka pande zote mbili; TAMISEMI na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuunda Mahakama ya Ardhi ila nataka kujua ni nani msimamizi wa kesi hizi; Halmashauri au Wizara? Naomba Waziri atakapo-*wind up* atupe ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atupe ufafanuzi wa hizi *City Park* ambazo amesema katika Hotuba yake kuwa atazijenga kwenye Bonde la Msimbazi kwa kushirikana na Manispaa ya Ilala na Manispaa ya Kinondoni ili na sisi Wabunge tutakapoulizwa na wananchi tujue namna ya kuwaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, nyumba walizojenga ni nzuri nawapongeza ila ni ghali sana; naomba walifikirie suala hili ili wananchi wa kawaida waweze kumudu kuzinunua. Pia naishauri Serikali waondoe ushuru kwenye vifaa vya ujenzi wa nyumba hizi, kama ndondo, saruji, mabati na vifaa vyote vinavyotumika kwenye ujenzi huu. Vile vile iondoe *VAT* ili wananchi waweze kumudu kununua nyumba hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nyumba za Ilala Mchikichini ni sawa na nyumba za Medeli Dodoma; ni *apartment* za vyumba vitatu. Nyumba za Medeli zimeligharimu Shirika shilingi milioni 60 kwa *apartment* moja. Kutokana na Shirika kujenga pia miundombinu ya umeme, maji safi na machafu na barabara, gharama zimeongezeka mpaka shilingi milioni 80 na kuuzwa shilingi milioni 100. Iweje nyumba za Mchikichini Ilala ziuzwe shilingi milioni 168 bila ya *VAT* mahali ambapo kuna miundombinu yote? *Excuse* waliyoitoa kwa nyumba za Medeli, Ilala Mchikichini haipo! Kwa nini nyumba wakazipandisha bei kwa zaidi ya asilimia mia moja; wanajengewa Watanzania wa daraja gani?

**MHE. ZAINAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa Hotuba nzuri iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yangu kwamba, yale yote waliyokusudia kuyafanya yatekelezwa ili kuleta maendeleo kwa wananchi na pia maeneo ambayo Serikali imebaini katika kuleta maendeleo kwamba kuna upungufu basi ni vyema kufanya jitihada za makusudi ili kuepuka huo

upungufu hasa kwenye kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba, upatikanaji wa miundombinu na huduma muhimu. Ningependa kujua ni mkakati gani ambao Serikali imepanga ili kupunguza gharama kubwa ya riba katika mikopo ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali inieleze ni kwa vipi inashindwa kushawishi wawekezaji waweze kuingia ubia na wananchi wa eneo husika katika kuwekeza ili kuepukana na migogoro na pia kuwafanya wananchi wa eneo hili kuwa wafanyakazi na pia kuchukuliwa ardhi yao. Napenda kupata majibu ni vipi Serikali imepanga kuepuka tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi Serikali imejipanga kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi hasa kwa maeneo ya vijijini ili kuweza kuepukana na migogoro na pia kuwawezesha wananchi hao kupata haki yao ya msingi ya kujua sheria zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini naomba nipatiwe ufafanuzi wa hoja zangu.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeipokea Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wake ya Mwaka 2012/13.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yao vizuri ni vyema Wizara ikatathmini utendaji na Sheria ya Ardhi (Na. 47) ya Mwaka 1967, inayoongozwa na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 ya tarehe 21 Mei, 1999. Matatizo ya ardhi ni mengi na sehemu kubwa yanasababishwa na

Viongozi wa Juu kwa lengo la kusaidia dhamira za ubinafsi, urafiki, undugu na tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa Mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa Mkoa wa Tanga na hasa Wilaya ya Muheza ni mengi na yanatesa sana wananchi. Licha ya kufuata kwa busara hatua zote muhimu kwa lengo la kupunguza migogoro kati ya Wawekezaji na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Ufutaji Hati haitekelezwi tangu 2001 – 2012! Ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mkuu wa Nchi, ya kufuta Hati za Mashamba ya Kibaranga, Kwafungo, Bwembwera, Songa, Kihuhwi, Lewa na mengineyo haitekelezwi. Sheria ya Ardhi ya 1999 chini ya *Fundamental Principles of Land Policy – Classification and Tenue of Land: All land vested in the President as Trustee.*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu Bungeni kwa awamu zote mbili majibu ni yale yale, maombi ya kufuta Hati za Mashamba Wilaya ya Muheza yapo mezani kwa Mheshimiwa Rais. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri inaonesha kwamba, mwaka 2011/12, Ilani za ubatilisho zilizotumwa ni 792, zilizobatilishwa na kutwaliwa ni 72 na zilizohamishwa ni 1,521. Mwaka 2012/13 Wizara itaendelea kushugulikia maombi 1,700 ya uhamisho wa milki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate ufafanuzi wa kauli hiyo ikilinganishwa na ukweli kwamba, maombi ya kufutwa hati miliki za mashamba zaidi ya sita ya Wilaya ya Muheza ya tangu 2005/2006 yapo mezani kwa Mheshimiwa Rais na Hati hizo hazijafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutofutwa kwa Hati ya Shamba la Kibaranga kumezuia uhamisho wa wananchi 1,128 waliohamishwa kutoka Hifadhi ya Msitu wa Amani tangu 2005/2006, baada ya Ahadi ya Serikali kuwezesha Benki ya Dunia kuwalipa wananchi hao. Malipo yamefanyika, Benki ya Dunia imeweka Mwakilishi wao kusimamia uhamisho wa wananchi hao kwa miaka miwili bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kujibu swali langu Bungeni mwaka huu wa 2012, Wizara iliahidi kuangalia kama utaratibu wa kufutwa hati ya Awali na kutoa hati mpya kwa mwekezaji *Silver General Distribution Limited, Title No. 17281, LO No. 20627, LD No. 15730/11 - 25 July 2003.*

Lengo ni kuona kama mfumo wa kisheria ulifuatwa na kama kweli Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kupitia Baraza la Madiwani 2002/2003 walishirikishwa ipasavyo hasa ukizingatia kwamba, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza katika mkutano wa hadhara na wanakijiji aliwaamuru wawekezaji kupitisha greda na kuvunja mazao ya michungwa ya wananchi wawili, akiwataja kwa majina hadharani na hivyo kukuza mgogoro kati ya wananchi na wawekezaji. Hapa Mkuu huyo alichukua jukumu la kisheria mikononi badala ya Mahakama. Itakuwa vizuri wananchi wakifahamu kwamba, mwekezaji alikuwa na hati miliki ya ardhi hivyo kisheria na ukweli ubainike iwapo wananchi hao ni wavamizi na hawalindwi na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi Hati ya awali ikifutwa eneo la shamba linakuwa huru na wazi kutokana na kuwa huru na wazi kunatoa fursa ya kurekebisha eneo jipya la uwekezaji baada ya kuondoa eneo lililoingiliwa na

wananchi kutokana na shamba kutoendelezwa kwa wastani wa miaka 25 – 40. Kwa burasa hiyo, hakutakuwa na migogoro kati ya Mwekezaji mpya na wananchi wanaoitwa wavamizi ambao wamekaa na kulima ndani ya shamba hilo kwa zaidi ya miaka 25 – 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inasema nini juu ya hali ya kuwepo shamba bila kuendelezwa bila taarifa kwa zaidi ya miaka 25 – 40 na hali ya kuingia kwa wananchi kuendeleza hali hiyo bila kusimamishwa kwa zaidi ya miaka 25 – 40? Tunaomba kupata maelekezo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri unaotolewa wa kukutanisha wananchi na wawekezaji ili kuondoa migogoro hautekelezwi. Rejea barua ya Wizara, Kumb. Na. *LD/15730/72* ya tarehe 1 Juni, 2011 na Kumb. Na. *LD/146475 Vol. III* ya tarehe 15 Mei, 2012. Kutokana na hali hiyo, nimemwandikia Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, barua yenye Kumb. Na. MB/JM2/WAM/244/12 ya tarehe 27 Juni, 2012, Wizara isimamie majadiliano ya usuluhishi huo. Pia waige mfano wa mwekezaji *AGRO Tanga Sisal* wa Muheza anavyoachia Ardhi iliyoshikwa na wananchi.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa bajeti ya kisayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa, nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba, kwa kazi nzuri ambayo anafanya, matokeo ya kazi yake yameshaanza kuonekana. Kazi hii nzuri inatiwa dosari na bei kubwa ambazo wananchi wa kipato cha chini hawawezi kumudu kununua. Hii inatokana na bei kubwa za kupaa za vifaa vya ujenzi. Hivyo, naomba Serikali ipunguze bei ya vifaa hivi ili bei za nyumba ziweze kushuka. Hii ina maana *VAT* itolewe kwa vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba Shirika la Nyumba lijenge nyumba za kuuza katika Jimbo la Kondoa Kaskazini, kuna eneo kubwa na zuri kwa ujenzi wa nyumba ili wananchi waweze kunufaika na fursa hii adhimu.

**MHE. JUMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ujenzi wa nyumba za Serikali zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* ambazo zinakusudiwa kukopeshwa wananchi ziwe za bei ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikaweka utaratibu mzuri wa matumzi bora ya ardhi, kwani wananchi wanapata usumbufu mkubwa ndani ya ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima, napenda kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo na madhumuni ya Shirika hili ni kuwapatia Wananchi wa Tanzania makazi bora

na salama na moja kati ya nguzo muhimu katika mahitaji ya mwanadamu ni makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiweka kando juhudi kubwa zinazoonekana kuchukuliwa sasa na Shirika hili, naomba nitoe ushauri kuhusu nyumba kongwe hasa katika katika Miji Mikuu. Tathmini ndogo tu iliyopo, nyumba hizi nyingi zinakaliwa na watu wenye uwezo mkubwa na kuwaacha wale ambao hawana uwezo wowote wakiwa hawana mahali pa kukaa. Ukifuatilia kwa makini utagundua wanaozikalia nyumba hizo ni hao hao ambao wanamiliki mahekalu makubwa katika maeneo mengine kama vile Mbezi Beach na maeneo mengine katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ifanye tathmini ili kulibaini jambo hili na ikubali kuwanyang'anya nyumba hizo wale wote wanaoishi kwenye nyumba hizi wakiwa wameacha nyumba zao au wanapangisha kwa bei mbaya nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba Serikali kupitia Shirika la Nyumba, ipunguze bei au kodi za nyumba; sasa Shirika haliendani tena na ile dhamira ya awali ya kuwasaidia raia wake na badala yake wanaangalia biashara zaidi. Hebu tuangalie hali ya kipato cha Mtanzania wa kawaida atawezaje kulipia kodi ya nyumba ya Sh. 500,000 huku mshahara si zaidi ya Sh. 200,000 kwa wale wa kima cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ilingalie jambo hili ili kuondoa pengo baina ya Watanzania kati ya

wenye kipato watakaomudu kukaa nyumba hizi na wenye kipato watakaoweza kulipia kodi kubwa za nyumba hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa *legacy* ambayo wataiacha kwenye Wizara hii nyeti; *keep up the good job.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye swala la mashamba makubwa kwenye Jimbo la Arumeru Mashariki. Ninajua Wizara inayafahamu vizuri mashamba hayo kwa sababu yamepelekea maafa makubwa kama vile uharibifu wa mali na hata vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaoimba Wizara itoe majibu ya sintofahamu iliyopo kwenye mashamba makubwa nitakayoyaorodhesha. Sintofahamu hizo ni kuhusu wawekezaji/mabepari kumiliki ardhi kubwa bila kuendeleza, kubadilisha matumizi kinyume na utaratibu na kuhodhi ardhi kinyume cha utaratibu. Mwisho kabisa, maelezo juu ya mashamba yaliyopata kibali cha Mheshimiwa Rais kufuta miliki na kuagiza kuyarejesha kwa wananchi kwa barua ya tarehe 1 Juni, 1999, yenye Kumb. Na. *CL/48 Vol. III* toka kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwenda kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha. Je, nini kilichofuata juu ya mashamba haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunaitaka Wizara ituambe nini hatima ya Shamba la *Karamu Estate* lililopo Kata ya Poli, Wilayani Arumeru.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachelea kuunga mkono hoja hii kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamishwe ni kwa nini Mji Mdogo wa Himo ulitangwazwa mwaka 2007 na kuwa na *TEO*, hadi leo haujulikani ni Mji au Kijiji? AnNayepanga Maendeleo ya Mji Mdogo wa Himo ni Wizara au Mahakama?

Kwa nini kesi imekuwa Mahakamani tangu 2002 hadi leo? *Court Injuction* iliyozuia Mji Mdogo wa Himo ilitolewa 2004 na ilipaswa kumalizika baada ya miezi sita lakini watu wabaya waliendelea kutumia amri hiyo kuzuia Mji huo usipimwe hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, kufika Himo na wananchi kukubali Mji Mdogo wa Himo upimwe na pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuagiza mji upimwe na wananchi wapimiwe viwanja, hadi leo agizo la Waziri halijatekelezwa. Hakuna amri yoyote ya mahakama inayozuia Mji wa Himo usipimwe. Hata kama kuna kesi mahakamani, kwa nini tusimwombe Hakimu au Jaji atoe hukumu kwa kesi hiyo ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali inachukua ardhi ya Mashamba ya Mkonge Himo, iliacha eneo kwa ajili ya Sekondari ya Ashira, *TTC Mandaka* na *TTC Marangu*. Tangu wakati huo tulijua eneo hilo litatumika kwa maslahi ya Kijiji cha Himo.

Eneo hilo litatoa nafasi ya kujenga Zahanati, Benki, Mahakama na kadhalika. Inashangaza eneo hilo limegawanywa kwa matajiri, watu wenye nguvu za fedha. Eneo hili amepewa tajiri mwenye Shule binafsi ya Skolastika na Mbunge wa zamani wa Vunjo niliyechukua nafasi yake. Yeye alipewa eka 11 eti ni mwekezaji na uwekezaji wenyewe ni kuweka Radio. Badala ya eneo hili kutumika kwa manufaa ya wanakijiji, linatumika kwa manufaa ya watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Masista wa *Holy Spirt Sisters Rauya*, Marangu Moshi, wamewekeza katika Shamba la Sanya Juu Siha, wamejenga Shule ya Sekondari, Kituo cha Afya, wanafuga mbuzi, ng'ombe na wanalima mahindi na kadhalika. Shamba hili lina Hati halali ya Serikali kabla ya mwaka 2004, wananchi waliokuwa 12. Mwenyekiti wa Kijiji amekuwa anauza shamba la Masista na hadi kufikia leo kuna wavamizi zaidi ya mia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo kampeni inayofanywa na Watumishi wa Serikali ya kuwataka Masista hao wawachie hao wavamizi ardhi yao. Wanajua kesi bado ipo mahakamani lakini wanathubutu kuwaambaia Masista hao wahame hapo ili wapewe eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwakamate watu wote waliouza Shamba hili na wanaoendelea kuliza kwa sababu kunyamaza ni kuwaunga mkono wavamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuiarifu Serikali kwamba, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi na wenzao, wamejimilikisha zaidi ya ekari 100 za Kijiji cha Mawala. Vijana 100 wa Kijiji hicho

hawana ardhi. Aidha, hao matajiri waliovamia eneo la mifugo ambalo tayari limekwishatengwa, waondelewe kwenye eneo hilo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia Hotuba ya Waziri Mkuu, niliongea sana kuhusu Hati za Kimila za kumiliki ardhi. Wilaya ya Chunya, Wataalam wa Wizara ya Ardhi walipima ardhi mwaka 2008 lakini mpaka sasa hakuna hati ambayo imetolewa hata moja. Sababu ni kuwa, Chunya hakuna Afisa Ardhi Mteule anayefaa. Naiomba sana Wizara ishughulikie jambo hili kwa haraka sana ili Wananchi wa Chunya waweze kumiliki ardhi na hivyo kukopesheka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naupogenza sana Uongozi wa National *Housing Corporation* kwa mpango wa kujenga makazi na kuuza kwa wananchi.

Pia katika kuuza nyumba hizi, Shirika linatafuta mabenki ya kuwakopesha wananchi ili waweze kumiliki nyumba. Jambo zuri sana hili na litafanya watumishi wasiwe na mawazo ya wizi au ufisadi katika kutafuta fedha za kujengea nyumba. Naiomba sana Serikali ilipe Shirika hili uwezo zaidi ili waendeleze vizuri Programu hii ya kujenga nyumba na kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasema; *"what goes around comes around."* Vyombo vya habari vimeanza kuandika kuwa Tanzania ni kinara kwa kuuza ardhi kwa wageni hapa Afrika. Je, ni kweli Serikali inawauzia wageni maeneo makubwa sana ya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwepo hapa salama. Kwa kuwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani umekaribia, niwatakie Waislam wote na Watanzania kwa ujumla; *Ramadhani Kareem*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara na Taasisi zake, kwa matayarisho mazuri. Pia nampongeza Msemaji wa Kamati na Kambi ya Upinzani, ambaye ni Mwana-Dar es Salaam mwenzagu; pia nakubaliana naye kwa mambo ya msingi hasa matatizo aliyoyataja hususan uvamizi wa maeneo na kuchukua sheria mkononi kwa baadhi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, akishirikiana na Waziri wa Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kulimaliza suala la ardhi ya ujenzi wa *Teaching Hospital* ya Mloganzila kama alivyoahidi katika bajeti ya mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, naamini Wizara hii ni sikivu na hivyo naomba mnisikilize kwa makini, naamini mtatafakari na kuchukua hatua na maamuzi dhabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza kwa makini sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nilikuwa nachelea aliyokuwa akisema mengi. Kwanza najiuliza ni kwa nini kama kweli tunataka pamoja na kupendezesha mji, kwa nini huyu mwananchi mwenye ardhi asiwe *part* ya Mradi huu; sawa apewe pesa apishe ujenzi lakini umiliki

utakaofanywa hapo uwe wa ubia. Mmoja katoa ardhi na mwingine katoa uendelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 50 na 51 wa Hotuba unatia mashaka sana. Kwanza, inaelekea hakuna chochote ambacho kimefanywa mpaka sasa. Imeorodhesha kazi za mwaka huu. Ukurasa wa 51 unasema, zimetengwa shilingi bilioni 60 (ambazo ni asilimia 66 ya makusanyo yote ya Wizara), ambazo ni asilimia kumi tu ya mahitaji ya mwaka huu. Hivi hizo asilimia 90 inatoka wapi? Mimi naomba tusiwape wananchi matumaini yasiyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kigamboni wamekaa miaka minne bila kuendeleza. Bidhaa zimepanda bei, hata yule aliyepata kiinua mgongo saa hizi kimeisha. Hawa wananchi wanafidiwa vipi?

Mpaka sasa hakuna mwekezaj; hivi Mradi huu upo kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa Mradi huu ni miaka 20, yaani 2012 – 2032, ukiongeza iliyopita ni miaka 24. Huu ni muda mrefu sana; kwa nini isiendelezwe Kata moja moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 52 unazungumzia juu ya *Kigamboni Development Authority*; ni kwa nini Mradi usiwe chini ya Manispaa ya Temeke kwa sababu Kata zinazoongelewa hapa ni Mjimwema, Kigamboni, Vijibweni, Kibanda na Samangila? Kwenye Kata hizo kuna Mradi Kabanda wa *NSSF*; wameshajenga *THB*, michoro tayari na Manispaa ya Temeke imegawa viwanja. Hivi huu siyo mgongano na *chaos*? Kulikuwa na mgongano kama huo

kwa *CDA* Dodoma na Manispaa ya Dodoma. Nashauri Wabunge wa Dar es Salaam, tukae na Wizara, tujadili kwa kina, maana mpaka sasa naona giza totoro kwenye Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii, kuchangia Bajeti hii kwa njia ya maandishi. Eneo la kwanza ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu mipaka ya Jeshi na Wananchi. Katika Jimbo la Muleba Kaskazini tumekuwa na matatizo ya mipaka kati ya Kambi ya Kaboya na Wananchi wa Kata za Izigo, Muhutwe na Mayondwe. Tatizo hili limekuwa la muda mrefu, hali inayoleta kuhasimiana kati ya Wananchi na Jeshi la Wananchi. Wananchi wanazo hoja zao na maamuzi ya Serikali yaliyopelekea Jeshi kuwa pale yako wazi. Ushauri hapa ni kuwa, maamuzi yafanyike ili kuondoa mgongano usiokuwa na maslahi kwa Serikali na hasa Chama Tawala. Uongozi wa Jeshi unaongeza au kupanua mipaka kila kukicha. Jeshi limechukua vyanzo vya maji hasa mto au kujitoa kinachotoka Kijiji cha Itoju. Hiki ni chanzo cha moji cha asili miaka nenda rudi hata kabla Mzungu mlowezi ambaye alirithiwa na Jeshi. Katika hali hii wananchi wanajenga chuki kwa kuzuiwa kuteka maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni milki au makazi katika maeneo ya Kata za Rutilo Wilayani Muleba na Bubale/Kakunyu katika Wilaya ya Misenyi. Tatizo la *NARCO* kuwamilikisha *(sub-lease)* wafugaji katika vitalu limeleta athari kwa wananchi. Tatizo hapa ni kuwa, pamoja na upungufu wote, Wizara ya Ardhi inahusika sana. Wizara

inahusika na kwa nafasi yake kwa sehemu kubwa inayo suluhu ya tatizo hili. Maeneo yenye wakazi/vijiji wametengwa ndani ya vitalu na maeneo hayo kupewa wafugaji wakubwa *sub-lease*. Zoezi la kutenga maeneo haya lilifanyika juu ya meza Dar es Saalam. Watanzania wamegawanywa na kumegwa kama manamba. Busara hapa inaonyesha kuwa hapa kuna sheria zimekiukwa. Busara hapa inaonesha kuwa hapa kuna Sheria, basi haki imekiukwa kwani ugawanaji wa vitalu haukuzingatia eneo husika walikuwepo watu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri na kuiomba Serikali kupitia Wizara hii, ijasirie kumaliza migogoro ya *NARCO* na wananchi kwa kuchukua nafasi ya Uongozi wa Wizara zinazohusika na tatizo hili. Hizi ni Wizara za TAMISEMI, Mambo ya Ndani, Maliasili na Ardhi yenyewe. Wizara iende mbali zaidi kwa kupima maeneo ya Wilaya ya Muleba kwa kuonesha matumizi bora ya ardhi hasa sehemu za wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la vijiji kupitia Serikali zake kujihusisha na uuzaji wa ardhi. Kumekuwepo na ukiukwaji wa Sheria za Ardhi kwa Serikali kuuza ardhi maeneo makubwa kuliko inavyotakiwa. Hali hii inachochea migogoro na hii ni rai yangu kuwa, Serikali ngazi ya Wizara, iingilie kati kwani Halmashauri haiwezi kutatua migogoro hii.

**MHE. CLARA DIANA MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii niweze kuchangia walau kwa machache juu ya Bajeti hii. Kwanza, napenda nizungumzie juu ya migogoro ya ardhi kwa upande wa mashamba. Kunakuwa na ugomvi wa hapa na pale hususan kati ya familia wa mashamba na mtatuzi ni Mahakama ya Ardhi. Kwa ngazi za Kata, napenda

niiambie Wizara ya kuwa, wahudumu wa kesi hizi hawana utaalamu kwa vile hawapewi semina, matokeo yake rushwa inashika nafasi kubwa sana. Utakuta mwenye haki kama hana pesa hata kama dai lake ni la haki kwake, haki hiyo hupewa mwenye fedha za kutolea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mahakama hii huwa ya Kata ikivuka hapo ni Mkoa. Hali hii huleta kero kwa wale walio wanyonge kwani huwa wanashindwa kufika huko Mkoani kwa kukosa uwezo wa nauli. Wakati huo huo kesi haziishi kwa mara moja huwa kuna nenda rudi. Hivyo, napenda kuishauri Wizara ishushe Wilayani pia ili watu waweze kufikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia pia juu ya viwanja; viwanja huwa vinapimwa kwa upunjifu. Maana utakuta kila kipimo huwa kina tofauti; kwa mfano, kiwanja cha ekari moja badala ya mita 70 kwa 70 huwa hazitimii na kwa vile vidogo pia. Hivyo, naomba Wizara iwataarifu Watendaji wake Mawilayani watende haki. Vile vile bei nayo huwa ni kubwa kiasi cha wanyonge kushindwa kupata. Upimaji wa viwanja na uwekaji wa alama, gharama ni kubwa; kupima Sh. 60,000, kuweka alama yaani mawe Sh. 500,000, sasa wengi huwa wanashindwa kupata hati miliki. Naiomba Serikali iliangalie hilo ili hata wale wa hali ya chini wapate.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja kwa ajili ya Wabunge; naomba tuangaliwe na tufikiriwe upande wa bei kwani tunafanya kazi ya kuwatumika wananchi. Kama ilivyo mishahara, haikidhi haja. Vile vile naomba Bunge lijenge nyumba kwa ajili ya Wabunge, maana nyumba za

wenyeji zinazopangishwa baadhi zipo mbali na Ofisi za Bunge. Pia usalama kwa sehemu zingine ni wa mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maoni mbalimbali yaliyowasilishwa kwangu kutoka kwa Wananchi wa Jimbo langu kupitia ziara mbalimbali nilizofanya Jimboni kwangu kupitia Kata, Vijiji, Vitongoji, Mitaa, watu binafsi, taasisi na kadhalika, kwa ujumla wao wananchi hao wamekuwa wa maoni na maswali yaliyohitaji majibu na au ufumbuzi wa hoja mbalimbali na kuniomba niziwakilishe katika vyombo vyenye mamlaka ya kujibia hoja hizo. Wananchi hao wamenipa hoja zifuatazo:-

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi: Migogoro ya Ardhi imekuwa ikichukua sura pana zaidi, ikizingatiwa kuwa ardhi ikibinafsishwa kwa wawekezaji, ongezeko la wageni katika nchi, ongezeko la idadi ya watu, mahitaji ya matumizi ya ardhi na kadhalika. Hali hii imefanya kila eneo kuwa na migogoro mikubwa kuanzia wakulima na wafugaji, wawekezaji na wanavijiji, wachimbaji wakubwa wa wadogo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali itoe tamko kuhusiana na Tume ya Rais iliyokuja Mjini Lindi, kuangalia Mashamba ya Mkonge ya Kikwetu, Mkwaya na Kitunda (Kitumbikwera). Je, imefikia wapi? Je, lini mashamba haya yatagawiwa wananchi na wanavijiji wa maeneo hayo?

- Serikali inatoa tamko gani juu ya fidia kwa wananchi waliovunjiwa majumba, kupoteza mashamba na

mali zao katika zoezi la ujenzi wa Barabara ya Mbwemkuru – Mingoyo na sasa upitishaji wa Mkongo wa Taifa na gesi asilia ya Mnazi Bay. Maeneo ambayo wananchi wanatakiwa wavunje nyumba zao kwa madai kuwa wameikuta barabara, kitu ambacho hakina ukweli. Hii katika Manispaa ya Lindi.

- Serikali inatoa tamko gani juu ya migogoro inayoendelea ya mipaka ya vijiji vilivyopo katika Manispaa ya Lindi na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi. Mgogoro uliopo ni wa Kijiji cha Nusura na Mkwaya.

- Serikali inatoa msimamo gani kuhusiana na mgogoro wa ardhi unaowakabili Wanakijiji wa Mkwaya Manispaa ya Lindi na Mkurugenzi wa Kampuni ya African Black Wood ya Mkwaya? Serikali imtaje mmiliki halali.

- Serikali inasemaje kuhusiana na watu walioomba kupatiwa hati miliki za kimila kabla ya maeneo hayo kuingizwa kwenye Mamlaka ya Manispaa ya Lindi. Maeneo yaliyoingizwa katika Manispaa kutoka Halmashauri ya Wilaya ni Mingoyo, Ng'apa, Tandangongoro, Mbanja na Chikonji.

- Serikali inasema nini kuhusiana na maeneo yaliyokuwa yanamilikiwa na *NHC* na baadaye kuyauza kwa wapangaji wao na baadaye kuzuia maeneo ya wazi na kutaka kuyatumia kwa kuyaendeleza wao kwa ujenzi badala ya kuyaacha kuwa maeneo ya wazi au kuwakabidhi waliyoyanunua?

- Serikali inaandaa mkakati gani kuhusu hali ya migogoro inayoibuka maeneo kadhaa kati ya wakulima na wafugaji ili isiendelee na kuweka mipaka bila mwingiliano?

- Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia ardhi Majeshi yetu ya Ulinzi kama Magereza ili waweze kupata maeneo ya makazi pindi wanapostaafu?

- Serikali ina mpango gani wa kuwapimia Wananchi Wakazi wa eneo la Nangurukuru katika Kitongoji cha Likotwa, Kata ya Rasbula, Manispaa ya Lindi ambao tokea mwaka 2007 walilipia viwanja hivyo na sasa wanaambiwa watoke? Maeneo hayo wameishi kwa takriban miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe ufafanuzi juu ya fidia wanazotakiwa kulipwa Wananchi wa Ng'apa na Tandangongoro ambapo kuna Mradi wa Upitishaji Nyaya za Umeme Kuelekea Rondo Lindi (Vijijini) na Mradi wa Upanuzi wa Barabara. Je, jukumu la kulipa fidia ni la *TANESCO,* Wizara ya Ujenzi au? Naomba ufafanuzi ili wananchi hao wa Jimbo langu wapate kufahamu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Vijiji na Kata yameshindwa kushughulikia kwa ufanisi migogoro ya ardhi. Je, wana elimu ya kutosha kutatua migogoro hiyo? Nashauri wapatiwe semina elekezi mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wa kutosha. Je, tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa Mabaraza ya Vijiji na Kata kuna tathmini

yoyote imefanyika ili kubaini kama kuna mafanikio yoyote yanayoweza kuhalalisha kuendelea kwa uendeshwaji wa Mabaraza hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Kijiji cha Kikatiti, Wilaya ya Arumeru Mashariki, wana malalamiko makubwa kuhusu ardhi yao iliyoporwa, kuvamiwa na kujengwa kimabavu. Kwa mfano, Mwenyekiti ambaye ni Diwani, Bw. Pendael G. Nassari, alijichukulia eneo la Soko akajenga nyumba ya biashara bila ridhaa ya Wananchi au Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Shule ya Msingi Kikatiti limechukuliwa kinyemela na kujengwa nyumba ya machinjio, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Wananchi wanaomba kwamba, eneo lililokuwa limetengwa na Kijiji kwa ajili ya shughuli za machinjio basi lipewe shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lililoko Kusini mwa Soko la Kikatiti la kujenga nyumba za Polisi, Mwenyekiti au Diwani Pendaeli Nassari, alilipunguza eneo hilo, yeye pamoja na Mtendaji wake Bwana Abeli Kaaya, wakawauzia watu kwa faida yao. Wananchi wanaomba eneo hilo lirudishwe mikononi mwa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja Na. 158, kilichokuwa wazi hapo hapo Kikatiti, Mwenyekiti Pendaeli Nassari, alijichukulia kinyemela na kujenga nyumba, akaweka mashine ya kugasa mahindi na wananchi walipolalamika akauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya ardhi katika eneo hili la Kikatiti yamekithiri. Wizara husika ifuatilie migogoro iliyopo hapo kwani Serikali ya Kijiji imekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hilo la Kikatiti limepimwa na nakala ya ramani ninayo lakini kwa kukosa Uongozi mzuri wa Kijiji, wananchi wenye uroho wa ardhi wamevamia maeneo ya ardhi kijijini hapo na kujenga bila kibali; kwa mfano, Kiwanja Na. 49 cha Posta kimejengwa na mtu aitwaye Nesele. Kiwanja Na. 53 kilichotengwa kwa ajili ya Kanisa, kimejengwa na mtu anayeitwa Martin Mbise.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakala ya ramani ninayo na ningependa kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ili kufutailia tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaliundwa kwa lengo la kusogeza huduma ya utoaji haki karibu na wananchi na hivyo kupunguza msongamano wa kesi za ardhi katika mahakama zetu ambazo zina kesi zilizorundikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya migogoro ya ardhi Meru na kwingineko ni mengi sana na siyo rahisi kwangu kuyaorodhesha yote hapa. Mengine nitayatoa moja kwa moja kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kama njia ya kupunguza migogoro hii ya ardhi kwa wananchi, Serikali iandae mpango madhubuti na kutenga fedha za kutosha na vifaa vipatikane ili kupima ardhi nchi nzima na hivyo kuondoa migogoro ya ardhi iliyodumu kwa muda mrefu sana sasa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa maendeleo ya watu yanategemea sana ardhi na nyumba, ili mtu yeyote afanye kazi zake za kimaisha lazima awe na ardhi ya kutosha na nyumba bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo makubwa ya migogoro ya ardhi na nyumba mijini na vijijini. Vijiji vingi sana katika Jimbo la Mufindi Kusini havijapimwa. Vijiji hivyo ni Mtambula, Kiliminzowo, Nyigo, Ihawago, Iramba, Udumuka, Isaula, Makungu, Kitawengwa, Lugema, Ulelo, Matanana, Nyololo Shuleni, Maduma, Lwing'ulo, Ikangamwani na Idumulavanu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kata zote 15 kwa ujumla, Wananchi wote wa Jimbo la Mufundi Kusini wanahitaji vijiji vyao vipimiwe na vipate Hati za Kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yafuatayo:-

- Kupimiwa ardhi na kuwapa Hati za Kimila katika Vijiji vya Jimbo la Mufindi Kusini.

- Kuweka mipaka katika vijiji ili kupunguza/kuondoa ugomvi kati ya kijiji na kijiji.

- Hati za Kimila zitolewe haraka ili wananchi waweze kutumia katika mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri ufuatao:-

- Kwa kuwa ardhi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu watu au wananchi ambao ni Wazawa wa Tanzania, watumie ardhi yao bila kunyanyaswa na wawekezaji ambao tumewakaribisha, kwa sababu wapo wawekezaji wengine wenye tabia ya kuwanyanyasa wananchi wetu kwa kufunga mipaka ili wananchi wetu washindwe kupita katika maeneo hayo.

- Mtanzania apewe ardhi ya kutosha ili awekeze katika ardhi yao.

- Mtanzania apewe ardhi bure.

- Hati za umiliki zitolewe haraka bila kuchelewesha.

- Wananchi wahamasishwe kujenga nyumba bora katika vijiji.

- Gharama za ujenzi wa nyumba zipunguzwe hasa bati, *cement* na vifaa vingine vya ujenzi.

- Nyumba zinazojengwa na *NHC* kwa mkopo kwa Wananchi ambao ni Watanzania, gharama au bei ya kukopesha zipunguzwe ili wananchi wengi waweze kupata nyumba bora ambazo zinajengwa na *NHC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.**

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kushiriki kikao hiki muhimu kinachojadili hoja ya Waziri wangu wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nakushukuru wewe, Spika - Mheshimiwa Anne Makinda, Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Syvester Massele Mabumba - Mbunge wa Dole na Mheshimiwa Mussa Azza Zungu - Mbunge wa Ilala kwa uongozi wenu makini mnaofanya mijadala ya Bunge kufanyika kwa mafaniko makubwa.

Pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia mimi na viongozi wote wa Wizara yangu kwa ujumla. Vilevile nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Daudi Lembeli - Mbunge wa Kahama, kwa ushauri mwema na wa karibu wanaotupa ambao umetusaidia kutekeleza ipasavyo wajibu wetu. Tunawaahidi kwamba tutaendelea kufanya kazi karibu nao, kwani ushauri wa Kamati na maelekezo yao yamekuwa na manufaa makubwa sana katika kupanga na kutekeleza mipango na mikakati ya utekelezaji wa sera na sheria za sekta yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kushika wadhifa wa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

Makazi katika mabadiliko aliyoyafanya mwezi Mei, 2012. Napenda kumhakikishia kwamba nitajitahidi kadri ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu kushirikiana na wenzangu wote ndani na nje ya Wizara ili kutimiza wajibu huu niliokabidhiwa.

Kwa fursa hii adhimu, naomba niwapongeze kwa dhati viongozi wetu wakuu wa kitaifa wakiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ghalib Mohamed Bilal - Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda - Waziri Mkuu kwa uongozi na maelekezo yao mema wanayotupatia mara kwa mara yanayotutia nguvu mpya na ujasiri wa kukabiliana na changamoto za sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua nafasi muhimu sana waliyonayo wananchi wa Arumeru Magharibi katika utendaji kazi zangu za Kibunge na Kiserikali. Nawashukuru sana wananchi na viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi na vyama vyote vya Siasa, viongozi wa Kata na Vijiji, Mabalozi wa Nyumba Kumi, Viongozi wote wa Dini na wapenda amani na wapenda maendeleo wote katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Nawasihi kuwa tuendelee kuombeana na kushirikiana ili Wilaya yetu ipate ustawi na maendeleo tuliyotarajia.

Mwisho, naishukuru sana familia yangu, akiwemo mama yangu mzazi, Nesiliga Kiingilisho Laizer, mke wangu Antonia pamoja na watoto wetu Renalda, Nesiligaki, Joan, Josephine na Gregory Longamuno kwa dua zao na faraja wanayonipa mara kwa mara na kunitia nguvu hata ninapofikia kukata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika Wizara yetu na Sekta ya Ardhi kwa ujumla yametokana na utendaji wa pamoja baina ya viongozi na Watendaji Wakuu na watumishi wote wa Wizara. Mazingira hayo mazuri ya ushirikiano yametokana na uongozi mwema wa Waziri Prof. Anna K. Tibaijuka - Mbunge wa Muleba Kusini ambaye hupenda kutushirikisha katika kila jambo.

Napenda kumrudishia shukrani nyingi sana kwa uongozi wake mwema na kumwombea Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, maisha marefu na amzidishie hekima na busara ili aendelee kutuongoza na kubeba dhamana kubwa sana ambayo Mheshimiwa Rais alimkabidhi. Napenda kumhakikishia kwamba, ushirikiano wangu wakati wowote ni katika jidihada za kujenga timu imara itakayopambana dhidi ya kero kwenye Sekta ya Ardhi na Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, namshukuru sana Katibu Mkuu - Bwana Patric Rutabanzibwa kwa upendo na ushirikiano mkubwa anaonipa na hivyo kutufanya tuaminiane na kufanya kazi kwa karibu sana. Nampongeza sana kwa kuendelea kusimamia vyema misingi ya utawala bora katika Wizara pamoja na misukosuko anayopata toka kwa wale wasiopenda haki.

Namshukuru pia Naibu Katibu Mkuu Bi. Baaria Biria kwa ushirikiano mkubwa na utendaji wake wa kazi. Nawashukuru Wakuu wa Idara na vitengo vya Wizara wote, Wakurugenzi Wakuu akiwemo Ndugu Nehemia Mchechu, Mkurugenzi Kuu wa Shirika la Nyumba, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi - Dkt.

Kitinku, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Mipango Bora ya Nyumba - Ndugu Mango pamoja na viongozi wengine wote ambao wamekuwa wakitusaidia katika kutekeleza wajibu wetu.

Mwisho, nawashukuru sana Wasaidizi wangu wa Wizarani, Ndugu Godfrey Machabe na Elibariki Ngorovili, Katibu Mahsusi - Khadija Karambo na dereva wangu Bwana Renatus Temba na Wasaidizi wangu wa Jimbo wakiongozwa na Bwana Julius Makala na Evelyne Kivuyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba kwa fursa hii nijibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Wizara yetu kwa maoni yao ya kijasiri na ukweli ambayo yameboresha mipango na mikakati tuliyojiwekea ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010, Mpango Mkakati wa Wizara pamoja na maelekezo ya Viongozi wetu wa Kitaifa, na ya Bunge lako Tukufu. Tunapenda kuwaahidi kuwa tumepokea maoni yao yote na kuwa tutayafanyia kazi ili kurekebisha mapungufu yaliyoelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameona, tulijitahidi kufanyia kazi kwa dhati maoni na maelekezo yote yaliyotolewa kupitia Bunge lako Tukufu mwaka 2011 tulipowasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yetu. Tumeona kwamba tuna upungufu kadhaa ikiwemo raslimali, lakini tutajitahidi kutekeleza kadri Serikali itakavyokuwa inatuongezea uwezo.

Tunashukuru sana kwamba Serikali imekuwa sikivu juu ya maoni mliyotoa mwaka 2011 na ikakubali kutuongezea raslimali ya fedha mwaka huu 2012 na hivyo kututia matumaini kwamba sehemu kubwa ya mipango yetu itatekelezwa. Tunaendelea kuwaomba ushirikiano wenu ili tuweze kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutambua nafasi ya raslimali ardhi kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Vilevile tunawashukuru kwa kutambua vikwazo vinavyotukabili, hususan nakisi ya bajeti na kuishauri Serikali ipasavyo. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia umuhimu wa Serikali kupunguza au kuondoa kabisa kodi zinazotozwa kwenye mauzo ya nyumba za Shirika la Nyumba kwa lengo la kupunguza bei zake ili wananchi wa kipato cha chini waweze kumudu kununua na hivyo kujipatia makazi bora. Tunayo matumaini makubwa kuwa Serikali yenu sikivu na yenye kujali maslahi ya raia wake imepokea ushauri huo na itaufanyia kazi yenye kukidhi matarajio ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaowasikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa napenda kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sehemu ya suala la nyumba. Hoja ya nyumba imechangiwa na Wabunge karibu wote waliozungumza na walioandika. Waheshimiwa Wabunge waliochangia, kwa mfano, kulikuwa na kauli kwamba kasi ya ujenzi wa nyumba za kipato cha chini, kati

na za juu, iongezwe ili wananchi waweze kupata nyumba bora. Hoja hii ilizungumzwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mbunge wa Wawi.

Napenda kujibu kwamba, Wizara yangu imepokea ushauri wa Mheshimiwa Hamad, na kwa kupitia Shirika la Nyumba, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano, yaani 2011/2012 hadi 2014/2015 ambapo pamoja na uwekezaji unaofanywa na Serikali, sekta binafsi itashirikishwa ili kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wabunge walishauri kwamba nyumba zinazojengwa bado ni za gharama za juu. Hili ni suala ambalo nimelitolea kauli sasa hivi, ambalo limezungumziwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis - Mbunge wa Chambani na ningependa kusema kwamba Serikali imeanzisha kampuni ya *TMRC,* yaani *Tanzania Mortgage Refinance and Company* ambayo itatoa mikopo ya masharti nafuu kwa mabenki ili wananchi wapatiwe mikopo yenye riba nafuu kupitia mabenki ili wajijengee au kununua nyumba.

Vilevile Serikali inakamilisha maandalizi ya sera ya nyumba ambapo inategemewa kuwa itaweka maelekezo kadhaa ikijumuisha kupinguza au kuondoa kodi ya vifaa vya ujenzi. Hilo ni jambo ambalo litakapowasilishwa kwenu Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimesema awali, majuma mawili nilipokuwa nikijibu swali hapa, nilisema kwamba rasimu ya sera hiyo italetwa kwenu ili muweze kuijadili na kuitolea maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje aliomba Shirika la Nyumba liende Wilayani kwake Chamwino ili kuweza kupata viwanja ambavyo vitajengwa nyumba, na wananchi wa Wilaya hiyo ambayo ni mpya nao waweze kunufaika. Ningependa tu kumjibu kwamba Serikali imepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge, na Shirika limeelekezwa kufuatilia upatikanaji wa viwanja kwenye Makao Makuu ya Wilaya hiyo na kujumuisha kwenye mpango wake wa maendeleo.

Mchango wa Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood alioutoa juu ya kwamba nyumba za Shirika zimechakaa, ama zinahitaji marekebisho, ushauri huo tumeupokea na Shirika linao mpango tayari ambapo limetenga bajeti ya kiasi cha Shilingi bilioni sita kwa ajili ya kufanyia nyumba zake marekebisho kwa nchi nzima na Morogoro ikiwa ni mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapendekezo pia kwamba Shirika la Nyumba la Taifa liangalie jinsi ya kupunguza bei ya nyumba zake mpya zinazojengwa ili Watanzania wengi wa kipato cha chini waweze kumudu kuzinunua. Hilo limechangiwa na Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya - Mbunge wa Viti Maalum kutoka Kigoma, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda - Mbunge wa Viti Maalum, Singida na Mheshimiwa Vincent Nyerere - Mbunge wa Musoma. Tunasema kwamba Wizara imepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na utawasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawasihi Waheshimiwa Wabunge waendelee kutuunga mkono katika jitihada za kutafuta mbinu za kupunguza gharama za ujenzi na bei ya

nyumba ili bei za nyumba kwa ujumla ziweze kushuka kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja kwamba riba ya benki ni kubwa na ipo juu sana na kwamba kutowezesha wananchi kununua nyumba hizo. Hilo limechangiwa na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes – Mbunge wa Karagwe, pamoja na Mheshimiwa Zakhia H. Meghji. Tungeomba kusema kwamba tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yao ambayo ni ukweli na kwamba kupitia kampuni ya mikopo ya *TMRC* inatarajiwa kuwa riba za mikopo ya nyumba zitaendelea kupungua, na hivyo kufanya wananchi wengi kumudu kupata mikopo na kumudu kumiliki nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mapendekezo pia kwamba Serikali iliondolee *VAT* Shirika la Nyumba ambalo Mheshimiwa Abdalla Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, Mheshimiwa Lucy F. Owenya - Mbunge wa Viti Maalum, pamoja na Mheshimiwa Gregory Teu, ndio walipendekeza hayo. Lakini tunasema kwamba mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge yamepokelewa na yatawasilishwa Serikalini ili yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge juu ya Shirika la Nyumba, na nimejaribu kutoa yale ambayo yamezungumzwa na Wabunge walio wengi na kwamba yale yaliyobakia mengine tutayajibu kwa maandishi kwa sababu tayari tunayo majibu na kuwapelekea Waheshimiwa Wabunge wote majibu hayo.

Mheshimiwa John J. Mnyika, aliitaka Wizara ieleze ni kwa nini wananchi wa Mloganzila, Kisopwa pamoja na Kwembe wapatao 1919 wanaopaswa kuhama kupisha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya, wameelezwa kuwa hawatalipwa fidia ya ardhi wakati Serikali iliahidi katika Mkutano na wananchi mwaka 2010 kuwa watalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapata majuma mawili yaliyopita, nilijibu swali hapa Bungeni na nilitoa ufafanuzi juu ya suala hilo kwamba ardhi hiyo ambayo wananchi hao wanaishi ni ardhi yenye hati miliki kwa kampuni ya KABIMITA, yaani Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania ambayo hadi leo hati hiyo iko hai. Kampuni ya KABIMITA ilikuja kukabidhi eneo hilo kwa *Tanganyika Packers* na kwa hiyo, kimsingi wananchi wale hawamiliki ardhi.

Wananchi hao wapatao 1919 na wengine wa awamu ya pili, maana yake kulikuwa na awamu ya kwanza na awamu ya pili, wananchi 614 walichofaidi ilikuwa ni fidia ya maendelezo yao na siyo thamani ya ardhi na fidia ya maendelezo imeshalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Esther N. Matiko aliulizia juu ya suala la wananchi wa Soronti ni lini watalipwa fidia zao kupisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania? Swali hili pia liliwahi kuulizwa na Mheshimiwa Chacha Nyangwine - Mbunge wa Tarime na tuliwajibu kwamba Wizara inawasiliana na Halmashauri ya Tarime ili kupata maelezo zaidi ya suala hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tuweze kupata ufumbuzi wa kudumu wa suala hili. Wizara ipo kwenye mchakato pia kuhusu suala la viwango vya fidia ambavyo pia alizungumzia kwamba Wizara inakamilisha ujenzi wa

takwimu madhubuti za viwango vya thamani ya mali katika eneo hilo ili kwamba wananchi waweze kulipwa fidia inayostahili, kwani ni mojawapo ya mambo ambayo ameyalalamikia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja kwamba Serikali ibadilishe sera ya umiliki wa ardhi ili wananchi waweze kumiliki ardhi pamoja na raslimali zake. Hili pia aliliulizia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ambalo tunasema kwamba mchakato wa kufanya marejeo ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 pamoja na Sheria Na.4 ya mwaka 1999 na sheria Na.5 ya mwaka 1995 ya ardhi ya vijiji umeshaanza na kwamba tunatarajia kukamilisha katika kipindi cha kwanza cha mwaka wa fedha 2012/2013.

Pia kuna pendekezo la Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa - Mbunge wa Ruangwa ambalo pia limeungwa mkono na Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje - Mbunge wa Chilonwa na Mheshimiwa Lucy F. Owenya pamoja na Mheshimiwa Augustino M. Massele kwamba Wizara isomeshe vijana wengi kwenye taaluma ya upimaji wa ardhi ili Halmashauri zijitosheleze na kwamba hii ingepunguza gharama kubwa ya kodi ya wapimaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi lengo la kuongeza wahitimu katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro, Wizara imekamilisha ujenzi wa Bweni jipya lenye kulaza wanafunzi wapatao 500 na ujenzi wa bwalo na nyumba za Walimu. Vilevile mawasiliano yanafanyika na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuona uwezekano wa wahitimu wa Vyuo vya Ardhi kuajiriwa moja kwa moja ili kupunguza upungufu mkubwa wa wataalamu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Omar Nundu kwamba uvamizi wa eneo la mwambao wa Pwani umekithiri na kwamba anaiomba Serikali ilishughulikie suala hilo ili maeneo hayo yarejeshwe Serikalini kwa manufaa ya nchi, na kwamba mandhari ya Jiji la Dar es Salaam yameboreshwa. Tunashukushuru sana. Vile vile alisema kwamba, baada ya Wizara kutilia mkazo uanzishwaji wa bustani za kijani za Jiji, naishauri Wizara ishughulikie na Majiji mengine likiwemo Jiji la Tanga ambapo kuna hekta zipatazo 63.852 ambazo zimezungushiwa ukuta eneo la Raskazoni na linastahili kuwa bustani ya kijani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba pendekezo lake tutalifanyia kazi na tutashirikiana na Halmashauri ya Jiji la Tanga ili kuona namna ya kutumia vizuri maeneo hayo ya wazi kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Augustino L. Mrema amezungumzia migogoro ya ardhi katika Jimbo la Vunjo na ameeleza kwamba eneo la wafanyakazi wa Kahe – Kajiji, Kijiji cha Mawela waliotengewa tangu mwaka 1973 na Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kujichukulia ekari 100 kwa kilimo na hivyo kuwazuia wafugaji hao wasiendelee kutumia ardhi ile. Vilevile amezungumzia suala la Mji mdogo wa Himo na kuulizia kwamba: Je, kile ni Kijiji au ni Mji? Mamlaka inayohusika ni ipi katika kupanga? Kwani mpango umekwama baada ya kesi kufunguliwa Mahakamani. Vilevile amezungumzia kero inayowapata Masista wa Rawia ambao shamba lao la *West Kilimonjaro* limevamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjulisha Mheshimiwa Augustino L. Mrema - Naibu Waziri Mkuu Mstaafu na Mbunge wa Vunjo kwamba suala hili tumelipokea na kwamba tutalitafutia ufumbuzi.

Kuhusu suala la Mji wa Himo, Mji wa Himo ulitangazwa kuwa ni Mji mdogo kupitia tangazo la Serikali Na. 353 la mwaka 2004, hivyo mwenye mamlaka ya kusimamia maendelezo yake ni Ofisi ya Waziri Mkuu wa TAMISEMI kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Kuhusu suala la Masista wa Rawia, suala hili linalohusu mashamba, ninaloweza kusema ni kwamba tutafika kuona maeneo hayo yanayolalamikiwa na kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro tutatafuta ufumbuzi wa kudumu wa kero hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji inayotokea Tabora na Kilosa huchangiwa kutokana na mipango mizuri ya matumizi ya ardhi kutokuwepo. Suala hili limezungumziwa na Mheshimiwa Christopher Chiza – Mbunge wa Buyungu pamoja na Mheshimiwa Abdallah Haji – Mbunge wa Kiwani, pamoja na Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya – Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, Halmashauri za Wilaya kama Mamlaka za Upangaji, zinahimizwa kutenga bajeti kwa ajili ya uandaaji wa matumizi ya ardhi hususan kupitia programu zenye tengeo la fedha kitaifa, *yaani Capital Grants* kama vile *ASDP, DADPS, DAS*, *PFM,* MKURABITA pamoja na mipango mingine iliyopo. Wizara yangu itakuwa

tayari kushirikiana nao kwa kutoa wataalamu na vifaa pale ambapo wataomba msaada huo.

Mheshimiwa Kaika Saningo Telele, ameuliza kwamba, ni lini Serikali itaondoa migogoro kati ya wafugaji wa Kimasai na wakulima wa Batemi na Wasonjo kwa kupanga matumizi ya ardhi, sambamba na hilo kuainisha maeneo ya wanyamapori?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna rasimu ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa Wilaya nzima ya Ngorongoro ambayo imeandaliwa na Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, na kwamba mpango huo baada ya kuandaliwa mwaka 2010/2011 ulirejeshwa kwa mamlaka za Wilaya hiyo ili waweze kutoa maoni; hatma yake, watakapokuwa wameridhia, uweze kusajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ya Mheshimiwa John P. Lwanji, angependa kujua Mabaraza ya Ardhi yanawajibika wapi? Ni TAMISEMI au Wizara ya Ardhi au Wizara ya Fedha? Kwa sababu kuna malalamiko ya wananchi kuwa kuna rushwa katika uendeshaji wa Mabaraza na hata watu wasio na sifa wamepewa nafasi ya kuongoza Mabaraza ya Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji pamoja na yale ya Kata yanasimamiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri zinazohusika kwa mujibu wa sheria. Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya linaundwa na Waziri wa Adhi na linasimamiwa kiutalawa na Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la mgogoro wa mashamba kule Arumeru alilouliza Mheshimiwa Joshua Nassari ambaye kwanza, kama pacha wangu katika Wilaya ningependa nimpongeze sana kwa imani kubwa ambayo wananchi wa Arumeru Mashariki wameonyesha kwake na kumchangua kuwa Mwakilishi wao hapa Bungeni, nakupongeza sana Ndugu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya masuala ya mashamba haya, kwanza Wizara inaendelea kufuatilia kutoka katika Mkoa wa Arusha kuhusu ufutaji wa hati miliki za mashamba hayo uliyoyataja. Kuhusu shamba Na. 90 na 91 la Madira, maelezo ya mashamba haya yameshawasilishwa Wizarani na kwamba Wizara imeshafanyia uchambuzi na uhakiki na kuwasilisha kwa Mamlaka ya juu kwa uamuzi zaidi.

Shamba la *Lucy Estate* pamoja na *Karangai Sugar*, mashamba yanaendelezwa na mmiliki kwa sababu yanamilikiwa na mmiliki mmoja na kwamba Serikali kwa sasa hivi haina nia ya kutoa mashamba haya kwa sababu mmiliki alishatoa sehemu kubwa ya mashamba yake miaka ya nyumba ambayo yaligawiwa kwa wananchi na sehemu ya mashamba hayo yalitumika kwa ajili ya kuanzisha Taasisi ya Nelson Mandela.

Shamba la *Doli Estate*, hili ni kweli kumetokea mabadiliko ya matumizi ya ardhi ambayo yamefanywa bila kuzingatia sheria, kwa sababu mamlaka pekee ya kuidhinisha mabadiliko ya matumizi ya ardhi yapo kwa Mkurugenzi wa Mipango Mmiji na Vijiji na siyo mtu mwingine yeyote. Serikali imechukua hatua dhidi ya Maafisa

waliohusika kuidhinisha au kufanya mabadiliko yale kinyume cha sheria. Kwa mfano, Msajili Msaidizi wa Hati ambaye ndiye aliidhinisha mauzo hayo, alishaondolewa kazini, yaani alishaachishwa kazi, na Afisa Ardhi aliyehusika pia anashughulikiwa kwa mujibu wa sheria, yaani anachukuliwa hatua za kinidhamu na Bunge lako Tukufu litajulishwa hapo baadaye hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la Doli sasa hivi ni kweli kwamba limegawanywa vipande vipande na uchunguzi bado unaendelea ili kubaini na kuweza kupata taratibu sahihi ambazo zitaweza kutumika kuona namna bora ya kurejesha matumizi ya shamba hilo katika hali yake ya kawaida.

Kuhusu mashamba aliyozungumzia Mheshimiwa Abdul Aziz Abood, napenda tu nimjulishe kwamba suala hili alishaliwasilisha Mbunge wa Mvomero na kwamba linafanyiwa kazi ili kuweza kupata ufumbuzi. Lakini tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Morogoro, yaani Mheshimiwa Abood pamoja na Mheshimiwa Makalla, wanajitahidi sana kuwatetea wananchi wanaowawakilisha hapa, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, tunawashukuru sana kwa jinsi mnavyowatetea wananchi wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba niseme kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake na kwa dhati kabisa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Mheshimiwa Ole

Medeye kwa kuchangia hoja hii vizuri sana. Nakushukuru sana. Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, kwa vile sote tunajifunza, niongoze kidogo kwa ufupi sana namna ambavyo baadhi ya Wabunge tunaitumia ile kanuni ya 68(8) kuhusu taarifa ambayo nitawasomea hapa.

“Vilevile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa, na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema kuketi na kusikiliza taarifa hiyo.” Natoa hili kama funzo kwa wote, kwa maana ya kwamba Mbunge huwezi ukanipa taarifa mimi. Taarifa mnapeana ninyi kwa ninyi.

Mheshimiwa Profesa Tibaijuka - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, karibu.

**MBUNGE FULANI: Mwongozo.**

NAIBU SPIKA: Nimeshamwita Mheshimiwa Waziri, naomba tuendelee baadaye tukiwa na muda tutasikiliza miongozo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine tena naomba niwaashukuru sana kwa ushirikiano mliouonyesha na mwongozo mliounyesha katika kuchangia hotuba yangu ya Wizara ya Nyumba, Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nilipokuwa natoa bajeti yangu ulikuwa hapo, naomba nichukue nafasi kukushukuru kwa kushirikiano unaoutoa na mwongozo ukishirikiana na Spika wetu Mheshimiwa Anne S. Makinda. *(Makofi)*

Aidha, kwa mara nyingine tena nasema kwamba ni jambo la kutia furaha kwa mtu kama mimi nikirudi nyumbani nikakuta demokrasia imekomaa na watu wanachangia bila uwoga, nawashukuru wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kupoteza wakati, naomba kwanza niwashukuru kwa kuwataja majina Wabunge waliochangia bajeti hii nikianza na wale waliochangia kwa maandishi, nao jumla yao ni 159. Nawashukuru sana. Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Abdulaziz Abood, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Amina Abdullah Amour, Mheshimiwa Lucy P. Owenya, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa

Esther N. Matiko, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mheshimiwa January Makamba, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Neema M. Hamid, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mheshimiwa Charles John P. Mwijage, Mheshimiwa Zarina Madabida na Mheshimiwa Salum K. Barwany. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Omary Badwel, Mheshimiwa Said M. Mtanda, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir**,** Mheshimiwa Dkt. Therezya L. Huvisa, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Yusuph Haji Khamis, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashid, Mheshimiwa Innocent E. Kalogeris, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Naomi M. Kaihula na Mheshimiwa Ignas A. Malocha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Janes Z. Mbene, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola,

Mheshimiwa Deogratias A. Ntukamazina, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu, Mheshimiwa Lameck Airo, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer, Mheshimiwa Sylvester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse na Mheshimiwa Phillipa G. Mturano. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Maulidah Anna Komu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Catherine V. Magige, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Anna MaryStella J. Mallac, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Cesilia Paresso, Mheshimiwa Zahra Ali Hamad, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mheshimiwa Albert O.

Ntabaliba, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Capt. John Chilligati, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Dkt. David Mallole, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Sara M. Ally, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina na Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Conchesta Rwamlazwa, Mheshimiwa Ali Kheri Khamis**,** Mheshimiwa Rose K. Sukum, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Esta Amos Bulaya, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Haroub Shamis, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, na Mheshimiwa Seleman S. Bungara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine walikuwa ni wachangiaji wa maandishi na wengine walichangia zaidi ya mara mbili. Sasa naomba niwatambue kwa heshima na taadhima waliochangia kwa kauli, hawa wako 33, naomba niwatambue kwa majina yao.

Kwanza ni Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Anne K.

Malecela, Mheshimiwa Mustafa B. Akunaay, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Abas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ezekia D. Wenje, Mheshimiwa Salim Hassan Abdallah Turky, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Joshua S. Nassari, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Silvesty F. Koka, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed na Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetambua michango katika bajeti hii na nataka kusema kwamba wachangiaji kama nilivyosema ni 159. Sasa katika hali hiyo ninaweza nikafanya kwa dakika ulizonipa ambazo sasa hivi zimebaki dakika 50 naweza nikajaribu kumjibu mchangiaji mmoja mmoja haitakuwa na tija. Kwa sababu tutaondoka hapa bila ya kuwa tumeelewa na kutafakari ni kitu gani sasa kimkakati tunakwenda kutekeleza. Kwa ridhaa yako na kwa ridhaa ya Bunge lako Tukufu nitachangia *symmetrical,* yaani kwa kuhusu ni kitu gani tunaangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kwa mara nyingine tena namshukuru Mheshimiwa James Lembeli - Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na Naibu wake Mheshimiwa Abdulkarim Shah - Mbunge wa

Mafia, ambao tayari kwangu mimi ndio Bodi ambayo inanisaidia katika kutekeleza shughuli zangu. Sasa kuna mambo mengine hapa ambayo yameibuka ambayo nitakuwa nawaelekeza kwa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, Kamati ambayo inaniongoza mimi na ukitaka unaweza ukaita Bodi ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kitu cha kwanza kabisa, kwanza niwashukuru wote ambao mmeona kwamba pamoja na matatizo tuliyonayo, lakini jamani wengi mmesema kwamba mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Nimejitahidi. Sekta ni ngumu, sekta ni mtambuka na ni sekta ni ya kudumu. Nawarudisha kwa Mwasisi wa Taifa hili, Baba wa Taifa alisema: "Kusudi nchi iendelee sharti vitu vinne vitimizwe. Kuwe na watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora". Kwa hiyo, hapa tunapozungumza bajeti hii miaka 50 baada ya uhuru lazima tuangalie kama kweli tumemuenzi Mwasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mungu amlaze mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniweka katika sekta hii kwa sababu ni ngumu na mimi sina wasiwasi katika hili kwa sababu kama nimemenyeka nalo kwa ngazi ya Kimataifa, iweje nishindwe hapa Tanzania? Kwa hiyo, nimejipanga, lakini pia nakiri kwamba mimi sina uwezo wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ndiye alisema pawepo na mwanga pakawa na mwanga.

Mimi nafanya kazi kufuatana na yale yaliyo mbele yangu bila ya uwoga, bila uvivu, lakini kufuata sheria na maelekezo ambayo yapo. Sasa kwa mtu yeyote kuwa na ndoto za kusadikika, kwamba matatizo yangepotea siku moja, tutakuwa tunajidanganya. Kwa hiyo, ndiyo maana nazungumza kimkakati na hasa kwa uzito wa suala lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sasa hivi nina karibu mwaka mmoja na nusu au miwili katika Serikali hii na tunafanya kazi kwa bidii, Serikali ya CCM tunaongozwa na Ilani ya CCM. Lakini kuna mambo ambayo miaka 50 baada ya uhuru, Ilani ya CCM imesema, haya inayoyatekeleza na mimi kama Waziri, Mheshimiwa Rais aliyenipangia kazi hii, nikiri kwamba ananielewa vizuri. Kama alikuwa anataka ubabaishaji, nadhani tusingekuwa hapa.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba hasa sasa tunafanya hii kazi bila kuangalia mtu usoni, bila ya kubabaisha, bila ya kuona aibu, lakini pia *without loosing the sense of reality,* kujua hali halisi inayotukabili. Sasa hali halisi inayotukabili miaka 50 baada ya uhuru, nchi yetu hii kubwa *square kilometre* za mraba 945,000 takriban asilimia 10 tu ndiyo imepimwa.

Kwa hiyo, katika hali hiyo ni kwamba tuko kwenye *cross roads* za sheria, kiusasa na kiutamaduni. Kwa hiyo, ndiyo maana unakuta tuna migogoro na nitaanza kwa migogoro ya ardhi.

Migogoro ya ardhi inatuhusu sisi, wewe, mimi na Mtanzania, mwananchi anayetusikiliza kwa ujumla. Naomba nifafanue kwamba migogoro ya ardhi tunaizalisha sisi. Wakati mwingine maendeleo ya Sekta ya Ardhi,

Nyumba na Mipango Miji tunachelewesha sisi. Nitatoa mfano mzuri ulioibuka katika kikao chetu hiki. Mradi wa mji mpya wa Kigamboni, kwa nini utugawe? Ni mmojawapo sasa hivi umeacha kuwa mradi, umeshakuwa mgogoro, au sio?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimekuja kufanya kazi, lakini sasa hivi nimeibuka nimekuwa Waziri wa migogoro. Hii haifai! Yaani ningependa ushirikiano wa kila mmoja wetu humu ndani. Tutatue tatizo kwa sababu wananchi wana imani na sisi.

Kwa upande wangu, wananchi wa Muleba ndio wameniwezesha kuwa hapa. Sasa wakinisikia na mimi niko huku Bungeni nalia, nikapewa wadhifa, wengi walikuwa wananitakia kila la kheri, sasa unapewa kazi na wewe unabaki kulia, ina maana gani?

Kwa hiyo, hapa tunajipanga kufanya kazi na ukitaka kufanya kazi yoyote lazima uwe na mkakati. *You have to have a strategy,* unaendaje *in action plan?* Sasa Wizara hii kama mnavyojua, bajeti yake ni ndogo hii, wala haina mjadala wowote. Kwa vyovyote vile utakavyoiangalia, ni ndogo.

Kwa mfano, gharama ya kupima kiwanja kimoja sasa hivi kwa wastani ni Sh. 50,000/=. Gharama ya kupima Kijiji au kupima mipaka yake ni Sh. 700,000/=. Gharama ya kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kijiji kimoja ukitumia Tume yetu ya Matumizi Bora ya Ardhi ni Sh. 6,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako hili Tukufu kila mmoja wetu hapa ana Jimbo lake, unaweza ukafanya hesabu za haraka kuangalia fedha unazozihitaji kutekeleza yale ambayo mnataka nitekeleze. Yako kwenye bajeti ambayo iko mbele, hayamo, lakini hiyo haimaanishi kwamba tunakata tamaa sasa. Hiyo inamaanisha kwamba tunaweka mkakati, tunaangalia *priorities* wapi tuanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba tuachane na tabia ya ku-*complain. Complaining is not solving any problem.* Mtu anasimama ana-*complain* mradi wa Kigamboni umechelewa miaka minne. Mnajua kwamba mimi hata miaka miwili sijafika. Sasa na mimi Waziri nibaki ku-*complain*, kulia au nitafute *strategy* ya ku-*move forward?*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ndugulile - Mbunge wa Kigamboni rafiki yangu sana huwa tunafanya kazi kwa karibu. Sasa Mradi wa Kigamboni kusudi uende mbele, Serikali imetangaza na inatangaza Kigamboni sasa hivi ni *autonomous district* kusudi tuweze kuipanga Wizara ya Ardhi, yaani kwa jina la Anna Tibaijuka, Ole Medeye, Patrick Rutabanzibwa na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kupanga sisi Kigamboni, tunahitaji Sekretarieti ya kufanya kazi. Sasa hiyo Sekretarieti, *we must be put in place!* Ni lazima tuiweke na katika kujaribu kushirikisha, niliunda Tume ya Kushauri kwamba tuendeje juu ya utawala wa eneo hili kama *autonomous district,* tuanze kufanya mipango ya mji ule mpya. Sasa kazi hii imekamilika, Serikali imejipanga, imejikomboa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nadhani naona *addendum* zina-*fly* hapa, yaani tuna *addendum*

hapa tunajipanga kufanya kazi. Sasa mtu analeta mgogoro; *what is this*?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mimi naomba niulize swali, hatuwezi kwenda namna hiyo. Kote nilikopita duniani, Umoja wa Mataifa, hakuna Taifa nililokuta limepiga hatua linakuwa na *complainers*. Sisi hapa kuwa viongozi siyo kulalamika. Sasa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile mimi kwa yale aliyoyasema juu yangu kupata sifuri kwa mara ya kwanza, elimu haina mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa sijawahi kupata sifuri katika utendaji wangu wa kazi. Lakini elimu haina mwisho, nikaibuka na sifuri Kigamboni, lakini sikati tamaa. Naomba anipe nafasi na mimi nirudie mtihani tuone itakavyokwenda mbele. Lakini sasa wananchi wa Kigamboni wanisikilize, wasisimamishe mradi. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa mfano, *Kigamboni Development Agency* ambayo imeundwa na Serikali na ambayo tunakwenda kuisimika, *as we speak* tunakazana sasa, naomba nikabidhi hapa kama *part* ya *Hansard*.

*(Hapa Mheshimiwa Waziri alikabidhi Mezani nyaraka alizokuwa akizizungumzia)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikusomee Wajumbe waliounda Taasisi hiyo inayokwenda kupanga Mji Mpya wa Kigamboni. Mwenyekiti wake alikuwa ni Katibu Mkuu Mstaafu, Mr. Solomon Odunga, nadhani mnamfahamu, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni... *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ya hongo hayanitishi sana. Kwani kuna ubaya gani nikiwakaribisha Madiwani wa Kigamboni kama wageni wangu? Nimepokea wageni wengi sana. Sasa hiki chombo ambacho kimeundwa kwa ushirikiano wa Mheshimiwa Mbunge wetu, kitakuwa na Madiwani kama Bodi yake. Sasa utakuwa na nani kama sio hawa ambao utakuwa unafanya nao kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mjumbe mwingine ni Neema Bunango, Profesa Joseph Kilondo wa Chuo Kikuu cha Ardhi na Mr. Karambo Kaisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu mambo ya malipo na nani kalipwa, mimi mtu mmoja tu ambaye nimewahi kumlipa ni Mheshimiwa Ndugulile, Amelipwa kama mshiriki wa Kamati hii. Kwa hiyo, sijamlipa Mbunge yeyote wa Kigamboni. Nadhani nimelimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Watanzania tusifanye mchezo dunia haitusubiri. *The world is not waiting for us.* Mkifanya mchezo tunabaki nyuma kwa kuzua migogoro ambayo haina maana. Mimi kitu ambacho kimekuja kunitatiza sasa hivi, mimi ndio nimekuwa Waziri wa migogoro, ndiyo Hakimu wa migogoro, wananchi hawana imani na ni kweli mmegusia. Taratibu tulizoweka na nimezigusia katika hotuba yangu zimekwama. Sasa hivi Mwanasheria Mkuu aliniwezesha, nina Wanasheria Waandamizi ndani ya Wizara yangu, wameanza kazi yao na wanaenda vizuri lakini sasa wananchi wanapopata barua kutoka kwa Wanasheria wakati mwingine wakisema kwamba labda waende Mahakamani, wanakuja kwangu

wanalia; yaani Waziri umenitupa, unataka mimi niende Mahakamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona hilo ndilo tatizo tulilonalo na hapa nazungumzia Mahakama Kuu si haya Mabaraza ambayo yapo chini ya utawala wa Wizara ya Ardhi. Sasa mimi napendekeza kwa michango yote mizuri niliyosikia na wengi mliokuwa mnasema mlikuwa mnasema mambo ya msingi na mambo ya kweli lakini kusudi sisi Wabunge tu-*add value* ni kuacha kulalamika, kutafuta tatizo liko wapi. Kwa sababu matatizo mengine yanatokea lakini wanaogombania ardhi ni akina nani? Si ni ndugu na majarani na ndiyo maana Mabaraza ya Ardhi yaliundwa lakini yalipoundwa tatizo lake ni kukosa bajeti ya kuyawezesha kuwa katika kila Wilaya. Yalitakiwa kupeleka huduma hii ya haki za ardhi karibu na Wilaya kusudi mashahidi waweze kuja kwa urahisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ilivyo na nimezungumza kwenye hotuba yangu ni kwamba tutafute namna ya kuhakikisha Mabaraza yanafanya kazi viziuri lakini tukijidanganya kama kawaida tukatafuta *excuses,* turudi kwenye mfumo wa zamani. Profesa Shivji ni rafiki yangu na mwenzangu *is a very radical person.* Sidhani kama kuna mtu hapa ambaye yuko *more radical* kuliko Profesa Issa Shivji. Ndiye alipendekeza kuundwa Mabaraza baada ya kuona kwamba *the other system is simply not working*. Ilikuwa imekwama wakati Mheshimiwa Rais Mwinyi akiwa amemteua kama Mwenyekiti wa Tume ya Ardhi iliyozaa Sheria zetu mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba tusije sasa tukaingia katika biashara ambayo

Muasisi wa Taifa hili alituzuia. Hakuna kufanya juhudi bila maarifa na Mao Tse Tung alisema *no research, no right to speak* kwa sababu hapa inatakiwa tuweke *facts on the table.* Tatizo lipo linatambuliwa, sasa hivi tatizo na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu anafahamu tunalishughulikia, yeye na mimi tunahangaika. Juzijuzi hapa tulikuwa na kesi mpaka kwenye *Court of Appeal*, ndiyo unaweza wakati mwingine ukapata haki. Sasa mwananchi wa kawaida uwezo wake wa kufika *Court of Appeal* kupata haki inakuwa vigumu wakati hatuwezi kuzungumzia *matters* ambazo ni *sub-judice*, ziko mbele ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima mimi nitoe taarifa kwamba mfumo wa sasa tulionao inakuwa vigumu sana, lazima tutafute ku-*fast track* kesi za ardhi kusudi ziamuliwe mtu mpaka afike ngazi ya mwisho. Hiki ndicho kitu ambacho nitakiomba na baada ya hapa kwa kupitia kwa Waziri Mkuu na kwa kupitia kwa Mwanasheria wetu Mkuu tutajaribu kuzungumza na *Chief Justice* kuona namna ya kutusaidia na hapa sina budi kumshukuru kwa mfano katika mgogoro ambao mlikuwa mnausikia, ninyi mmesema migogoro ya kwenu, sisi ardhi tuna migogoro mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamenikaribisha kwenda kuwatembelea na namshukuru mwenzangu tumegawana kazi kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri amepata nafasi kuliko mimi. Mimi siwezi kwenda kwenye mgogoro kama sina ufumbuzi. Waziri wa Ardhi unafika kwenye mgogoro unaanza kulia na walalamikaji? *What is this?* Kusema kweli ndiyo maana yake lakini haimaanishi kwamba tumelala. Kwa hiyo, tunapopokea malalamiko, sasa hivi tunaunda Sekretarieti ya kutatua migogoro ya ardhi, tunafanya *research,* tunaangalia *facts* tunakwenda.

Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mbunge wa Mkinga, mtakumbuka katika bajeti iliyopita ilinileteа matatizo au sio na kusema kweli baada ya ile bajeti nilikwenda Mkinga nimejiandaa nikafanya *research* na nikaona kwamba kweli wataalam walisema ardhi ipo na yule mtu amepewa hekta 25,000 lakini kufuatana na matatizo nikaenda kuangalia mimi mwenyewe Mkinga na nikienda siwezi kwenda *hit* and *run*, lazima nije nimejiandaa. Siku tatu nilikuwa Mkinga, nikazunguka vijiji vyote, nilikuwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa tukazunguka na ikaonekana kwamba kweli ardhi haipo na hata kama ingekuwepo huwezi kuchukua ardhi yote kwenye vijiji ukalima jatrofa jambo ambalo mimi nimezunguka duniani sijawahi kuona shamba la jatrofa mahali pengine duniani yaani *experimental crop* kwa hiyo ikaonekana hapana, wataalam kidogo walikuwa wametupoteza tukaamua sasa yule mwekezaji apewe 5000. Kilichotokea ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nashukuru kwa wananchi wa Mkinga kwamba mgogoro wa Mkinga umekwisha kwa sababu ile ardhi haipo, yule mwekezaji hawezi kupata ardhi. Kwa hiyo, uamuzi niliufanya kwa dhati na kwa niaba ya Mheshimiwa Rais na wale waliosema kwamba nifanye kazi hii kwa ufanisi, lakini mgogoro huu haujaisha upo ofisini kwangu. Sasa hivi mnavyoniona msishangae tuko katika hali ya kushtakiwa na mwekezaji. Anasema mpaka apewe hekta 25000 Mkinga yaani sisi tuchukue Wadigo tuwatupe baharini yeye alime jatrofa, mambo gani hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa hiyo kama mfano. Sasa nikaenda kwenye mgogoro wa Vicky Fish Mwanza. Wewe Mheshimiwa Lwenje rafiki yangu nitakuacha,

unasema kwamba; mimi siwezi kudanganya; unavyoniona hapa mimi ni mtu wa kudanganya mtu? Kusudi iweje? Sidanganyi nakwambia kitu kama kilivyo. Pale Mwanza kwenda kwetu Muleba inabidi nipite Mwanza, sasa huyu anasema sijafika Mwanza. Sasa kati ya sisi wawili anayesema uongo ni nani hapo? Siwezi kufika Muleba bila kupita Mwanza. Huyu anasema sijaonekana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikaenda Magu baada ya kutafakari na kujua kwamba sasa huo mgogoro unaisha pale Vicky Fish, amekwenda kwenye kijiji cha wananchi Magu, amenunua ardhi hekta 600, anataka sijui kufanya mashamba ya samaki badala ya kuwavua Ziwa Victoria. Sasa wananchi wale wamemuuzia kweli na pale ziliungua zaidi ya milioni 200/- lakini mbona ule mgogoro ulikwisha kwenye *Town Hall Meeting* tukiwa na Mkuu wa Wilaya? Kwa sababu huwezi kununua ardhi ya kijiji kama Rais wa nchi hajakubali ihawilishwe. Sasa nikamwambia Vicky Fish, wewe umenunua kwa mtu mmoja mmoja, unajua kuna watu wengi wanatapeliwa. Hizi hati mnazofikiri watu wanazipata kama wanazipata ni batili na kwangu mimi hati yoyote batili ambayo haikufuata sheria tuko tayari kupambana kwa niaba ya mustakabali wa nchi yetu mpaka zifutwe. Kwa hiyo, sioni kwa nini mnakuwa na wasiwasi na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama hapa kuomba *trust,* lazima tu-*build trust*. Popote pale nilipopita, nimekuta mahali ambapo kuna *trust*. Kama hakuna *trust*; kama sasa hivi *we can not do a permanent election*. Uchaguzi ulishaisha na tunatekeleza Ilani ya CCM. Kwa hiyo, lazima tu-*build trust*, tuko kwenye nyumba moja. Kama kifo au vurugu; wengine mnasemasema vurugu lakini vurugu tunasema ni *ultimate revere*. Mbele ya vurugu *we*

*are all equal*. Ikitokea vurugu hapa kila mtu anabeba sanduku anakimbia bila kujali ulikuwa *opposition* au kwenye Serikali kila mtu ni mkimbizi. Kwa hiyo, tusifike hapo na wote hapa ndani ya nyumba hii bila kujali upo chama gani *we are all reformers.*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi katika kuchangia alizungumzia *about revolution. Yes, agrarian revolutions, that's what makes revolutions. If you fail agrarian reform a revolution is guaranteed.* Yaani ukishindwa kumiliki ardhi, utapata mapinduzi kwa sababu ya ardhi. Katika hili Mheshimiwa Tundu Lissu amesema kama ilivyo. Lakini ukiwa ndani ya nyumba hii ya Bunge wewe si *revolutionary*, wewe ni *reformer*. Ndiyo maana tuko Bungeni. Hakuna *revolutionary* hapa. Sisi ni *reformers*, tuko hapa tunajaribu kuweka mambo yawe mazuri. Tunachangiana mawazo, tuna-*add value*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili na katika mambo yenu mengi mliyoyasema ambayo mimi nimesema kabisa katakata siwezi kuyaangalia mojamoja, nachukua yale ya msingi, kwamba l*and reform* tunayoifanya ni muhimu, Sheria tunazo za kutosha. Tuna Sheria 14 za Ardhi. Kuna migogoro mingine tunaibua sisi wenyewe kwa kutokutekeleza sheria. Sheria ni nzuri tu. Serikali ya CCM katika miaka yote hii imetengeneza sheria nzuri, Bunge hili limetengeneza sheria nzuri. Sheria ya Madini, Ibara ya 97 inasema, ukishapewa leseni ya madini ni lazima ufanye *compensation* na *resettlement* ya wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na tukitoka hapa, migogoro ninayoisikia ya madini, kwanza watu ambao wanachimba na nimeshazungumza na Profesa mwenzangu Mheshimiwa

Muhongo bahati nzuri sasa hivi mambo yanakwenda *professorial*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitoka hapa tutakuwa na semina yetu, tutayatafakari na wachimbaji wote kuanzia Barrick sijui Kahama nini, lazima tuone kwamba wana hatimiliki za maeneo yale. Kwa sababu kama hawana hatimilki inamaanisha labda upungufu ambao ulikuwa kero ulijitokeza kwa sababu wananchi hawawezi kukaa kwenye *mining area,* lazima wawe *resettled* kwa mujibu wa Sheria ya Madini 2010 ambayo nadhani wengi mliopitisha Sheria ile mko humu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, ikitekelezwa, hakuna matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mdogo niliobakia nao ngoja sasa nigusie; hili la kero za wananchi na naomba wanisikie na wengi wananiletea *message*. Nyumba zao zime-*crack* kule Geita kwa sababu ya zile *blasting.* Hawatakiwi kuwa kwenye yale maeneo na ilitakiwa wale wenye migodi wawalipe na sio kuwalipa fidia ile ni *resettlement* yaani kama mtu alikuwa na shamba lazima pia apate shamba. Ndiyo *resettlement programs!* Tunakwenda kutekeleza *resettlement programs* na nadhani kero nyingi zitaondoka. Kwa hiyo, unaweza ukasema sijajipanga kimkakati na kunipa sifuri kweli? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kwamba kama hivi ndivyo ilivyo, upimaji, Mkurugenzi Mkuu wa Upimaji Tanzania yupo Wizara ya Ardhi, ni Dkt. Mayunga, tunaye hapa. Sasa wanatoka wapimaji wengine ni vihiyo kabisa na wenyewe wanapima. Sasa wanapopima wanafanya makosa. Unaweza kuwa na elimu, hata na mimi hapa ni mtaalam wa uchumi lakini siwezi kuchukua ile *total*

*station* ya siku hizi nikapima lazima utafute *the competent people*. Sasa naomba tabia ya watu kujipimia kuanzia sisi wenyewe Serikalini, wenzangu nimeshawaambia, nimeshazungumza na Waziri wa Ulinzi, Wizara itakwenda kupima maeneo ya Jeshi tupunguze migogoro. Kwa sababu Serikali imetenga kwa ajili ya ulinzi na ni muhimu lakini lazima ile mipaka ipimwe na Wizara ya Ardhi, haiwezi kupimwa na Wanajeshi wenyewe. *TANAPA*, maliasili hawawezi kupima wenyewe. Kuna *conflict of interest* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme kwamba mtu unapotaka kupimiwa, sasa wenzangu wa misitu, Ndugu yangu Mheshimiwa Kagasheki nimeshamwambia naye kwamba tujipange. Kuna msitu wa Kazimzumbwi kwa ajili ya *record* ya *Hansard* na mimi niwe *factual*, nimesema kama huna *research* usiongee, nyamaza. Sasa nimefanya *research*. Hapa kuna ramani inayoonyesha kwamba msitu wa Kazimzumbwi haujachakachuliwa na sisi Wizara ya Ardhi ila walipokwenda kupima walikosea. Kwa hiyo, hapa mnaweza mkaangalia...

*(Hapa Mheshimiwa Waziri alikuwa akionyesha ramani ya Kazimzumbi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakaacha eneo la msitu wakaingilia eneo la kijiji cha Chanika. Sasa tulipokwenda kwenye *verification,* ikaonekana kwamba na hii ndiyo tatizo la watu kutokuzungumza pamoja lakini hili tunalifanyia kazi Serikalini na kwa hawa *private surveyors* wote wanasajiliwa. Tuna vyombo vya kuwadhibiti lakini hatimaye ni lazima Mpimaji Mkuu aweke *stamp* yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uthamini. Mthamini Mkuu wa Serikali kama mnavyojua yupo Wizara ya Ardhi na Sheria zinasema kabisa kwamba uthamini utakwendaje. Ni lazima uwe ni *market value*. Sasa hii inamaanisha kwamba lazima ufanye *cross section research* uangalie kwa wakati ule ikoje lakini pia uwe na *time series data,* kuangalia *trend*. Huwezi kupima sasa hivi ukasema umemaliza. Unaangalia inavyo-*move over the years*. Sasa hii *land valuation bank* nimeizungumzia kidogo katika *speech* yangu ingawaje muda ulikuwa mfupi mtaisoma wenyewe. Sasa nataka kusema kwamba jamani mimi mnavyoniona nimerudi nyumbani kupigana na umaskini sio kupigana na maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili nalo lieleweke. Mtu adhulumiwe kwa faida gani? Yaani tunathamini kusudi mtu aibuke *better off. You have to be able to build back better* yaani unapothaminiwa uibuke *better off*. Kwa hiyo sasa suala la Kigamboni *New City* tunajipanga, mimi nakubali kabisa sasa hivi Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ameshasikia kwamba mimi nimeshamsamehe, yamekwisha kabisa, tuendelee, ni marafiki, kwamba badala ya wananchi kugoma wakubali kuthaminiwa lakini pia wananchi wasikaidi na wasiwe na uwoga kwamba wanakuja kudhulumiwa. Kama kulikuwepo na dhulumadhuluma jamani Mheshimiwa Rais ameshapanga safu na tena nikaibuka kidedea, kwa hiyo hakuna shida. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hiyo, tujipange, uthamini unafanyika. Tatizo linalotukumba sasa ambalo naomba Bunge lako Tukufu litambue, sisi Wizara ya Ardhi

hatuna shughuli yoyote mbali na utawala wa ardhi. Hatuna shamba sisi, hatuna mifugo, hatuna shule hata na hizi bustani mnazoniambia Mheshimiwa Huvisa Waziri wa Mazingira yupo pale. Unaona juzijuzi hapa nimemkabidhi maeneo yake oevu anaanza kuyashughulikia na yeye alikuwa anasubiri watu wa ardhi waje kulinda maeneo oevu, sio kazi yetu. Ukipewa kiwanja sio kazi ya Wizara ya Ardhi au Maafisa Ardhi kukilinda. Naomba hili lieleweke kwani litapunguza migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu umepewa kiwanja umekitelekeza, unakuja sijui unatoka wapi, unaibuka unasema mtu amevamia kiwanja chako, wewe ulikuwa wapi? *These are the issues* kwa sababu tusipolitambua hili, hatutaendelea mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuna swali la *dauble allocation. Double allocation* ni kweli hivi vitu vimetokea lakini sasa hivi *double allocation* hazipo na kama kuna mtu ana mfano wa *double allocation,* mimi ni Waziri ailete hapa mbele ili niimbe na yule aliyetoa *double allocation. (Vicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna kesi ya *double allocation* mtu aniletee lakini tuna *backlog,* matatizo yalikuwepo lakini lazima na sisi wananchi tukiri kusudi tu-*move forward,* hii sekta inataka nidhamu. Mimi nilipokuwa Nairobi, nimepanga Mji wa Nairobi, Nairobi nilifanikiwa na Serikali niliwaambia kuwa Mji wa Nairobi unahitaji *Metropolitan Authority* na imeundwa na kwa wale ambao mmefika Nairobi mmeona nini kimetokea, kwa Dar es salaam tunajipanga na tumenza na *Kigamboni District.* Kwa

*Kigamboni District* hatuwezi kurudi nyuma, misahafu inasema tutageuka chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wawekezaji kwa upande wa ardhi labda mtu anizunguke, mimi maslahi ya Taifa ndiyo moyo wangu na nilipofika hapa Mheshimiwa Rais akanipa kazi hii nilikwenda kumuuliza kitu cha kwanza kwamba tunafanyaje kuhusu *Land Policy,* hii *Land for equity* ninayoizungumzia ina ridhaa na imepitishwa siwezi kuitangaza hapa kama Mkuu wa nchi hajaikubali, tunachukua hisa katika mashamba na kama kuna mashamba yoyote ambayo yamepewa ardhi tunapata 25% ndiyo *minimum.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya kazi, inajiandaa kuleta Sheria na ninyi mridhie lakini kwa sasa hivi kama Sera, *Land for Equity* tumeanza kwenye *backyard* ya Rais mwenyewe. Wasweedish wamepewa shamba pale Bagamoyo, *Eco Energy,* Serikali ina 25%, Mthamini wetu Mkuu alikuwa anataka watulipe milioni 14 wakakataa wakasema ni nyingi, *this land has no value* (ardhi haina thamani), sasa wakaja kusikia kuwa Mama Tibaijuka yupo, wengi wananifahamu, wakaja kuniona nikawauliza hivi mnataka iweje? Mnataka mimi niwe kwenye historia kwamba ni Waziri aliyeuza ardhi ya Tanzania, *you forget*, tunachotaka sisi ni *shares.* Wakasema lakini hiki ni kitu kipya. Nikawaambia hapana kinajadilika na sasa Mungu bariki mchakato unaendelea kumalizika lakini tumeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo shamba pekee ambalo mimi ninaweza kuwaambieni limepata baraka kufuatana na utaratibu tulioweka, tunapata 25%, 15%

zinabaki Serikali Kuu kwenye *Land Bank,* 5% zinabaki kwenye Halmashauri yenye mradi na 5% tuna *float shares* kwa Watanzania, akina nyie na nyie muwepo kwenye hayo mashamba. Hizo ndizo Sera, hapo unaweza kusema nimepata sifuri? *(Vicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendeshwa na wataalam, mimi siyo mtaalam, watu wanasema kuwa mimi ni mtaalamu wa upangaji. Mimi ni Mchumi lakini hata kule Umoja wa Mataifa, Kofi Annan aliamua kumpeleka Mchumi kwenye sekta ya kupanga miji kwa sababu vitu vingi vinavyoingia mle pia vinataka uelewa wa uchumi unavyokwenda. Nchi yetu ya Tanzania kwa sasa hizi fukwe ambazo mnazungumza kuwa zimechukuliwa ni kweli sikatai lakini ndiyo hazina tuliyonayo, madini haya yatakwisha lakini fukwe tutakuwa nazo, tusipolinda fukwe *we have lost everything.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imebarikiwa na mnajua kila mtu anajua historia ya nchi hii, hili ni Koloni la Mjerumani. Katika Mkutano wa Berlin, Mjerumani alikuwa na nguvu na alikuwa na *the best maps,* ndiye alikuwa anajua madini yako wapi, hata Mwalimu Nyerere alisema kwa sisi tuliomsikiliza, anasema anajua madini yapo, ramani za Mjerumani ninazo lakini hatuna uwezo wa kuyasimamia hivi sasa, kama mnavyoona ndiyo tunaingia kwenye *resettlement programmes,* kuchimba tuchimbe, kule kwetu Wahaya tunasema "*usifanane na chura kwenye maji".* Chura anaimba yangu, yangu, yangu lakini hanywi maji, sasa siyo, hatuwezi kufa na umasikini wakati tunaweza kupata watu wa kutusaidia lakini haimaanishi wenyewe wanufaike sisi tuumie, sekta ya ardhi inatusaidia*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge mchangiaji kutoka Kilwa yeye amesema kuwa kama watu wa Kigamboni hawataki mradi, nimeshakaribishwa Kilwa. Kwa hiyo Kigamboni mmeanza kuwa na *competition.* Tulipofikia Kigamboni siyo pabaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeulizwa swali na Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Madabida, waliuliza swali la msingi, walisema una 10% ya fedha utafanyaje, tunakwenda ku-*float Municipal Bond. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi mmeongelea hapa, tunakwenda ku- *float Municipal Bond.* Uki-*float Municipal Bond,* hela unaipata *within a week provided you are credible,* hakuna mtu atanunua *bond* yako kama huna imani. Mmeshaanza kuona *stock exchange* inavyokwenda au siyo na Mheshimiwa Mgimwa alikuwa anaelezea hapa kuwa kuna *excess liquidity* kwenye *economy* kwa hiyo, tutakapo-*float bond* ya Kigamboni mahali pa kwanza kui-*float* ni Dar es Salaam *Stock Exchange,* tukitoka hapo tunaenda *Wall Street tu-float bond,* tukitoka hapo tunaenda *Hong Kong* tuna *float bond,* tuna *move forward* hatuwezi kukaa tunalia na kulalamika na sisi ndiyo viongozi, *we have to move forward.* Mimi nataka kusema kwamba katika hii sekta tupeni nafasi, viongozi wa nchi wameshaona tunaendelea, wametupa nafasi lakini inahitaji ku-*build trust.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapa badala ya ku-*work on the Municipal Bond* naanza sasa kukutana na watu wanaoandamana Kigamboni, sasa itanisaidia kitu gani? Nitakwama, nitapoteza muda na *time has no friend* (wakati hauna rafiki), haumsubiri mtu yeyote na Tanzania wakati hautatusubiri tusipoangalia watu wengine watafaidi kama

unavyooona sisi tutabaki kuwa watazamaji. Kwa hiyo, nataka kusema katika suala hili tunaliangalia tena kwa Uzalendo wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingekuwa mzalendo sidhani kama ningekuwa hapa ninahangaika na wezi wa ardhi hapa Tanzania lakini kwa uzalendo inafika *point* ni lazima ufanye kazi na wale watu ni wajanja, Mheshimiwa Nchimbi ameshaniwezesha *Land Rangers* mliwaona tumeshawaweka. Sasa hivi tumeshakubaliana na Waziri wa Mambo ya Ndani tunataka pia *Land Police* kwa maana kila mtu hapa ana leseni, kwa nini tunahitaji *Traffic Police? Traffic* wa nini wakati kila mtu ana leseni, si kila mtu anajua kuendesha gari lakini tunao kwa kuwa sisi sote ni binadamu na tuna upungufu wetu kama huna *speed governor* unaweza ku-*over speed* sasa ni hivyohivyo kwenye sekta ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomna nifafanue kwamba inapokuja kwenye mipango miji tunahitaji *displine.* Watu wanazungumzia Rwanda, ni *displine* kama eneo ni wazi, ni wazi. Unajua hakuna kitu kinachoniumiza kama kubomoa nyumba za watu. Kama unanijua vizuri kwa hulka yangu, kimsingi mimi ni mtu mwenye huruma sana lakini sasa huruma haimaanishi uwe mlegevu, ushindwe kufanya kazi, sasa watu wanajenga kwenye maeneo oevu makusudi kabisa, kama nilivyosema Mahakama zetu na wengine wamezungumza kuwa Mahakama nazo zina ulegevu maana kwenda Mahakamani haimaanishi kwamba lazima kesi yako ipokelewe, kesi za kipuuzi za ardhi inabidi zifukuzwe na Mahakama na katika hili Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na *Chief Justice* watanisaidia kwa sababu pia Hakimu lazima aangalie iko chini ya Sheria gani,

kwa mfano kuna sheria ya kumsaidia mtu *injunction* amalize kujenga nyumba kwenye eneo oevu? Ndiyo mambo yanayoendelea!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mdee huwa anapenda kunitania sana, Mbunge wangu wa Kawe, anapenda sana kunisumbua na mimi nampenda sana. Sasa yeye ananisumbua, anasema Kawe kule mimi sijatekeleza ahadi nilizoahidi, ahadi unaziweka lakini unakuta vipingamizi, kwa hiyo huwezi kuwa *overwhelmed* lakini nataka kusema kwamba watu waliojenga siyo kwamba hatuwaoni, nyie mnasema Serikali ya CCM ilikuwa imelala usingizi haikuona wanaojenga, wanaojenga nao ni wajanja wanakimbilia Mahakamani wanaweka *injunction* kusudi wamalize. Sasa hapa Bunge lako Tukufu liamue, tuko katika mchakato, vitu vingine tunavyozungumza hapa ni vya Kikatiba kwa sababu Mahakama nazo haziendeshwi na malaika, hatuwezi kuwa *outmoded systems, subjudice,* mtu anasaidia mtu mwingine avunje sheria, mambo ndiyo hayo. Kwa hiyo, hizi ndiyo c*onstrains* ninazokutana nazo na tunazokutana nazo katika sekta ya ardhi. Naliambia Bunge Tukufu kuwa nimejipanga na timu yangu inajipanga, ninapangua kusudi nipange, sasa huwezi kujenga mji bila kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanjelwa amezungumzia *squatters every where* katika Jiji la Mbeya, Waheshimiwa Wabunge nyie wote mnapanda ndege, Dar es Salaam *is what we call the mushroom farm* (shamba la uyoga). Ukiwa angani Dar es Salaam wakati mwingine ukikaa na mgeni unaangalia pembeni, unasema Mungu wangu sijui anafikiria nini, shamba la uyoga. Sasa mashamba ya uyoga tutakuwa nayo mangapi? Inabidi

tujipange na ili tujipange ni lazima niwape wadau elimu ya *study tours* na siyo hongo. Naposema kuwa ninaanza na *study tours,* ni lazima nitoe elimu, *mass education,* wananchi wa Kigamboni wana haki pia na kuwa na wasiwasi, wao wanaona kuwa ni sawasawa. Wahaya tuna methali, "*akana katagenda, katuma wachumba"* yaani katoto kasikotembea katasema mama yangu ni mpishi kweli kwa sababu hakajawahi kula chakula cha mwanamke mwingine, sasa watu wanaona wako sawa. Kigamboni *squatter* ni *the most strategic land,* ni *squatter,* sasa Serikali ambayo imewekwa madarakani na wananchi na yenyewe iache *squatter* iendelee? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima nichukue wananchi na siyo Madiwani tu, nitachukua pia wananchi wa kawaida na vijana. Kwa mfano, Madiwani wengi siyo vijana, ni wazee kama mimi ingawaje wengine wapo wachache, Mheshimiwa Ndugulile na mwenyewe nitakwenda naye kwa sababu huwa nakuwa naye kwa ajili ya kutengeneza sekretarieti, waende wakaone miji ili waelewe ninaposema *greed* ninamaanisha nini**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda niseme na nisisisitize, mfumo tulionao tunafanya kazi na TAMISEMI, ninashukuru wengine mmeliona, ni gumu kwangu lakini sasa unafanya kazi na sheria zilizopo. Kwa hiyo, ni juu ya Bunge hili Tukufu kubadilisha utaratibu kwa sababu wapimaji hao na *planners* ni *professions* za kiufundi, ni *professions* za kimahesabu. Kwa hiyo, uwezo wa kusimamia tumekubaliana kwamba umeshindikana au siyo? Sasa tupeni tuwasimamie sisi maana kuna wengine wako kule wanababaisha hapa na pale ili kusudi niende mbele, vitu vingine nimeshaona siyo wao. Wakati mwingine

wanatumiwa na *vested interests,* sasa mtu anajikuta yuko katika hali ngumu kwamba usipofanya hivi itakuwa hivi. Kwa hiyo, anaona kwa nini nipoteze kazi yangu, anayaacha kama yalivyo. Suala hili tulipo ni kwamba tunajipanga na hili mimi mwenyewe nitalirudisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu liko chini ya uwezo lakini ninalitambua. Katika changamoto nilizonazo, hii ni changamoto kubwa kwamba watendaji wa sekta ya ardhi wanahitaji *central direction,* sasa hapa ilipo haifanyi kazi kama hiyo ikipatikana itakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli mambo muhimu nimejaribu kuyazungumzia kimkakati lakini kwa zile kero mojamoja siyo kwamba nazipuuza. Ni kwamba hizo kero mojamoja tutaziangalia na migogoro mimi mwenyewe nitakuwa mgeni wenu, nawashukuru sana wale ambao mmenialika lakini na mimi sasa niingie pale kama Waziri wa Ardhi, niingie pale, wataalam wangu wakiwa wameshapita, wameonyesha kuwa iko hivi na hivi na wadau wengine wameshapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa simtendei haki Mheshimiwa Ester Bulaya, amezungumzia suala la vijana. Suala la vijana ni muhimu sana. Nchi yetu imepungua mara sita yaani *per capital,* tulipopata uhuru kama kila Mtanzania angepewa ardhi angepata hekta 1,200 sasa hivi ukitaka kuigawa kwa kila Mtanzania atapata hekta 200 tu. Kwa hiyo, kuna *land pressure* na isitoshe ardhi katika vijiji ni ile tunaita *five kilometre radius* kwa sababu watu wanatembea, ardhi ambayo iko mbali na hapo huna kazi nayo, sasa vijana ambao wapo katika vijiji ambao hawana ardhi ya kutosha, Waheshimiwa Wabunge naomba mnisaidie katika *resettlement programmes* na kwa hili

nitaanzia kwangu Muleba. Muleba kuna vijiji kama Nshamba mnaona mambo yanayotoka, nichuke nafasi hii kusikitika kwamba vikongwe wanasumbuliwa, ni aibu kubwa. Sidhani kama iko Muleba peke yake, Taifa hili lina *culture of silence,* watu wananyamazanyamaza, mambo mabaya yanatokea, watu wananyamaza. Tatizo la Albino halijaisha, mliona juzijuzi huko Geita wanasema wanawake ni wachawi, nani hajui kuwa fisi aliumbwa na Mwenyezi Mungu, mtoto kauwawa na fisi wakasema wanawake ndiyo wanamroga. *Resettlement programmes* zitakuwa muhimu na kwa upande wa wanawake wawezeshwe kwa kupewa hati za kimila kama kuna mtu anawasumbua, waje moja kwa moja, hao nitashughulika nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na Mama Helen Mrutu. Mheshimiwa Anne Kilango, naomba umwambie kuwa suala hili ninalichukua kama langu maana yule ni mjane mwenzangu kama ulivyosema na mimi ninaijua hiyo hali kwanza umefiwa na mume hata Quran na Biblia inatuzungumzia sisi wajane kwa sababu ni watu wa kuhangaika na inaonekana kwamba ana viwanja vyake vinne kule na kuna watu wanajaribu kumsumbua. Sasa hilo ninalichukua kama langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa upande wangu, kwanza kabisa, nakushukuru sana wewe na Mheshimiwa Makinda kwa miongozo mnayotupa. Nimshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, nishukuru misaada ninayoipata pamoja na kuwa na bajeti finyu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ananiwezesha kwa kunisaidia, nimshukuru mwenzangu Mheshimiwa Ole-Medeye kwa kuwa tunafanya kazi kama *team, we are a winning team,* hatuna nafasi ya kusukumana na niwashukuru watendaji wote,

nimshukuru Bwana Patrick Rutabanzibwa, yeye alipoona chupuchupu kufungwa akijaribu kutetea *open space* za *Osterbay,* alikuwa afungwe yeye na Mkurugenzi wa Mipango Miji, ilibidi tukimbilie kwa *Chief Justice,* ndiye aliyetuokoa maana yalikuwa mawili aidha unaasi amri ya Mahakama hutaki kugawa viwanja au unakwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijazungumzia sana nyumba kwa sababu mwenzangu alizungumza, niseme tu kuwa suala la nyumba kwa kumalizia ni kwamba tutaleta Sera, tunaifanyia kazi kama mlivyoiomba Mheshimiwa Makamba. Hatuwezi kuja na Sheria hapa Bungeni bila Sera maana Sera ni lazima ipite kwenye Baraza la Mawaziri, wote tukubaliane, sasa ile Sera isije ikaturudisha nyuma. Katika fani ya Uchumi, kama huna nyumba za kutosha hata ungekuwa na vyombo vya kudhibiti mara ngapi, tusije tukajikuta tunaunda vyombo vya ulaji tu, watu wanakaa pale wanalipwa lakini hawana kazi yoyote wanayofanya. Kwa sababu haitakuwa *effective* kama hakuna nyumba za kutosha lakini pamoja na hayo nakubaliana na hoja hii kwamba kuna haja ya kuangalia utaratibu huu ambao sijawahi kuona popote wa kukipa mwaka mmoja lakini na wenyewe unatokana na *market forces.* Hili suala la nyumba tunalo na Naibu Waziri ameigusia mambo ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niseme kwamba naomba kutoa hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na tunakushukuru sana. Nimeona Wabunge wawili kwa kifupi sana naomba mzungumze, nawapa nafasi Wenje na Lugola, kwa kifupi sana.

Kabla ya kuwapa nafasi, niwaambie watu wa *Hansard,* kuna wakati Mheshimiwa Waziri alitaja jina la Mheshimiwa Lwenge lakini alimaanisha Mheshimiwa Wenje. Kwa hiyo, waweke sawa tu hapo Wenje Mbunge wa Nyamagana, Mheshimiwa Wenje kwa kifupi sana.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nimesimama kuomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Naomba Mwongozo kwa sababu muda mfupi uliopita ulipokuwa unazungumza na Mheshimiwa Halima Mdee, umetamka maneno kwamba, "wananchi wa Kawe mnaona mlivyochagua kituko".

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kauli kama hii na wewe ndiye unayeendesha Bunge, unadiriki kutoa kauli kama hii, sisi Wabunge tutajifunza kutoka kwa nani, naomba uifute. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Wenje, unaweza ukasema maneno hayo kama hukuona vituko alivyokuwa akivifanya. Kwa hiyo, nilisema hivyo ili wananchi waone vituko alivyokuwa akivifanya alipokuwa pale, huo ndiyo mwongozo wangu. *(Kicheko)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira ambayo niliomba kutoa hoja ya kuahirisha Bunge nikakosa nafasi, wakati nina jambo ambalo kwa kweli ni la dharura, ninaomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7) nitafanyaje katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mkononi kwangu nina gazeti la Uhuru ambalo ninaomba nilisome; linasema, *Comrade Auction Mart Company Limited*, Tangazo la Mnada wa Hadhara. Kwa amri tuliyopewa na Mahakama Kuu, *Division* ya Kazi Dar es Salaam, kuhusiana na utekelezaji wa deni tuzo, tutauza kwa mnada wa hadhara kiwanja kilichosajiliwa kwa *plan* Na. 14768, kinachomilikiwa na *General Tyre* Arusha, pamoja na majengo yaliyomo ndani ya kiwanja hicho kutokana na shauri la *Execution* Na. 75 ya mwaka 2000 baina ya *TUICO* kwa niaba ya wanachama wa *General Tyre East Africa Limited* yaani Washinda Tuzo na *General East African Limited Arusha* Mshindwa Tuzo. Mnada utafanyika tarehe 14 Mwezi Julai, 2012 yaani kesho kutwa Jumamosi kuanzia saa nne asubuhi, mahali kiwanja kilipo, Arusha, *General Tyre.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako endapo Serikali haitachukua hatua kuanzia leo, Jumamosi mali ya Watanzania itauzwa kwa mnada na sasa hivi tunavyozungumza tayari watu wameshaanza kusogea Arusha ili Jumamosi waweze kununua Kiwanda hiki cha Watanzania kwa bei ya kutupwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wabunge wote hapa tulisema kwamba sasa ni wakati wa kufufua viwanda na kujenga viwanda kwa ajili ya kuondoa tatizo la ajira.

Kiwanda hiki cha *General Tyre* historia yake kilikuwa na deni la dola milioni kumi za *NSSF* ambazo zilitafunwa na Menejimenti ya kiwanda hiki na sasa wafanyakazi hawa wanadai shilingi bilioni 1.8 tu ndiyo sababu walipeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, Serikali haioni kwamba inawajibika katika Bunge hili kwa sasa kutoa kauli kama kweli na siku yenyewe imebaki ni kesho, wataenda kuji-*commit* kulipa fedha hizi kwa hawa wafanyakazi ili kiwanda hiki ambacho Serikali inamiliki asilimia 74 na Mbia mwenza anamiliki asilimia 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona jambo hili ni la dharura, sasa katika mazingira ambayo nilikosa nafasi, naomba mwongozo wako nifanye nini kama Serikali haitatoa kauli juu ya jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kifupi sana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kulikuwa na amri ya Mahakama kama anavyosema Mheshimiwa Lugola, lakini Serikali kwa sasa imeshachukua hatua na kwamba amri hiyo imeshapata *injunction* ambayo Waziri wa Ardhi alikuwa anaisema, tumepata na sisi *injunction* ili kusudi tusikilizwe kwanza. Kwa hiyo, mnada huo hautakuwepo siku ya Jumamosi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda uliobakia ni vema na haki tuingie katika hatua inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 48 - WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Kif. 1001- *Administration and HR Management*..........................................*TShs*. 6,418,495,100/=

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua kuhusu yale mashamba ya mkonge ambayo hayaendelezwi, Waziri anachukua hatua gani ili yafutiwe hati zao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwamba suala la mashamba ya mkonge tayari tunalifanyia kazi. Katika Sekretarieti yetu ya Migogoro na ni kweli mashamba ya mikonge kuna sehemu zingine kama nilivyosema kuna *land pressure* kubwa ambapo itabidi Serikali itwae yale mashamba. Ni kweli kuna mashamba mengine ambayo yametelekezwa, tutayachukua chini ya *section* ya *adverse possession* ya watu waliotelekeza mashamba. Kwa hiyo, zoezi hili ni lazima tulifanye kwa uangalifu, kuna vikwazo vya kisheria hapa na pale lakini kwa wananchi ambao wapo katika mashamba ya mikonge yaliyotelekezwa, mchakato

unaendelea wa kuyatwaa ili kusudi yagawiwe kwa wananchi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inaiagiza Serikali kuanzisha Mabaraza ya Ardhi kumi kila mwaka. Je, ni lini Wilaya ya Ngara itafikiwa? Nilishamwandikia Waziri, kwamba wananchi wa Ngara kuna kesi nyingi za ardhi, wanahangaika kwenda Chato ambapo ni kilomita 250 huku wakipata shida. Naomba Waziri aeleze ni lini Ngara tutapata Baraza la Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, najua tatizo la Ngara, ingawaje sasa hivi *Alhamudulilah* tunamshukuru Mheshimiwa Magufuli barabara ya kwenda Chato siyo mbaya sana, lami inapatikana. Kwa hiyo, hali halisi kwa mwaka huu Ngara ipo kwenye bajeti lakini kwa vyovyote vile ninaelewa tatizo na tutalipa *priority* tukipata nafasi.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Napenda kuuliza swali langu ambalo kwa kweli halikujibiwa kwenye mchango wa maandishi, kwamba tangu miaka ya 1996, Serikali au Wizara ilifanya upimaji wa ardhi katika kugawa mipaka ya Mikoa, Wilaya na Vijiji lakini cha kushangaza ni kwamba kwenye suala la utawala wananchi hawafahamu kwamba mipaka yao iko wapi, kama wapo mipaka ipi, kwa mfano kama ni Singida au ni Manyara. Napenda kujua mstakabali wa kuondoa migogoro hii ya ardhi ya muda mrefu tangu mwaka 1996 mpaka leo haijakamilika. Tunarukia kwenye migogoro mipya hiyo ya zamani itaondokaje katika nchi hii?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa kabisa, kama nilivyosema, suala la kuhakiki mipaka ya ndani na nje ya Tanzania ni jukumu letu, pale ambapo panaibuka migogoro ya mipaka, wakati mwingine mipaka ilikuwa…

*(Hapa umeme ulikatika)*

**WABUNGE FULANI:** Endelea!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba mipaka tunaihakiki tukishirikiana na TAMISEMI na pale ambapo pana ubishi mwingi inatokana hasa na *natural boundaries* kuhama. Nifafanue tu kwamba kwa wale ambao wana mipaka ya Ziwa hususani lile la Iramba, kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya tawala za maji, kama kuna Ziwa, huwezi kuchukua Ziwa ukaliweka sehemu moja ya Wilaya na nyingine ikabaki haina Ziwa. Hapo tunarekebisha ramani zetu, mpaka wetu unakuwa katikati kila sehemu inapata nusu, hali kadhalika kwa mito. Kwa hiyo, labda niseme tu pale ambapo kuna *specific problem* tunashirikiana na wenzetu TAMISEMI kuliweka sawa, lakini tuna *principles* zinazotuongoza ni kwamba mipaka kama *waterboard* tunaigawanya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tujaribu kuendelea huenda hali ikajirekebisha, Mheshimiwa Mendrad!

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kuuliza swali dogo. Kwanza

nashukuru Wizara kwa kuchukua hatua ya kupima vijiji vyetu ili wananchi wote waweze kupata hati ya kimila. Je, mtu akipimiwa asubiri muda gani ili aweze kukabidhiwa ile hati ya kimila?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mwananchi kupimiwa ardhi yake, utaratibu ni kwamba hati itaandaliwa, itasainiwa na Mtendaji pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji na baada ya hapo itapelekwa Wilayani ambapo Afisa Ardhi ana wajibu wa kutia saini pamoja na kusajili hati ile kisha inarudishwa na kukabidhiwa mwananchi anayehusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muda, haipaswi kuchukua muda mrefu kwa sababu kutoka kijijini hadi Wilayani hakuna kijiji ambacho utasafiri zaidi ya siku moja hadi kufika Wilayani. Kwa hiyo, tunategemea kwamba katika muda mfupi usiozidi wiki mbili mwananchi angepaswa kuwa amepata hati yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tutakubaliana kwamba ni vigumu sana kuendelea katika hali tuliyonayo, kwa hiyo Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**WABUNGE FULANI:** CCM!

**WABUNGE FULANI:** Juu!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane, kwa sababu ya hali tuliyonayo, hatuwezi kuendelea kwa utaratibu huu. Kwa hiyo, naomba kuahirisha

shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.22 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 13 Julai, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*